

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Arobaini na Moja – Tarehe 7 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Wajumbe walianza kupata wasi wasi walipoona kiti kiko wazi! Nikaona mambo leo yanakuwaje! Lakini nashukuru sana tena siku yetu ya Alhamisi, tunaanza na kipindi cha dakika 30 kwa Waziri Mkuu. Maswali kwa Waziri Mkuu siyo sawa sawa na Maswali tunayouliza hapa. Kwa hiyo, kama limejibiwa kama litatendeka, usianze tena kudadisi tena Maswali ya Nyongeza yasiyokuwa na sababu. Kwa hiyo, tutaanza na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu leo yupo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2006 wafugaji ambao walikuwa katika Bonde la Ihefu walihamishwa na.

**NAIBU SPIKA:** Inaelekea hatukusikii vizuri!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mnamo mwaka 2006 wafugaji waliokuwa katika Bonde la Ihefu walihamishwa na katika *exercise* hiyo au katika hatua hiyo, kuna baadhi yao mali zao zilizharibika na haki za binadamu kwa kiasi fulani zilivunjwa hadi kufikia Rais akaunda Tume ya Jaji Chande.

Je, Serikali ni lini italeta Bungeni taarifa ya Tume ya Jaji Chande ili Wabunge na wananchi wapate kujua hasa yale yaliyotokea na zile mali hasa zilizopotea na wale ambao haki za binadamu kwa upande wao zilivunjwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hamad Rashid kama ifuatavyo:- Ni kweli kwamba Serikali iliunda Tume na ilikuwa Tume ya Ngazi ya Juu sana iliyoongozwa na Jaji Chande na walimaliza ile kazi

kulingana na maelekezo ya Serikali na taarifa ile iliwasilishwa Serikalini kwa ajili ya matumizi yake.

Hatua mbalimbali zilifuatiliwa baada ya hiyo Tume kumaliza kazi yake, lakini sehemu kubwa vile vile bado hazijakamilika, zingine zinahitaji kidogo uchunguzi na upelelezi wa kiasi fulani.

Lakini, ametaka kama inawezekana taarifa ile iwasilishwe Bungeni kwa lengo la kuliwezesha Bunge lako kuweza kupata fursa ya kujua kilichotokea. Kimsingi sidhani kama lina tatizo. Tumefanya hivyo kwa taarifa zingine ambao nazo ziliwasilishwa Bungeni. Kwa hiyo, nitamshauri Mheshimiwa Rais, akiona inafaa basi nitaiteta ile taarifa kwa sababu siyo jambo la siri sana, ni mambo tu ya kawaida ya kiutendaji. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba hakuna tatizo la taarifa hiyo kuletwa; anaweza kutuambia katika Bunge hili ni lini anafikiria taarifa hiyo inaweza kufika hapa hasa akizingatia kwamba Bunge katika Katiba, Ibara ya 63 lina mamlaka ya kuisimamia Serikali. Pili, kwa mujibu wa Sheria ya *Immunities and Privileges Act*, Mbunge anayo haki ya kupata taarifa. Kwa hiyo siyo suala la kwamba ni hiari, Bunge linayo mamlaka ya kupata taarifa, na kutokana na Mwongozo wa Spika alioutoa hapa katika Bunge lako tukufu kwamba Mbunge anapodai taarifa, basi taarifa hiyo iletwe. Je, ni lini taarifa hiyo italetwa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hamad anasahau kwamba Bunge lina pande mbili; Yuko Rais upande mmoja na wako Wabunge upande wa pili. Ndio maana nimesema, kimsingi halina tatizo kwa sababu ni taarifa ambayo haina mambo ambayo mnaweza mkasema pengine ni mambo yanayohitaji usiri, hapana, ni *public document* ambayo nafikiri mnaweza kuipata.

Lakini kwa sababu Tume ile iliundwa chini ya Mamlaka ya Rais ambaye ni sehemu ya Bunge hili, ndio maana nimesema nitamshauri Rais, akiona inafaa, nitaiteta hapa ili muweze kuona kilichomo ni nini. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru! Mheshimiwa Waziri Mkuu, sote humu ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na pamoja na mambo mengine tuna wajibu mkubwa wa kuisimamia Serikali na kuwatumikia wananchi wetu ambao ndio wadau wakubwa waliotuchagua wakatuleta hapa. Sasa ni kwa nini katika Bodi hizi za Mashirika ya Umma Wapinzani hawashirikishwi?

**WAZIRI MKUU:** Sina hakika! Umesema Wapinzani au?

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema katika Bodi hizi za Mashirika ya Umma, Wabunge wa Kambi ya Upinzani hawashirikishwi!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama nina jibu zuri sana kwa hili. Lakini, mwenye mamlaka ya kuteua wajumbe wa Bodi hizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wenyeviti wa Bodi mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na kwa mujibu wa Katiba ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa, kama anaona yeye inapendeza kumweka Mheshimiwa Mnyaa kwenye Bodi mojawapo, mimi naamini kama hajafanya, iko siku atafanya. Lakini, sidhani kama ni jambo ambalo naweza nikajibu moja kwa moja kwa niaba ya Rais. Lakini kwa sababu umeliuliza, nadhani yuko Iringa atakuwa amesikia, nadhani ataona kama inapendeza kufanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru! Swali langu kwa Waziri Mkuu litahusu mfumuko wa bei. Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo asubuhi mfumuko wa bei umekuwa asilimia 9.3. Mwezi uliopita mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 9.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua jitihada za makusudi za Serikali za kudhibiti mfumuko wa bei. Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mfumuko wa bei huo huo katika upande wa chakula hivi sasa umefikia asilimia 55, ni dhahiri kwamba bei za vyakula kama mchele, sukari, ngano, vimepanda maradufu. Hivi Serikali hili hailioni?

Je, Waziri Mkuu anasemaje katika haya mawili?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa N'hunga swali lake kama ifuatavyo: Maswali yake *actually* yako mawili pale! Kimsingi yote mawili yanahusiana na mfumuko wa bei na mfumuko wa bei unasababishwa na mambo mengi.

Lakini kwa sasa mambo makubwa ambayo yanachangia katika suala hili ni kupanda kwa bei za mafuta ambako kumekuwa kukiongezeka kwa kasi kubwa sana na kwa wakati mwingine hata yanapofanya mabadiliko ambayo kidogo yanaweza kuteremsha bei ya mafuta, si rahisi mfumuko wa bei mara moja na wenyewe kujirekebisha.

Kwa hiyo, Serikali inalijua hili, lakini ni juhudi ambazo lazima ziwe si zetu peke yetu, kwa kweli ni suala pana sana kiasi kwamba sisi tunajaribu kujitahidi tu kwamba tuhakikishe tunadhiti vizuri bei za mafuta kwa maana ya uwezo uliomo ndani ya uwezo wetu kwa kutumia vyombo vyetu vya Mamlaka ya Udhibiti ili tuhakikishe kwamba hawapandishi bei kiholela.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukishafanya hivyo, ujue vile vile kwamba gharama nyingine zitaongezeka. Sasa mahindi mengi yanalimwa Mikoani na usafirishaji wa vyakula hivi hasa kuja Dar es Salaam unategemea usafiri wa malori. Kwa hiyo ni dhahiri kabisa kwamba bei za vyakula nazo zinapanda kutokana na sababu hiyo nyingine ambayo nimeieleza. Lakini, tunachoweza kusema tu hapa ni kwamba kubwa ni tuhakikishe tunakuwa na chakula cha kujitosheleza sehemu kubwa ya Watanzania, hiyo inaweza kutusaidia sana kuweza kuhimili kishindo hiki cha mfumuko wa bei.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo ni miaka 10 tangu Ubalizi wa Marekani pale Dar es salaam ulipopigwa mabomu. Wakati nikichangia Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, nilieleza masikitiko yangu juu ya kiwango au fedha kidogo ambacho Wizara hii imekuwa ikipewa kila mwaka ukilinganisha na majukumu iliyanayo hasa ya ulinzi wa usalama na mali za wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Je, Tanzania ambayo inasifika kama kisiwa cha amani na utulivu duniani, itaendelea kwa muda gani kudumisha amani hiyo katika mwenendo huu wa Bajeti kama hiyo wakati idadi ya watu inaongezeka na ujambazi hapa nchini unaongezeka? Ahsante sana! (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa James Lembeli swali lake kama ifuatavyo:- Ni kweli tunakubali kabisa kama Serikali kwamba Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni ndogo ukilinganisha na mahitaji yake ambayo ni makubwa sana. Na niongeze tu kwamba si Wizara hii tu, Wizara nyingi ninyi nyote hapa najua mmekuwa mkilisea sana kwa ujumla wake kwamba Bajeti zake zimekuwa hazilingani na mahitaji. Hili linatokana na jambo moja kubwa tu kwamba bado uwezo wetu Kibajeti ni mdogo sana. Lakini, mimi naamini uwezo huo utakapopatikana kwa juhudi ninazoonza tunazifanya kwa pamoja, Bajeti hizi kwa ujumla wake zitaendelea kuongezeka kidogo kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili mahsusi linalohusiana na suala la Ulinzi na Usalama wa Taifa letu. Kwanza, niseme kwamba Serikali inaendelea pamoja na matatizo haya ya fedha, kujitahidi kuimarisha Jeshi la Polisi kwa maana ya ajira zao, kujaribu kuhakikisha wana vitendea kazi ili waweze kumudu majukumu hayo inavyowezekana.

Lakini, nataka nitoe wito kwa Watanzania kwamba suala hili la amani, suala la ulinzi kwa ujumla wake kwa kweli ni jukumu la kila Mtanzania kama mnataka kweli nchi hii iendeleo kuwa ni kisiwa cha amani. Serikali tutajitahidi, lakini kila Mtanzania lazima vile vile ajitahidi sana. (*Makofi*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati ukitoa hotuba yako ya Bajeti hapa Bungeni mwezi wa sita, ulisema uzoefu uliopatikana kwa miaka minane ya utekelezaji wa muundo mpya wa Jiji la Dar es Salaam, unaonyesha kuwa kuna matatizo ya kiuendeshaji na hivyo kutokidhi matarajio yaliyokusudiwa ya kutoa huduma kwa wananchi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Jiji la Dar es Salaam linapaswa kuwa kioo cha nchi yetu. Ikulu iko pale, Ofisi zote za Mabalizi ziko pale, shughuli nyingi za Serikali ziko pale. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa miezi ya hivi karibuni, Jiji la Dar es Salaam limekuwa chafu sana, chafu sana! Barabara ni chafu, mitaro imejaa taka taka na mvua zikinyesha Jiji linakuwa limekuwa kama bahari.

Swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Inashindikana nini kununua magari ya kuzoa taka kwenye Jiji la Dar es Salaam pamoja na matrekta ya kusafisha Jiji la Dar es Salaam kama wanavyofanya wenzetu wa Majiji mengine? Hivi kweli tunangoja watu gani

wakatuonyeshe Jinsi ya kusafisha Jiji letu ambapo vyanzo vya mapato viko vingi na vya kutosha?

**NAIBU SPIKA:** Siyo kumhutubia Waziri Mkuu jamani! (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kimaro, bado Dar es Salaam itaendelea kuwa ndio kioo cha Taifa letu. Sasa, kioo wakati mwingine kinajaa vumbi, inabidi usafishe, kioo kinaweza kikapasuka, itabidi ununue kingine. Kwa hiyo, kwa kweli tunachofanya hivi sasa ndio maana tumelazimika kuunda Timu ya Wataalam chini ya Uenyekiti wa aliyekuwa Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ndugu Mmari.

Kwanza, kutazama muundo wenyewe kama unakidhi mahitaji na matakwa ya Jiji la Dar es salaam. Tume ile inaendelea na kazi yake na tumeomba wananchi wa Dar es Salaam washirikiane na wajumbe wale kujaribu kutoa mawazo yao tuweze kuona muundo unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa pili, Mheshimiwa Kimaro unaweza ukawa na matrekta haya ambayo mimi nakubali kabisa ni muhimu na magari ya takataka ambayo sasa hivi tunajitahidi tumeweka Mawakala wanakusanya takataka.

Lakini, bado utamaduni wetu nao lazima vile vile ubadilike kwa sababu tabia nyingine hizi huwa zinachangia sana katika matatizo ambayo yanaonekana katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa sababu kama mtu unasema mifereji imejaa taka taka, barabara zimejaa taka taka, wakati mwingine ni utamaduni tu, mtu anakula ndizi haoni aibu kutupa popote pale. Mtu anakunywa maji, haoni tatizo kutupa chupa la plastiki popote pale.

Kwa hiyo, wakati tunaendelea na juhudi hizi, naomba vile vile na Watanzania hasa wakazi wa Jiji la Dar es salaam tubadilike katika kutunza usafi. Zipo juhudi nyingi sana zinafanyika pale, tumeweka makasha kwa ajili ya kutupa taka, tuyatumie.

Lakini tuone aibu vile vile mtu kutupa taka kila anapona inafaa. Tukishirikiana kwa njia hii, tunaweza kabisa tukapunguza tatizo la Dar es Salaam. Lakini, nakubaliana nawe kabisa, Serikali inaendeleza juhudi zake kwa nguvu, tuwe na magari ya kutosha na yale makampuni yanayokusanya yaweze kufanya kazi inavyotakiwa.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu ni la kuhusu kilimo. Miaka ya hivi karibuni Serikali ilijaribu kuwashawishi wananchi kupanda zao la mbegu ambalo litatoa mafuta, kwa mfano; alizeti, ufuta. Lakini hivi karibuni nimepata habari kuwa mafuta ya kutoka nje yameteremshwa bei.

Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakulima wetu Watanzania tunawaweka mahala gani?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu mama yangu, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, kama ifuatavyo:- Swali lake ni zuri, lakini linataka maelezo kidogo. Tanzania sasa ina wakazi karibu milioni 36, mahitaji ya mafuta kwa maana ya matumizi yetu kwa chakula nayo ni makubwa.

Kwa hiyo, swali lake kusema kweli anajaribu kuniuliza kama Je, wewe huoni kwamba ndani ya nchi hapa sasa tumeishafikia uwezo wa kuzalisha mafuta kwa ajili ya kuwahudumia Watanzania milioni 36 na kwa maana hiyo kusiwe na umuhimu wowote wa kuingiza mafuta mengine hapa nchini? Na mimi nasema, ndio maana mara ya mwisho nilisema ni vizuri Wizara inayohusika na niliwaomba wafanye hivyo kwamba kaeni na hawa wenye viwanda vya mafuta ambao kwa bahati mbaya si wengi. Niliambiwa Kiwanda cha Morogoro si kizuri sana, kiko katika hali ambayo haitii matumaini sana.

Lakini inawezekana kuna viwanda vingine vidogo vidogo. Kwa hiyo, hatua ile ilikuwa kwanza ni kwa sababu tulikuwa tunajaribu kuwianisha kulingana na taratibu zetu ndani ya Afrika Mashariki. Lakini, tulikuwa vile vile tunaogopa hili kwamba isije watu mkasema mnaweka viwango vya juu kuzuia wakati ninyi ndani hamna uwezo wa kutosheleza mahitaji. Lakini, kwa upande mwingine, uzoefu umeonyesha vile vile kwamba wakati tulipokuwa tumeweka ule ushuru, mafuta yaliingia kutoka nchi jirani kwa wingi sana kuja hapa Tanzania kwa kutumia vichocho na njia ambazo siyo rasmi, kwa nini, kwa sababu hapa mahitaji ni makubwa na wao waliona ndio mahali pa kuweza kupata faida kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mama Maghimbi, kwa hiyo mimi naomba tu niseme kwamba ni jambo kidogo labda Serikali ilianganalie tulitazame, tukiona mwanya huo mzuri upo, hatuoni tatizo la kuzungumza na wenzetu Wakenya na Waganda kurejesha ule utaratibu tuliokuwa tumekubaliana nao.

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali moja. Utakumbuka kiasi cha miaka 20 iliyopita Wabunge wengi walikuwa wakipiga kelele kuhusu ofisi zao za Wabunge.

Lakini katika juhudi ambazo zilikuwa zikiendelea, ambazo ni lazima tuipongeze Ofisi ya Spika, imeorodhesha baadhi ya Ofisi za Wabunge zijengwe na miongoni mwao bahati nzuri Jimbo langu limefaidika na kazi hiyo njema. Lakini, utaratibu uliotumika ambao ningeliomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie Wabunge sote kwa sababu baadhi ya Wilaya ambazo fedha zimepelekwa, baadhi ya Wabunge hatuna taarifa yoyote kwamba fedha zile zipo au la.

Sasa, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu haoni kwamba sisi Wabunge ndio wasimamizi Wakuu wa fedha zile za Bunge ambazo tuliziomba kwa juhudi zote ili zijenge ofisi zetu, lakini matokeo yake fedha zimewekwa katika Wilaya zetu, lakini wenyewe Wabunge hatujapewa taarifa yoyote ile kuhusu fedha hizo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Masoud kama ifuatavyo:- Kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali

Bungeni, lazima niseme kama imetokea hiyo, ni mapungufu makubwa kwa upande wa Serikali. Lakini, tutalisimamia, tutahakisha kwa kweli tunatoa maelekezo ya kusisitiza maana jambo hili kwa kweli linaeleweka, ndivyo tulivyotaka iwe.

Kwa kiasi kikubwa Mbunge ajue kwamba Wilaya yake imepokea fedha kiasi fulani na ujenzi umeanza, unaendeleaje, utaratibu umetumikaje kwa sababu hatimaye ile ofisi ni ya Mbunge. Sasa kama kwa kweli kuna mambo yamejitokeza ambayo siyo mazuri, tutawaagiza tena Wakuu wa Mikoa walisimamie vizuri zaidi na mimi nakuhakikishia Mheshimiwa Masoud hata kwako huko tutahakikisha hili nalo limesimamiwa inavyotakiwa. (*Makofi*)

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 36, fasiri ya 2, Mheshimiwa Rais amepewa madaraka ya kuteua watu mbalimbali wa kushika nafasi za uongozi na utendaji katika Wizara, taasisi na mashirika ya umma hapa nchini.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Taasisi ya Utafiti wa Wanyama Pori (*TAWIRI*) na Shirika la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, hayana watendaji wakuu kwa miaka miwili, mitatu mfululizo licha ya Taasisi hizo kuwa nyeti Kitaifa na Kimataifa. Nafasi hizo kwa kawaida zinajazwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama Katiba inavyoelekeza.

Je, hali hii haiathiri utawala bora na utawala wa sheria ambao huwa tunauhubiri? Naomba ufafanuzi!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Telele swali lake kama ifuatavyo:- Tungekuwa nje, ningesema *message received!* Kwa hiyo, nitalifanyia kazi naelewa. Naelewa kwamba ni kweli anachokisema *TAWIRI* hata pale Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na kumekuwa na juhudi zinaendelea kujaribu kupata mtu ambaye anaweza akafaa kuongoza vyombo hivyo.

Lakini, kama nilivyosema, basi ujumbe umefika Ndugu yangu, tutajitahidi kuhakikisha tunamshauri Rais mapema zaidi kidogo tuweze kumaliza tatizo la muda mrefu. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuanzia mwaka 2006, Serikali imewahamasisha wanawake waanzishe Benki ya Wanawake na sisi Wabunge wengi tumewachangia akina mama waanzishe Benki hiyo, lakini naona huu ni mwaka wa tatu suala hilo linaendelea. Sasa namwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Benki ya Wanawake itakuwepo au haitakuwepo?

**NAIBU SPIKA:** Unadhani umeliwa fedha? (*Kicheko*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Wanawake itakuwepo maana tulishaamua hivyo. Itakuwepo na Baraza la Mawaziri lilisharidhia utoaji wa

kiwango kile cha fedha bilioni 2.1. Lakini juzi nilimsikia Ndugu yangu Mheshimiwa Mkullo akijaribu kutoa ufafanuzi, sina hakika kama alieleweka maana inawezekana pengine mliona kama anachimba mikwara Benki isiwepo.

Lakini mimi nilimwelewa kwa maana alikuwa anajaribu kusema tu kwamba upande wa Serikali, ndani ya Serikali hii tuko tayari wakati wowote tuweze kuhakikisha Benki hiyo inaanzishwa.

Lakini, nikamsikia anasema tatizo ni taratibu zinazotakiwa kufuatwa ambazo ziko chini ya Mamlaka ya Benki Kuu kwamba ni lazima nazo zile taratibu, waanzishaji wa Benki hiyo wahakikishe nazo zimetokelezwa. Sasa mimi napenda kuamini kwamba masharti yale si makubwa au mazito ya kuweza kuwashinda waanzilishi wa hiyo Benki.

Kwa hiyo, nataka tu nijaribu kusema kwamba sidhani kama Mkulo alikuwa na nia ya kusema “shauri yenu, msipofanya hivyo, hatutafanya”. Hapana, na sisi tunalo jukumu vile vile la kuhakikisha Benki Kuu nayo inafanya kazi yake inavyotakiwa ili Benki ianzishwe. Mimi naamini jambo hili litakamilika ndani ya kipindi kifupi kijacho.

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Swali kwa Waziri Mkuu; kwa kuwa Mkoa wa Kigoma, Halmashauri ya Kigoma Vijijini, Maafisa Watendaji wa Kata na Maafisa Watendaji wa Vijiji tangu mwaka 1993 huwa wanahamishwa tu hawalipwi hela za uhamisho mpaka leo. Ni lini Halmashauri hiyo itawalipa pesa zao?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mama Sijapata kanionea hapa kwa kweli.

Lakini, ngoja, nitamwambia Mama Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa afuatilie jambo hilo kwa karibu zaidi kwa sababu mara nyingi kila tunapohamisha watalaam hawa, mara nyingi wanastahili kwenda na posho zao za uhamisho na stahili zingine.

Sasa sina hakika Mkurugenzi wako kwa nini hamjambana huko inavyotakiwa ahakikishe analipa. Lakini Mheshimiwa Kombani atalifuatilia tuone kama tunaweza tukakupa jibu zuri zaidi.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Ahsante sana Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Zanzibar ilipata matatizo ya kukosa umeme na wananchi wa Unguja walikosa umeme karibu miezi miwili na nusu, na kulikuwa na dhana kwamba *TANESCO* inahusika na ukosefu wa umeme ule. Je, Serikali inasema nini kwa hili, na Serikali ya Muungano inasaidia vipi Zanzibar kutokana na maafa hayo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Sereweji, kama ifuatavyo:-



Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tukiri kulikuwa na tatizo hilo kubwa kwa upande wa Zanzibar na Serikali kwa kweli ilitusumbua sana lakini jitihada zilifanywa kubwa za kushirikiana kati ya *TANESCO* na *ZESCO* kutatua tatizo lile ambalo lilikuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kiwango gani sisi tumesaidia ninachoweza kumhakikishia tu Mheshimiwa ni kwamba kazi ile imefanywa kwa pamoja na mashirika yote mawili lakini kuhusisha vilevile Serikali zote mbili katika juhudi ambazo zilizaa tunda ambalo hatimaye lilimaliza mgogoro wa muda mrefu.

Sitaki kuingia kwa undani sana kwamba nani alichanga nini, lakini kwa ujumla nataka tu nikuhakikishie kwamba pande zote mbili zimeshirikiana sana kuhakikisha tatizo lile linakwisha.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika Ahsante, nitamwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu kesho unafunga Maenesho ya Nane Nane hapa Dodoma, na kwa mtazamo ukiangalia MaonYesho yale ni kwa ajili ya wakulima lakini Maonyesho yapo Mjini:-

Je, wakulima wa vijijini wanafaidikaje na Maonyesho ya Nane Nane?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kupanga ni kuchagua, tulidhani uamuzi tulioufanya huo ungeweza ukawakusanya watu wengi kidogo kuweza kufika hapa na kuona shughuli hizo za maonesho zinavyoendelea, na ninasema hili kwa sababu unaposema kwa nini pengine isingepolekwa kwa wakulima na mimi nauliza wapi, kwa sababu pale tulipoweka bado wakulima wa maeneo mbalimbali wamepata fursa ya kuja ingawa najua ungependa pengine tupeleke labda Kongwa au Mpwapwa au sehemu nyingine ambazo zinaonekana ni *more rural* kuliko pengine maeneo ya Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zipo sababu nyingine nyingi tu ambazo zinafanya maamuzi haya yafanyike namna yalivyofanyika, inawezekana ikawa ni *debate* ndefu lakini mimi nadhani kila mahali tumefanya ukienda Arusha, Morogoro, hapa Dodoma penyewe, nenda Makao Makuu karibu ya Mikoa yote iko hivyo, isipokuwa tulichoagiza na ndicho kinachofanyika katika kila Halmashauri na wao wanakuwa na maonesho yao ya Nane Nane katika maeneo yao kulingana na maamuzi yao katika Kata tofauti mwaka hadi mwaka, yale pia yanasaidia kumlenga mkulima kwa karibu zaidi. Haya ya Dodoma kwa sehemu kubwa ni kama sehemu ya kubadilishana mawazo, kujaribu kuona uzoefu ukoje ili tukirudi kule tuweze kufanya kazi zetu ziwe nyepesi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hiyo ndiyo sababu moja kubwa lakini jitihada zilizoingia nafikiri zitasaidia kuoyesha kwamba na huko tupo vilevile tunafanya maonyesho.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, muda wa maswali kwa Waziri Mkuu umekwisha, tunakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba ukae. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana tena nami pia kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli anamudu maswali karibu yote, ni pale tu mtu atakapouliza maswali ya kijijini kwake. Kwa kweli itakuwa vigumu sana kwa Waziri Mkuu. Leo mmejithahidi kuuliza maswali ya Kitaifa, mazuri kabisa na imewezekana, tuendelee kufanya hivyo ili kusudi kipindi kiweze kuboreka zaidi kuliko tulikoanzia.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na sasa tunaendelea na utaratibu wetu wa kawaida wa leo.

### **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya kawaida Waheshimiwa Wabunge kwenye *Order Paper* yenu kumetokea makosa. Swali 360 limeandikwa kwamba ni swali la Mheshimiwa Aziza Ally. Swali hilo siyo la Mheshimiwa Aziza Ally ni swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aziza utauliza swali lako siku nyingine.

Na. 357

### **Tume ya Rais ya Uendelezaji Makao Makuu**

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tume ya Rais ya Uendelezaji Makao Makuu iliyoundwa mwaka 1984 ilipewa majukumu mazito ya kutoa Sera, Miongozo na msukumo wa kuhamishia baadhi ya taasisi muhimu Dodoma ili kuharakisha Maendeleo ya ujenzi wa Makao Makuu:-

- (a) Je, Wajumbe wa Tume hiyo ni akina nani na hukutana mara ngapi kwa mwaka?
- (b) Je, Tume hiyo imekutana mara ngapi tangu iundwe?
- (c) Je, kwa nini Tume hiyo haijatekeleza majukumu yake kikamilifu kama yalivyoainishwa kwenye sheria husika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE, SERA NA URATIBU** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ephraim Nehemia Madeje Mbunge wa Dodoma Mjini, na pia Mkurugenzi wa Bodi ya Ustawishaji ya Makao Makuu Dodoma, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu ina Tume iliyoundwa kwa Tangazo la Serikali la Serikali – *GN. No.230* la 1973 na limekuwa likirekebisha kila mara kulingana na mabadiliko yaliyofanywa katika Serikali.

Tangazo hili limetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na lengo kuu likiwa Uhamishaji Makao Makuu kuja Dodoma toka Dar es Salaam. Tume hii ni chombo juu ya Bodi ya Wakurugenzi ya *CDA*. hutoa maamuzi ya Sera na miongozo ya kusimamia Ustawishaji Makao Makao Makuu Dodoma. Kwa kuzingatia tangazo hilo, Wajumbe wa Tume huteuliwa kuendana na nyazifa zao Serikalini kama ifuatavyo:-

- (i) Mheshimiwa Waziri Mkuu..... Mwenyekiti;
- (ii) Mheshimiwa WN-OWM- Sera, Utaratibu na Bunge..... M/Mwenyekiti;
- (iii) Mheshimiwa WN-OWM-(TAMISEMI) .....Mjumbe;
- (iv) Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu.....Mjumbe;
- (v) Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji....Mjumbe;
- (vi) Mheshimiwa wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi –SMZ.....Mjumbe;
- (vii) Mheshimiwa Waziri wa Nchi Mipango na Uwekezaji-SMZ...Mjumbe; na
- (viii) Mkurugenzi Mkuu *CDA*.....Katibu wa Tume.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imekutana mara kumi na sita (16) tangu kuundwa kwake mwaka 1984.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Tume imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria za Nchi kwa ufasaha na ukamilifu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba matokeo na mafanikio yaliyopatikana hapa Dodoma hadi hivi sasa katika suala zima la kuimarisha na kuboresha Ustawishaji Makao Makuu yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na Tume hiyo na wananchi.

Tume inatoa Sera na miongozo na inasimamia utekelezaji wa programu ya uhamishaji Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja hapa Dodoma. Napenda ifahamike kwamba dhamira ya Serikali iko palepale kinachotukwamisha ni ufinyu wa Bajeti na vipaumbele.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Katika majibu yake amekiri kwamba tangu Tume hii iundwe miaka minne iliyopita imeshakutana mara 16 tu na kwa taarifa za kuaminika nilizonazo kwa sababu mimi ni mjumbe wa bodi ya *CDA* katika miaka mitatu iliyopita Tume hii bado haijakutana, nina swali moja tu la nyongeza nalo ni:-

Je, Tume hii kwa mara ya Mwisho ni lini ilipokutana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE, SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nirejee kusema kwamba Tume kazi yake ni kutoa sera na miongozo kwa Bodi. Kwa hiyo, siyo lazima ikutane mara kwa mara, na mara ya mwisho ilikutana miaka mitatu (3) iliyopita.

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema jukumu la msingi la Tume hii ilikuwa ni kuhamasisha uhamiaji wa Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, na kwa vile wamekutana mara 16 wakitumia fedha za umma, wanaweza kulieleza Bunge hili Tukufu mpaka sasa wameweza kuhamisha Taasisi au Wizara gani kuja Dodoma?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE, SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina orodha kamili ya Taasisi za Serikali ambazo sasa hivi zimeshahamia Dodoma lakini sote tunafahamu kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI yote ipo Dodoma, Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Muungano wa Tanzania liko Dodoma, Makao Makuu ya Jiolojia na sehemu kuu ya Idara ya Madini iko Dodoma. Hata hivyo tuko tayari kutoa orodha ya Taasisi ambazo zimekwishahamia Dodoma.

Na. 358

#### **Utekelezaji wa Azimio la Bunge.**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge, Serikali iliahidi kutekeleza mapendekezo ya Bunge yaliyotolewa na Kamati Teule. Je, hadi swali hili linapojibiwa, utekelezaji wa mapendekezo hayo umefikia hatua gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE, SERA NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Mkutano wa 10 wa Bunge, Serikali iliahidi kutekeleza mapendekezo 23 yaliyopitishwa kwa Azimio la Bunge yaliyotolewa katika Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge Iliyochunguza Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulioipa Ushindi “*Richmond Development Company LLC*” ya Huston, Texas - Marekani Mwaka 2006. Kamati ya Wataalam iliundwa mwezi Februari, 2008 ili kuchambua mapendekezo ya taarifa hiyo na kupendekeza namna ya kuyatekeleza. Kamati ya Wataalam iliwasilisha mapendekezo ya

utekelezaji Serikalini mwezi Machi, 2008. Ni kweli pia kwamba Serikali iliahidi kutoa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo hayo katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge. Mapendekezo ya Kamati Teule ya Bunge yametokelezwa katika hatua na viwango mbalimbali na taarifa kamili inaweza kuwasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mkutano huu wa Bunge iwapo muda na ratiba ya Mkutano huu utaruhusu. Hivyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie hadi hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapowasilisha taarifa hiyo.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa majibu aliyotoa Mheshimiwa Waziri ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anatarajiwa kutoa maelezo kamili ya utekelezaji wa suala hili katika Mkutano huu. Lakini kwa mujibu wa ratiba tuliyokabidhiwa na Bunge haionyeshi siku au muda wowote ambapo taarifa hii itatolewa. Je, Serikali inasemaje katika hili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, BUNGE, SERA NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipangi ratiba ya Bunge hili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, hayo ndiyo majibu mazuri namna hiyo. (*Kicheko*)

Na. 359

### **Ikama ya Watumishi wa Kituo cha Afya Bonga**

**MHE. MICHAEL L. LAIZER (K.n.y. MHE. OMAR S. KWAANGW')** aliuliza:-

Kwa kuwa, kituo cha Afya cha Bonga ni kituo pekee kinachomilikiwa na Serikali kwenye Halmashauri ya Mji wa Babati; na kwa kuwa, kituo hicho kwa sasa kimekarabatiwa ili kiweze kutoa huduma bora zaidi:-

- (a) Je, ni nini ikama ya Watumishi wa kituo hicho na vifaa vinavyotakiwa?
- (b) Je, hadi sasa kituo hicho kina uwezo wa kutoa huduma kwa kiwango gani kulingana na idai ya watumishi na vifaa vilivyopo?
- (c) Je, kituo kina upungufu wa Watumishi wa kada zipi, upungufu wa vifaa vipi muhimu sana na nini sasa mipango ya haraka na ya muda mfupi ya kuondoa upungufu huo ili kupunguza rufaa zinazopelekwa hospitali ya Wilaya ya Manyara ambayo tayari imezidiwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Shaban Kwaangw', Mbunge wa Babati Mjini lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwongozo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kituo cha Bonga kinapaswa kuwa na watumishi 29 watumishi hao ni Madaktari Wasaidizi (AMO) 2, Maafisa Tabibu 3, Wauguzi 11, *Dental Therapist* 1, *Pharmacy Assistant* 1, Wahudumu wa Afya 4, *Laboratory Assistance* 1, Afisa Afya 1, Mhasibu 1, Mtunza Kumbukumbu 1, Walinzi 2 na dereva 1. Kituo cha Afya pia kinapaswa kuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wa kulaza (IPD), wagonjwa wa nje (OPD), huduma za Mama na Mtoto, huduma za maabara na upasuaji mdogo (*minor surgery*).

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kituo cha afya cha Bonga kina watumishi saba ambao ni Mafisa Tabibu (2), Wauguzi (3) na wahudumu wa afya wawili (2). Kulingana na idadi hii kituo cha afya cha Bonga kinakabiliwa na upungufu wa watumishi wa afya wapatao 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha afya cha Bonga kina jengo kwa ajili ya kutoa huduma za nje (OPD). Jengo hili linatumika kutolea huduma za tiba na maabara. Pia kituo hiki kina jengo kwa ajili ya kutolea huduma za mama na mtoto ambapo huduma hizi hutolewa kila siku.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika sehemu (b), kutokana na upungufu wa watumishi unaokikabili kituo hiki huduma za wagonjwa wa ndani zimekuwa hazitolewi kama inavyopaswa kwa sasa ni wale wagonjwa wanaohitaji kupumzishwa kwa muda mfupi tu ndiyo wanaolazwa katika jengo hili la IPD. Tatizo la upungufu wa watumishi sio tu kwa kituo cha afya cha Bonga bali hili ni tatizo ambalo linavikabili vituo vingi katika Halmashauri zetu.

Ndiyo maana Serikali kwa mwaka 2005/2006 iliamua kulegeza masharti ya ajira kwa watumishi wa afya kwa kuanzia utaratibu wa kuwapanga wataalamu wa kada za afya wanaotoka vyuoni moja kwa moja bila kufanya usaili. Serikali pia inafikiria kufufua vyuo vya kada mbalimbali za afya ambavyo awali vilifungwa na pia inafikiria kurejesha kada za afya zilizokuwa zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya mji wa Babati imeomba kibali cha kuajiri wataalamu wa afya wapya 12. Pia Halmashauri imeagiza vifaa muhimu kutoka Bohari kuendelea kukitengea Bajeti kituo cha Afya cha Bonga ili kuweza kukiimarisha pia kutumia vema fursa mbalimbali kama mfuko wa pamoja wa afya. (*Makofi*)

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza?

(a) Kwa kuwa, kituo cha Afya cha Bonga kiko Mjini na *population* ya watu pale ni wengi. Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu kuwapeleka watumishi pale ili wananchi wapate huduma kuliko kuhangaika kwenda maeneo mengine?

(b) Kwa kuwa, Serikali imeahidi katika kampeni ya mwaka 2005 kwamba itajenga zahanati kwa kila kijiji na vituo vya afya kwa kila Kata. Je, ni lini Serikali itanza kujenga majengo hayo katika maeneo yaliyotajwa ili wananchi wapate huduma kwa karibu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu mkubwa sana wa kupeleka watumishi katika kituo cha Afya cha Bonga tatizo kama tulivyosema na kama Wizara ya Afya ilivyosema katika Bajeti yake kwamba kuna upungufu mkubwa katika sehemu mbalimbali. Watumishi hao pindi wakipatikana, tutawapeleka katika kituo hiki ambacho kina upungufu mkubwa pamoja na vituo vingine Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pili ni kweli katika ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 imesema wazi kwamba tutajenga vituo vya afya katika kila Kata na zahanati katika kila kijiji. Kwa sasa Serikali kama mlivyoona kwa mwaka huu katika Bajeti ya Serikali zimetengwa shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuanza kujenga majengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi zitakapopatikana zitapelekwa sehemu mbalimbali kulingana na vituo vya afya na zahanati zilizoko katika sehemu hizo na fedha hizi niseme tu kwamba hazitotosheleza kwa kiasi kikubwa kwa sehemu zote bali tutapeleka katika mikoa mbalimbali. Mikoa nayo itaangalia ni sehemu gani waanze kujenga hivyo vituo vya afya pamoja na zahanati.

Na. 360

### **Uhaba wa Watumishi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo**

**MHE. VITA R. KAWAWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ni miongoni mwa Halmashauri mpya zilizoanzishwa hivi karibuni, hivyo ina uhaba mkubwa wa Watumishi:-

Je, ni kwa nini Serikali haikutoa kibali cha kuajiri watumishi wa sekta ya kilimo na mifugo wakati Halmashauri iliidhinishiwa ajira hizo wakati wa majadiliano ya Bajeti ya mishahara ya watumishi kwenye Menejiment ya Utumishi wa Umma.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENT YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makisio ya Ikama na Bajeti ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, kwa mwaka 2007/2008

Halmashauri hiyo iliidhinishiwa jumla ya nafasi tisa za ajira mpya ya kada ya Kilimo na Mifugo. Kati ya nafasi hizo, nafasi tano ni za Maafisa Kilimo Wasaidizi na nne ni za Maafisa Mifugo Wasaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kuidhinishwa kwa Ikama hiyo, Ofisi yangu imekwishawasiliana na makatibu Wakuu wa Ofisi za Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika, pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, ili kuwapangia vituo vya kazi wahitimu wa fani za kilimo na mifugo mara tu wanapomaliza masomo yao katika vyuo vya fani zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa wataalam husika katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Ofisi yangu imetumia utaratibu huu ili Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika wawapangie kazi wahitimu wa fani za kilimo na Mifugo Wilayani Namtumbo mara wanapo maliza masomo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu ndiyo unaotumika kukabiliana na upungufu wa wataalam hao katika soko la ajira kwa kada zenye wahitimu wachache wasiotosheleza mahitaji.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake na ufafanuzi wake huo. Pia naomba niishukuru Serikali mwaka jana ilitupangia Wauguzi 12 na Wahudumu 6 lakini matatizo tunayopata ni kutoripoti kwa watumishi hao. Walioripoti mwaka jana ni Muuguzi mmoja (1) tu na Mhudumu mmoja (1) wa Afya.

(a) Kwa kuwa, katika Bajeti ya 2007/2008 pia tulipitishiwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Tabibu Daraja la Pili (22) na Fundi Sanifu Daraja la Pili (1) lakini hawakuja kuripoti. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutusaidia upatikanaji wa Watumishi wa Kada hiyo au kuturuhusu kutangaza sisi wenyewe katika Halmashauri yetu?

(b) Kwa kuwa, katika Wilaya yetu ya Namtumbo hatuna Katibu wa Afya ambaye ni kiungo muhimu katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za afya Wilayani. Je, Serikali sasa inaweza kutupatia Katibu wa Afya katika Wilaya yetu ya Namtumbo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matatizo ya kutokuripoti kwa Watumishi na ombi lao la kuomba kutangaza wenyewe ili watumishi waweze kufika kule; Kimsingi suala la kuajiri Watumishi kwa Halmashauri ya Namtumbo ni wajibu wa Halmashauri ya Namtumbo. Lakini kutokana na uchache wa Watumishi hao ndiyo maana tuliwaruhusu Wizara ya Afya iajiri kwa niaba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wanaweza kuwashawishi Watumishi wanaowafahamu, ambao wanaweza kufanya kazi katika Halmashauri ya Namtumbo ili kuondoa upungufu mkubwa wa watumishi wanaokabiliwa nao. Kwa kweli Ofisi yangu haina matatizo yoyote na ipo mifano ya namna hiyo. Ninapenda kuchukua



nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Shibiliti Mbunge wa Misungwi ambaye yeye mwenyewe aliamua kutumia ubunifu wake na kuwashawishi watumishi kwenda kuripoti katika Halmashauri yake na alipotuletea majina Ofisi yangu haikuwa na pingamizi cho chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wana-Namtumbo kama wanawapata watumishi tunawaruhusu kutangaza lakini wawasiliane na Ofisi nilizozitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukosekana kwa Katibu wa Afya katika Halmashauri yao kama yupo katika Ikama ya mwaka 2008/2009 basi tutashauriana na tutaomba Wizara ya Afya iwapangie Katibu wa Afya katika Halmashauri hiyo. Kwani itasaidia Waganga waliopo kufanya kazi zao za taaluma badala ya kufanya kazi za utawala. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona, kwa kuwa Halmashauri hii ya Namtumbo imetokana na Halmashauri Mama Halmashauri ya Wilaya ya Songea, ambapo wakati Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo inapoanza tuligawana hao Watumishi na hivyo bado Halmashauri ya Wilaya ya Songea ina shida sana ya Ikama ya Watumishi wa kufanya kazi katika Halmashauri hiyo.

Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari nimletee matatizo makubwa yanayoikabili Halmashauri ya Wilaya ya Songea ya Ikama ya Watumishi ambayo wengine wameshapata vibali na hawajafika, na wengine ambao hatujapatiwa bado vibali vya kuwaajiri ili aweze kutusaidia kuondokana na tatizo hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENT YA WATUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba alete matatizo yake.

Na. 361

### **Biashara ya Chuma Chakavu**

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa biashara ya vyuma chakavu inachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu baadhi ya miundombinu nchini, kama vile vyuma vya madaraja, reli, mifuniko ya chemba za mifereji ya maji machache hasa barabarani na kadhalika na kuhatarisha maisha ya wananchi na hasara kubwa kwa Serikali:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa kiasi gani biashara hiyo imeathiri miundombinu nchini hadi sasa na imechukua hatua gani kudhibiti hali hiyo?

(b) Je, ni kampuni zipi zinazofanya biashara hiyo na Serikali imenufaika vipi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, Mbunge wa Liwale lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa biashara ya vyuma chakavu imeanza kuonekana kuwa ni tatizo kwa kuchangia katika uharibifu wa miundombinu nchini na hata kuhatarisha maisha ya wananchi. Baadhi ya taasisi ambazo zimekumbwa na uharibifu na hujuma za miundombinu na makadirio ya hasara walizozipata ni pamoja na *TANESCO* shilingi bilioni 8.90, *TTCL* shilingi bilioni 13, *DAWASCO* shilingi milioni 486, Shirika la Reli Tanzania (*TRL*) shilingi milioni 278, *TAZARA* shilingi milioni 812.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara hizi hazijumuishi athari wanazozipata watumiaji wa huduma zinazotolewa na taasisi hizi. Hivyo makadirio ya hasara yanaweza kuwa ni makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na hujuma hizi, Serikali na taasisi mbalimbali zimechukua hatua zifuatazo:-

(i) Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, alikutana na wadau wote wa chuma chakavu kujadili hasara na athari zote zinazotokana na uharibifu wa miundombinu.

(ii) Kuunda Kamati za Ulinzi zikishirikisha wananchi na vyombo vya dola.

(iii) Kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari kuhusu athari ya hujuma hizo ili washiriki kikamilifu katika kudhibiti tatizo hilo.

(iv) Wizara ya Viwanda, Biashara na masoko imeanda waraka wa Baraza la Mawaziri unaopendekeza kutungwa kwa sheria ya kusimamia biashara ya chuma chakavu ili kuwa na ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaofanya biashara za chuma chakavu ni pamoja na:

(i) Kampuni zinazohusika na uzalishaji wa chuma chakavu chenye kama vile, *TAZARA*, Shirika la Reli Tanzania, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na *TANESCO*;

(ii) Gereji mbalimbali;

(iii) Wakusanyaji wa chuma chakavu ambao wanajumuisha mtu mmoja mmoja na kampuni zilizosajiliwa;

(iv) Wafanyabiashara wanaouza chuma chakavu nje na ndani ya nchi; na

(v) Viwanda vinavyozalisha bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya chuma chakavu inainufaisha Serikali kwa namna mbalimbali ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mazingira, upatikanaji wa ajira na kodi kwa Serikali kutokana na uzalishaji viwandani na mauzo nje ya nchi. Mauzo ya chuma chakavu nje ya nchi yalikuwa Sh. 16,848,508,602/= katika kipindi cha mwaka 2007 hadi Aprili, 2008.

Aidha, upatikanaji wa malighafi, viwanda vya kuyeyusha vyuma, kutengeneza bidhaa mbalimbali za ujenzi na matumizi mengine, uliwezesha viwanda hivyo kuzalisha na kuuza bidhaa za chuma zenye thamani ya Sh. 46,228,500,000/= mwaka 2007 katika soko la ndani na kuajiri wafanyakazi 1,054. Vile vile, viwanda hivyo viliuza bidhaa za chuma nje ya nchi zenye thamani ya Sh. 7,411,200,000/= na kulipa kodi mbalimbali kiasi cha Sh. 7,324,500,000/= mwaka 2007.

**MHE. HASSAN CHANDE KIGWALILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekiri: Je, haioni sababu ya kuleta Muswada huo haraka iwezekanavyo ili kuepusha hizi athari ambazo zinaendelea kutokea?

La pili, kwa kuwa baadhi ya Mikoa pamoja na Mkoa wangu wa Lindi tunaathirika sana, nimeshapiga marufuku uuzaji wa chuma chakavu: Je, Serikali inasema nini na Mikoa mingine inaruhusiwa kufanya hivyo pia? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara inajitahidi kuharakisha Muswada huo ufike hapa Bungeni. Mara tu baada ya kupata kibali cha Baraza la Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wangu ataleta hapa Bungeni.

Pili, niseme kwamba kwa ile Mikoa ambayo imepiga marufuku uuzaji wa chuma chakavu katika Mikoa ile, nafikiri Mikoa hiyo imetumia sheria ambayo inaruhusu mamlaka za Mikoa kufanya hivyo na endapo Mkoa wake Mheshimiwa Mbunge, ataona kwamba ni muhimu kufanya hivyo, Wizara yangu haitakuwa na kipingamizi ilimradi Mkoa huo ushirikishe wadau wote wa chuma chakavu katika eneo hilo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mwongozo wa Spika, kanuni ya 68 (7).

**NAIBU SPIKA:** Kanuni nyingine ipi kwa sababu hiyo inakwambia tu kuhusu utaratibu?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kanuni ya 68 (7) tu naomba mwongozo wako tu mama.

**NAIBU SPIKA:** Soma tu hiyo inasemaje?

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Kanuni ya 7 inasema hivi: “Hali kadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo au baadaye kadri atakavyoona inafaa.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo. Endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Said Ali alisema kwamba Serikali haipangi ratiba. Lakini naomba mwongozo wako kwamba Spika siye anayejibu maswali ya Bunge, Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo Bunge ndiko liliko kwa maana ya utawala ndipo anapojibiwa maswali yake: Je, ni kwa nini Waziri alikwepa kujibu swali ambalo linahusu Bunge na yeye ndiyo mwakilishi wa Serikali katika Kamati ya Uongozi ya Bunge? Naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kama nilielewa sawa sawa, alichosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu haipangi *Order Paper* zetu, wala ratiba ya Bunge. Hata wewe mwenyewe Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed unafahamu kwamba Kamati ya Uongozi ndiyo inapanga ratiba za Bunge. Nadhani ndiyo swali hapa. Kama swali lake halijajibiwa hilo ni swali lingine kabisa. Anaweza kabisa kwa kutumia kifungu cha 45 na kifungu cha 46 kuweza kumhoji Mheshimiwa Waziri tena. Lakini anayepanga ratiba za Bunge ni Kamati ya Uongozi. Nadhani hilo ni *clear*. Kwa hiyo, kama swali halikujibiwa atumie kifungu cha 45 na kifungu cha 46. (*Makofi*)

Mheshimiwa Malecela nilikuona kuhusu utaratibu au ilikuwa nini? *Okay*. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengi leo, lakini nitawaita tu kwa makundi. Kwanza kabisa kuna wageni wa Mheshimiwa Mwapachu, hawa ni Waheshimiwa Madiwani wa Tanga Mjini na Watendaji wa Manispaa ya Mji wa Tanga na msafara huo unaongozwa na Mstahiki Naibu Meya - Mheshimiwa Yusuf Mwambamvua. Naomba asimame Mstahiki Meya kama yupo na Waheshimiwa Madiwani wote na Watendaji wasimame walipo. Karibuni sana. Ni vizuri Waheshimiwa Madiwani mkakutana na Waheshimiwa Wabunge mkaona wanavyofanya kazi zao. (*Makofi*)

Wageni wengine ni Mheshimiwa John Chiligati. Hawa ni wafanyakazi Ofisi ya Makao Makuu ya CCM wakiongozwa na Ndugu Paul Ndui. Naomba asimame na

wengine wote waliokuja wasimame walipo maana yake ni wengi *page* mbili hapa. Karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu nina wageni wa Mheshimiwa Dunstan Mkapa. Hawa ni Waheshimiwa Madiwani wa kutoka Wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Ndugu Dua Mkurua. Ndugu Mkurua na Madiwani wengine wasimame walipo. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Telele kutoka mamlaka ya hifadhi ya Ngorongoro wakiongozwa na ndugu Veronika Ufunguo, Ndugu Veronika Ufunguo na wale wengine wote wasimame. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna wageni 20 wa Mheshimiwa Ezekiel Chibulunje kutoka kikundi cha umoja wa akina mama Farahani wakiongozwa na Ndugu Mdala Sala Lusinde, ndiyo mlezi. Huyu Mdala Lusinde yuko wapi na wamama wengine wote wasimame. Ahsanteni sana karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Damas Nakei ni Mchungaji, Ezekiel Dankalo wa Kanisa la TAG Magugu na ndugu Nyange Salehe Mwenyekiti wa CCM Magugu naomba wasimame hawa walipo. Ahsante sana, karibu sana.

Kuna wanachuo 40 wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu Mzumbe. Karibuni sana. Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Mariam Mfaki, yuko Mzee Musa Mfaki mume wake, karibu sana Mzee Mfaki. Yuko Bwana Nuru Juma Makota, mjukuu wake; kwa hiyo babu na mjukuu wamekuja. Karibuni sana.

Tuna wageni sita wa Mheshimiwa Dr. Haji M. Haji wao ni wakulima wa Jimbo la Muyuni, wako wapi wakulima wetu? Karibuni sana. Nadhani mmekuja kwa ajili ya Nane Nane. Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Kisasa na walimu wao wasimame walipo, karibuni sana wanafunzi. Bunge liko kwenu kwa hiyo, mnakaribishwa wakati wowote ule. Kuna uwezekano wa kuwa wengine wamesahauliwa hapa.

Matangazo ya kazi. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, naomba Waheshimiwa Wabunge punguzeni kiongea kwa sauti, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwamba kesho tarehe 8 saa Tatu Asubuhi kutakuwa na kikao Ukumbi Na.231 ghorofa ya pili jengo la Utawala.

Matangazo mengine ni kama barua. Kuna Mheshimiwa John Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa 7.00 kutakuwa na kikao katika Ukumbi Na.231 saa 7.00 mchana hii ni Kamati ya PAC.

Halafu Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi, hii Kamati inajulikana kwa Mheshimiwa Shah siyo Kamati ya Kibunge. Yeye anaomba niwatangazie, anasema Mwenyekiti wa Kamati Ndogo ya Mifugo ya Maendeleo ya Uvuvi anapenda kuwatangazia Wabunge wote ambao Majimbo yao yana wananchi

ambao wanajishughulisha na shughuli za uvuvi kukutana leo tarehe 7 Agosti, 2008 chumba Na. 227 jengo la Utawala saa nne na nusu.

Waheshimiwa Wabunge wanaombwa wajitokeze kuja kujadili masuala mbalimbali yanayohusu wananchi wetu wanaofanya shughuli za uvuvi. Kwa hiyo, ni wale wanaofanya shughuli za uvuvi Wabunge wote mnatakiwa kukutana chumba Na. 227 hii siyo Kamati ya Kudumu. Kwa hiyo, ni kikundi.

Halafu kwa niaba ya Kaimu Katibu wa Bunge, Bwana Mrema anatangaza kwamba Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Jumamosi tarehe 9 kutakuwa na semina kwa Waheshimiwa Wabunge wote itakayoanza saa Tatu Asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo inahusu kazi za *African Peer Review Mechanism* waandaji wa semina hiyo ni Taasisi ya *African Peer Review Mechanism*.

Waheshimiwa Wabunge, hili zoezi ni la muhimu sana kwa sababu ni kila nchi iliyokubali kuweza kujifanyia tathmini yenyewe inakuwa na utaratibu huo.

Kwa hiyo, ni jambo kubwa sana na linahusu mambo ya demokrasia, mambo ya haki za binadamu jinsi nchi hii inavyotawaliwa. Kwa hiyo, maoni yenu ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa maeneo mbalimbali kuhusu wageni itakuwa ni manufaa sana. Inafanyika nchi nyingi na siyo zoezi la kulidharau, ni zoezi muhimu sana. Naomba mhudhurie tarehe 9 saa Tatu Asubuhi. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anaomba kueleza kwamba siku ya tarehe 11 mpaka 13 hii ni Jumatatu mpaka 13, kutakuweco na maonyesho ya kuhusu mambo ya sheria kwenye viwanja vyetu vya maonyesho pale Bungeni. Anawakaribisha wote mfike, kuna mambo mengi mtajifunza huko. (*Makofi*)

Halafu Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati za Bunge zifuatazo kwamba kutakuwa na vikao vya kamati kwa siku mbili, Jumamosi tarehe 9 na Jumapili tarehe 10.

Kamati hizo ni za Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, Kamati ya Huduma za Jamii na Wajumbe wote wa Chama cha Wabunge wanawake *TWPG* kwamba Jumamosi tarehe 9 kikao kitaanza saa 7.00 mchana mara baada ya semina ya Wabunge wote na Jumapili tarehe 10 Kikao kitaanza saa 5.00 asubuhi. Vikao hivyo viwili vimeandaliwa na *TGNP* na vitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Kwa hiyo, ni tarehe 9 na 10 saa 7.00 tarehe 9 na saa 10.00 siku ya Jumapili. Jana jioni Mwenyekiti alitangaza kuhusu matangazo hayo ninayotangaza sasa na narudia tena kwamba Naibu Waziri Mheshimiwa Bendera anatangaza kwamba kesho tarehe 8 timu zetu za Bunge *Football* na *netball* watacheza na shirika la *PPF* uwanja wa Jamhuri saa 10.00.

Halafu tarehe 9 Agosti, 2008 Jumamosi timu zetu zitacheza na *NMB combine* saa 9.00 mchana Uwanja wa Jamhuri. Sasa Ijumaa na Jumamosi usiku saa 1.30 mpaka saa 6.00 usiku kuna *Dinner Dances*. Sasa Wabunge wote wanaalikwa na watatumbuizwa na Bendi za *TOT respectively*. Sijui wapi hakusema, nadhani katika Ukumbi maarufu hapo chini. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba tuendelee na shughuli kama kawaida.

## **KAULI ZA MAWAZIRI**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa fursa hii kuweza kutoa kauli ya Serikali kuhusu Ubinafsishaji wa Kiwanda cha *Southern Paper Mills Limited* au *SPM Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii imetokana na mchango wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa - Mbunge wa Karatu aliyeitoa wakati akichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

## **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu, kumetokea nini? Nani amesema kuhusu utaratibu!

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mimi hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Mwongozo wako. Kanuni ya 68.

**NAIBU SPIKA:** Ndiyo Mwongozo kuhusu nini?

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Kanuni ya 49 fasili ya 3.

**NAIBU SPIKA:** Soma Kanuni hiyo.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Kuhusu Kauli za Mawaziri.

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, fasili ya 33 inasema: “Waziri mwenye kutoa kauli atawajibika kutoa nakala ya kauli yake kwa Wabunge wote wakati anapoiwasilisha Bungeni.”

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ni rafiki yetu, umruhusu aendelee kutoa kauli hii, lakini Mawaziri baadaye wawe wanatoa nakala kwetu wanapotoa kauli. Naomba Mwongozo wako. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri endelee kutoa kauli, karatasi zitagawiwa. Si ndiyo hivyo! Kanuni hiyo inasema kwamba atatoa hiyo kauli lakini atazisambaza hizo nakala. Kwa hiyo, naomba aendelee. Nategemea hizo nakala zitasambazwa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge kunikumbusha wajibu wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kukupa shukrani kunipa fursa hii kuweza kutoa kauli ya Serikali kuhusu Ubinafsishaji wa Kiwanda cha *Southern Paper Mills Limited (SPM)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hii imetokana na mchango wa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa - Mbunge wa Karatu aliyotoa wakati akichangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu akitaka Serikali itoe tamko Bungeni kueleza *Angel Hurst Industries* ni nani na kwa nini hawapo popote katika Mkataba wa kuuza *SPM Limited*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha kutengeneza karatasi cha *Southern Paper Mills* kilianzishwa na Serikali mwaka 1985 na uzalishaji ulianza mwaka 1986. Uwezo wa uzalishaji uliowekezwa au kwa lugha ya Kiingereza *installed capacity* ulikuwa ni tani 60,000 kwa mwaka ukiwepo uwezekano wa kupanua uwezo huo hadi tani 75,000 kwa mwaka. Uzalishaji huo ulikuwa unafanyika kwa kutumia mashine mbili zenye uwezo wa kuzalisha tani 30,000 kwa mwaka kila mmoja. Malighafi kuu ya kiwanda hicho ni magogo kutoka msitu wa kupanda wa *Sao Hill*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufanisi wa Kiwanda, tangu *SPM* ianze uzalishaji mwaka 1986 kiwango cha juu ya uzalishaji kilikuwa asilimia 53 ya uwezo uliowekezwa ambacho kilifikiwa mwaka 1989. Hata hivyo, ufanisi ulishuka na kufikia wastani wa tani 10,000 kwa mwaka kati ya mwaka 1991 na 1995 tani 5,189, mwaka 1996 na tani 1,800 mwaka 1997 sawa na 3% tu. Ilipofika mwaka 1998 uzalishaji ulisimama kabisa. Ufanisi duni ulisababisha kiwanda kuzalisha kwa hasara muda wote wa uhai wake ambapo mwaka 1994 hasara ilikuwa shilingi bilioni 3. 81, mwaka 1995 shilingi bilioni 4.21 na shilingi bilioni 6.32 mwaka 1996.

Kiwanda kilianza kikiwa na wafanyakazi 1,800, kutokana na kushuka kwa ufanisi na uzalishaji wa kiwanda wafanyakazi walipunguzwa kidogo kidogo na kufikia 1,296 mwaka 1996 na mwaka 1998 walipunguzwa zaidi na kubakia wafanyakazi 786. Wafanyakazi hao 786 walibakizwa kiwandani ili kutunza mali na kuzungusha mitambo



na hivyo kupunguza kasi ya kuharibika kwa mitambo ya kiwanda na hasa matanki ili kuepusha kuvunja kwa madawa yaliyokuwa yamehifadhiwa kwenye matanki na ambayo yangeweza kuharibu mazingira na kuhatarisha maisha ya watu.

Gharama za kutunza na kuzungusha mitambo ili kuepusha madawa kwenye matanki kuganda wakati hakuna uzalishaji zilikuwa shilingi milioni 127 kwa mwezi bila kujumuisha makato mbalimbali. Pamoja na gharama hizo za kila mwezi, ili kuongeza uhai wa mitambo, uzalishaji ulikuwa unahitajika ufanyike kila baada ya muda ili kuzungusha mitambo yote ya kiwanda au *preventive runs*. Mwaka 2001 uzalishaji huo ulifanyika na kugharimu Serikali zaidi ya shilingi bilioni 1.8. Mwaka 2002/2003 Menejimenti ya *SPM* ilipendekeza uzalishaji wa kuhifadhi mitambo ufanyike tena ambapo Serikali iliharimia *dollar* za Kimarekani milioni 2.8.

Wakati gharama za kutunza kiwanda zilikuwa mzigo mzito kwa Serikali, Serikali iliendelea kukabiliana na jukumu la kukinga athari ya uchafuzi wa mazingira na kuhakikisha usalama wa watu wanaoishi karibu na kiwanda kutokana na uwezekano wa kuvunja kwa matanki yaliyokuwa yanahifadhi madawa, kutishia usalama wa watu na mfumo wa ikolojia katika Bonde la Mto Rufiji ambako madawa hayo yangetiririka endapo uvunjaji ungetokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya *SPM*, ufanisi duni wa kiwanda ulitokana na matatizo mbalimbali baadhi ikiwa ni gharama na mahitaji makubwa ya nishati ambapo kiwanda kilihitaji umeme wa wastani wa Megawati 18.5, mahitaji makubwa ya mtaji wa uendeshaji na mahitaji makubwa ya uwekezaji. Wakati kiwanda kinazalisha karatasi gharama ya umeme pekee ilikuwa shilingi milioni 350 kwa mwezi.

Matatizo mengine ni kiwanda kuzalisha aina nyingi za karatasi, uzalishaji kutofikia kiwango cha faida zinazopatikana kutokana na uzalishaji mkubwa au kwa lugha ya Kiingereza, *economies of scale*, kutokana na uwezo mdogo uliowekezwa, gharama kubwa ya kusafirisha madawa kutoka Bandarini Dar es Salaam hadi Kiwandani na kusafirisha karatasi kutoka Kiwandani hadi Bandarini.

Mahitaji ya uwekezaji yalibainishwa na michanganuo iliandaliwa wakati wa kutafuta mwekezaji ilionyesha kwamba zingehitajika *dollar* za Kimarekani milioni 29, kati ya fedha hizo *dollar* za Marekani milioni 23 zingekuwa ni kwa ajili ya kufufua na kupanua kiwanda hadi tani 75,000 kwa mwaka na *dollar* za Kimerikani milioni sita zikiwa ni gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ubinafsishaji ulilenga katika kupata mwekezaji mwenye uwezo wa kufufua kiwanda, kuwekeza siyo chini ya *dollar* za Kimerikani milioni 23, kuzalisha umeme na hivyo kupunguza utegemezi kwa *TANESCO* kwa vile bei ya umeme ya *TANESCO* ilikuwa kubwa ya senti za kimarekani 13 kwa *kilowatt*. Kuiondolea Serikali gharama za uendeshaji na kuondokana na tishio la usalama wa watu na uchafuzi wa mazingira. Kwa maana hiyo, mpango wa biashara (*business plan*) wa kila mwekezaji ulitakiwa uonyeshe wazi jinsi ya kukabiliana na changamoto hizo hususan mahitaji makubwa ya umeme na ya mtaji wa kufufua kiwanda na uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa ubinafsishaji. Mchakato wa kutafuta mwekezaji ulianza mwaka 1992 na kuendelea kwa miaka 12 hadi mwaka 2004 mwekezaji alipatikana. Jitihada hizo zilianza kufanywa na taasisi shirikishi ya Benki ya Dunia inayoitwa *International Finance Corporation* au *IFC* ambayo ilijitoa mwaka 1994 baada ya kuona hakuna mafanikio.

Shirika la Taifa la Maendeleo na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma. Katika kipindi hicho cha miaka 12 zaidi ya wawekezaji 30 walijitokeza na kuonyesha nia ya kuwekeza *SPM*, lakini wawekezaji hao aidha, walishindwa kuthibitisha jinsi ya kutatua matatizo ya *SPM* yaliyoelezwa katika aya ya 1.2 hapo juu na kufafanuliwa katika aya hii ya tatu.

Baadhi ya wawekezaji waliweka masharti magumu kwa Serikali. Baadhi ya masharti hayo ni pamoja na Serikali kutoa ruzuku kwenye bei ya umeme ambao ungetumiwa na kiwanda. Mfano mmoja, mmoja wa wawekezaji alitaka bei ya umeme iwe senti ya Kimarakeni 4 kwa kila kilowatt, wakati huo bei ya umeme ilikuwa senti za Kimarekani 13 kwa kila *watt*. Masharti mengine ni kukubali kwanza kupewa kiwanda ndipo wathibitishie mapendekezo yao.

Kupewa ripoti ya kiuhandisi ya uwezo wa kiwanda ya kuthibitisha kuwa mitambo ilikuwa katika hali nzuri ya kuzalisha kwa vile kiwanda kilikuwa kimekatiwa umeme. Wawekezaji waliojitokeza tangu mchakato wa ubinafsishaji ulipoanza hadi kiwanda kilipobinafsishwa ni kama ilivyoonyeshwa katika kiambatisho.

Aidha, ingawa jukumu la kupata mtaji ni la mwekezaji, Serikali ilikuwa na jukumu la kujenga mazingira bora na uwezeshi ya kufufua kiwanda cha *SPM* ikiwa ni pamoja kuangalia uwezekano wa kupunguza mahitaji ya mitaji kwa kupunguza kiasi cha fedha za kununua mali au hisa za *SPM* ili kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia juhudi za muda mrefu zilizofanyika za kutafuta wawekezaji bila mafanikio mwaka 1998 ulipendekezwa mkakati wa ubinafsishaji wa kutumia utaratibu wa kupunguza thamani (*dilution*) ya hisa za Serikali au kuahirisha malipo ya sehemu kubwa ya bei ya mali au hisa *deferred payment* ili yafanyike baadaye kupitia kodi itakayolipwa na kiwanda kutokana na uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati huo ungesaidia pia sekta nyingine mfano sekta ya usafirishaji, malipo ya kodi na utoaji wa ajira. Hivyo, Serikali ilishauriwa kupunguza bei ya mali au hisa za *SPM* ili kuwezesha ubinafsishaji wa *SPM* na uwendeshaji wake kibiashara.

Kiwanda cha *SPM* kilibinasishwa kwa kampuni ya *Rai Group Limited* ya Kenya na kukabidhiwa kwa mwekezaji huyo mwezi Februari, 2004. Hatua hii ilikuwa ni ya manufanikio makubwa kwa Serikali. Vigezo vilivyoivezesha kampuni ya *Rai Group* kupata kiwanda cha *SPM* ni pamoja na yafuatayo:-

Kwanza, mpango wa biashara wa kampuni ya *Rai Group Limited* ulikuwa bora kuliko ya wawekezaji wengine waliokwisha jitokeza;

Pili, mpango wa biashara ulio toa suluhisho na matatizo ya kiwanda kwa kupunguza utegemezi wa umeme wa *TANESCO* kwa kuzalisha umeme wao wenyewe kwa kutumia mabaki ya magogo.

Tatu, kupunguza aina za karatasi za kuzalisha ili kutatua tatizo la kutokidhi kiwango cha faida zinazopatikana kutokana na uzalishaji mkubwa au *economies of scale* ikiwa ni pamoja na kupanua uwezo wa kiwanda wa kuzalisha.

Nne, kupunguza matumizi ya umeme kutokana na kuachana na matumizi ya teknolojia iliyokuwa inatumia umeme mwingi.

Tano, kupunguza athari za uchafu wa mazingira kwa kubadilisha teknolojia ya kuzalisha karatasi.

Sita, mpango wa biashara ulipendekeza kuwekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 25.

Hata hivyo baada ya kukabidhiwa kiwanda kampuni ya *Rai Group Limited* ilifanya tathmini ya kina ya mahitaji ya uwekezaji ili kufikia uwezo wa uzalishaji wa tani 130,000 kwa mwaka zaidi ya mara mbili ya uwezo uliowekezwa *SPM* pamoja na kufanya *modernization* ya kiwanda na kubainisha kuwa mahitaji ya fedha yangukuwa takriban dola za kimarekani milioni 70. Mwekezaji amepanga kuwekeza jumla ya dola za kimarekani milioni 61.251. Aidha, mwekezaji alibadilisha jina la kiwanda toka *SPM* na kuwa *Mufindi Paper Mills* au kwa kifupi *MPM*. Ufufuaji wa kiwanda cha *Mufindi Paper Mills Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa mwekezaji tayari amekwishawekeza katika kiwanda jumla ya dola za kimarekani dola milioni 40 baada ya kulipa Serikalini dola za kimarekani milioni moja. Uwekezaji huu umewezesha kiwanda kufufuliwa na kuanza uzalishaji kwa kutumia mashine moja kati ya mashine mbili za kiwanda ambapo kwa sasa kina uwezo wa kuzalisha karatasi tani 36,000 hadi 39,000 kwa mwaka kwa kutumia mashine moja kuzalisha karatasi ambazo hazijatolewa rangi.

Kwa sasa kiwanda kinazalisha kwa kutumia uwezo wote wa hiyo mashine moja. Nia ni kuhakikisha kuwa uwezo wa mashine hii moja unafikia tani 65,000 kwa mwaka. Ukarabati wa kufufua mashine ya pili ya kuzalisha karatasi nyeupe au *commercial grade* kwa kutumia teknolojia isiyotumia kemikali zinazoharibu mazingira na kuondokana na kemikali ya *elemental chlorine* iliyokuwa inatumika awali umeanza. Aidha, kiwanda kimeweza kuzalisha umeme wa kutosha mahitaji ya kiwanda kwa asilimia 80 hadi 85. Vile vile kiwanda kimeajiri jumla ya wafanyakazi 520.

Ukarabati wa mashine ya pili utakapokamilika na uzalishaji kuanza wafanya kazi wengi zaidi wataajiriwa. Pia kiwanda kinalipa kodi Serikalini. Hali kadhalika, tangu

kiwanda kianze uzalishaji wa kibiashara katikati ya mwaka 2005 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2008 jumla ya tani 76,679 za karatasi zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 46.1 zilikwishazalishwa ambapo tani 25,705 zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 13.8 ziliuzwa kwenye soko la ndani na tani 52,974 zenye thamani ya dola za kimarekani milioni 32.29 ziliuzwa nje ya nchi. Nchi ambazo karatasi ziliuzwa ni pamoja na nchi ya Kenya, Uganda, Malawi, Zambia, India, Sri Lanka, Bangladesh, Malaysia, Vietnam, Iran, Misri na Soud Arabia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwekezaji wa kiwanda cha *SPM*, wakati kiwanda *SPM* kinabinafsishwa hisa za Kampuni ya *Rai Group Limited* zilikuwa zinamilikiwa na Bwana Tarochan S. Rai, Bwana Jesuanti S. Rai na Bwana Saswant S. Rai. Kampuni ya *Angle Hurst Industries Limited* ni kampuni ya uwekezaji au *investment company* inayomilikiwa kwa asilimia 100 na familia ya Ray. Kampuni hii imesajiliwa katika Visiwa vya *British Virgin*. Hivyo kampuni zote mbili za *Rai Group* na *Engle Hurst Industries Limited* zinamilikiwa na familia ya Rai.

Kwa vile kampuni ya *Engle Hurst Industries Limited* ni ya uwekezaji, ndiyo iliyotumika kuwekeza katika kiwanda cha *MPM* hivyo jina la kampuni ya *Engle Hurst Industries Limited* halikutokea kwenye mkataba wa kuuza mali za *SPM* kwa vile kampuni hiyo haikuwa mnunuzi wa mali za *SPM* bali imehusika katika zoezi la kuwekeza na kufufua kiwanda na ndiyo maana jina la kampuni hiyo limejitokeza wakati wa kusajili vivutio vya uwekezaji au *investment incentives* za kiwanda kwa *Tanzania Investment Centre* jukumu kubwa la *Engle Hurst Industries Limited* ni kuwekeza tu.

Utaratibu huu unatumika katika viwanda au biashara mbalimbali zinazochukua mikopo ya kufufua viwanda au biashara ambapo baadhi ya taasisi zinazotoa mikopo hupenda kumiliki sehemu ya hisa kwa kipindi chote cha zoezi la ufufuaji. Hivi sasa hizo hisa za kiwanda cha *MPM* zinamilikiwa na kampuni ya *Engle Hurst Industries Limited* kwa asilimia 99.513, Bwana Jaswant S. Rai hisa asilimia 0.242 na Bwana Sarbjit S. Rai hisa asilimia 0.242. Mwaka 2004 wakati *MPM* iliposalijiwa na Kituo cha Uwekezaji *TIC* umiliki wa hisa ulikuwa kama ifuatavyo:- Kampuni ya *Engle Hurst Industries Limited* kwa asilimia 99.988 Bwana Jaswant S. Rai hisa asilimia 0.006 na Bwana Sarbjit S. Rai hisa asilimia 0.006.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ulipaji wa mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa *MPM* liko Mahakamani kutokana na waliokuwa wafanyakazi wa *MPM* kufungua kesi Mahakamani wakiwa na madai mbalimbali. Hukumu ya kesi hiyo ilitolewa na Mahakama Kuu, Kitengo cha Kazi mwezi Novemba, 2007. Ingawaje hukumu ilitoa adhabu kwa pande zote, kiwanda na wafanyakazi, hukumu hiyo ilikuwa kubwa zaidi kwa kiwanda.

Hata hivyo, kiwanda cha *MPM* na *Consolidated Holding Corporation* iliyochukua shughuli za Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (*PSRC*) zimeomba marejeo au (*Revision*) ya hukumu hiyo katika Mahakama Kuu, Kitengo cha Kazi. Maombi hayo bado hayajatolewa uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwambalaswa alikuwa ameniomba mwongozo kuhusu kifungu cha 49(iii) ambazo kinahusu kauli za Mawaziri. Kwa hiyo, Waziri mwenye kutoa kauli atawajibika kutoa nakala ya kauli yake kwa Wabunge wote wakati anapowasilisha Bungeni. Kwa hiyo, naona hili halikufanyika. Napenda lifanyike hivyo siku zijazo. Kwa sababu Spika mwenyewe hana, kwa hiyo, hiyo ni *omission*. Tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa Mwaka 2008/2009 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

(Majadiliano yanaendelea)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao bado wachangiaji kama tisa. Lakini lengo letu ni kwamba wote waishie asubuhi hii, kusudi jioni Mheshimiwa Waziri aweze kupata muda mzuri wa kuweza kujibu hoja zilizochangiwa na Wabunge. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninashukuru kwa kuweza kupata nafasi hii, ikizingatiwa kwamba nilichelewa kuomba, lakini mmeweza kunifikiria kwa sababu sijawahi kuchangia. Lakini kabla ya yote naomba nitume salamu za pole kwa familia ya Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe. Nalisema hili kwa sababu wakati wa kifo chake hadi katika taratibu zote za mazishi nilikuwa sijarudi bado. Mungu ailaze roho yake pema Peponi na kwa ufupi ni kwamba tuko pamoja na familia.

Nitachangia kwa kifupi sitarajii kama nitamaliza dakika 15. Nina machache ya kuchangia. Kwanza kabisa, nianze na suala zima la tatizo la uuzwaji wa viwanja mara mbili mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waheshimiwa Wabunge wengi wanapochangia hapa, imeonekana kwamba tatizo la ardhi hasa hasa kwa *double allocation* ni kubwa sana. Mimi nitatoa mfano wa maeneo ambayo ninatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba hii ni picha ya Tanzania nzima. Eneo husika kutokana na mada yangu hapa ni Halmashauri ya Kinondoni na ni wazi kabisa na nafahamika kwamba Halmashauri ya Kinondoni ni moja ya maeneo ambayo yanaongoza kitaifa kwa *double allocation* kitaifa ya viwanja au kugawa viwanja mara mbili mbili na vile vile naomba nieleweke kwamba ninavyozungumzia hili, siwalaumu kabisa wale wamiliki wanaopewa mara ya pili, ila nina-*deal* na watendaji kwa sababu kama siyo hawa watendaji ambao wanafanya vitu vya kihuni, hawa watu wasingeweza kupata ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendele moja kwa moja kuhusiana na uuzwaji wa viwanja viwili eneo la Kawe. Inasikitisha sana ukiona kwamba watendaji wetu wanadiriki kuuza maeneo ya shule, wakati tunaambiwa kwamba malengo yetu ni kupanua shule na kupanua elimu kwa ujumla. Lakini ni watendaji hao hao ambao wanashiriki katika kuuza maeneo ya shule. Viwanja ambavyo nitavizungumzia leo hii naamini siyo kitu kigeni, wahusika wanajua. Ni kiwanja namba 696 na 695. Hiki cha 696 kiko eneo la Ukwamani na kiwanja namba 695 kiko Kawe 'B'. Hizi zote ni shule za *Primary* na *Secondary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ramani, kwa sababu tunakwenda kwa vielelezo. Ramani inaonyesha kwamba hili eneo lilikuwa limetengwa kwa ajili ya shule za Halmashauri. Kila kitu kiko wazi hapa. Kiwanja Na. 695 kiko hapa kiwanja namba 696 kiko hapa. Kimetengwa maalumu kwa ajili ya kujenga shule za Halmashauri. Sasa cha kusikitisha, japokuwa limepimwa na *evidence* ziko hapa, wajanja wachache katika Halmashauri ya Kinondoni wakashiriki katika kukigawa hiki kiwanja.

Naomba nirudie tena, silaumu waliopewa, nalaumu huyu Mtendaji ambaye kwa makusudi kabisa anaamua kugawa kiwanja. Katika ramani hii, katika kiwanja Na. 696, tunaona kwamba eneo ambalo limegawanywa, wananchi tayari walikuwa wameanza kujenga maabara. Mimi mwenyewe nilikwenda kushuhudia kwa miguu yangu kwamba kuna jengo la maabara liko ndani ya kiwanja cha huyu tajiri aliyekuja kununua. Lakini tukizungumza yanaanza kuletwa masuala ya kidini, kitu ambacho ambacho sio cha kweli. Tunasimamia pale kwenye mstari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa kuwa Sera ya Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa Rais anazungumzia maeneo ya shule yanatakiwa yaweje. Tumekuwa tukiambiwa maeneo ya shule yanatakiwa yawe na viwanja. Lakini kutokana na hivi viwanja kuuzwa, lile eneo madarasa hayawezi kuongezwa *effectively* kukawa kuna nafasi za kutosha, nyumba za walimu zimeshindwa kujengwa kiasi kwamba tunaambiwa, nakumbuka niliwahi kuhoji hili suala na kujibiwa hapa hapa Bungeni kwamba Serikali inachotaka ni shule zijengwe. Kwa mujibu wa ramani shule inayotakiwa kujengwa ni shule za Halmashauri/wananchi na sio *private school*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule zinazojengwa pale ni *private* ambazo ni kama *international school*. Wakazi wa pale ni watu wa kipato cha chini. Sasa ile shule inamnufaisha nani? Inamnufaisha mkazi wa Kawe 'B' ambaye ni maskini au inanufaisha watu wengine kwa ajili ya kuja pale kuvamia eneo na kuleta watu wengine ambao siyo wakazi wa pale? Kwa sababu kama ingekuwa ni shule ya kawaida ambayo maskini wa kawaida anaweza aka-*afford at least* ingeweza kusemekana kwamba sawa, imejenga shule hapa, lakini watoto wa Kawe 'B' wanafaidi.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili na nimewahi kufanya kazi naye akiwa katika Wizara ya Kazi, ninaamini kwamba ni mchapa kazi. Hili suala limepitia hatua mbalimbali, linapigwa dana dana za ajabu, mpaka unajjuliza, au kuna kigogo amehusika katika haya maeneo mawili? Mwaka 2006, kuna barua ilitoka kwa

Mwenyekiti wa Kamati ya Wazazi kwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi. Hii ilikuwa mwaka 2006. Lakini Serikali ilikuwa mwaka 2006 kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, iliandikwa barua kwa Waziri Mkuu, kipindi kile akiwa Msheshimiwa Lowassa, kimya. Wananchi waliandamana pale, wakaishia kuonana na Msaidizi, wakaambiwa nendeni zenu. Kuna Barua ilitoka kwa Mwenyekiti wa Mtaa wa Mzimuni, ikaenda Manispaa kwa Mkurugenzi, ikaenda kwa Meya Londa ambaye analaumiwa kwamba yeye ndiyo injinia wa hii shughuli yote na inasemekana kutokana na maelezo ya huko huko kwamba Londa analindwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa kipindi kile, wakati sakata hili linatokea ambaye alikuwa ni Mheshimiwa Makamba, inasemekana hivyo. Kwa sababu hili suala linakwenda, linarudi, *facts* zote zipo.

Inawezekana hawa watu wa pili (wavamizi) wa hatimiliki, wana *offer* na kila kitu, lakini mwisho wa siku inabakia, kulikuwa kuna yule mtu wa kwanza ambaye ndiye alikuwa mmiliki halali. Kwa hiyo, huyu mtu wa pili kuja huku kupewa *offer* ya pili haihalalishi huyu mtu wa kwanza kunyimwa eneo lake. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili.

Vile vile kuna taarifa kwamba, ili kulifanya hili suala life, (ninaamini kwamba kwa vile ni Wizara yako Mheshimiwa Waziri utafuatilia) kumekuwa kuna mtindo wa kuanza kufukuza au kuwahamisha wafanyakazi kidogo kidogo Manispaa ya Kinondoni.

Kwa hiyo, watu waliokuwepo na wanaOjua ile siri, wanatolewa mmoja mmoja ili ambao walikula pesa waweze kukaa kiulaini na kuendelea na masuala ya kifisadi. Kwa hiyo, nakuomba kwa dhati ulifuatilie hili suala na ninaamini kabisa wewe unajua Kinondoni kuna matatizo. Kila mtu anasema Kinondoni kumeoza. Huyu Londa ni nani Kinondoni? Ni Mungu mtu?

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana ulifuatilie hili suala. Vile vile kuna ushahidi unaoonyesha kwamba kuna Mheshimiwa mmoja alipewa pesa milioni 50 na inasemekana kabisa kwamba Mwenyekiti wa Mtaa, mwenye jina la Mwakininda, yeye ndiye alikuwa mfikisha huo mzigo na yeye akapewa pesa yake laki moja.

Kwa hiyo, naomba ulifuatilie hili suala ili tuweze kupata ukweli na hatimaye eneo la shule libakie kuwa shule na vile vile kuna majibu mbalimbali ambayo aliyatoa Mheshimiwa Londa alipohojiwa. Akasema kwamba uamuzi wa kuuza kiwanja ni wa Chama cha Mapinduzi. Najua wewe ni Kada Mahususi. Kwa hiyo, kama kuna uamuzi wowote unaotoka kwenye Chama lazima wewe utakuwa unakijua.

Kwa hiyo, kama kweli Chama cha Mapinduzi ndiyo kilitoa baraka ya kuuzwa kiwanja cha shule, kitu ambacho mimi sitaki kuamini, nitaomba unijibu. Vile vile inasikitisha sana kuona kwamba Kiongozi anadiriki kusema kwamba yeye aliagizwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya, Bibi Hawa Ngulume, kwamba watu wa aina fulani wanataka kiwanja, kwa hiyo, wapewe. Sasa katika taratibu za kawaida, sijui kama Mkuu wa Wilaya ana mamlaka ya kuagiza tu mtu.

Kwa hiyo, mimi naona kuna uhuni wa hali ya juu ambao umefanyika ambao inabidi watu wachukuliwe hatua, japokuwa kuna majengo wameshaanza kuyajenga na

yamefika magorofa sijui ya mara ngapi. Lakini mwisho wa siku ukweli unabakia pale pale kwamba lile eneo ni la shule hata kama watu wanataka au hawataki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna tatizo lingine. Tunateua au tunachagua viongozi wetu wa Mitaa au Vijiji lakini tunakuwa tunawadharau. Kuna huyu bwana anaitwa Nyeri. Eneo hilo hilo la Kawe, amediriki kuziba barabara ya wananchi waliotumia miaka 20 amejenga nyumba yake. Kuna ushahidi hapa kunaonyesha hapa unaonyesha kwamba hadi Manispaa ilikwenda ikaweka 'X'. Lakini anachofanya yeye anakuja anafuta ile 'X'. Kuna barua zinaonyesha kwamba Watendaji wote kuanzia ngazi ya chini wamekuwa wakimwita kwenye Kikao cha uvamizi, lakini amekuwa anapuuza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee! Ukiwa na viambatanisho namna hiyo una-*lay on the Table*. uki-*lay on the Table*, Spika atampa Waziri ili Mheshimiwa Waziri atakapojibu aweze ku-*refer* huko. Sasa ukionyesha namna hiyo *Hansard* yenyewe kwanza hawezi kuona. Kwa hiyo, fanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nitamkabidhi. Yaani kama hivyo ilivyotokea kwa Mheshimiwa Nagu leo asubuhi. Lakini mimi ninavyo hapa, nikimaliza nitamkabidhi ili aweze kwenda kufanya kazi vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Kabidhi kwa Katibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Sawa Mheshimiwa Naibu Spika, nitakabidhi kwa Katibu. Kwa hiyo, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, huyu ndugu Nyeri ambaye ameziba barabara ya wakazi wa Kawe ambayo wametumia kwa miaka 20 na ambaye anadiriki kuitwa kwenye Vikao halali vya kuanzia Mtaa hadi Kata anadharau. Naomba afuatiliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kabla ya kengele ya pili haijagonga, naomba nizungumzie suala zima la Serikali kuchukua ardhi ya wananchi bila makubaliano. Hili ni tatizo ambazo limekuwa linajitokeza sana. Ni kweli kwamba sote tunakubali maendeleo. Hakuna mtu ambaye anakataa kwamba kama sehemu fulani kinataka kijengwe Chuo, watu wasihamishwe. Lakini huwezi kuwa unahamisha watu kiholela. Unahamisha watu bila kufanya majadiliano na kukubaliana ni kiasi gani cha pesa mlipane kutokana na thamani ya ardhi kipindi kile.

Kumekuwa na matatizo kama hayo Kibamba, yameishia ishia tu hatujui yamekwendaje. Zilitolewa ahadi nzuri tu na aliyekuwa Waziri wa Ardhi. Sijui kama zimeteteleka, lakini inaonekana bado kuna tatizo. Juzi hapa tumeona wananchi wa Mbweni, tatizo hilo hilo. Sasa hivi kuna tatizo kubwa Keko Matangini. Inaonekana kwamba bandari sasa hivi kama tunavyojua bandari inaingiza pesa.

Kwa hiyo, inaonekana yale makontena yanayokaa pale yanahitaji yaongezewe maeneo ili kuongeza kipato cha Serikali. Hiyo ni kweli, lakini kuna umuhimu wa kuangalia ni kwa jinsi gani mnakutana na wale wananchi ili kuweza kuwafidia inavyopaswa. Kwa sababu inaonekana sasa hivi shughuli zinafanywa kwa usiri siri sana.



Zinafanywa kwa usiri kwa haraka haraka, huna ushirikiano kiasi kwamba watu wanakuwa wanajiuliza labda kuna mkubwa ambaye amepewa kidogo kidogo. Unakuta kwamba siyo kweli. Lakini sisi wenyewe tunatengeneza mazingira ambayo yanawafanya wananchi wanakuwa wanajenga hisia ambayo sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Nategemea nitapata majibu.

**NAIBU SPIKA:** Unaunga mkono hoja? Tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma. Mheshimiwa Mporogomyi ajiandaye, halafu atafuatia Mheshimiwa Ligallama. *(Kicheko)*

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu. Nasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga kwa asilimia mia moja nisije nikasahau. Nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya pekee, kwani nilikuwa nimechelewa na ninakushukuru sana na ninashukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii kuongea kwenye Bunge hili Tukufu, kwani kwa kuchangia kwa kuongea ni mara yangu ya kwanza. Nimechangia mara nyingi kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, natoa shukrani nyingi sana kwa Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa mbele yenu namshukuru sana. Natoa shukrani zangu za haraka sana kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliyeniteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, mpaka Mafia ni Mkoa wangu. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza nitoe shukrani nyingi nyingi, nishukuru sana Waheshimiwa Wabunge wanaozidi kunipa ushirikiano nikiwa hapa Bungeni. Shukrani za pekee ziende kwa Wabunge wangu wa Mkoa wa Pwani, pia na Wabunge wa Mkoa wa Morogoro kwa ushauri wote wanaonipatia. Naupokea wote, naukubali.

Nisisahau sana kuwashukuru akina mama, wanawake wa Morogoro walioniwezesha kufika hapa. Ninawapenda sana akina mama wa Morogoro, ni wa kweli na wa haki. Ahsante sana kwa kura zenu zilizoniwezesha fika hapa Bungeni. *(Makofi)*

Nisisahau sana kuwashukuru walimu, wahadhiri na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sokoine, pamoja na Mzumbe kwa ushirikiano wote walionipatia mpaka nikafika hapa. Nawashukuru sana. Mwisho kabisa kwa shukrani zangu, napenda sana kumshukuru mume wangu mpendwa Prof. Ishengoma pamoja na familia yangu yote na marafiki kwa maombi yao walionipatia. Sasa narudi kwenye hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Capt. Chiligati pamoja na Katibu wake, rafiki yangu Mama Salome, Wakurugenzi kwa kazi yote wanayoifanya kwenye Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi ni kubwa sana na ni Wizara muhimu sana kwani bila ya ardhi huwezi kufanya kitu chochote. Maisha yote yako kwenye Ardhi. Hata Mwenyezi Mungu aliumba kwanza mbingu na ardhi, ndiyo vitu vingine vikafuatia. Kwa hiyo, naomba tuwe tunaipa kipaumbele kwenye mambo yote muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia kwenye mambo ya mashamba pori, mashamba ambayo yameachwa wazi bila kuhudumiwa. Kwa upande wa Morogoro, kuna mapori mengi na kwa upande wa Pwani mapori yamezidi, kiasi watu huwa wanasema Pwani hatulimi. Lakini sasa naomba kuwaambia kuwa kilimo Pwani sasa hivi kinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia kwenye Bunge lako hili Tukufu, niwaombe kwanza Waheshimiwa Wabunge wote walio humu ndani, niwaombe wananchi wote walio huko nje wanaonisikiliza hapa, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, wengine ni viongozi wakubwa, ni vigogo. Lakini nawaomba tafadhali sana tuweze kuhudumia mapori yetu yaliyo hasa Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alisema kuwa Halmashauri ziweze kuainisha mashamba yaliyoachwa kwa muda mrefu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kuwa baadhi ya Mikoa tayari walishaorodhesha mambo haya yaliyoachwa wazi na ninaomba sana Mheshimiwa Waziri yaweze kuchekiwa kusudi tuweze kuyaendeleza yaweze kupelekwa huko mbele na yaweze kufutiwa hati kusudi yaweze kugawiwa kwa vijana wetu na wananchi ambao hawana ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili napenda kuongelea kwenye jambo la Wilaya yangu ya Bagamoyo. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kutupatia hela za mkopo za kupima viwanja kwenye Wilaya yangu ya Bagamoyo. Napenda kueleza kuwa mkopo huo tumeutumia vizuri, viwanja vimepimwa, tayari tumeshamaliza kupima na sasa hivi kitu tunachomalizia ni kuweka miundombinu.

Kwa hiyo, hivi karibuni wananchi ambao tayari walishalipia, tutawatangazia kupitia kwenye vyombo vya Wizara ili waweze kuja kupewa viwanja vyao, ila naomba waelewe kuwa sio Sh. 300,000/= kama walizolipa kwa sababu kwa kuweka miundombinu fedha itakuwa zaidi kidogo na viwanja viko tayari, wananchi wasiwe na wasiwasi wataweza kupata viwanja vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuishukuru Wizara hii muhimu ya ardhi kwa kutujengea maghorofa Chalinze, lakini naomba kukumbushia kuwa maghorofa hayo ninavyofahamu bado Mheshimiwa Waziri anaombwa kuongezea kwa sababu bado yanaendelea kujengwa mengine kama nilivyoelezwa mpango ulivyokuwa.

Tatu, kwa sababu sisi tuna bahati Morogoro na Mkoa wa Pwani pia, tunaiomba sana hii Wizara, tutazidi kuisumbua iweze kutujengea majengo mengine hasa ya wapangaji kwa sababu unakuta wananchi wengi wanakaa Dar es Salaam, lakini

wanafanya kazi Kibaha au Bagamoyo, Chalinze, hii haiji. Hatuwezi kupata ufanisi mzuri wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye kuuza ardhi. Nawaomba sana wananchi wangu kupitia Bunge lako hili Tukufu waache kuuza ardhi ovyo ovyo kwa sababu ardhi ni mali na watu sasa hivi wanakuja kwa nguvu. Sijui walikuwa wapi kuchukua ardhi ya Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Morogoro!

Mwisho kabisa mimi nilikuwa nachangia machache, ila nawaomba sana wananchi wa Mkoa wa Morogoro, Pwani na Mikoa mingine kama Kagera, Mwanza na mingine yote tuweze kuhimiza kilimo kama kauli mbiu hii ya Nane Nane inavyosema ya kuwa kwenye kilimo cha kijani ili bila ya kilimo au ardhi hatuwezi kufika mbali kusudi tuweze kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania. Maisha bora kwa kila Mtanzania, naamini yatawezekana lakini hayawezi kuwezekana kwa kulala na kukaa tu. Ni lazima tufanye kazi, ndio maisha bora yataweza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninasema ahsante sana kwa kunipatia nafasi. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa naomba na mimi nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kuniweka hai mpaka wakati huu. Ninamshukuru sana kwa makubwa ambayo amenitendea mimi katika maisha yangu. Lakini nashukuru zaidi kwa sababu moyo wangu unaamini Mungu ni mwema na anawalinda walio wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru wapiga kura wangu katika Jimbo la Kasulu Magharibi ambao wamekuwa karibu nami sana katika muda wote ambao nimekuwa Mbunge katika jimbo lile. Naomba niwashukuru sana kwa kuwa wavumilivu sana. Lakini pili naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Mwijage na familia yake, kwa kuondokewa na mwanaye mpendwa pamoja na dereva wake.

Pia natoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Chacha Wangwe, mtu ambaye mara kwa mara nilibahatika kuzungumza naye na ambaye alikuwa anonyesha mapenzi makubwa sana na watu wake. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Chiligati pamoja na Katibu Mkuu wake Mama Sijaona. Ninawapongeza sana kwa sababu nimepitia ripoti yao, inavutia, imeandikwa kwa umahiri mkubwa na ni ripoti nzuri kusema kweli. Imejaribu kugusa maeneo mbalimbali na mimi ninafarijika kwamba ripoti hii pengine ingekuwa mfano kwa ripoti zote zinazoandikwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Chiligati kwa kazi nzuri na ripoti hii ni nzuri kwa sababu pia naamini ana Katibu Mkuu mzoefu, mchapa kazi, mwanamke, hongera sana. Lakini nampongeza pia kwa sababu yule Kamishna aliyenaye mimi nimesoma naye, alikuwa anaimba nyimbo tulipokuwa tunasoma shule, anamjua Mungu, nampongeza sana naye ni mchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa natoa pongezi hizi, lakini pia nieleze machache ambayo nafikiri yanaweza kuboresha shughuli za Wizara hii. Naomba nianzie kule ninakotoka. Hati miliki za vijiji ni muhimu sana ili kuepuka vurugu zinazoweza kutokea baina ya vijiji hadi vijiji. Ninao uzoefu, kule nyumbani nina vijiji viwili ambavyo vimekuwa na ugomvi. Kijiji cha Muhinda na Kijiji cha Nyarugoza, wamekuwa na ugomvi wa mipaka na Kijiji cha Nyarubanda ambayo Nyarubanda iko Kigoma Vijijini.

Mara ya kwanza niliwahi kwenda pale nikaomba Maafisa ardhi wote wawili wa kutoka Kigoma Vijijini na Kasulu Wilayani wakutane pale, wakutane na wananchi wajaribu kueleza mipaka ile na kuonyesha mipaka ile inavyokwenda. Nikaenda pale mara ya pili nikaambiwa amekwenda lakini mmoja hakufika. Mara ya tatu nimekwenda nikaambiwa kumetokea ugomvi na watu wamepoteza maisha. Sasa huu ni ugomvi ambao kwa kweli tusingependa utokee katika nchi kama yetu, ugomvi ule ni mkubwa kwa sababu unahusisha vijiji viwili ambavyo haviko Wilaya moja na ni muhimu sana Maafisa Ardhi kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa na uongozi wa Wilaya wakajihusisha sana na kuangalia mpaka ule ili waweze kuutengeneza na kuuonyesha kwa wananchi ili vurugu zote zilizopo ziweze kumalizika.

Sio vizuri kuwa tunasikia watu wanapigana, wanagombana, hawaishi kwa amani tuliyoizoea, hawana maelewano kama hivi ilivyotokea katika vijiji hivi. Kero kubwa katika kijiji cha Muhinda na Kijiji cha Nyarugoza ni hili la ardhi yao kuchukuliwa na watu wanaotoka Wilaya nyingine na wao wamekuwa wakiomba kwamba ni vizuri tu wakae, wale ni ndugu zao wakaena kisha wamalize hili tatizo vizuri tu. Ninaimani wataelewana na watasaidiana katika kulimaliza. Lakini naiomba Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, alishughulikie jambo hili ili tuweze kuepusha ugomvi wa aina yoyote ambayo unaweza kutokea katika vijiji vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niipongeze Wizara kwa kweli kwa kuja na hiki kitu wanaita *Enterim Land Use Plans*. Wilaya yangu ni Wilaya mojawapo ya Wilaya zile zikazofaidika na mpango huu. Mimi naomba yale yote yaliyoandikwa chini ya kifungu kile yatekelezwe vizuri, maana yakifanywa yataelezea mambo mengi na muhimu ambayo yanaweza kuturahisishia maendeleo katika vijiji vyetu. Liko tatizo moja ambalo mimi nina *experience* nalo na tatizo hili ni tatizo la kupata hatimiliki. Kwanini hatimiliki ni tatizo kubwa sana kutoka Wizara ile?

Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, wakae walipatie ufumbuzi. Unanunua nyumba leo unakwenda pale Wizarani, utazungushwa, nenda Kinondoni, rudi Wizarani, nenda Kinondoni, rudi Wizarani, mpaka mwenyewe unachoka unaamua kupumzika uje upate nguvu nyingine ya kufanya kazi hiyo. Sio rahisi kupata hatimiliki kwenye Wizara ile. Kwa hiyo, naomba nijaribu kurahisisha maana kama mimi Mbunge naweza kupata shida ya namna hiyo, nina imani mtu wa kawaida anapata shida kubwa sana na mwishowe kiwanja anapoteza. Mtu wa kawaida anahangaika kweli kweli maana hajui hata pa kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna utaratibu umeuwekwa watu wananunua viwanja, wakishanunua viwanja anakuja analipia pengine nusu au analipia robo anaondoka, hujui tatizo lililompata, hujui nini, hakuna *notice*, unamwambia kiwanja kilishauzwa na hela yako Sh. 1,500,000/= umepoteza. Kwa Mtanzania wa kawaida Sh. 1,500,000/= ni pesa nyingi jamani. Ni vizuri atafutwe ampatiwe taarifa kwamba bwana kiwanja chako kitauzwa kama hufanyi hivi na hivi, mwandikieni hata mara mbili mara tatu, Sh. 1,500,000/= ni hela nyingi. Mimi naomba kama hiyo sheria ya kuchukua hizo hela ilitengenezwa, kweli mimi naomba awe anarudishiwa hizo hela kama mmepata mtu wa kununua. Kwanini mnachukua pesa, mchukue na nyingine tena zinazokuja? Mimi naomba arudishiwe hela zake, maana watu wanakuwa wananung'unika tu hawajui pakwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lingine linalofuatana na hilo, hili sitalificha nitalisema angalau huku nafumba fumba, hili ni la *CDA*. Sisi tunataka watu wengi waje hapa *CDA* wakajenge katika Mkoa wa Dodoma, wajenge hapa. Urasimu ulipo hapa kupata kiwanja ni mbaya sana! Unaomba kiwanja, wanakuzungusha mpaka sijui utoe rushwa, mpaka ufanye nini! Wanakwambia tunapitisha ramani lakini, mimi ni shahidi, nilikuwa na kiwanja ninawaomba wanipeleke kunionesha, hawakunionesha walipoki-*locate* kile kiwanja nikaja kuambiwa kimeuzwa, sikupewa *notice*, wala sikuambiwa nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba huyu Mkurugenzi wa *CDA*, anipe kiwanja changu. Mkurugenzi wa *CDA* anipe kiwanja changu, sitapenda, nakwenda pale ninakuta mtu amemwaga mchanga, eti mimi sikulipa. Hawakuniambia! Nimekuwa nawaomba waende kunionyesha, mtu mwingine na yeye akakipata eti hapa kuna kiwanja, kilipojulikana tu kilipo kile kiwanja kimeuzwa.

Barua ninayopata ni kwamba kimeuzwa, mimi sina haki ya kuwa na kiwanja kile, *no notice, nothing*. Sheria gani hii? Eeh! Hii ni sheria ya rushwa, kwa kweli mimi nitawashitaki! Lakini sina sababu ya kuwashitaki maana Mkuu wa Wizara, ninamwamini yeye ni muadilifu na anajua kazi hii, nitapata kiwanja changu. Eeh! Yeye ni muadilifu, wala sina wasiwasi na Katibu Mkuu wake mimi nawapenda sana, sina sababu ya kuwashitaki wala kufika huko. Najua hawatashindwa na mimi nina imani nitarudishiwa kiwanja changu hicho. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ardhi, ardhi ni mali. Ule mpango wa *MKURABITA* wa kurasimisha *properties* za watu katika sehemu mbalimbali za nchi hii ni mpango mahususi wa maendeleo ambao umesaidia nchi nyingine kama zile za Peru na kule *Latin America*, hakuna njia *you can manage your Microfinance program* bila mpango huu wa kurasimisha mali. *So it is a good plan*. Inakwenda vizuri, lakini nafikiri mpango huu uende vizuri zaidi na uende haraka zaidi mali za watu zirasimishwe waweze kupata mali.

Kinachotakiwa hapa ni utaratibu wa *in built methodologies* za ku-*manage Microfinance programs* kutumia hizi, rasilimali zitakazokuwa zimerasimishwa na sio urasimu mwingine. Watu wetu wana matatizo makubwa vijijini huko, ukikuta *demand*

*for financial services* ni kubwa sana, lakini hawawezi kupata *alternative finance* kwa sababu hawana aina yoyote ya mali iliyorasimishwa na ambayo wanaweza kuiweka kama *security* kama *collateral* ikawasaidia kupata pesa mahali pengine. Hata wewe Mbunge uliyeko humu ndani kama una nyumba kijijini *it is not an asset*, haikupimwa, haina nini, *it is not an asset*, haikusaidii. Nyumba nyingi hazikupimwa!

Ninaishukuru Wizara kwa sababu imehamishia mipango yote Mikoani, itaharakisha kasi ya uandikishaji wa hizi kurasimisha hati hizi na ndipo tutapata kasi ya maendeleo kuwa nzuri zaidi. Miaka inayokuja nchi hii watoto wetu watakuwa wanapigana vita wasiyojua, tunauza ardhi bila mpango, tunatoa ardhi bila mpango. Nilimkuta mtu anasema: *“If you want property my friend go to Tanzania, you get property without paying nothing. You only need to buy property and register the property free. If there is difficulties just marry a Tanzanian,”* au anakuwa *girlfriend* wako tu, unampleka unakwenda naye unasema huyu ni mke wangu ndio tunataka tupate mali na wanapata mali kweli kweli, sio kidogo, eeh! Anasema huyu ndio mume wangu na mali inachukuliwa. Sasa hii ardhi tunaitaka, ujanja wa kuwanyima Watanzania mali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie habari ya Dar es Salaam, Dar es Salaam kuna mmoja amesema inakuwa, sasa inajengwa na watu wanne matajiri wakubwa. Wale matajiri wanne wana-*harass* kila mmoja pale Dar es Salaam, Wahindi wengi sasa hivi wana hofu kubwa wanasema wenye pesa wanatutesa. Mimi Mheshimiwa Waziri, nitampa dokezo wameniidikia, naomba alifanyie kazi. Ahsante sana nakushukuru, naunga mkono hoja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi kwa hotuba hii. Mimi nimeisoma, ina maslahi kwa wananchi wetu wengi, kwa wamiliki na watumiaji wa ardhi. Pia napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kilombero, kwa kunipa ushirikiano kwa kipindi chote hiki cha uwakilishi. Mchango wangu utahusu hasa maeneo ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, *TAMISEMI* na baadaye vijiji hivi vikapimwa na Wizara ya Ardhi, vikawekewa alama, baadaye ikachorwa ramani ambayo imethibitishwa na Mkurugenzi wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Kilombero kuna mgogoro wa siku nyingi sana. Sasa mgogoro huu una takribani miaka 13 kati ya wananchi wa kijiji cha Ikule na Chita na Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, *KJ 837*. Mgogoro huu unahusu mipaka. *JKT Chita* wakati wanatafuta ardhi kwanza walienda kwenye Kata ya Mchombe. Hapa napenda ku-*declare interest*, ni Kata ambayo mimi nimezaliwa.

Kwa kuwa Kata ya Mchombe ilishakuwa na shamba kubwa la *Korea Tanzania Cooperation* wakasema sisi hapa hatuna ardhi ya kutosha labda mjaribu Kata ya jirani ambayo ndio Chita, wakaenda Chita wakapewa ardhi pale. Wakati huo Kata ya Mchombe, kijiji ambacho kilikuwa kinapakana na *JKT Chita*, kilikuwa kijiji cha Mkangawalo na mpaka wao ulikuwa wa kudumu wa mto Mkaja na mto ule mpaka hivi

naongea haujabadilisha *course* yake, unapita vilevile ulivyokuwa unapita miaka mingi iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Mkangawalo kilipokua na kuwa kikubwa kikazaa kijiji cha Ikule. Hapa napenda ninukuu hati ya kijiji cha Ikule, “MG/KIJ/557.” Hati hii ilitibitishwa kwamba, “Kijiji kijulikanacho kama Ikule kilicho katika Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro leo kimeandikishwa kama kijiji kwa mujibu wa kifungu cha 22 cha Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Sheria Na. 7 ya Mwaka 1982.

Hati hii imetolewa na kutiwa sahihi na mimi. (Kwa wakati huo alikuwa Tarishi MK) leo tarehe tatu ya mwezi Julai, 1999.” Kijiji hiki kiko mpakani na Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa. Kuanzishwa kwake Kijiji hiki mwaka 1999 hakuondoi haki ya kuwa na mipaka ile ile ya kijiji mama cha Mkangawalo. Sasa wakati Jeshi lilipositisha shughuli za *JKT*, hapa katikati pakatokea maaskari ambao sio waaminifu, wakaanza kufanya vurugu kuvuka mto ule wa Mkaja ambao ndio mpaka, wakaja kwenye kijiji cha Ikule. Kila mwaka wanachukua ardhi kidogo kidogo na kuwafukuza wananchi, kuwapiga na mwaka juzi waliwachomea moto nyumba zao na picha tunazo zikihitajika tutakuwa tayari kuzitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro umeendelea, mwaka 2006/2007 wakanijia mimi tukaenda ofisi ya *TAMISEMI*. *TAMISEMI* ikatuma Tume, lakini pia wakati huo huo wanakijiji walikuwa wamemwandikia Mheshimiwa Rais, naye akatuma watu. Pamoja na hizi Tume mbili, bado mpaka leo mgogoro upo na mimi Mbunge wao nalaumiwa sana katika hilo. Lakini sheria ni sheria, kijiji kimeandikishwa, pamoja na Tume hizo mbili kufanya maamuzi na kutoa taarifa kwanini mgogoro unaendelea?

Juzi juzi Mwenyekiti, amepata barua ambayo inasema Mheshimiwa Rais amesema wakiri kwamba wao wamevamia ardhi ya *JKT*, lakini jinsi ninavyomfahamu Rais wetu, sikuamini kwamba ule ushauri umetoka kwa Mheshimiwa Rais na kama ameutoa, amepotoshwa na watu ambao wamekaa pembeni. Wanaujua ukweli, lakini hawataki kusema kweli. Mimi nililifanyia kazi hilo, baada ya hapo nione ni kitu gani, kweli Mheshimiwa Rais anaweza kuwaambia hawa watu, wamekaa, tumewasajili tangu mwaka 1999 leo awaambie wakiri wamevamia ardhi ya Jeshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ni mto na wao ndio waliovuka mto. Nimelifanyia kazi, nikagundua kuna watu wamepotosha ukweli hapa katikati. Kwa sababu sheria ya vijiji imeanza mwaka 1975 kama sikosei na kijiji mama cha Mkangawalo ndicho kilikuwa kinapakana na kijiji cha Chita. Lakini kuna watu hapa katikati ikiwa hiki Kijiji cha Ikule kimepata hati ya Usajili mwaka 1999, kuna watu wamekuja kuchoresha ramani tena mwaka 2002, sasa hii ramani ndio iliyotumika nafikiri kumpotosha Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, ramani hii nimeiangalia haikufika kwa Mkurugenzi wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, inaishia kwa *Regional Secretariat Land Surveyor*, pale Mkoani Morogoro. Tatizo hili limedumu miaka mingi, uhusiano kati ya

kijiji na Jeshi ni mbaya kiasi ambacho wanajuta ni kwanini waliwakaribisha. Tusifike hapo.

Mimi ninaomba kitu kimoja, bahati nzuri hawa waliochora ramani majina yao yanaonekana hapa, samahani kidogo. Hii ramani imeandikwa *plan drawn by Mzuzuri S. na Machage J. V. na waka-certify that*, wakasema, “*I hereby certify that the survey represented by this plan was carried out in accordance with the surveyor regulations.*” Wakampelekea huyu *Regional Secretariat Land Surveyor* wa Morogoro, bwana mmoja anaitwa W. R. Mgalula, akasaini tarehe 08 Machi, 2002 na hii *registered plan* ikapewa Na. 34,685 hapo ndio kwenye matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Bwana Mgalula naomba atafutwe kama yuko Morogoro na hao akina Mzuzuri na Machage watafutwe. Walitumwa na nani kwenda kuchora ile ramani? Ramani hii ukiingalia Kijiji cha Ikule hakionekani tena, kimefukiwa. Sasa Serikali haiwezi kujipinga yenyewe. Wewe ndio umetoa hati ya kuanzisha kijiji cha Ikule, leo inachoresha ramani ya kukifuta Kijiji cha Ikule, ionekane Jeshi linapakana na kijiji mama, haiwezekani! Hapa kuna kitu kimefanyika!

Sasa huu udhaifu ndio uliotumika kumshauri Mheshimiwa Rais kwamba angalia ramani, labda Mheshimiwa Rais, walimpelekea ramani hii, hawa wanakijiji hawana ramani hii hapa inaonesha ni Jeshi la *JKT* linapakana na Kijiji mama cha Mkangawalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, naomba tufikishe hili suala mwisho na nina imani kabisa kwamba wewe unaweza ama kwa kuunda Tume, twende na ramani zile za vijiji ambazo zilimfanya *TAMISEMI* asajili kile kijiji. Au twende na ramani inayoonyesha kabisa Kata ya Mchombe mwisho wake wapi na Kata ya Chita inanzia wapi? Haliwezi kutushinda hilo, lakini hawa waliofanya ramani hii kiuficho uficho watafutwe tuone walitumwa na nani kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamekwenda watu wengi sana, amekwenda Mheshimiwa *Prof.r* Kapuya, alipokuwa Waziri wa Ulinzi, aliporudi akaniambia aah, bwana Ligalama, tatizo ni watu wako bwana. Lakini wote wanaishia Jeshini, hawaendi kwa wanachi. Akaenda ndugu yangu Yussuf Omar Mzee, tena huyo tuliongeanaye akiwa Morogoro, nakuomba ukishakwenda Jeshini nenda na kwa wananchi uwasikilize. Amekwenda *CDF* ndio amekwenda mara ya mwisho, lakini maamuzi yaliyokuja sasa wale wakiri kwamba ardhi hii wamevamia ardhi ya Jeshi na ingawa cheti wanacho. Cheti cha usajili wa ardhi yao wanacho na ni sheria ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina imani kabisa kama Mheshimiwa Waziri atatupatia ufumbuzi katika majumuisho yake atalisemea au la sivyo tuunde Tume, ili twende kule tukahoji pande zote mbili na bahati nzuri wale waanzilishi wa vijiji hivi, watendaji wa mwanzo kabisa miaka ile ya 1975 wapo hai, watakuwa wa msaada mkubwa katika kutatua tatizo hili mara ya mwisho. Wananchi wakinyang’anywa ardhi yao wakitaka kuilima, walikuwa wanachajiwa pesa kulipa Jeshi, Nyarubanja *system*. Ardhi yako; yaani uthibitisho ni kwamba ina minazi, ina mazao ya kudumu, michikichi, miembe, kweli hawa wamevamia Jeshi? Jeshi limekuja kupanda miembe hii kama sio



kuwapora tu? Kwa hiyo, hili linaleta sura mbaya, linaleta chuki ya watu kwa Serikali yao bila sababu na ni jambo rahisi sana kulitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niishie hapo na nina imani kabisa Mheshimiwa Waziri utalichukulia kwa uzito wake suala ili wananchi wangu waishi maisha mazuri na wazalishe chakula bila kuwa na wasiwasi kwamba leo watafukuzwa katika sehemu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusu ardhi. Nilitoa tahadhari wakati Waziri wa Kilimo anatoa bajeti yake kuhusu shamba ambalo Rubada wameingia mkataba na mwekezaji toka nchi za nje. Pamoja na kwamba Waziri, Mheshimiwa Stephen M. Wasira, alijibu kwamba mapendekezo mliyokubaliana na Rubada ndiyo hayohayo, wananchi wale wakaambiwa wanapewa muda mpaka Oktoba, waondoke, kijiji cha asili! Mimi Baba yangu amezaliwa kule mwaka 1922, waondoke waende wapi? Napenda sana suala la uwekezaji lakini napenda sera ya uwekezaji kwa maana kwamba ni uwekezaji shirikishi siyo kufukuza wenyeji, uwekezaji shirikishi unitoe mimi ambaye umenikuta halafu uje uwekeze? Hiyo sikubaliani nayo, siyo dhana ambayo mimi naiunga mkono hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge hili na kupitia Waziri wa Ardhi, naomba wananchi wasibughudhiwe. Wananchi wa Kitongoji cha Mbasa katika Kijiji cha Lukorongo, tumewaambia wale wa Rubada, tafuteni eneo sehemu nyingine, pori, wapeni hawa fidia lakini wale hawawezi kutoka pale, ni kijiji chao cha asili, wamesumbuliwa mwaka 1974 kwenda kulinda reli wanarudi nyumbani kwao wanaambiwa tena waondoke, waende wapi? Kwa hiyo, hili hatutakubali kama ni uwekezaji wa namna hii basi yatakuwa mambo ya Kapunga tena hayo na tusingependa tufike huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanatoa ushirikiano mkubwa, tumekubaliana hapa mbele ya Rubada, wanakwenda wanaitisha mkutano wanawapa siku, jana waliniipigia simu wakasema kwamba kilimo kile cha kiangazi ambacho huwa tunalima kwenye mabonde yale yenye unyevu, hawatalima mwaka huu kwa kuogopa kwamba wakilima Rubada itachukua. Lakini kwa nini tufike hapo? Yaani tuwathamini zaidi wawekezaji? Mimi nakubaliana kwamba uwekezaji ni namba mbili lakini kwanza mwananchi lakini kama tukiwa na dhana tofauti juu ya uwekezaji basi afadhali hata tuache uwekezaji. Mwananchi awe mtu wa kwanza akishatimiza masharti yake na ndiyo nilikuwa najua wanakuja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa anafuata Mheshimiwa Prof. Idris A. Mtulia, Mheshimiwa Charles Keenja na Mheshimiwa Felister A. Bura, wajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika hoja iliyo mbele yetu.

Awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara hii, Waziri wake Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Katibu Mkuu, Mama Salome, Kamishna na Wakurugenzi wote pamoja na Watumishi wote wa Wizara hii, kwa kutuletea hotuba hii nzuri ambayo inaleta matumaini ya kupunguza kero na kasoro nyingi za wananchi kuhusiana na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamjua Mheshimiwa Waziri Capt. John Zefania Chiligati, yeye ni mchapakazi motomoto, muadilifu na hana majungu. Ninawaomba watumishi wote wa Wizara hii, wamuunge mkono ili alete mabadiliko yanayostahili, ya kuleta heshima kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali, ardhi ni kila kitu. Niruhusu kidogo ninukuu mstari mmoja tu wa aya moja ya Qurani Takatifu inayozungumza juu ya ardhi na hii ni:-

*“Surat-l-jumaa, Bismillah Rahman Rahim, Faidha kudyat swalaa fantashiru fil ardhi”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasema mkimaliza kuswali nendeni mkatafute riziki zenu katika ardhi, ardhi ndiyo nafaka, ndiyo mazao tunayouza, ndiyo miti tuliyokalia, ardhi ni kila kitu yaani ni mtambuka na kumpata Mheshimiwa Capt. John Chiligati pale, nadhani mambo yetu yatanyooka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, tumemtwisha mzigo mkubwa sana huyu bwana maana hana Naibu Waziri halafu anatakiwa huyu Bwana apime mipaka yote ya Tanzania, apime vijiji vyote, miji midogo ya Wilaya, miji ya Mikoa, Majiji, kisha apime bahari, atoe ramani, hati za vijiji, za mtu mmoja mmoja, lakini pesa hizi ni finyu mno, tusijidanganye. Ninapiga maneno na kelele kubwa, naomba Serikali ikubali, ametwisha mzigo mkubwa bila kumpa nyenzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo nakuomba kidogo nitoe nukuu ya Sir Winston Churchill awinzon Church katika Vita ya Pili ya Dunia, aliwaambia Wamarekani:

*“Give us the tools we shall do the job”* Tupeni nyenzo Marekani tupigane vita hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali itoe nyenzo na kumpa Mheshimiwa Capt. John Chiligati ili Wizara yake ifanye kazi. Bila hivyo, tutakuwa tunajidanganya kwamba tunakuwa na mipango miji, hii hadithi itakuwa hivyo hivyo kwamba akija atafanya hivyo na mwingine atafanya hivyo hivyo, waliopita watafanya hivyo hivyo, hakuna maendeleo. Maendeleo ni kuamua. Nini maana ya maendeleo? Maendeleo ni miji, miji midogo, vijiji vyenye nyumba nzuri, hayo ndiyo maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, hakuna mtu atakuwa mstaarabu kama hana nyumba nzuri, mifereji ya kutolea maji machafu (*disposals*). Nawaombeni mnaofanya kazi Wizara hii mjue kuwa mna dhamana kubwa kweli kweli katika maendeleo ya nchi hii na ustaarabu wake. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ikubali hilo na bajeti iongezwe mara dufu yaani mara mbili ya bilioni 27 ili sasa akishindwa kazi tunamwambia Bwana Waziri uadilifu wako na uchapakazi wako uko wapi kwani fedha tumekupa hujafanya kitu umetuangusha, lakini bila hivyo nadhani tutajidanganya kwamba tuna Wizara itakayoleta ustaarabu na maendeleo wakati hatuipi pesa ya kutosha. Naomba sana Wizara hii ipewe fedha ya kutosha ili ifanye kazi na kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tukubali kufikiri kama wenzetu miji mingine mikubwa duniani wanavyofikiri kwamba mji ukijaa sana *over crowding*, majiji haya yana *slams, shanties* yataendelea hivyo hivyo, hakuna *sewerage system*, barabara nzuri, hakuna namna ya kufanya *emergence services* kwa mfano kama moto ukitokea, utapitisha wapi gari la zima moto? Hakuna! Wanafanyaje wenzetu? Wenzetu wanaangalia nchi yao yote ile kwa mfano sisi tuna Wilaya, zile Wilaya ndiyo unajenga nyumba za bei nafuu katika Wilaya zile na bwana umeme, namuona ndugu yangu Mheshimiwa William Ngeleja yupo pale, anapeleka umeme katika vijiji na miji ile, viwanda vidogovidogo vinazuka kule, utakuta *population* yenyewe inaondoka kukataa hali duni ya kuishi katika *shunts* za Manzese kule warudi katika miji waliyozaliwa au hata hawakuzaliwa lakini ina nafuu wa nyumba nzuri, ina *sewerage system*, barabara, taa na viwanda vidogovidogo na wakulima wanaweza wakawa na *processing industries* za mazao yao kulekule walipo, hiyo unakuwa kama unatapisha miji mikubwa yote, unaondoa *over crowding* ili upate nafasi ya kujenga miji mikubwa au majiji yenye heshima na hadhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watauliza tu, fedha zitatoka wapi? Jamani! Dunia imeshabadilika, huwi tajiri mpaka ukope, tuingie katika mpango wa *Sovereign Guarantee System* ambayo nchi kama hii inaweza kutathminiwa na kupewa hii *guarantee*? Ikitathminiwa na ikipewa *Sovereign Guarantee*, inaweza ikakopa fedha nyingi, ikajenga nyumba za bei nafuu. Mheshimiwa Capt. John Chiligati msisahau Wilaya ya Rufiji hasa pale Utete, zinatakiwa nyumba nyingi kwani wafanyakazi wanapata taabu sana ya kupata nyumba. Jenga kule ukishajenga, hawatakaa bure, watalipa *rent* na wewe utalipa mkopo wako kule ulikochukua *katika Sovereign Guarantee, it is possible my brother. Tell the Government*. Tunaiambia Serikali sasa twende katika mpango huu watu wa mahesabu, watu wa *economics* wanajua maana ya *Sovereign Guarantee* inavyoweza kubadilisha nchi katika kujenga *infrastructure* yenye *humanitarian nature* kama ilivyo *infrastructure* ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisamehe, nirudi Rufiji kidogo. Naomba nisifu Wizara hii kwa kupima vijiji vya Rufiji vingi sana lakini haijamaliza hiyo kazi kwa sababu bado hatujapata hati. Ninaomba vijiji vya Rufiji vipatiwe hati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini isitoshe kuna kasoro zimetokea, wapimaji hawa sijui walikuwa na haraka sana basi kuna migogoro ya mipaka kati ya kijiji na kijiji. Mimi Mbunge nimesikiliza maneno yale, nakuarifu Mheshimiwa Waziri, uiamrishe Wizara

yako, ikabadilishie mipaka ile kwa sababu italeta vurugu kubwa kabisa hasa sisi ambao tunapata huluwa na kazi kwa ajili ya kura. Hao wapiga kura hawana raha hata kidogo na ninaomba nivitaje. Kijiji cha Ikwiriri na kijiji cha Nyamwage kuna matatizo ya mpaka, kijiji cha Mbunju Darajani na Ruwe kuna matatizo ya mpaka, kijiji cha Mbunju Mvuleni na Mpima (Mgomba) kuna matatizo ya mpaka, kijiji cha Chumbi na kijiji cha Mbwara kuna matatizo ya mpaka, kijiji cha Bungu na Kijiji cha Upunda kina matatizo ya mpaka, Mchukwi na Kibiti “A” kuna matatizo ya mpaka. Kwa kuwa, kazi nzuri imeshafanywa kupima vijiji karibu 98 vya Rufiji ila hivi 10 tu, naomba uwatume hawa jamaa wakamalize hii kazi mara moja ili shida, ugomvi na migogoro ya mipaka ya vijiji hivyo uimalize mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ucheleweshwaji wa kutoa Hatimiliki. Bunge lako hili lilipitisha Sheria ya Ardhi, Na.4 na 5 ya mwaka 1999 ambayo imesema waziwazi kwamba Hatimiliki ni haki itolewe kwa wakati, *‘justice delayed is justice denied’* hayo ndiyo mafunzo ya hapa. Sasa anapokuja Waziri kutuambia kwamba sasa hivi nataka kupeleka utoaji Hatimiliki katika Kanda, huu ni ukombozi. Naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri maana ni ukombozi mkubwa, utaondoa kero nyingi na watu wataisifu Wizara yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijakaa, naomba hili jambo moja la mwisho la *speech* yako nzuri hii na mambo uliyotuahidi uyasimamie, hasa hasa utoaji wa Hatimiliki kwa wanaostahili, ukishafanya vizuri, itakuwa *legacy* na watu watasema kwamba alikuja hapa Mheshimiwa Capt. John Chiligati, aliyepeleka utoaji wa Hatimiliki katika Kanda na tumepata Hatimiliki hizo kwa haraka sana. Hili jambo litabaki pale na ni alama nzuri ya uongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Bahati mbaya Mheshimiwa Susan Lyimo amemsindikiza Mheshimiwa Grace Kiwelu ambaye amefiwa na Kaka yake. Kwa bahati mbaya pia Mheshimiwa Willson Masilingi amefiwa na Mke wa Kaka yake, kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Charles N. Keenja atafuatiwa na Mheshimiwa Felister A. Bura na Mheshimiwa Riziki O. Lulida ajiandae.

**MHE. CHARLES N. KEENJA :** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hotuba hii muhimu sana kwa maendeleo ya miji na nchi yetu kwa ujumla.

Kwanza nianze kama walivyofanya wenzangu kwa kumpongeza sana Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa hotuba nzuri sana waliyoandaa, iliyopangika vizuri sana na yenye maelezo mengi fasaha. Tunawapongeza sana na baada ya kufanya kazi hii nzuri tunategemea miaka ijayo, wataendelea kufanya kazi nzuri kama hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri amekaa katika Wizara hii kwa muda mfupi sana lakini tumeanza kuona utendaji wake mzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza alilofanya, ni kujenga mawasiliano kati yake na Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba mambo yanayofanywa na Wizara yanaeleweka katika Serikali za Mitaa. Ukisoma hotuba hii, unaona mambo mengi sana mapya ambayo yanafanyika ikiwa ni pamoja na kuanza sasa kutoa hati za kumiliki ardhi kwenye Kanda. Tunampongeza na tunamshukuru sana kwa hizi kazi nzuri anazofanya na tunamuomba aendelee kuzifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wetu wa Dar es Salaam, tulikuwa na tatizo pale Luguruni, lililotokana na uthamini wa mali za watu waliotakiwa waondoke katika eneo lile ili kupisha mpango wa kuanzisha vituo vya huduma katika eneo lile. Nashukuru, katika hotuba hii, Waziri anatuambia kwamba tatizo lile limekwisha. Wananchi wale sasa wanalipwa fidia na wakishalipwa fidia anasema, wataondoka. Sasa tatizo langu ni kwamba wataondoka kwenda wapi? Kwa hiyo, ninamuomba ajibu hilo swali pia kwamba atawapatia mahali watakapokwenda, yaani atawapatia viwanja ili waende wakajenge wapate mahali papya pa kukaa. Lakini nashukuru sana kwamba tatizo lile limemalizika na wananchi sasa wanaweza wakaishi kwa amani katika nchi yao na kuendelea kuiamini Serikali na Chama cha Mapinduzi, nakushuru sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ushughulikie pia suala la eneo lile lililotengwa kwa ajili ya kujenga Chuo Kikuu cha Sayansi za Tiba linaloanzia Kwembe linapita Kisopwa linazunguka mpaka linakaribia kurudi barabarani. Tumekwenda pale na Mkuu wa Wilaya kuzungumza na wananchi, tukawaeleza faida za kujengwa kwa Chuo Kikuu pale pamoja na hospitali ya kufundishia. Tukaelekea kukubaliana na baadhi ya wananchi lakini wakatokea wachache wakorofi kweli kweli wakafanya ukorofi kwenye kikao kile na ambao umeendelea mpaka leo. Lakini Serikali imekubali kulipa fidia na mimi nashukuru sana Serikali kwa uamuzi huo. Naomba Mheshimiwa Waziri hii fidia ilipwe, hii mipaka ya eneo hili ionyeshwe waziwazi na mipango ya kuendeleza eneo hili iendelee. Nilimsikiliza Mheshimiwa Rais akizungumza alipokuwa Tanga, nikasikitika sana kwa sababu siyo tatizo lililotakiwa lifike juu mpaka kwa Rais. Hili ni tatizo ambalo kwa kweli, tulitakiwa tulimalize katika ngazi zetu za Kata, Manispaa na tukiongozwa na Wizara yako, naomba hili nalo tulimalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale pana tatizo lingine lililofichika ambalo naomba nalo ulitazame, nalo ni mpaka kati ya Kisarawe na Kinondoni. Katika eneo la Kwembe, pana utata pale. Unapata viongozi kutoka Kisarawe wanadai kwamba ndiyo wanahusika na eneo lile, unapata Viongozi kutoka Kibamba wanasema nao wanahusika na eneo lile na kinachotokea ni matatizo. Kwa hiyo, naomba suala hili lishughulikiwe na likamilishwe mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka yote niliyokaa hapa Bungeni, nimekuwa nazungumzia umuhimu wa kuandaliwa kwa mpango wa kuendeleza jiji la Dar es Salaam na miji mingine ya Tanzania. Unasema 70% ya miji yetu haikupangwa. Katika jiji la Dar es Salaam tunakaribia 100%. Hali ya Dar es Salaam ni mbaya, eneo letu kubwa sana

halikupangwa. Huwezi ukamuelekeza mtu akufuate mahali popote Dar es Salaam kwa sababu hatuna barabara, kila mtu amejenga katika eneo alilonunua kwa mtu aliyedai kwamba ndiye anamiliki eneo hilo. Huwezi kufika mahali popote Kimara, kwa mfano ambayo ni Kata moja kubwa na yenye watu wengi sana lakini kila mtu kakaa alivyokaa. Ukiagiziwa kwa mtu ukafika basi una bahati ama una akili za kipekee za kijiografia. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba mwaka kesho tutaanza kuandaa *Master Plan* ya Jiji la Dar es Salaam na miji mingine na ninaomba kazi hii ifanyike kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba pamoja na kufanya kazi ya kuandaa *Master Plan* ya jiji la Dar es Salaam, tuangalie vilevile miji inayozunguka Dar es Salaam inaendelea vipi kwa sababu Dar es Salaam haitaweza kuendelea kama jiji peke yaani kama *a stand alone entity*. Jiji la Dar es Salaam lina *influence* kubwa sana kwa ukuaji wa Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Bagamoyo na kadhalika na ninafikiri kama tunataka kuandaa mpango mzuri wa kukua kwa jiji la Dar es Salaam, ni lazima tuangalie vilevile hii miji mingine midogo inayozunguka jiji la Dar es Salaam nayo inakua namna gani ikiwa ni pamoja na kwamba jiji la Dar es Salaam linakua kuingia katika maeneo yaliyopo nje ya Mkoa wa Dar es Salaam. Kwa mfano, ukielekea Kusini kama unakwenda Mkuranga, jiji la Dar es Salaam limeshavuka mpaka wake na liko katika eneo la Mkuranga sasa hivi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia kwamba haya maeneo nayo tunayapanga ili yaendelezwe vipi. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumefanya vizuri sana, tusipofanya hivyo, tutaendelea kuwa na haya matatizo tuliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mambo ambayo Mheshimiwa Waziri anazungumzia katika hotuba yake, ni udhibiti wa uendelezaji wa maeneo ya jiji na miji mingine Tanzania na anasema katika hotuba yake kwamba hali ni mbaya, kwamba miji yetu kutokana na kukosekana kwa udhibiti huo si salama. Sasa sidhani kama inatosha kusema hivyo, sidhani kama inatosha kusema hali ni mbaya, udhibiti ni mbaya halafu ukakaa kimya, lazima Mheshimiwa Waziri tuongeze hatua inayofuata kwamba ni hatua gani tutakayochukua kusitisha hali hii iliyopo na kurudi nyuma kurekebisha hali ambayo imesharuhusiwa kuwepo na mimi nafikiri kwamba Wizara hii ina wajibu wa kusimamia Halmashauri ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake ipasavyo na kwamba zinaepuka kuingia katika matatizo haya ambayo yanaendelea sasa hivi. Haitoshi kusema kazi ya kudhibiti ukuaji na uendeleaji wa maeneo haya ni jukumu la Serikali za Mitaa, haitoshi, ni lazima Serikali Kuu ikubali kwamba ina jukumu la kuzisimamia Serikali za Mitaa ili zitekeleze wajibu huo na ziutekeleze kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Dar es Salaam, baadhi ya maeneo unapata hati inasema ni kwa ajili ya jengo moja kuu na majengo mengine ya kusaidia, ukienda unakuta yamejengwa maghorofa sita au saba, yaani majumba mengi yamewekwa katika kiwanja kile ambacho kinatakiwa kiwe na jengo moja halafu tunakutana barabarani tunalalamika kwamba hali gani hii mbona mbaya? Sasa kwa nini hatuchukui hatua za kuidhibiti na kuisimamia na kuhakikisha kwamba inarekebishwa?

Mheshimiwa Halima Mdee hapa, amezungumzia juu ya maeneo ya huduma yanayomewegwa na kutumika kwa shughuli ambazo hazihusiani na utoaji wa huduma na tuna tatizo kubwa sana sasa hivi la maeneo ya kujenga shule, hospitali na kadhalika kwa

sababu maeneo yaliyotengwa yalibadilishwa yakawa ni maeneo ya makazi na huwezi kubadilisha eneo kutoka matumizi yake yaliyokusudiwa lilipopimwa kwenda katika matumizi mengine bila kibali cha Wizara. Sasa naomba Wizara ikubali kwamba inawajibu, ikishirikiana na TAMISEMI, kusimamia Serikali za Mitaa, kuhakikisha kwamba hali mbaya hii iliyopo inaacha kuwepo ama sivyo miji tunayojenga Tanzania ni miji ya ajabu kwelikweli na siamini kwamba kuna nchi nyingine yenye miji kama ya kwetu yaani miji ambayo haina barabara, huwezi kujua ni wapi utakapopitisha bomba la maji, nyaya za umeme kwani kila mtu kajijengea kama alivyoona inafaa. Ninafikiri hapa tulipofika tungsimamisha sasa ujenzi huu holela, tujirekebishe ili tuanze kujenga kwa mipango iliyoandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilifanya kazi nzuri sana ya kupima viwanja 20,000 na tukatangaziwa hapa Bungeni, tukapiga makofi, tukafurahi kabisa. Sasa naomba nijue tangu tupime vile viwanja 20,000 tumeshapima vingapi zaidi? Ama tulipima 20,000 halafu tukakaa tukaona inatosha? Tungeendelea kupima viwanja kwa wingi zaidi, tungeendelea kuanzisha “*satellite town*” hizi kama tunazotaka kuanzisha Luguruni na kwingine kwa wingi zaidi kwa sababu vile viwanja tukipima atakayepewa hicho kiwanja atalipa gharama za kukipima mpaka kukifikisha hapo kinapotakiwa kifike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri tuendeleo na kasi ileile ya kupima viwanja katika miji yetu yote ili miji yetu ianze sasa kupangika maana ukimwambia mwananchi asubiri mji upangike wakati hakuna mahali atakapopata kiwanja unamdaganya. Kiwanja cha kupanga hawezi kupata lakini anaweza akapata kishamba kutoka kwa mzee fulani akajenga hapo kibanda chake akakaa, kwa hiyo, miji yetu itaendelea kuvurugika kama upimaji wa viwanja hautaharakishwa. Mimi ninaomba sana ifanyike mipango maalum ya kuhakikisha kwamba vinapimwa viwanja vya kutosha katika miji yote na wananchi wanaweza wakavipata kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii habari ya kupata kiwanja halafu inachukua miaka kupata hati, ni jambo ambalo linaweza kurekebishwa na Wizara ilionyesha kwamba inaweza kurekebishwa katika viwanja hivi 20,000 kwa sababu ulikuwa ukipata kiwanja ukienda Wizarani ukishalipia anapata hati yako bila usumbufu. Sasa utaratibu huu mzuri tuliofanya tungeendelea nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuendeleza upya miji yetu. Miji yetu ina maeneo ambayo yamechakaa, maeneo ambayo yamezeeka, yanatakiwa kuendelezwa upya na ninafikiri kuna haja ya kuandaa sasa mipango ya kuhakikisha suala hili linafanyika ili tusipate matatizo tunayopata Kariakoo sasa hivi, maana Kariakoo inaendelezwa na wawekezaji kwa kufuata vichocho vile vyembamba vilivyokuwa vimewekwa wakati watu waliokuwa wanakaa pale ni wachache bila kufikiria maji machafu yatakayotoka katika eneo lile yatahudumiwa namna gani. Kariakoo itafika siku mtu ukiingia na gari utashindwa kutoka kwa sababu ya msongamano wa magari katika eneo lile na majengo makubwa sana yaliyopo. Sasa tusiruhusu likaendelea Ilala, Magomeni na maeneo mengine tuanze kufikiria tunafanya nini ili kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ili kuwawezesha wananchi kujenga, imezungumzwa hapa kwamba huwezi kujenga nyumba kuanzia msingi mpaka ukamaliza bila mkopo. Zamani tulikuwa na Benki ya Nyumba, naamini ikahujumiwa ikafa. Tunaomba Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha benki nyingine ya nyumba itakayokopesha wananchi wanaotaka kujenga, bila mikopo hiyo, tutapata matatizo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Wizara iangalie katika ujenzi mijini, tunatumia *regulations* ambazo zimeandaliwa maalum. Tanzania hakuna mji hata mmoja wenye *Building Regulations*, hakuna! Kwa *Dar es Salaam Building Research Unity* wakati ule lakini sasa hivi ni *Agency*, walikuwa wameanza kuandaa rasimu ya *Building Regulations*. Ile rasimu haikukamilika, naomba Mheshimiwa Waziri ufuatilie rasimu ile, uitazame, irekebishwe, iwekwe sawa ili tuwe na *Building Regulations* zitakazotawala ujenzi mijini. Pamoja na hilo basi tuwe na Benki ya Nyumba itakayotuwzesha kupata mikopo ya kutuwzesha kujenga na kujenga kwa utaratibu unaofaa. Bila mikopo, hatutaweza kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa nisipigiwe kengele ya pili. Naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na sasa nitamwita Mheshimiwa Felister Bura halafu kwenye *list* yangu Mheshimiwa Riziki Lulida atakuwa wa mwisho. Kwa hiyo, tutakuwa na dakika kama 30 ambazo hazina mwenyewe. Mheshimiwa Felister Bura, karibu!

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Lakini kwanza nimshukuru Mungu kwa upendo wake na kwa ulinzi wake katika maisha yangu ya kila siku na kwa kuniwezesha kuwahudumia vizuri wapiga kura wangu wa Mkoa wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kazi kubwa anayoifanya kwa sababu yeye huyo huyo ni Katibu Mwenezi wa Chama cha Mapinduzi na ni Waziri asiye na Naibu wake. Lakini pamoja na hayo, ameonyesha umahiri mkubwa katika kufanya kazi zake za Chama na pia za Serikali kwa ujumla. Kwa hiyo, nampongeza sana Waziri, Mheshimiwa Capt. John Chiligati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana, Dada yangu Mama Salome Sijaona, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara ya Ardhi kwa sababu tumeona juhudi zake tangu aingie Wizara hiyo pamoja na kwamba katika kazi huwezi kukosa changamoto mbalimbali lakini tunaona juhudi zake anazozifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa kuona umuhimu wa kuanzisha na kusimamia mfuko wa kuwakopesha wananchi kujenga au kununua nyumba. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana kwa sababu wananchi wengi hawana uwezo wa kujenga nyumba, wafanyakazi wengi hawana uwezo wa kujenga nyumba na ushahidi tunauona kwa wale wanaostaafu, wengine wanastaafu hawana makazi. Zile pesa wanazopata kwa ajili ya kustaafu ndiyo wanazotumia katika ujenzi wa nyumba na matokeo yake baada ya miezi sita mtu anapururuka kama vile hakuwahi kufanya kazi katika Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliona hili na namwomba lifanyike haraka ndani ya mwaka huu wa fedha ili wale ambao wanakaa *National Housing* au wale ambao hawakai *National Housing*, waweze kukopa fedha kwa ajili ya kujenga makazi au kununua makazi. Amesema kwamba wale ambao wanaishi katika *flats*, nadhani ni *flats* za *National Housing*, wataweza kununua nyumba hizo na wakawa wamiliki wa nyumba badala ya kuwa wapangaji. Mheshimiwa Waziri, nampongeza sana na namuomba Mungu atimize malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 44, ameongelea pia lengo la mwaka wa fedha uliopita, 2007/2008 kwamba, alipanga kupima viwanja elfu ishirini katika Mkoa wa Dar es Salaam, lakini cha ajabu Wizara hii ikapima viwanja elfu moja tu kama inavyosomeka katika hotuba ya Waziri na akapima viwanja mia tano Mwanza, Kibaha, viwanja mia tano na Bagamoyo akapima viwanja elfu mbili na mia tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba Wizara hii iliomba pesa kwa ajili ya kupima viwanja elfu ishirini na kama hawakuomba fedha basi walitegemea kupata msaada mahali fulani ili wapime viwanja elfu ishirini Dar es Salaam lakini badala yake wakapima viwanja elfu moja tu. Naomba huku kupima viwanja nusu nusu isivyotarajiwa katika bajeti ndiyo inayoleta uvamizi katika maeneo ya mijini na ndiyo maana wananchi wanajenga holela lakini baada ya wananchi kujenga holela ndiyo Serikali hiyo hiyo inakuja kuwabomolea nyumba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili pia limetupata hata sisi wa Mkoa wa Dodoma, wananchi baada ya kusubiri kwa miaka mingi wapimiwe viwanja, wakaamua kujenga kwa sababu fedha zao ni za kudunduliza. Kwa kuwa wanapata fedha kwa kudunduliza, mtu anaona bora ajenge nyumba ya kuishi na watoto wake lakini Serikali inapokuja kupima viwanja watu hao wanabomolewa nyumba zao, hawana uwezo wa kujenga tena, hawalipwi fidia kwa sababu wamejenga kiholela. Naiomba sasa Wizara hii kama imepanga kupima viwanja ishirini, wapime hivyo hivyo ili wananchi wanunue kwa sababu fedha hizo zitarudi si kwamba hazitarudi, zitarudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Dodoma, tuna kilio kikubwa kutokana na *CDA* kutopima viwanja kwa wakati, watu wanabomolewa nyumba zao, hawalipwi fidia, wanabaki wanatulalamikia viongozi wao, namuomba Mheshimiwa Waziri alizingatie suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesema kwamba ana Mfuko katika Wizara yake kwa ajili ya kukopesha Halmashauri, *CDA* hapa hawana Mfuko huo, nakumbuka

waliomba Sh. 20m/= wakaambiwa hawastahili. Sasa ili kujua kwamba hawastahili basi wajibiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kujua kwa nini *CDA* hawastahili kwa sababu wanapima viwanja kwa wananchi wa Tanzania! Naomba kujua kwa nini *CDA* hawastahili kupewa mkopo wanaopewa Halmashauri zingine. Serikali siku zote hazina pesa na *CDA* siku zote hawana fedha kwa ajili ya kupima viwanja pamoja na matatizo waliyonayo *CDA*, lakini nao wanasema hawana fedha za kutosha kwa ajili ya kupima viwanja. Serikali iangalie namna au uwezekano wa kuwakopesha hawa *CDA* ili wapime viwanja kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Mporogomyi ametoka kulalamika muda si mrefu, kwamba kiwanja chake kimegawiwa kwa mtu mwingine lakini sababu aliyopewa anajua mwenyewe. Naomba Wizara iangalie namna ambavyo *CDA* nao wanaweza kupata mkopo huu kwa sababu ni mkopo wala si fedha zinazotolewa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niliposoma hotuba ya Waziri, ukurasa wa 46, nikakuta kuna mipango ya uendelezaji wa miji na vijiji na nikafurahi kwamba katika mpango huo mji wetu wa Kibaigwa upo katika mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Kibaigwa unajengeka kwa kasi ya ajabu. Wafanyabiashara wapo pale wengi lakini cha ajabu kila mtu anajenga anavyojua, hakuna mitaa, maeneo ya wazi, viwanja vya michezo, hakuna shule, lakini Maafisa Mipango Miji wapo, hivi wanafanya kazi gani hawa watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 50, napenda kunukuu ili aone alivyolalamika tu lakini hatua za kuchukua hakusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kunukuu, anasema:-

*“Hali ilivyo katika usimamizi na udhibiti katika miji yetu hairidhishi. Majengo mengi yanajengwa bila vibali vya ujenzi, bila kuzingatia matumizi ya ardhi na kadhalika, hii inafanya miji yetu isiwe mahali salama pa kuishi”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amelalamika tu lakini mikakati ya kutoka hapo ili wananchi wasiendeleo kujenga majengo yasiyoridhisha, ili wananchi wazingatie matumizi ya ardhi. Hili halikuzungumzwa, sana sana amesema kwamba, Halmashauri wakachukue mikopo katika Mfuko ambao upo katika Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wale Maafisa Mipango Miji ambao hawazingatii utaratibu, wameachwa tu, yaani uzembe unaonekana lakini wameachwa tu, Serikali inalalamika lakini hawana la kuwafanya. Nadhani sasa Serikali iwe *serious* kwa watendaji wake, anayepuuzia kazi, achukuliwe hatua za kisheria, kazi aliomba mwenyewe na asipopata mshahara analalamika, asilalamike kwa kudai mshahara,

mtumishi alalamike baada ya kutimiza wajibu wake. Naomba sana mji mdogo wa Kibaigwa uangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mji pia unainuka pale Mlali katika Wilaya ya Kongwa. Basi Wizara hii iangalie namna ya kuendeleza ule Mji kwa kupanga miundombinu katika Miji hiyo midogo niliyoitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Wilaya ambazo ni mpya katika Mkoa wa Dodoma. Tuna Wilaya ya Chamwino, Bahi, kama Serikali haitasimamia kupanga Wilaya hizo, kutakuwa na *squatter* chungu nzima, wananchi wataendelea kujenga kiholela, hawatafuata matumizi bora ya ardhi kwa sababu hakuna anayesimamia. Naiomba Wizara hii kwa kushirikiana na Maafisa Mipango Miji kule waliko wasimamie hasa Wilaya hizi mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa Serikali ilitenga Wilaya kama sita sikumbuki vizuri, mpya kabisa ambazo zinatakiwa ziwe na muundo mzuri na usimamizi katika kupanga miji yetu, isiwe kama ilivyokuwa Dodoma kwa sababu Dodoma tulikuwa na mpango mzuri wa kujenga na kuendeleza Mji wa Dodoma lakini mpango huo haujatekelezwa mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango ule ulionyesha Ofisi za Mabalazi ni wapi, Ofisi za Serikali ni wapi, maeneo ya wazi ni wapi lakini kama alivyosema Mheshimiwa Aziza, mpango huo ukatekelezwa Abuja. Naomba mipango ya Wilaya zetu, itekelezwe katika Wilaya husika na siyo nchi za nje kuja kuchukua mipango yetu na kuitekeleza, ni aibu kubwa kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichangie katika upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam. Nimesoma katika hotuba ya Waziri, katika ukurasa wa 48, anasema analipa Sh.10.34bn/= kwa ajili ya kuwahamisha wakazi, nilitegemea kwamba Serikali sasa inategemea uwezekano wa kujenga miji midogo ndani ya Dar es Salaam, wangeweza kujenga miji midogo Bunju au kuelekea Kibaha lakini bado Bandari ni Kurasini, kwani bandari ikiwa Mkoa wa Pwani kuna tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari kavu inaweza kujengwa Mkoa wa Pwani na pia kuna maeneo mengi kama vile kuelekea Tanga, wakaondoa msongamano ndani ya Jiji la Dar es Salaam na hizi Sh.10bn/= ambazo zimetengwa na Serikali zikafanya maandalizi makubwa katika maeneo hayo ambayo yatakuwa yametengwa kwa ajili ya kujenga miji midogo au kujenga bandari kavu nje ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha ajabu ni kwamba, Wizara hii bado inaona kwamba, katikati ya Mji wa Dar es Salaam ndiyo pa kuendeleza, nashangaa kwamba hawasikitishwi na msongamano mkubwa ambao upo Dar es Salaam, magari, watu, maana mtu unatokwa jasho kwa ajili ya pumzi ya mwenzio, Dar es Salaam watu wamebanana kama kuku ndani ya tenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ione namna ya kupanua miji nje ya Dar es Salaam lakini miji itapanuliwa tu kwa kugawa viwanja nje ya Jiji la Dar es Salaam, maeneo yako mengi, Mheshimiwa Christina pale ana maeneo mengi kwa ajili ya upanuzi, kinachohitajika ni viwanja tu vipimwe na wananchi watajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimesoma kwamba, *National Housing* ni Mkandarasi Daraja la Pili lakini Mkandarasi huyu kwa nini asipewe tenda za kujenga majengo ya Serikali? Serikali ina kazi nyingi kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu lakini nimesoma, wanafanya ukarabati na kuingia ubia na Wakandarasi wengine kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba hili ni Shirika la Serikali, ubadhirifu hautakuwepo, watafanya kazi yao vizuri inavyotakiwa na kwa sababu ni Mkandarasi Daraja la Pili, naamini kabisa, wana uwezo wa kufanya kazi za Serikali jinsi inavyotakiwa lakini je, wanapata *contract* za kujenga majengo ya Serikali? Wizara nyingi zinajenga pale Dar es Salaam na nje ya Dar es Salaam pia majengo yanajengwa, hata hapa Dodoma majengo yanajengwa, kwa nini na wao wasiingie kwenye kutenda zabuni za kujenga majengo ya Serikali na ndiyo namna ya kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *National Housing* haitaki kuingia kwenye zabuni na makampuni mengine hawawezi kukua, watabaki hivyo hivyo, pamoja na kwamba wana wataalamu lakini hawa wataalamu wanatakiwa sasa wajishindanishe na makampuni mengine ya ujenzi. Naiomba sana Wizara hii kuhakikisha kwamba Shirika la *National Housing* linaingia katika kutenda zabuni za Serikali ili wapate uzoefu wa kufanya kazi vizuri zaidi, ili wapate uzoefu wa wajenzi wengine ambao wanatoka katika maeneo mbalimbali au makampuni binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara hii ina mambo mengi ya kufanya, kupima vijiji, wanavijiji vingi, nimesoma kwenye hotuba ya Waziri, vijiji vingi havijapimwa lakini bajeti iliyopangwa kwa ajili ya Wizara hii haitoshelezi. Naomba Wizara hii itazamwe kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia leo hii na pia nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Chiligati, kwa kazi anayoifanya katika Wizara hii ambayo ni ngumu lakini nina imani kuwa ataiweza. Napenda vilevile kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara hii, Mama Sijaona, ni mwanamke mkakamavu ambaye nina imani kuwa amejitahidi kuifikisha hapa Wizara hii. Tunaomba Mheshimiwa Rais amwongeze Naibu Waziri ili angalau na yeye aweze kupumua na kufanya kazi kwa umakini zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia katika utoaji wa miliki katika Kanda ambazo zimeorodheshwa. Katika *page* namba 26, ameandika kuwa sasa hivi kutakuwa na Kanda tano ambazo zitakuwa zinatoa Hatimiliki. Lakini naomba kitu kimoja, watuongezee Kanda ya sita ambayo aidha iwekwe Makao Makuu Mtwara au Lindi ili iweze kutuondolea kero ya msongamano wa watu kutoka Lindi kwenda Dar es Salaam, kama tunavyoambiwa Dar es Salaam mji wa wajanja, itakuwa watu wengi wanaotoka Tandahimba wakija hapa wanakuja kuchanganyikiwa, itawawia vigumu, Dar es Salaam waitengenezee Kanda ya peke yake, iweze kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivyo kwa maana, kwa sababu leo kumtoa mtu Ruvuma mpaka afike Dar es Salaam kuja kushughulikia Hatimiliki wakati mtu mwenyewe anatoka kule hali yake ngumu, atakaa Dar es Salaam mwezi mzima bila kufanikisha hivyo itamweka katika mazingira magumu na kumwongezea kero, kitu kidogo kwake kitakuwa ni kikubwa sana. Hivyo, naomba Mheshimiwa Waziri alisikilize hilo neno na kulifanyia kazi ili kuweza kutupatia Kanda nyingine ya sita ili angalau kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie migogoro ya ardhi hasa katika vijiji. Migogoro mingi inayotokea katika vijiji, tukubaliane kwanza kulikuwa na Azimio la Arusha na Ujamaa *Village*, watu kutolewa katika vijiji fulani kupelekwa katika mazingira fulani ili waweze kuwa na mazingira mazuri ya hospitali, shule na vitu vingine. Napenda hizi Wizara mbili ziwe na ushirikiano wa karibu, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Ardhi ziwe na ushirikiano wa karibu ili iwapunguzie kero hasa katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinapitishwa katika vijiji, miji ya watu ambao tayari walishapelekwa pale lakini inapofikia kulipwa wanasema, wewe umeingia katika hifadhi ya barabara. Kwa kweli inaleta masikitiko kwa mtu wa kijijini ambaye hana elimu ya kutosha, hakupewa mafunzo, ni Serikali iliwapeleka pale wanavijiji, leo barabara inapita pale na kumwambia unambomolea nyumba yake bila kumlipa fidia, kwa kweli hiyo ni kero, Serikali iangalie jinsi ya kuwashirikisha wanavijiji ili kujua kero zao na kuweza kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kufikia kujenga nyumba yake kijijini, kwa kweli huyu mtu ame-*sacrifice* vya kutosha sana, hivyo utakapombomolea bila kumwonyesha atakwenda kukaa wapi, kweli hii ni kero kubwa, hivyo hili naomba liangaliwe, baadhi ya wanavijiji waondolewe kero hiyo na wapate fidia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kuzungumzia kwa mfano, kujenga barabara ya kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi, ni hali nzuri ambayo itatuletea mafanikio mazuri lakini je, wale wanavijiji waliobomolewa nyumba zao fidia zao zinakuwaje? Maana mpaka leo ukienda ni kero, ukienda Kilanjelanje unasimamishwa, mama hupiti hapa tupe uhakika wa malipo yetu, ukienda Mandawa pia unasimamishwa, unaambiwa, tunaomba tujue haki zetu, tungeshukuru sana kama Wizara ya Ardhi itashirikiana na Wizara ya Miundombinu ili ziwe na mazingira mazuri ya kujua kwamba watu hawa wanapotolewa wanasaidiwa vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kuzungumza isipokuwa napenda kusema kwamba, ardhi ni uchumi, ardhi ni uhai, leo sisi Watanzania tukiitegemea ardhi yetu tutakuwa tumeendelea na kupata uchumi mzuri kwa mfano Kenya, ardhi yao kwao ni thamani kwa Mkenya asilia, ukienda Uganda vilevile, uchumi wa Uganda umeshikwa na wenyewe Waganda wenye ngozi nyeusi lakini sasa hivi Tanzania ardhi yetu kubwa inachukuliwa na watu ambao sio wazawa wenye ngozi nyeusi, maana yake utafika muda ambapo Watanzania wenye ngozi nyeusi watakuwa wanakaa maporini, matajiri wakubwa watahika sehemu nzuri na kuendelea kuushika uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mfano wa *National Housing*. *National Housing* lilikuwa ni Shirika la Nyumba la Taifa, nia na madhumuni ya Shirika hili, ni kuwakomboa Watanzania wenye hali ngumu wapate makazi bora na maisha bora. Naomba nilizungumzie Jiji la Dar es Salaam, sasa hivi *National Housing* hasa *city centre* imekuwa ni ya watu wachache, watu wachache hao ni Wahindi, Wasomali na Waarabu ndio wanashika hizo nafasi na sasa hivi wamechukua mpaka Oysterbay yote, je, ubaguzi huu unaletwa na nani, ni hawa *National Housing* kwa kuhakikisha kuwa wanawapa wale kipaumbele kuliko wazawa ambao nao wana haki vilevile kama watu wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, limeingia suala la kuingia katika ubia, kama walivyozungumza Wabunge wengine, ubia huu unaingia kwa watu wachache, baadhi walikuwa na makampuni ya kuuza magari, wameacha shughuli za kuuza magari wameingia kununua vile viwanja vyote, nina mifano hai ambayo nitakaa na Waziri nimwonyeshe na nimwambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, wakimgundua huyu mama ni *widow*, basi watamwambia, mama chukua hizi Sh.15m/= ondoka, sisi hii nyumba tumeshampata mbia na vielelezo ninavyo, nitampatia Waziri nikitoka hapa. Halafu yule mbia anajenga nyumba kwa kuchukua mikopo katika benki zetu hizi hizi halafu baada ya pale zile nyumba wewe tena hutakuwa na uwezo wa kuzipangisha na wala hutakuwa na uwezo wa kukodi kwa sababu kwanza, wanasema tunakodisha kwa *dollars* na wanaingia watu wa kabila moja na aina moja, je, huko tunakwenda wapi? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *National Housing* wanataka wabia mbona kuna ubia mkubwa Tanzania? Kuna mashirika kama *NSSF*, sasa hivi naona angalau wanakwenda vizuri katika kujenga nyumba na sisi tunapata mahali pa kulala pazuri lakini haiwezekani *National Housing* kukaa watu wa aina moja, *city centre*, maduka yote ni ya watu hao hao na wanaendelea kuvunja maduka yale na kukabidhiana wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli uvumilivu wa namna hiyo haupo, ifike mahali wawaone Watanzania wenzao nao vilevile wanahitaji kujikwamua kiuchumi. Yale maduka ya mjini na Watanzania wenye ngozi nyeusi wakapange ili wafaidike na hii lakini sio kuwaweka watu wa aina moja, wanaendelea kiuchumi na Watanzania wanabaki kama ni vibarua wao kwa kufanya kazi katika maduka hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na mengi ya kuzungumza lakini kwa kweli hili naliona ni kero, hata leo ukisema jamani naifuatilia nyumba kwa kupitia Mahakama watakwambia mama wewe ni namba moja umepata nyumba lakini watakuhelewesha, wanazunguka kuwatafuta wafanyabiashara watakaowapa Sh.15m/= na kuendelea, wanakwenda kumweka pale, wewe unabakia kuitafuta nyumba, *National Housing* imefikia mahali hapo? Naomba Mama Sijaona, aliangalie lile Shirika na aiangalie mikataba yao ya wabia ili angalau ufanisi uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeiangalia hotuba ya Waziri, ni nzuri sana, lakini kuna baadhi ya mambo ambayo nadhani ni vizuri Waziri atakapokuwa anajibu atuambie anataka kutupeleka wapi kwa maana ya makazi ya miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwanza na Mji wa Dar es Salaam. Ukienda leo Dar es Salaam, wanajenga majengo mengi sana Kariakoo na kule Mijini, ni jambo zuri, lakini sioni katika mipango hii ya ujenzi hakuna anayejadili suala la mifumo ya maji safi na maji taka, suala la barabara, kwa hiyo mifumo yote ya miundombinu ya jengo lile siyo hoja yao, hoja ni kujenga tu, sasa tunaupoleka wapi mji huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri wakati anatumjibu, atuambie anakubali vipi tuendeleo kujenga majengo wakati mifumo ya maji safi na maji taka bado ni ile ile ya nyumba zile ndogo za zamani, tunafanya nini? Hili limekuwa linanisumbua sana nikaona nianze na hilo kwamba umefika wakati sasa tujitahidi mipango hii tuiweke pamoja tunapotaka kuendeleza mji wetu kwa sababu suala la mipango miji ni la msingi sana na makazi ya watu na mifumo hiyo vina mahusiano makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tusije kujaza *skyscrapers* peke yake ambayo mwisho wa siku mvua ikinyesha mji unakuwa ni wa ajabu, watu watatushangaa, karne ya ishirini na moja haiwezekani tuwe na mipango ambayo haiendi pamoja. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ana mkakati gani wa kufanya maendeleo yetu yawe *integrated*, lazima atuambie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nizungumzie Mji wa Kigoma, Mji wote ule ni nyumba za *National Housing*, nyumba zile zimechoka sana. Naomba leo nimwambie Waziri kwamba tunataka kukaa kwenye Halmashauri tuzi-*condemn* kwamba hazifai. Kwa hiyo, nawaomba sasa waanze kufikiria watu wa *National Housing* namna ya kuendeleza Mji wa Kigoma kwa sababu yale majengo yamechoka sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri waanze kulifikiria hili kwa sababu haya ndiyo maendeleo yenyewe. Maana Wizara hii ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

lakini unaona hapa tunaongelea zaidi ardhi. La kwangu ni suala la makazi ambalo ni la msingi sana kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la *National Housing* wengi sana wamelisema. Nataka baadaye Waziri anijibu, ukisoma historia ya kujenga nyumba duniani, maeneo yote ambayo watu walijenga maghorofa sababu ya kwanza ilikuwa ni ku-*minimize space*, hii ndiyo ilikuwa sababu ya msingi lakini *National Housing* wamekuja na *style* ambayo haipo duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo *National Housing* wamejenga maghorofa porini ambako tungeweza kujenga nyumba ndogo ndogo nyingi, ukawasaidia hawa Watanzania, ukiwa unapita barabarani unakwenda Chalinze kuna maghorofa porini, hakuna matatizo ya *space* pale, kwa nini wasijenge nyumba ndogo ndogo nyingi wakawasaidia watu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1970, Mwalimu alijenga nyumba za *National Housing* nchi nzima kwa nini hakujenga maghorofa maana yake kama hoja ingekuwa ni hiyo ardhi, ilikuwepo na ndiyo maana ukienda mpaka leo miji mingi hata hapa Dodoma zile nyumba za *National Housing* bado zina unafuu. Unaona kuna miji ilikuwa imepangwa, nenda katika Miji mingi sana nyumba za *National Housing* zimejengwa lakini leo wamekuja na *style* ya kujenga maghorofa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza haya maghorofa wanayojengwa kwa sababu kuna ardhi kubwa kwa *rationale* ipi? Naomba leo Waziri atujibu kwa nini inakuwa hivi au ni suala la kupoteza fedha, kwa sababu fedha ni nyingi kwa hiyo lazima uzitumie? Inawezekana pia ni *style* kwamba unazo fedha nyingi lakini unajiuliza kama wana uwezo wa kujenga maghorofa hayo huko Wilayani maporini kwa nini kwenye kuendeleza Dar es Salaam, ili Shirika liwe na fedha waingie ubia wakati fedha wanazo, sielewi hapa, kuna *contradiction* hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana unapoingia ubia ni kwamba, mimi nina kiwanja lakini sina fedha nyingi za kujenga ndiyo maana natafuta mtu tufanye pamoja, ni jambo zuri sana lakini kwa *National Housing* tatizo si fedha ndiyo maana waka-*manage* kwenda kujenga porini ambako inawezekana hata watu hawapo, wakakae Makatibu Kata na Makatibu Tarafa, ni jambo jema lakini hivi kweli Makatibu Tarafa na Makatibu Kata wetu wanahitaji maghorofa au nyumba za chini kwa sababu watu wale wanakoishi kule vijijini wanahitaji nyumba za chini, hawahitaji maghorofa. Maghorofa ni ya watu wa mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watu wa *National Housing* watuambie, wameingia mikataba mingi sana na watu na hapa imesemwa, sina tatizo na hiyo mikataba lakini najiuliza inawezekana wana fedha kwa nini wasijenge wenyewe ili waweze ku-*maximize*, wapate *profit* kubwa zaidi wao kama shirika na shirika liweze kuendelea mbele zaidi? (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mimi na dada yangu Aziza mlitutuma tukaenda Abuja. Naomba niseme tuliona *story* ya ajabu sana. Ukifika Abuja ule Mji unasema hii si Afrika ambayo niliitarajia. Lakini tukaenda mbali tukauliza wakasema ni ramani ya Dodoma lakini ukiangalia tulichokiona Abuja na kilicho hapa Dodoma ni vitu viwili tofauti, sasa unajiuliza tatizo letu ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, walituambia kwamba, alikuja Waziri mmoja wa Abuja maana wao ule Mji wa Abuja una Waziri, alivyofika yeye alichofanya alikwenda kutafuta ramani ya Mwanzo ya Abuja akachukua ma-*bulldozer* akaanza kuvunja, hakujali kuna msikitini, makanisa, shule ili mradi vitu ambavyo havikutakiwa kuwepo alibomoa na mji wa Abuja sasa unapendeza, unaona kweli hapa kuna wenzetu wamefanya maamuzi, kuna wenzetu wamefikiria, unajiuliza sisi tuna tatizo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama watu wanakuja wanachukua ramani nzuri kwetu, kwao kunakuwa kuzuri, kwetu ni miji ambayo ukiangalia kila siku haieleweki. Ukiwa unashuka na ndege Dar es Salaam, unajiuliza Mungu wangu karne ya ishirini na moja ndiyo hii na Watanzania hawa hawana tatizo la fedha, maana hii ndiyo nchi peke yake ambayo tunajenga bila mikopo. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni *planning*, watu wa Mipango Miji wanafanya nini? Kazi ya Mipango Miji si kutoa fedha ni kuwaambia tu kama unataka kujenga ndugu yangu jenga kwa mstari huu, hilo nalo linatushinda, jamani haiwezekani kuwa tunakwenda namna hii! Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ana mkakati gani wa kufanya Miji yetu sasa ipendeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa unapita kwenye ndege unaangalia Mji wa Kigoma ukapita Switzerland, ungetamani Switzerland ungeiona Kigoma na ile milima iwe mizuri. Tuna *Lake Tanganyika* pale lakini kila mtu amejenga anavyotaka yeye, anaangalia anakotaka, watu wa Mipango Miji wapo kwa sababu gani na Wizara ipo? Ili mradi mtu anakwenda ofisini na jioni anarudi mambo yake yanakwenda basi, hatuwezi kwenda jamani, umefika wakati tubadilike, Watanzania hawa wanahitaji maisha mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kuwafundisha watu kufyatua tofali vijijini, tusimamie hilo kwa sababu unapoongelea maendeleo ya makazi, tusingalie mijini, twende mpaka vijijini kwetu kuwasaidia watu kwamba unapojenga nyumba yako iwe kwenye mstari huu, hilo tu bado watu wetu wa Mipango Miji hawafanyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka majibu. Nani atatufanyia haya? Matokeo yake ukisoma hii *speech* ya Mheshimiwa Waziri, unaona Waziri naye analalamika kama sisi, ndiyo ninachokiona hapa. Sasa kama Mheshimiwa Waziri analalamika kama sisi, nani atafanya mwisho wa siku na lazima aje na mkakati. Kama mkakati unahitaji kubadilisha Sheria basi tubadilishe ili aende kutekeleza, lakini kama tutakuwa na *society* ya kulalamika inakuwa si sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo, hii ndiyo nchi pekee ambayo tunajenga nyumba kwa pesa za *cash*. Kwa hiyo, lazima tutafute jawabu, *mortgage* ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. *Mortgage Financing* ndiyo itatusaidia hata katika suala la *employment*. Kwenye Ilani ya Chama chetu tumesema tutaleta ajira milioni moja,

tukianzisha *Mortgage Financing* ajira milioni moja ndani ya miaka miwili itakuwa imepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili huoni kama ni jambo ambalo watu wanalishabikia hivi, inaonekana ni sawa tu, ili mradi watu wanajenga nyumba zao wanalala, *no one is concern*, hatuwezi kuongoza *society* ya namna hii! Kwa hiyo, tunaomba sana Waziri na watu wa *BOT* suala la *Mortgage Financing* tulipe kipaumbele ili watu waanze kujenga nyumba bila *cash*. Ni hatari kuwa na *society* inayotumia *cash* peke yake. Ukisikia kuna *corruption* huwezi kukataa, hakuna mtu anayeweza kujenga kwa *cash* na mishahara inajulikana lakini unakuta watu wanajenga kila siku. Naomba watu wa Mipango Miji watusaidie kupanga miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana majengo yanayojengwa katika Miji yetu, yasiyengwe kabla hatujahakikisha mifumo ya maji safi na maji taka nayo imepanuliwa, haya ndiyo maendeleo. Leo Dar es Salaam ukitaka kujenga *fly over* za barabara unajenga wapi, kila kona kuna nyumba. Wanasema tuna program ya kupanua barabara, kesho mtu amepewa kibali anajenga ghorofa, sasa unauliza mbona tunaiongezea gharama Serikali!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, barabara ya Mwenge, ukiwa unakwenda Mwenge kutoka Kinondoni tumesema tutaweka reli nne, sasa hivi wamefika reli tatu, jambo zuri Serikali imetusaidia, *fine* lakini pale pale pembeni kuna watu wanajenga maghorofa wakati hiyo reli ya nne ambayo tunatakiwa tuijenge tukipata fedha, sasa najiuliza haya maghorofa yamekuta *plan* hizi waliotoa kibali cha kujengwa maghorofa haya ni akina nani ambapo kesho Serikali itabidi iwa-*compensate* kwa hawa watu lakini kwa sababu mipango yetu haipo *integrated*, kwa hiyo, kila mtu anapanga vyake, Halmashauri inapanga vyake, Wizara inapanga vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana watu watusaidie, tunachohitaji ni mipango mizuri ili angalau tuone *value* ya watu wetu waliosoma vizuri. Lakini kuna mipango mpaka unajiuliza hivi kweli kuna *planners* hapa, haiwezekani, naomba sana watusaidie kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, namuomba Mheshimiwa Waziri, tuliunda Tume ya Kutatua Matatizo ya Ardhi, tumefanya hivyo katika Wilaya zote. Tunaomba sasa yale yaliyowekwa mle ndani yatekelezwe, watu wetu bado wana matatizo makubwa sana ya viwanja na ardhi, hatuwezi kama hatutatatua yale matatizo. Tume ilifanya kazi nzuri sana kwa hiyo tuanze kutatua kwa sababu mpaka leo kwenye Manispaa yetu ya Kigoma matatizo ya watu ambao wamepewa kiwanja kimoja watu wawili bado yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unajiuliza watu wanatoaje viwanja kwa watu wawili na yule Afisa Mipango Miji anayefanya hivyo bado yupo mpaka leo. Akikaa sana anabadilishwa, kesho anabadilishwa tena, maana yake ni nini? Tunaomba sana Waziri atusaidie aje na mikakati ambayo kweli itatupeleka kwenye karne ya ishirini na moja ili miji yetu na sisi iweze kupendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwenye orodha yangu, huyu ndiye alikuwa msemaji wangu wa mwisho, kwa hiyo tukirudi jioni, tutamwita mtoa hoja aweze kuhitimisha kwa kujibu yale yote mliyozungumza, halafu tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi.

### MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wa Wizara na taasisi za Wizara kwa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ufafanuzi katika maeneo mawili, kwanza, mipaka iliyoidhinishwa ya mji wa Lushoto ni ipi? Pili, mpaka wa Wilaya ya Korogwe na Lushoto, eneo la Mombo inabainishwa na alama za asili na *beacons* zipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja. Hoja yangu ninayotaka kuchangia, ni wakazi waliokuwa wamefanyakazi *Tanganyika Packers* (Kawe). Wafanyakazi hawa wameishi katika nyumba hizo tangu vijana kuanzia mwaka 1962 hadi sasa ni wazee wana watoto na wajukuu. *Tanganyika Packers* imekufa lakini wafanyakazi bado wapo katika nyumba hizo. Ninachotaka kufahamu, je, nyumba hizo ni mali ya nani mpaka sasa? Kwa nini nyumba hizo wasiuziwe wale ambao wanaishi ndani ya nyumba hizo na kwa kuwa nyumba hizo zimekwisha kuwa mbovu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hati za nyumba, kwa kuwa wananchi wanajenga nyumba ili waweze kupata hati na kwa kuwa kuna ucheleweshaji wa kupata hati hizo, je, Waziri anasemaje kuhusu muda wa kupata hati hizo kwani kuna wananchi wengine hawana hati kwa muda mrefu na wanashindwa kupata mikopo benki kutokana na kutokuwa na hati za nyumba? Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje?

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na watendaji wote wa Wizara hiyo kwa kazi kubwa wanayoifanya. Baada ya pongezi hizo, nina maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kupata viwanja kwa ajili ya huduma kwa umma. Kutokana na watendaji wa Wizara/Halmashauri na hasa baadhi ya Maofisa Ardhi kutokuwa na wazalendo katika nchi yao, wamesababisha mipango ya Serikali kutokamilika. Hali hii imetokana na watendaji hao kutotilia maanani maombi ya viwanja kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Mkoa wa Ukonga katika eneo la Chanika, ukubwa wa ekari 20 (kwa ajili ya kituo na nyumba za Askari). Angekuja mwekezaji ambaye anasamehewa kodi angepata kwa kunyenyekewa na kwa muda mfupi lakini ombi la Polisi limechukua miaka miwili na nusu tangu mwaka 2006, je, hii ni haki?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi ni cha kutoa huduma kwa umma. Wananchi wa maeneo hayo hutafuta huduma hiyo kwa karibu kilomita 30 na ujambazi umekithiri sana, kutokana na wingi wa watu waliohamia huko. Ninaomba Wizara kupitia Halmashauri, itenge eneo la viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya vijana na kina mama kwa kila Wilaya za Mkoa wa Dar es Salaam (Ilala, Temeke na Kinondoni). Tusipoangalia vizuri, Mkoa wa Dodoma utaharibika kwa kujengwa kiholela kama jiji la Dar es Salaam ulivyoharibika kwa kuwa na nyumba kama kambi za wakimbizi. Umefika wakati tubadilike tuwe wazalendo ili kizazi kijacho kirithi miji iliyoendelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya jitihada za makusudi za kurekebisha mifumo ya miliki na matumizi ya ardhi hapa nchini, lakini jitihada hizi hazielekei kuwa na tija kwa sababu moja muhimu. Sababu hiyo ni kwamba taswira (*concept*) yetu katika nchi hii, haizingatii ongezeko la watu na viumbe wengine (kama mifugo na wanyama pori) wanaotegemea ardhi hiyo hiyo isiyoongezeka badala yake inaendelea kuharibiwa na kutofaa tena kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watu wamekuwa wakiongezeka sana hasa katika maeneo fulani fulani ya nchi na sUala hili hatulizungumzi sana, badala yake tunawahamisha watu (na mifugo) kwenda maeneo yasiyo na watu au yaliyo na watu wachache. Hii ni suluhisho la muda mfupi kwani hata huko tunajaa na hatutakuwa na maeneo ya kuwahamishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa kiasi fulani kwa kuzingatia taswira (*concept*) ya “*Carrying Capacity*” yaani namba ya watu au wanyama wanaoweza kuishi katika eneo fulani la ardhi bila kumaliza rasilimali zilizopo au kuharibu mazingira ya eneo husika. Taswira hii (ya *carrying capacity*) yaweza kuonekana kama haitekelezeki, lakini lazima tujitahidi kuzingatia uwezo wa kila kipande cha ardhi katika kumhudumia binadamu na mifugo yake na kisha kushughulikia changamoto zinazojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anipe maelezo ni kwa nini Wizara hii haizingatii suala hili la “*Carrying Capacity*” ya ardhi ili kuondokana na misongamano inayotokea Mikoa mbalimbali kama Mwanza, Shinyanga na kadhalika. Kama vile uharibifu mkubwa wa rasilimali (ardhi, vyanzo vya maji na kadhalika) na mazingira pamoja na njaa na pengine vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia, Jumamosi tarehe 2/8/2008, Mheshimiwa Rais Kikwete, alipokuwa Mkomang’ombe (Ludewa) ambako kuna mpango wa kuwahamisha wananchi wa kijiji hicho ili kupisha maendeleo ya mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma. Mheshimiwa Rais alisisitiza kuwafidia wananchi kwa haki na kuandaa makazi yao na miundombinu mipya huko kwenye makazi mapya kabla ya kuwahamisha watu. Mie kama Mbunge na mwakilishi wa wananchi wa Mkomang’ombe na Mundindi (Liganga), sitakubali kitu hadi maagizo haya ya Rais yatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi katika suala la fidia ni namna mazao ya kudumu (kama miembe na miti mingine ya matunda) yanavyothaminihwa. Wakati mti mmoja wa mwembe unauweza kuzalisha embe kwa zaidi ya miaka 100 (mia moja) na kumpatia mkulima na vizazi vyake mamilioni ya pesa kwa kipindi cha uhai wa mwembe huo, mkulima wa Mundindi/Mkomang'ombe anatarajiwa kulipwa eti TSh.20,000/= ambacho chaweza kuwa ni kipato cha mkulima kwa musimu moja kwa mwembe mmoja. Waziri haoni kama tunawapunja sana wananchi na kuwapa umaskini mkubwa baada ya kuwa na maendeleo tayari na kuwafanya waanze upya. Naomba maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. DR. OMARI M. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, sina budi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba aliyowasilisha hapa Bungeni kwa jinsi ilivyokuwa nzuri lakini pia kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kero kubwa ninayoiona ni miji yetu kuanzia midogo hadi mikubwa kujengwa kiholela bila mpangilio (*master plan*). Utakuta miji yetu mingi imejengwa bila utaratibu hata kuweka au kuingiza miundombinu imekuwa vigumu sana. Kama kupitisha barabara au *system* ya maji safi na maji taka, utakuta Halmashauri zetu hazina mpango au kama upo unaenda kwa kusuasua. Pamoja na uhaba wa fedha lakini kama wangukuwa na malengo maalum, saa hizi tungekuwa tumeshafika mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ya kutokuwa na mipango maalum, ndiyo inayoleta migogoro mingi kati ya wananchi wenyewe lakini pia kati ya wananchi wenyewe lakini pia kati ya wananchi na Serikali. Hivyo basi naomba sana mipango ya upimaji miji yetu iwe ndiyo kipaumbele, ili kupunguza vurugu lakini pia kupendezesha miji yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata zile sehemu ambazo tayari wananchi wameshajenga bila utaratibu maalum basi sasa Serikali iongeze kasi kuwapimia humo waliomokwishajenga ili wananchi hao waweze kumiliki nyumba zao kihalali ili ziwasaide hata katika mikopo ili waboreshe maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata katika mpango wa MKURABITA, wananchi hawa wanapata matumaini makubwa sana ili waweze kutumia rasilimali zao ili ziwaokoe katika dimbwi la umaskini lakini wananchi hawa sasa wanaanza kukata tamaa kwa vile ipo mipango ambayo haitekelezeki iwe sasa basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia suala la fidia kwa wananchi ambao nyumba zao zinabomolewa kwa ajili ya upanuzi aidha wa barabara au majengo ya maendeleo ya aina yoyote kama, shule, hospitali au kiwanda ama mgodi, kwa Serikali au mwekezaji binafsi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza hapa ni kwamba inapofikia ulipaji wa fidia ndipo mambo yanapokuwa tatizo kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza fidia hailipwi kulingana na gharama iliyopo kulingana na Sheria ya Ardhi No.4 na No.5 ya mwaka 1999. Pili, Sheria tumetunga wenyewe hivyo basi lazima tuzifuate bila kujali gharama. Tatu, wakati wa ulipaji fidia ungefaa wananchi walipwe kwanza na wapewe muda ili waandae makazi mapya. Sasa unapomwambia bomoa nyumba yako uondoke, je, atapata wapi fedha ya kumuwezesha kubomoa, kusafirisha na kujenga makazi mapya? Hapa naomba sana ufafanuzi wa kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Tahadhali, wananchi hao walipwe kwanza na wapewe muda wa kutosha kwani kuna dharura gani, maana kila jambo lazima lifanywe kwa mipango. Cha msingi, wakati wa utoaji fidia hiyo kuwe na maandishi chini ya Mwanasheria au Mahakama kwa vile baadhi ya wananchi hao sio waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuitakia kheri Wizara kwa maana ya Waziri na watendaji wake. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia machache kuhusu “*Land planning*” na ugawaji wa viwanja. Mimi naamini Mawaziri wa Awamu hii ya Nne ni wa “*Speed and Standard*” kama lilivyo Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, sisi Wabunge tunatumaini kuona mabadiliko na hasa katika kuiga mambo mazuri yanayotokea katika nchi nyingine za Afrika na yale mabaya tuyaache. Mfano halisi wa hili ni ugawaji wa ardhi unaofanywa Zimbabwe. Kabla ya kugawa viwanja, yafuatayo huwa yanaandaliwa mapema kabla ya ploti yenyewe hajapewa mwananchi:-

(i) Ramani ya aina ya nyumba zinazohitajika kujengwa katika *Block* hiyo (zinakuwepo ramani za aina mbalimbali kama 4 – 6) kutegemea daraja au uwezo na thamani ya nyumba inayohitajika katika eneo hilo;

(ii) Serikali inaweka au inajenga “*foundation*” kabisa ili ukikabidhiwa kiwanja tayari kimeshajengwa “*foundation*” ili aliyepewa anyanyue tu na kulipia gharama ya “*foundation* na ramani”;

(iii) Barabara zinajengwa kabisa tena za lami;

(iv) Miundombinu ya umeme, maji safi na maji taka inakuwa tayari imeshatayarishwa;

(v) Kwa wakati ule wa zamani miundombinu ya waya za simu na hivi sasa “*cable television*”; na

(vi) Maeneo ya “*super markets*”, nyumba za ibada, “*garages*” na “*open space*” za viwanja vya michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nini kinashindikana kwa Tanzania kufanya au kuiga mfano huo? Ikiwa Nigeria, Malawi walikuja Tanzania wakapata uzoefu wa CDA, kuna sababu gani sisi tusipate na kufanya suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo au nyumba zilizojengwa bila utaratibu. Ipo haja kubwa sasa ya Serikali kupitia Wizara hii, ikishirikiana na Mifuko ya Maendeleo ya Jamii, kurekebisha mji wa Dar es Salaam hasa maeneo ya Buguruni, Ilala, Mwananyamala, Temeke na kadhalika ambamo mpangilio wa baadhi ya nyumba za sehemu hizo ni za aibu kuambiwa ziko Dar es Salaam tunaloliita jiji. Ni aibu leo kuna vichochoro ambavyo anapotokea mgonjwa gari haliwezi kufika eneo hilo. Maji taka au mitaro ya maji haitiririki hasa wakati wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati umefika kujengwa kwa makusudi nyumba za maana na mipangilio ya miji mizuri bila ya wananchi wanaomiliki maeneo hayo kuhamishwa bali wapewe makazi mapya katika nyumba zitakazojengwa kwa mpangilio maalum wa maghorofa. Hili linawezekana penye dhamira madhubuti.

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ya Dar es Salaam (maghorofa) ambayo ni mazuri lakini hakuna barabara za lami na wakati wa mvua ni aibu. Hili nililizungumzia hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI akasema Serikali ina mipango maalum na Halmashauri zote za Dar es Salaam ili Serikali kuu isaidie. Mheshimiwa Waziri, hebu nisaidie mimi suala moja kuhusu hili. Hivi inawezekanaje watu wenye uwezo wa kujenga maghorofa wasiweze kuchangia barabara za lami katika maeneo yao waliyojenga? Naomba jibu.

**MHE. AMEIR ALI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima mimi na familia yangu na kunijaalia uwezo na hamu ya kuchangia hotuba hii iliyowasilishwa na Mheshimiwa John Z. Chiligati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake. Pia niwapongeze wote waliotayarisha hotuba hii kwa kazi kubwa walioifanya na kufuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kuhusu *sector* ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi, imeweza kuwalazimisha wananchi, ardhi na nyumba zao ili waweze kuzitumia kupata mikopo ya benki. Kwa kupitia (MKURABITA), hili ni jambo la kuigwa na la kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limeanza lakini bado spidi yake ni ndogo kutokana na umuhimu wake. Kwa sababu kila Mkoa, Wilaya na vijiji, wanahitaji

huduma hiyo ya (MKURABITA), kwa hivyo, ninaiomba Serikali kupitia Wizara inayohusika kuharakisha huduma hiyo ili kuenea kwa haraka ili wananchi wengi wafaidike na mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yaliyofanywa na idara pia kuna migogoro mingi ya ardhi na haina budi kushughulikiwa. Migogoro hii mara nyingi inasababishwa na Halmashauri, wenye fan,i pia kutokana na baadhi ya Maofisa wetu kutokuwa waaminifu kwa kuuza baadhi ya sehemu kinyume na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua na kukinga matokeo hayo yasiendeleo, ninaiomba Serikali kwanza itafute wataalamu katika Vyuo vyetu vya Ardhi kwa kuwaajiri katika Halmashauri zetu. Pia kuwachukulia hatua kali wale Maofisa au wajanja wanaouza mashamba na kupima viwanja kwa kutumia cheo chake, bila kuwaonea haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu CDA, Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu mji wa Dodoma, kuna malalamiko mengi yanayohusu ardhi, wanatoa viwanja katika maeneo ya watu bila kuwafidia chochote pia kuna viwanja vya watu waliopewa pamoja na kumiliki hati viwanja hivyo wamepewa watu wengine bila ya wahusika kupewa sehemu nyingine. Hii inaudhi na inakera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo Mheshimiwa Waziri, mamlaka haya waliopewa CDA kama yako chini ya Wizara yako, sasa umefika wakati shughuli hizo za upimaji viwanja na ramani kabla ya ugawaji, Wizara ifanye uchunguzi wa eneo lile kama hakuna malalamiko yoyote bila ya hivyo Serikali isubiri mapigano ya kugombea viwanja katika Mkoa wa Dodoma ambao tayari moshi unafukuta kwa chini. Kama suala hili haliko kwenye Wizara yako Mheshimiwa Waziri alipeleke linakohusika kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Wapo wananchi na wengi ni viongozi ambao wanamiliki mashamba makubwa sana kuzunguka mji wa Morogoro. Hawa viongozi na matajiri ambao wamechukua maeneo makubwa Dakawa, Mgongola, Mvomero, tatizo mashamba hayo hayalimwi au kuendelezwa. Walichofanya ni kuhodhi ardhi na hivyo wenyeji wanatafuta maeneo ya kulima au inawapasa watembee masafa marefu kwenda kulima, jambo hili linawakatisha ari ya kulima wenyeji hawa. Wapo watu wana zaidi ya hekta 1000 ambazo hazilimwi, Serikali inasaidiaje hawa wananchi?

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, matumizi ya ardhi ya Fukwe kwa Watanzania. Nchi za wenzetu kama vile Barbados na baadhi ya nchi za Carribean, mwekezaji anapojenga hotel katika ardhi iliyoko karibu na fukwe, basi sheria inamtaka mwekezaji huyo aheshimu wananchi wa hapo na kuwa ufukwe huo hauingii katika milki ya mwekezaji. Hivyo, ni huru kwa mwananchi kutumia eneo hilo, kwa mfano kupita, kuogelea na kadhalika. Je, utaratibu huo si mzuri ambao na sisi hapa Tanzania tungeweza kuiga?



Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunapochukua ardhi (yaani Serikali) kwa madhumuni ya maendeleo, sheria inazungumzia *fair compensation*. Tafsiri ya *fair compensation* ni hafifu sana, maana unapomng'olea mwananchi mwembe au mnazi au mkorosho, mkawapa *respectively* Sh.15,000/=, 10,000/= au 30,000/= kwa mfano; hiyo sio fair compensation. Naomba sana Serikali iwatizame wananchi wake hawa kwa suala hilo la "*fair compensation*".

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, moja katika matatizo makubwa yanayowakabili wananchi wetu na jamii kwa ujumla, ni suala la ardhi. Ugomvi wa ardhi unaweza kuleta matatizo ya ugomvi baina ya mtu na mtu, familia na familia na kijiji na kijiji. Mahakama hizi (Mabaraza) ya Ardhi na Nyumba ni muhimu kutiliwa mkazo na kuimarishwa. Nchi yetu ni kubwa na ni rahisi ili kutatua migogoro hiyo haraka basi ni lazima Mabaraza hayo yaongezwe ili kuondokana na mlundikano mkubwa wa kesi, ambao unaweza kuleta matatizo makubwa hapo baadaye. Ni imani yangu kuwa suala hili litapewa kipaumbele kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Mfuko wa Nyumba, ni muhimu sana ingawa una changamoto kubwa. Ushauri wangu, ni kwa nini mfuko huu haudhibitiwi na Idara ya Nyumba ambayo kwayo itajenga nyumba hizo halafu na kuwauzia wananchi kwa mkopo. Mkopo huo utakuwa na masharti maalum kama vile:-

- (i) Mkopaji kutowa *down payment* ya 40% ya bei ya nyumba;
- (ii) Pesa zilizobakia azilipe katika kipindi cha miaka kumi (10) (kwa mfano) kwa kiwango kitakachowekwa; na
- (iii) Ifikapo miaka 10 kama hajalipa basi nyumba ichukuliwe, iuzwe na pengine arudishiwe 40% yake *minus service charges* na kadhalika. Hii pengine inaweza ikasaidia sana kupunguza tatizo hili la makazi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tulinde sana matumizi ya ardhi kwa shughuli ambazo hazina tija sana na pengine inaweza kutufikisha mahali ambapo ardhi yetu itakuwa *exhausted* bila ya kuwa na tija ambayo inabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante sana.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri, aidha, kwa kazi nzuri aliyofanya mwaka uliopita. Nampongeza Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kutayarisha bajeti nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia kwa wananchi wa Manispaa ya Dodoma kwa ardhi iliyotwaliwa na Serikali na kumilikishwa CDA mwaka 1989. Kwanza, ni eneo la Kati ya mji wa Dodoma ambalo baadhi ya wananchi walishalipwa fidia. Je, ni haki kweli

kwa Serikali kutwaa ardhi ya mtu/watu ikaigawa hiyo ardhi kwa taasisi fulani; na fidia kwa baadhi ya watu hao ikaendelea kutolipwa kwa zaidi ya miaka 20 iliyofuata? Hivi ndivyo sheria inavyokusudia kwa wananchi ambao ardhi yao imeshatwaliwa ki-sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wananchi ambao ardhi yao imekwishatwaliwa kisheria katika Manispaa hii na wao bado hawajalipwa fidia ni waathirika wakubwa ki-maendeleo wananchi hawa wanaishi bila matumaini kwani aliyemilikishwa (yaani *CDA*), amekuwa na haki ya kuwatimua wakati wowote ule anaotaka yeye (*CDA*) licha ya kwamba hawajalipwa fidia. Wananchi hawa hawana hamasa ya kuendeleza ardhi hiyo na wananyimwa fursa ya kujiletea maendeleo yao wenyewe ki-uchumi. Je, kwa nini serikali/*CDA* isiainishe maeneo ambayo wana uhakika wa kuyaendeleza katika kipindi mahsusi (tuseme miaka 50 ijayo) na watoe fidia kikamilifu hivi sasa kwa wahusika ili wananchi watakaokuwa nje ya eneo hilo waendeleze ardhi zao bila bugudha!!.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tahadhari! Wizara ya Ardhi ndiyo inasimamia masuala yote ya ardhi nchini (pamoja na ile inayomilikiwa na *CDA*). Kwa hiyo, siyo sahihi kwa Wizara kutojihusisha na matatizo ya fidia kwa wananchi wa Manispaa ya Dodoma kwani ndiyo iliyotoa Hatimiliki hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu, napenda kutamka rasmi kwamba ninaunga mkono hotuba ya Waziri aliyotoa kwa asilimia mia moja. Nampongeza yeye binafsi pamoja na wataalamu wake wote kwa ushirikiano waliuonyesha na kuwaza kuandaa taarifa ambayo inaeleweka. Pia kwa mantinki hiyo, sina budi kuunga mkono hotuba kwa asilimia moja. Baada ya kueleza hayo, Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuyaelezea yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nalipongeza Shirika la *NHC*, kwa jitihada wanazozionyesha za ujenzi wa nyumba katika Mkoa na hususan kwa jengo ambalo limejengwa na shirika Makao Makuu ya Mkoa wa Kigoma. Bado wananchi wa Mkoa wa Kigoma wanaomba juhudi hizo zisiishie Makao Makuu ya Mkoa tu bali yaende hadi Wlayani na hasa Wilaya ya Kibondo ambako wananchi wameniomba kufikisha ombi lao la kujengewa nyumba (*flats*) kwa ajili ya kupunguza tatizo la nyumba kwa watumishi wa Serikali hapo Wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma unayo ardhi kubwa ambayo haijapimwa kiasi kwamba kwa harakati za kuondoa umaskini kwa kila Mtanzania, ni sharti ardhi ipimwe ili wananchi waweze kutumia hati za ardhi kuchukulia mikopo benki ili kujiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wengi wa Wizara hii hawana elimu ya kutosha kiasi kwamba ndiyo inakuwa chachu ya migogoro ya upimaji wa viwanja huko Mkoani. Kwa makusudi mazima, ni vema Wizara ijipange kwa kuwaendeleza watumishi wake ili kujiendeleza kitaaluma. Hiyo iende sambamba na uchache wa watumishi wa

Idara hiyo katika Wilaya. Hapo ninaomba Wizara iweke utaratibu wa kuongeza watumishi katika ofisi hiyo iliyopo katika Halmashauri ya Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine sugu la ofisi za idara hiyo kushindwa kutekeleza majukumu kutokana na kukosa nyenzo za kutendea kazi kama vile magari na vifaa vya *survey*. Ofisi ya Idara ya Ardhi imekuwa ikishindwa kutimiza majukumu yake na hasa pale wanapotakiwa kwenda vijijini kupima maeneo. Nimetumwa na wananchi wa Jimbo la Muhambwe kuiomba gari Idara hiyo ili kuweza kuwafikisha kwenye maeneo ya kupima ambayo yako mbali na Makao Makuu ya Wilaya mahali ambapo ndipo ofisi hiyo ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya kutaka vijiji vya Kigina na Magarama viwe vijiji yalikuwishatumwa tangu mwaka 2003 lakini hadi sasa bado vijiji hivyo havijapata usajili. Matokeo ya hali hiyo, ni wananchi wa vijiji hivyo kuishi bila kuwa na huduma muhimu kwa jamii kama vile, zahanati na soko. Si hali hiyo tu bali hata kutengenezewa njia zindazo huko haziwezi kusimamiwa ipasavyo. Vijiji hivyo vina idadi ya watu zaidi ya 5000 kila kimoja. Naomba wananchi hao waelezwe hatima yao.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusifu utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa John Chiligati wa haki, uadilifu na motomoto katika Wizara hii. Naiomba Serikali, iongeze fedha za bajeti ili ilingane na majukumu makubwa ya Wizara hii. Kazi kubwa za kupima vijiji vyote nchi nzima, kupima miji na majiji yote Tanzania, kuna kazi kubwa ya ujenzi na maendeleo ya nyumba Tanzania nzima, shughuli hizi zinahitaji fedha nyingi sana kuliko zinazotolewa na Hazina. Tunaomba Serikali Kuu itoe fedha nyingi ili kuifanya Wizara itimize majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya upimaji vijiji vya Wilaya ya Rufiji. Tunashukuru sana Wizara kwa kupima vijiji vya Rufiji. Hata hivyo, kuna matatizo makubwa ya mipaka kati ya vijiji vyetu kama ifuatavyo:-

(a) Mogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Ikwiriri (*Agrieved*) na kijiji cha Nyamwage. Wananchi wa Ikwiriri wanalilia sana haki yao ya kupata mpaka halali ya kijiji chao;

(b) Mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Ruwe na kijiji cha Mbunju darajani (Mbande). Wananchi wa kijiji cha Mbunju wanalalamika sana na kulia kwa kutaka wapewe haki zao za mpaka halali kati yao na wa kijiji cha Ruwe;

(c) Mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Mbunju Mvuleni na kijiji cha Mgomba (Kitongoji cha Mpima), Mbunju Mvuleni wanalalamika sana kuwa mpaka kati yao umewapendelea wanakijiji wa kitongoji cha Mpima. Nataka wapate haki yao ya mpaka wa halali; na

(d) Mgogoro wa mpaka kati ya kijiji cha Chumbi na kijiji cha Mbwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonyesha hapo juu, upimaji Rufiji haukuwa makini. Inaonekana wamefanya kazi kwa kulipua tu. Tunaomba sana Wizara isaidie haraka ili migogoro iliyojitokeza ipate kurekebisha haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata matatizo kukubali kwamba inawezekana mimi Idris Ali Mtulia, nilipewa kiwanja Plot 1273, Msasani Peninsula – Dar es Salaam City, 12<sup>th</sup> February, 1990. Ref. No.LD 83912/4/CCC. V.RE.No.53275 ya 13/2/1990, baada ya kulipia kodi ya ardhi hadi 2007, baada ya kumwandikia barua Katibu Mkuu – Ndugu Salome Sijaona ya tarehe 04/6/2004 na baada ya kumuandikia barua Mheshimiwa Waziri (aliyekuwa) Mheshimiwa John Pombe Magufuli ya tarehe 30/4/2007 barua zote zilikuwa zinadai kupatiwa hati yangu lakini mpaka leo bado sijapata hati hiyo. Naomba huruma ya Wizara yako nitayarishiwe Hatimiliki ya plot yangu No.1273 Msasani Peninsula ili mtende haki. Tafadhali nisaidieni ndugu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninaunga mkono hoja hiii kwa asilimi mia kwa mia. Mungu awabariki ili mtende haki, ahsante.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii (hongoreni kwa kazi). Mambo machache tu ya msisitizo na maombi kwa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la vijiji vilivyo karibu sana na hifadhi ya wanyama pori la Moyowosi na pori la Msitu wa hifadhi la *Kasulu East Forest Reserve* na *Makere Forest Reserve*, Wilayani Kasulu/Kigoma. Vijiji hivyo ni pamoja na Kagera Nkanda, Mvinza, Kwaga, Kigembe, Makere, Mvugwe, Rangwe Mpya, Zeze. Tatizo ni mipaka ya hifadhi hizo kwa mujibu wa GN zilizotolewa 1954 na *Village Scheme* ya *operation Kigoma* 1972. Ufafanuzi wa mipaka ni jambo muhimu sana kwa sababu baadhi ya vijiji inadaiwa eti vimo ndani ya hifadhi. Ni vyema Wizara yako itume wataalamu ili jambo hili lipatiwe majibu na ufumbuji wa tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi la Halmashauri ya Kasulu la kupima ardhi ekari 50,000 katika vijiji vya Makere, Mvugwe, Nyarugusu, Hevu Ushirgo na Nyamidaho. Lengo na shabaha ni kupata kibali cha kupima ardhi na ku-*determine* matumizi bora ya ardhi hiyo. Aidha mwekezaji – *TonyTan Plantations*, wapo tayari kulipia baadhi ya gharama za upimaji. Kampuni hii ina *Certificate of Incentive* iliyotolewa na *TIC – Dar es Salaam, 2006*. Uharaka katika jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida kubwa ya uhaba wa wataalam katika sekta hii kwa mfano wapimaji wenye sifa, Wadhamini na Maafisa Ardhi wateule ambao wanaweza kuandaa hati za viwanja na mashamba. Wizara yako ionyeshe njia ili TAMISEMI wazinduke na waguswe na uhaba huu mkubwa wa wataalam katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mji wa Kasulu umepanda hadhi na kuwa Halmashauri ya mji basi Wizara yako niombe itume wataalamu wa mipango miji ili waje Kasulu kutusaidia kupanga vizuri mji wetu ambao kwa kiasi kikubwa tatizo la ujenzi holela bado ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi kwa Shirika la Nyumba – *NHC* kuja mji wa Kasulu kujenga kitega uchumi na nyumba za kuishi watumishi katika mji huu. Mji huu una sifa zote za kibiashara ikiwa ni pamoja na kuwa mji uliopo mpakani na nchi jirani ya DRC na Burundi. Biashara kubwa ipo, idadi ya wakazi ni kubwa *Kasulu Urban has a population of 200,000 inhabitants.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Ardhi iliyopo Kigoma Mjini. Mahakama hizo/baraza hilo, lianzishwe katika mji wa Kasulu ambapo Wilaya yote ya Kasulu ina wakazi zaidi ya 760,000 ikiwa ni Wilaya ya pili kwa ukubwa iliyopo vijijini baada ya Wilaya ya Geita (*we one the 2<sup>nd</sup> largest rural district in Tanzania*). Kigezo hicho ninaamini kitasukuma kuanzisha baraza hilo mjini Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda za “Hati”. Kwa Mkoa wa Kigoma iko Mwanza, ni mbali mno. Anzisha Kanda mpya ya Kigoma ili itoe pia huduma kwa mji wa Tabora, Kigoma – Tabora ni karibu zaidi kuliko Kigoma – Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, wafikirie na wabuni namna ya kutatua matatizo sugu, kwa mfano, wavamizi wa maeneo ya wazi na viwanja vya michezo; *double allocation* ya viwanja katika maeneo ya mijini na vijijini; watumishi wa Wizara walaji rushwa; ujenzi wa vituo vya mafuta (*petrol station*) katika maeneo ya shughuli nyingi za kijamii sehemu za masoko, maduka na hata sehemu za vituo vya huduma zingine. Mfano hai, kituo cha Mafuta na soko la Tabata Bima. Aibu hii ya kutisha, jibu lake ni nini? Mamlaka ya Manispaa ya Ilala/Dar es Salaam wanasemaje? Ucheleweshaji wa upatikanaji Hati za viwanja na tatizo la kuchelewa kuandaa michoro katika maeneo mengi na hasa Wilaya ya Kasulu na Kibondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma hauna hata “*Surveyor*” hata mmoja tatizo ni nini? Tafadhali tatua jambo hili. Shirikiana na TAMISEMI (Katibu Mkuu) ili Halmashauri ya Kasulu ipate Afisa Ardhi Mteule haraka iwezekanavyo. *It is indeed urgent.*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa kazi njema anayoifanya Wizarani hapo. Nina jambo moja tu muhimu ambalo ni mpaka kati ya Malawi na Tanzania sasa imekuwa ni tatizo sugu ambalo halina majibu hadi sasa. Tangu nimeingia humu Bungeni, nimekuwa nikipigia kelele hapa ndani kwa majibu yasiyoridhisha. Kila Waziri naambiwa kuwa juhudi zinafanywa na Wizara ya Mambo ya Nje, hadi lini? Je, hii ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya kwa jambo hili itatimia lini? Wenzetu wa Malawi sasa wanavua hadi ufukweni mwa nchi yetu bila hatua zozote za kisheria kuchukuliwa, nataka liishe sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NHC*, imeonekana kupendeka sana katika kujenga nyumba zake, Wilaya ya Mbinga hasa mji wa Mbinga ni *potential* sana kibiashara na kipesa kwa wananchi wake. Je, ni lini shirika hili litaleta mradi wa ujenzi wa nyumba hasa za ghorofa mjini Mbinga?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENTIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upimaji vijijini. Ardhi ni moja ya sababu kubwa inayosababisha vita kati ya koo za Wanchari na Wakira na pia kati ya Wanchari na Warechoka Wilayani Tarime, Mkoa wa Mara. Koo hizi zinang'ang'ania kipande cha ardhi kinachowatenganisha na hii ni kutokana na kutokamilika upimaji wa ardhi vijijini.

Aidha, agizo la aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, linachukua muda mrefu kutekelezwa. Naiomba Wizara iratibu utekelezaji wa agizo hilo kuwa kipande hicho kinachowagombanisha kipewe Serikali kwa matumizi ya umma. Naamini hii itasaidia sana kumaliza mgogoro huu unaoibuka mara kwa mara ambao umemaliza watu wengi lakini pia shule ya Sekondari ya Mwema, iliyoko kwa Wanchari haina wanafunzi tena hasa wa koo zile nyingine kwa kuogopa kuuawa. Kwa kweli hali ni mbaya kijamii katika eneo hilo. Lakini naomba upimaji wa ardhi vijijini upewe kipaumbele Wilayani Tarime kwani migogoro ya aina hiyo ni mingi sehemu nyingi Wilayani Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa kazi nzuri sana Waziri, Mheshimiwa Chiligati na watendaji wote chini ya Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona, nasema *keep it up!*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga tena mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsanteni!

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi - kaka yangu Mheshimiwa Capt. John Zephania Chiligati, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii mahiri sana iliyoonyesha bayana utekelezaji wao pamoja na vipaumbele vya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, napenda kutamka rasmi kuwa ninaunga mkono hotuba hii na ninawaomba Mwenyezi Mungu awape afya, maisha marefu na uwezo wa kutekeleza yote waliyoainisha kwa maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua juhudi za Serikali katika kupima viwanja, zoezi ambalo limefikia kwenye miji midogo ingawa sio miji yote midogo imekamilisha

zoezi la upimaji. Kwa kuwa zoezi hili linaendeshwa pole pole sana ninaiomba Serikali kuongeza kasi ya upimaji kwani wananchi wanategemea sana hatimiliki kwa ajili ya kupata mikopo kwenye benki mbalimbali, hata kudhamini mtuhumiwa Polisi au Mahakamani. Hivyo basi, kukosa hati miliki za nyumba, jamii inapata taabu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja hadi vijijini ili wananchi wapate hatimiliki ambazo ni dhamana zao katika mambo mbalimbali kama nilivyoeleza hapo juu. Nimesema, jambo hili nikielewa wazi kuwa Wilaya zote za Mkoa wa Singida yaani Manyoni, Iramba, Singida (V) na Manispaa upimaji ni bado sana, hata Singida Manispaa bado upimaji haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasikitika kuifahamisha Serikali kuwa bado kuna migogoro ya viwanja kati ya aliyepewa kiwanja na mwenye shamba kwa sababu Serikali inagawa viwanja wakati wenye mashamba huwa bado hawajafidiwa mimea yao iliyoko kwenye kiwanja husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali kuhakikisha wanawafidia wenye mashamba ndipo wagawe viwanja. Hii imejitokeza Singida Manispaa kwenye kiwanja nilichopewa mimi mwenyewe. Nategemea Mheshimiwa Waziri atatoa ufafanuzi wa ujumla ili Watendaji wazingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini Serikali inatambua umuhimu wa wananchi kupata hatimiliki (*lease*) kwa haraka na kwa gharama nafuu. Napenda kuleta ombi kutoka kwa wananchi wa Singida kuwa safari ya kufuata *lease* Dodoma Kanda linawawia vigumu sana kwa sababu gharama kubwa za nauli, chakula na malazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, azma za wananchi wengi za kupata lease zinashindikana kwa kukosa pesa za kusafiri na gharama nyingine nilizoziainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali mambo mawili ili kuwarahisishia wananchi wa Singida upatikanaji wa *lease* kwa gharama nafuu. Kwanza, ninaishauri Serikali kufungua ofisi ya kutoa *lease* Makao Makuu ya Mkoa wa Singida ili kuwatua wananchi mzigo na wengi kupata *lease*.

Ninaishauri Serikali kuanzisha mpango wa *website* ili kila mwananchi akitaka hatimiliki yake apate popote penye kompyuta (mtandao wa kompyuta).

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika mpango huu utakuwa rahisi sana kwa wananchi kupata *lease* zao kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongea kuhusu ujenzi wa nyumba za makazi ya wananchi kupitia mabenki na mashirika mfano *NSSF*. Ninaipongeza Serikali kwa kuwa ilikuwa na mpango mzuri wa kujenga *National Housing Quarters* kwa ajili ya watumishi na viongozi mbalimbali waliokuwa wanaishi kwenye Miji, Manispaa na Majiji hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mpango huu sasa hivi kasi au umuhimu wa kujenga *National Housing Quarters* ni mdogo sana. Kwa kuwa tatizo la uhaba wa nyumba Manispaa ya Singida na Makao Makuu ya Wilaya ya Iramba na Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali kuhamasisha mabenki yetu pamoja na *NSSF* kujenga nyumba za *National Housing Quarters* kwa ajili ya watumishi, wafanyabiashara, viongozi na wengineo kupata nyumba za kuishi wanapokuwa wameamua kuishi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Capt. Chiligati (Waziri) Waswahili husema: “Mwamba ngoma, ngozi huvutia kwake.” Basi atoe kipaumbele nyumba Singida ili wengi wanaokosa nyumba za kuishi wapate, watoe vivutio kwenye mabenki yetu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba waziri atoe maelezo wakati wa majumuisho yake kuhusiana na niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarudia tena kuunga mkono mia kwa mia bajeti ya kaka yangu mpendwa Capt. Chiligati Mungu awe naye pamoja na watendaji wake wote watimize azma yao vyema.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa John Chiligati (Mb), Waziri wa Ardhi na Mheshimiwa Salome Sijaona, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wa Wizara ya Ardhi kwa kuleta hotuba yao ya bajeti. Nampongeza zaidi Mheshimiwa Waziri ambaye hana Naibu Waziri, katika Wizara kubwa kama hii na shughuli zinakwenda sawa tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inajitahidi sana kuendeleza dhana ya matumizi bora ya ardhi, lakini kwa bahati mbaya, kuna baadhi ya watumishi wasio waaminifu, wanatia dosari sana maendeleo mazuri ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ingawa hatimiliki ni haki ya mteja aliyepewa miliki, kuna baadhi ya watendaji ambao wanazichezea hatimiliki ili ionekane kuna *double allocation*. Toka hapo kukazuka mtafaruku mkubwa katika mchakato wa umiliki. Hili linazua matatizo makubwa na usumbufu ambao hatimaye hakuna maendeleo yoyote ya ardhi husika. Nategemea katika utaratibu mpya wa hati za *electronic* huenda tatizo hili litaondoka. Pamoja na hayo, Wizara ichukue hatua dhidi ya watumishi waliosababisha matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo pia wakati wa ku-*mortgage* hatimiliki ili kupata mkopo toka vyombo vya fedha kwa mfano benki. mchakato wake ni mrefu mno kiasi kwamba kama kuna mwekezaji toka nje, basi anaweza kughairi kutokana na umangimeza wa pale Wizarani. Wizara ijitahidi kuondoa matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.



**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kuamka hali nikiwa mzima. Nasema *Allhamdulillah*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake iliyojengeka na mategemeo ya kupiga vita bomoa bomoa. Baada ya maelezo yangu hayo sasa niende katika kutoa mchango wangu katika hotuba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuzungumzia suala la ardhi. Katika nchi yetu kuna utofauti wa umiliki wa ardhi. Wako waliomiliki ardhi kwa ukoo, yaani ardhi ya mirathi na wengine wawekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi maeneo haya ya ardhi hutokezea umgovi mkubwa kati ya mmiliki na maamuzi ya Serikali. Watu wengi waliomiliki ardhi kwa njia ya ukoo – (mirathi) humiliki ardhi bila ya hati. Hapo ndipo panapotoa mwanya wa hitilafu na hatimae ugomvi hutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ingepaswa iandae mipango mahsusi ya kuhakikisha wamiliki ardhi kwa njia ya ukoo wapewe hatimiliki ya ardhi ili kuondoa migogo ya kila siku, jambo ambalo ni kunusuru damu kumwagika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pana udhaifu mkubwa jambo ambalo pia ni dosari kwa nchi yetu. Kwa nini Serikali haitoi kikomo cha watu wanaomilikishwa ardhi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ongezeko la watu mijini, jiografia ya miji yetu hasa Dar es Salaam ni tatizo kubwa, jambo ambalo hupelekea msongamano wa watu, pia bomoa bomoa. Mambo haya ndio chachu ya wananchi kupambana na dola na hatimaye kuitia Serikali hasara na wakati mwingine Serikali kwa makusudi kuwatia umasikini wananchi kwa kuwavunja ovyo makazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapaswa Serikali isiogope hasara. Serikali ina maeneo mengi makubwa ambayo haiyatumii kwa kuyajenga? Kwa kufanya hivi tutaweza kupunguza msongamano wa watu mijini jambo ambalo litapelekea Serikali kupata ongezeko la uchumi. Ama kuyapima na kuyaandalia jiografia nzuri na wakapewa wananchi. Mfano wa maeneo hayo ni kama vile Kigamboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mojawapo ya eneo la maendeleo. Tukiweza kuwa tayari, ardhi yetu itaitoa nchi katika dhana za umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi yalio bora kwa wananchi wetu, ni kujenga nyumba zenye ubora na kwa bei nafuu. Kwa kufanikisha haya mapato, maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana. Inawezekana, timiza wajibu wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nampongeza Mheshimiwa Waziri (Mwanasiasa) kwa nia yake itakayopelekea kila mwananchi kujua haki yake. Ahsante.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa dhiti kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wataalamu wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa hotuba nzuri na utendaji mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga ina mahitaji makubwa ya huduma za Wizara hii na Taasisi zake, kama Wilaya mpya ina mahitaji makubwa ya kupimiwa ardhi ya vijiji, Makao Makuu ya Wilaya na mipaka ya maeneo mapya ya Kata na Tarafa. Aidha, upimaji wa mashamba chini ya MKURABITA bado haujakamilika kwa sehemu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mkinga inakabiliwa na kero kubwa ya uhaba wa ardhi kutokana na sehemu nyingi za ardhi kuhodhiwa na wamiliki ambao hawatumii ardhi hiyo bali wameihodhi bila kuitumia ipasavyo na wananchi wengine kuzuilika kuitumia ardhi hiyo kimanufaa. Baadhi ya wananchi sehemu kubwa ya ardhi bila kuitumia ipasavyo na kikamilifu pamoja na Kambi ya *JKT* Manamba, Shamba la Mbegu la Mwele, Shamba la Mkonge la Lugongo, Mashamba ya Mohammed *Enterpises* ya Mjesani, Lonsoni na Bamba, Mashamba ya Moa Kihuhu na Boma.

Mheshimiwa Naibu Spika,, nashauri ama waliomilikishwa ardhi hii watakiwe kuitumia ardhi yote waliyomilikishwa kikamilifu, waruhusu sehemu wasizozitumia kwa muda itumiwe na wananchi au taasisi nyingine kwa muda au wanyang'anywe ardhi hii ili iweze kutumiwa na wananchi ama taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Mkinga, Kasera bado ina mahitaji makubwa ya kimaendeleo. Kwanza, ipo haja ya kuendeleza na kukamilisha upimaji wa Kasera ili uwe mji mzuri wa kisasa kama alivyoelekeza Mheshimiwa Rais katika ziara yake Mkoani Tanga hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ni kuifikia na kuipa kipaumbele Kasera kwa kulielekeza Shirika la Nyumba la Taifa kuipatia nyumba kama vile ilivyokuwa Chalinze, Chato na kwingineko mapema iwezekanavyo. Hili ni muhimu sana kwa kuzingatia kwamba mpaka sasa kuna ofisi ya Mkuu wa Wilaya na nyumba kumi kwa ajili ya watumishi wakuu wa Wilaya pekee. Kwa kuanzia Kasera itahitaji kiasi cha nyumba 40 kwa ajili ya wafanyakazi wa Serikali kuu, Halmashauri ya Wilaya pamoja na nyumba kwa ajili ya walimu, waganga na wauguzi wa hospitali, zahanati na shule zilizopo jirani ya Kasera. Aidha, kuna mahitaji makubwa ya makazi bora kwa wananchi wengi waliopora wanaotarajia kuhamia Kasera. Nitashukuru kwa kupatiwa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FUYA GODWIN KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Hai ninaomba niwapongeze sana kwa hotuba nzuri nikianza na

Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Makamishna/Kamishna na Watendaji wengine wote. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, ile mikopo kwa ajili ya Halmashauri kupima viwanja ni muhimu sana na ninashauri mfuko huo uimarishwe kwa ustawi wa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ubia katika ujenzi/kuendeleza viwanja vya mijini uzalendo upewe kipaumbele. Tuongeze kasi ya kujenga nyumba za kupangisha/kuuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. LUCY FIDELIS OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba (*NHC*), Marehemu Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Nyere kwa nia njema nyumba za *NHC* zilitaifishwa ili kuweza kusaidia watu wa kawaida kuishi huko. Lakini hali hii haipo hivyo kwenye shirika hili badala yake wanafanyabiashara bila kujali watu wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu cha kushangasha kwa sasa hivi *NHC* wanapandishwa bei ya kodi mara mbili kwa mwaka kwa mfano kodi kama ilikuwa Sh. 220,000/= sasa hivi ni Sh. 440,000/=. Hivi kweli Serikali ina nia ya kuwasaidia Watanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *NHC* kurithisha madeni, hainiingii akilini, shirika hili linatumia sheria gani kurithisha madeni kwa watu? Katika Wilaya ya moshi mjini katika nyumba za kuishi za *NHC* unakuta mteja aliyekuwepo kahama nyumba na kuacha deni zaidi hata milioni tatu na nyingine mpaka milioni tisa mpaka kumi na mbili. Lakini akija mteja mpya anaambiwa alipe lile deni kwanza wakati hilo deni siyo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, shirika lilikiwa wapi mpaka pakatokea madeni makubwa kiasi hicho? Ni sababu gani zinazotumika kumdai mteja mpya wakati sio deni lake? Hii ni kuwaumiza wateja kwa sababu tu ya uhaba wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri shirika lirudi kwenye kazi yake ya mwanzo na kujenga nyumba nzuri kwa bei nafuu ili watu wote waweze kuishi huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mji wa Dar es Salaam, watu wanajenga holela tu. Je, ni lini *masterplan* ya Dar es Salaam ilikuwa *reviewed*? Ni kitu cha kusikitisha kwamba majengo yanajengwa Dar es Salaam yanaporomoka kama vile hakuna Maafisa wa kukagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jengo la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa kuanzia hapa tu, ni kitu cha aibu kujenga lile jiko nyuma ya jengo lile. Lile jiko limejengwa chini ya nyaya za umeme. Hivi moto ukilipuka kule jikoni gari la Zimamoto litapita wapi? Jiko lile livunjwe mara moja na pia nipate maelezo ya kina kwa nini jiko lile lijengwe mahali pa hatari kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kwanza, wanaofanya *survey* hawana vitendea kazi vya kutosha na pia bei ya kufanya *survey* ni ghali sana. Hivi mtu wa kule kijijini ambaye hana uhakika wa mlo mmoja ataweza kulipia gharama hizi kweli? Kwa kuwa kuna *Mortgage Finance* wa kujua na itabidi watu kuwa na hati za viwanja bila kuwasaidia hawa watu wa vijijini tukajikita tu mguu na ukizingatia watu wengi wapo vijijini, ile adhima ya maisha bora kwa kila Mtanzania haitakaa itimie.

Kama ile Benki ya Nyumba ilikufa: je, haya ya *Mortgage Finance* yatafanikiwa? Hii ni siasa tu! Kajengeni nyumba hizi vijijini na siyo kujikita tu mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na matatizo na migogoro mingi sana ya ardhi hasa vijijini, lakini Mahakama za Ardhi hazifanyi kazi kwa sasa hivi kwa sababu mikataba imekwisha na hakuna Mahakimu wa kutosha. Je, watu hawa watasaidiwaje? Wizara iharakishe kutoa mikataba hiyo haraka ili kuondokana na usumbufu huu unaotokea, watu wanasafiri kutoka mbali kufuatilia kesi zao, lakini hukuta wafanyakazi hawapo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wengine wote wa Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri mnayofanya kuendelea mambo ya ardhi na makazi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri ahadi ya Serikali aliyotoa juu ya kutatua mgogoro wa mpaka ambako ulisababishwa na watumishi wa ardhi Iramba Kiomboi. Mpaka kati ya Iramba Magharibi na Iramba Mashariki huwa unafuata mlima (ukuta) wa bonde la ufa unaoanzia kilomita tano toka kijiji cha Tumuli unapita Kinampanda, Kinakumi hadi kufika mpaka wa eneo la Kidaru, eneo lote lingine lililoko chini ya mlima huo ni eneo la Iramba Mashariki. Vijiji vya Tumuli, Lyelembo, Yulamusoni, Msingi Kitula Mando, Kina Nkamba, Mgimba, Mkiko na Lugongo. Mpaka sasa eneo la Kina Nkamba kuna sehemu watumishi wa ardhi (Manase) ambaye kwao ni Kunakumi yeye na wenzake walilazimisha kuwa eneo hilo lipo Iramba Magharibi. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri waliotangulia walitoa ahadi ya kumaliza tatizo hilo haraka sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwanza kwa sababu alikuwa Mkuu wa Wilaya Iramba na anayafahamu sana maeneo haya, asaidie kuondoa mgogoro mkubwa unaoendelea sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi wanataka wapimiwe maeneo yao nchi nzima, lakini gharama ni kubwa sana na pia wapimaji hawatoshi. Tunaomba sana gharama ziangaliwe upya na wapimaji waongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kupeleka miliki ya ardhi kwenye Serikali za vijiji na pia vijiji kupewa uwezo wa kutatua matatizo yanayojitokeza. Mpaka sasa viongozi wengi wa Serikali za vijiji hawaelewi sheria hii na pia mpaka leo hawajapata Sheria ya Ardhi iliyotafsiriwa Kiswahili. Tunaomba sana uongozi wa vijiji na Mabaraza ya Kata wapewe elimu ya kutosha kuhusu sheria hii na kazi za Mabaraza

husika ili wananchi wetu wasiendeleo kuumia mpaka sasa watendaji wa vijiji na Kata bado wanawaonea sana wananchi kuhusiana na mambo ya ardhi.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake kwa kuendelea kutupa uzima tulionao leo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna na Watendaji wote kwa kuandaa bajeti hii inayotoa mwelekeo wa kutekeleza Ilani ya CCM 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kupima vijiji 112 katika Wilaya ya Bukombe na kubakiza vijiji vingine vitano. Naomba Serikali ilete/itoe cheti cha kijiji ili wananchi waweze kupata hatimiliki za mashamba yao. Inavyoonekana, Sheria No.4 na Na.5 ya mwaka 1999 haijatumika vizuri. Hii ni kwa sababu wananchi hawajapata hatimiliki. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho awaeleze wananchi wa Bukombe ni lini vyeti vya vijiji vitatolewa ili waanze kupata hatimiliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia kuhusu mpango wa matumizi bora ya Ardhi. Kwa kuwa vijiji vingi vya Bukombe vimepimwa, naomba Serikali waje waweke mipaka kwa ajili ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bukombe, wafugaji wanapata shida sana na mifugo yao katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa mifugo na uvuvi alisema wafugaji ni wawekezaji ndani ya nchi. Kwa nini hatuweki mipaka hii katika Wilaya ya Bukombe? Naomba Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Bukombe ni lini sasa maeneo ya wafugaji yatatengwa rasmi katika Wilaya ya Bukombe?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa, napongeza kwa jitihada zake wanazoendelea kuzifanya kwa kujenga nyumba za bei nafuu. Naomba Serikali na shirika hili wapate uwezekano wa kuja kujenga Bukombe. Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wanaishi kwa shida kwa kukosa nyumba.

Kama kuna vigezo vinavyotakiwa ili shirika hili liweze kuja kujenga, naomba taratibu na masharti nipatiwe au wapatiwe uongozi wa Halmashauri ili waweze kuyatekeleza. Naamini uhitaji wa nyumba katika Wilaya ya Bukombe ni mkubwa mno.

Hata hivyo, wananchi wanahitaji nyumba hizi za gharama nafuu kwa ajili ya kununua. Naomba sana katika mipango yenu Bukombe ifikiriwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasimali muhimu kwa maendeleo ya nchi yoyote. Ardhi pia ni chanzo cha machafuko iwapo ardhi itatumiwa vibaya kwa manufaa ya wachache badala ya watu wengi. Napenda kumshukuru Mungu

kwamba tishio hilo halipo katika nchi yetu, lakini yapo matukio ya hapa na pale kati ya wakulima na wafugaji, matumizi bora ya ardhi yanapaswa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo kwa kipindi kirefu ambacho Serikali haikufanya maandalizi ya kutosha na matokeo yake kuwepo kwa makazi holela katika miji yetu mingi nchini, Lakini pia yalikuwepo makazi ya wenyeji na kwa kuwa miji inakua na kupanuka wanaondolewa katika ardhi zao na wanapaswa kulipwa fidia sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya kuanzisha Chuo Kikuu Dodoma nayapongeza sana na ni muhimu. Pamoja na umuhimu huo na ni mpango ambao haukuwepo katika *master plan* ya Dodoma, matokeo yake ardhi ya wenyeji imechukuliwa na kupewa fidia ambayo wananchi hao wamekuwa wakilalamika kwamba fidia hiyo hailingani na thamani ya ardhi na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma ni mfano tu. Yapo maeneo kama hayo ambapo wananchi hawakuridhika na fidia zilizotolewa. Ni vyema basi zoezi la kulipa fidia linapotokea liwe wazi na kwa uadilifu mkubwa na pasiwepo mwanya wa kuwanufaisha watu wachache wanaosimamia mazoezi hayo. Tathmini izingatie sana bei ya soko ili wananchi hao wapate thamani halisi ya ardhi au mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la kuongezeka kwa kasi idadi ya watu nchini, hivyo pia mahitaji ya ardhi yanajitokeza. Lakini lipo tatizo la ardhi ambazo zimehifadhiwa na Serikali kama akiba ya misitu, yaani *Forest Reserves*.

Lakini kutokana na mahitajio ya makazi na matumizi ya ardhi kwa ajili ya kilimo na ustawi wa maisha yao wamevamia maeneo hayo, na kwa sababu hakuna maandalizi ya makazi kwa wananchi hususan katika vijiji na wala elimu kutolewa hivyo wanaamua kuvamia ardhi kwa ajili ya uhai na ustawi wao. Katika hali kama hii ni lazima yawepo majibu ambayo yatazingatia mahitaji ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa limejikita zaidi katika miji mikubwa tu. Lakini Watanzania wote wanastahili kufaidi kupata nyumba hata katika miji kama Mpanda. Tunayo ardhi ambayo ipo tayari kuendelezwa, imepimwa na miundombinu ya awali ya kama barabara, mahitaji ya nyumba kwa watumishi na wananchi wa kawaida yapo juu. Sasa shirika hili litabadili mwelekeo wake na kuanza kujenga katika miji yetu ili kweli liwe shirika la Taifa na siyo la miji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio yangu kwamba Wizara imepokea maombi yangu ya msingi mawilli la shirika la nyumba kuwekeza na kujenga makazi Mpanda. Aidha, suala la makazi kwa wananchi waohitaj ardhi kwa makazi na kuingia katika hifadhi za Serikali waweze kurahisishiwa kwa kufuata taratibu kutokana na ongezeko la watu na mahitaji yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. SABELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika. Napenda kuchangia Wizara hii. Nimepata malalamiko mengi kuhusu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi. Naomba kujua kuhusu malalamiko ya wananchi wa Mkoa wa Kagera, hasa Bukoba Mkoani, kuna baadhi waligawiwa viwanja na Wizara. Baadhi ya sehemu za Kyabitembe, Mshambya, Kahoro, sio sehemu 120 tu ni nyingi tu watu wanalalamika na baadhi ya wengine walishatuma barua zao za malalamiko. Je, Wizara inawasaidia vipi baadhi ya watumishi wanye mchezo mchafu wa kula rushwa? Ni kuidhalilisha Wizara hii! Naomba Wizara itoe tamko ili wananchi wasikie Wizara inasemaje. Wananchi wengi wanalalamikia kitu cha kuendelea kulipia viwanja hivyo na ofisi inakataa kuwapimia.

Mtu anakuta majina yapo kwenye ubao, wananchi wanakwenda kupimiwa, kama hajatoa chochote wanamzungusha. Je, Wizara inajua kama kuna nyumba za *NHC* kuna watu wamekaa kwa muda mrefu sana na ofisi inapokea kodi kila mwezi, ni kwa nini Wizara isizikarabati nyumba hizo? Zimechakaa sana! Zinatia aibu sana! Je, ni kwa nini Wizara isiwauzie wananchi ambao wameishi mle kwa muda mrefu zaidi ya miaka 35 mpaka 40 wakazinunua na viwanja mbavyo vimezungushwa walivigawa? Je, ni sheria gani ya kugawa viwanja vya *open space*? Au ndiyo rushwa yenyewe? Kwa sasa wengine hawana sehemu ya kumwaga uchafu au kulima bustani.

Naomba nipatiwe majibu. Naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro kati ya ofisi ya Mheshimiwa Waziri,, mipaka ya wafugaji kwenye ranchi pamoja na Kijiji cha Bubale Kyaka, naomba Wizara ifuatilie. Mheshimiwa Rais alitoa uamuzi, lakini wananchi wanaendelea kunyanyasika kwenye ofisi za Wilaya na Mikoa.

**MHE. VICTOR KILASILE MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukanda wa kuiunchumi baharini: Tanzania inatazamia kuwasilisha maombi umoja wa Mataifa ili kuongezewa kilometa za majini 200. Serikali ya Norway imetoa dola milioni 4.6. Tanzania ilitakiwa itoe shilingi bilioni mbili. Imetoa shilingi bilioni moja tu na mwisho wa kupeleka maombi hayo ni mwezi Mei, 2009. Kama Tanzania haitakamilisha, haiwezi kuomba tena milele. Naomba Mheshimiwa Wizara aniambie kwa nini Tanzania inashindwa kujitoa hiyo shilingi bilioni moja ingine. Hii itakuwa aibu kwa nchi kama tutashindwa. Hizo kilometa 200 hapo baadaye zitakuwa na manufaa sana kwa gesi, mafuta na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko wilayani Chunya, naishukuru sana Wizara kwa kukamilisha upimaji wa mipaka ya vijiji. Lakini kuna kijiji kinachoitwa Lualaje ambapo mpaka umekigawa Kijiji katikati. Sehemu iko Chunya na sehemu iko Mbarali. Najua wamefuata *natural boundary* ya mto lakini Wizara ingeona ubaya wa kukigawa kijiji katikati. Namwomba Mheshimiwa Waziri afikirie upya mipaka ya kijiji hicho maana upande mmoja kuna makazi na shule na upande mwingine kuna makazi na makanisa na ofisi za kijiji.

**MHE. MOHAMED ABOUD AZIZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba nianze kwa kutoa pongezi za dhati kwa Shirika la Nyumba kwa kazi zuri inayofanywa na Shirika, kiasi cha kumudu kujiendesha. Tatizo kubwa linalolikabili shirika hili na madeni sugu kutoka kwa baadhi ya wapangaji. Tatizo lingine kubwa ni Taasisi za Serikali na nyingine zikiwa ni taasisi nyeti ambazo hazilipi madeni yao. Naishauri Serikali iingilie kati na ikiwezekana, mpangaji wa nyumba za *NHC* awe ni msajili wa hazina kwa watumishi wote wanofanya kazi chini ya Serikali kuu ili malipo ya pango yalipwe moja kwa moja na Hazina ili kuondoa tatizo la malimbikizo ya madeni na Hazina itakata fedha hiyo katika bajeti ya Wizara au Idara iliyopanga nyumba au majengo hayo.

Sheria ya fidia imekuwa ikilalamikiwa sana na wananchi wanoahamishwa katika maeneo mbali mbali. Napenda kutoa ushauri kwamba elimu ya ardhi itolewe kwa kina katika vyombo vya habari ili kueneza elimu hii ya ardhi ni kupunguza malalamiko ambayo hayakuwa ya lazima.

Bado lipo tatizo la ugawaji wa viwanja hasa katika maeneo ya mijini. Tatizo la *double allocation* ya viwanja limekuwa sugu na baya zaidi ni hatua zinazochukuliwa na mamlaka zao za nidhamu ambazo bado hazifahamiki kwa wananchi. Ni vyema sasa Serikali iwe inatoa taarifa kuhusu hatua za kinidhamu zilizochukuliwa dhidi ya watumishi wa Idara ya Ardhi wanaogawa viwanja kwa zaidi ya mtu mmoja.

Katika eneo hili, naomba niipongeze Ofisi ya Kamishna wa Ardhi kwa kazi nzuri inayofanywa katika usimamizi bora wa utoaji wa *Title Deed* ambazo kwa umakini wa Ofisi ya Kamishna wa Ardhi imeweza sana kudhibiti migogoro ya ardhi kwani ni kama vile haiwezekani (*next to impossible*) kwa kiwanja kimoja kuwa na *Title Deed* moja. Aidha, utaratibu wa uwekaji kumbukumbu katika Wizara ya Ardhi limeboreshwa kwa kiasi fulani, lakini Serikali inatakiwa kuongeza uwekezaji zaidi hasa katika *computer* ili kusaidia kuweka vyema kumbukumbu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya kuandaa hoja hii kwa ufafanuzi mzuri sana. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo kadhaa ambayo ningependa nipewe maelezo ya ufafanuzi kuhusu ombi langu la zamani na la kila mwaka kuomba shirika letu na *NHC* kwa kutusaidia Mkoa wa Rukwa kuwa na kitega uchumi cha nyumba za kupangisha. Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa Mikoa iliyoagizwa ipewe kipaumbele na Mheshimiwa Rais katika kuimarisha miundombinu. Sote tunajua watumishi hawaendi Rukwa kutokana na uhaba wa nyumba kwa watumishi. Pamoja na hilo, ofisi za hadhi hazipo za kutosha mjini Sumbawanga. Kwa sasa barabara ya lami ikianza tu kujengwa, kutakuwa na watu wengi watakaokwenda huko. Tunaomba tupatiwe majengo mjini Sumbawanga.



Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mengine ambayo ninampongeza Mheshimiwa Waziri kuanzisha kanda tano, mojawapo ikiwa Mbeya. Nashukuru sana uamuzi huo. Lakini naomba sasa utaratibu huu uanze haraka iwezekanavyo maana wananchi wa Rukwa tunaisubiri ofisi hii ianze ili matatizo ya kuyapeleka Dar es Salaam yawe karibu nasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa kuendelea na upuuzi wa baadhi ya watumishi kutoa *double allocation* kwa viwanja, lazima tuukemee kwa nguvu zote. Tumwombe Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu awachukulie hatua kali wale wote wanaochafua jina zuri la Wizara hii. Tuseme, afadhali tubaki na watumishi wachache waaminifu kuliko wengi wakorofi na walafi wa nguvu za wananchi wenye kipato kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la mipaka ya nchi, sehemu nyingine ni adha kubwa. Ninatoa mifano ya mipaka ya Kagera/Uganda eneo la Kakunyu ambako magomvi huwa yanatokea mara kwa mara. Pia eneo la Kyela na Malawi kwenye mto Songwe sijui nalo limeshughulikiwa namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa matumizi bora ya ardhi unasuasua sana. Ukichukua mpango wa mwaka huu, vijiji 100 tu ndivyo vitaingia kwenye mpango. Je, kwa nini wadau na Makampuni binafsi kwa kuwatumia pia wanafunzi wa vyo vyetu wakavamia nchi nzima ili tuwahi kuiweka nchi yetu katika mipango mizuri? Bila ya njia hii, mafanikio ya nia nzuri ya Wizara haiwezi kufanikiwa kwa siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CDA* kwa miaka ya nyuma, ilikuwa na mpango wa kuandaa *master plans* za miji mbali mbali. Wakati huo, miji ya Mwanza na Hai ilikuwa miongoni mwa waliofaidika katika mpango huo. Sijui hatima ya mpango huo imefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuamua ipi iwe bei ya kiwanja kwa eneo la mjini? Kwa nini viwanja vinavyopimwa katika maeneo ambayo kulikuwepo na wamiliki kimila, hupewa fedha kidogo kama fidia, lakini kulazimika kumgawia tena kiwanja eneo hilo hilo kwa bei kubwa? Vigezo gani vinavyotumika? Tupatiwe maelezo maana wananchi wanalalamika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri asimamie vizuri Wizara hii maana ina malalamiko mengi sana na nafurahi kuwa anaye Kamishna mwenye uzoefu mkubwa katika kusaidia kazi. Lakini nashauri Mheshimiwa Waziri amtumie sana Katibu Mkuu wake - Mama Sijaona ambaye naye kwa kipindi hiki alichokaa Wizarani, amenyoocha mambo mengi, watumishi wao wa Wizara wa Makao Makuu nao siku hizi huchakarika sana. Wapewe kila msaada ili kazi zisiwaelemee!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Namtakia Mheshimiwa Waziri kazi njema.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii, pia natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri za usimamizi wa Wizara muhimu kwa umma wa Watanzania, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wa Wizara wanajitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kulipongeza Shirika la Nyumba ambalo linajiendesha bila ruzuku ya Serikali, kazi zake pia ni nzuri. Katika Kamati tulipokutana Dar es Salaam tulishauri Serikali itafute utaratibu wa kuongeza mtaji ili shirika liweze kujenga majengo mia kwa mia, sio kwa kutegemea ubia. Ni vyema Serikali ikalieleza Bunge juu ya hatua zilizotekelezwa kukiunda chombo chao hicho. Hii itasaidia kujenga nyumba na kuuza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa kuendeleza viwanja (*plot development revolving fund*) PDRF kitu hiki iwapo tutakiendeleza tutaifanya miji inayokuwa kupangwa vizuri na kuepusha uvunjaji wa nyumba zilizojengwa bila utaratibu. Wilaya ya Misungwi inavyo viwanja vilivyopimwa tayari. Tatizo ni fidia kwa wenye ardhi hiyo, Serikali itekeleze ahadi yake kwa Wilaya hiyo ili watu waweze kuendeleza viwanja watakavyoziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa viwanja mijini, mradi wa upimaji viwanja 20,000 umeanza vizuri, kwani maeneo waliyopima walipeleka huduma muhimu kama vile barabara, maji umeme na kadhalika. Vitu hivi hufanya mjenzi atumie barabara kufikisha vifaa sehemu ya ujenzi kwa urahisi na pia maji humfanya atekeleze ujenzi wake kwa urahisi. Kitendo hiki kimefanyika JKT Mbwani na maeneo mengine yote yaliyopimwa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo ni kwa viwanja vya Kibada; ni kwa nini barabara hazipo na maji hakuna jambo ambalo linawafanya wajenzi kubuni njia na kupitisha lori ndani ya *plot* za watu na kuharibu viwanja vya wananchi ambao hawajaanza ujenzi? Ni kwa nini kumekuwa na mapungufu hayo au ndiyo mradi umemalizika? Naomba kufahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa Wizara hii wamekuwa na matatizo ya motisha ndogo hasa Watendaji ambao muda mrefu huwa nje ya ofisi kwa sababu ya kuonyesha watu viwanja na mipaka yake na hii imetokana na kazi nzuri ya upimaji viwanja. Ni utaratibu upi hasa kwa Watendaji wa Serikali kwa ujumla kupishana malipo yao wakati kazi wanazofanya zinafanana mfano idara ya Uhasibu? Watumishi hawa huanza asubuhi kupomewa pesa kwa kuandika risiti na matangulizi ya malipo mbalimbali, lakini posho au malipo yao yako tofauti na Watendaji wa TRA. Ni kwa nini wasiwe kama wao? Naomba nifafanuliwe suala hilo. Inaonekana ni kama kuwaonea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uthamini wa mali unahitaji kuangaliwa kwa karibu sana. Idadi ya wathamini ni ndogo, hawatoshi, mfano Jiji la Mwanza. Mthamini huyo ndiye hulazimika kuthamini mali za Misungwi pindi panapohitajika. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kuajiri watu hawa kwa wingi. Hii itasaidia sana kama kila Wilaya itakuwa na watumishi hawa wa uthamini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la baadhi ya Halmashauri zilipima viwanja na kuvigawa wakati ramani ya eneo husika haijapitishwa. Jambo hili limewafanya waliojenga kukosa huduma za mikopo kutokana na kutokuwa na hati. Mfano ni eneo la Kilimahewa Mwanza, hadi sasa bado ramani haijatoka. Ni vyema Serikali ifuatilie eneo hilo ili ramani itoke na watu walio na viwanja waweze kupata hati wakope waendeleze viwanja na shughuli zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lina Bodi ya Ukandarasi kama mkandarasi daraja la pili. Chombo hiki ni chombo cha Serikali na zipo shughuli za umma zinazoweza kutekelezwa na chombo hiki. Hivyo ni vyema chombo hiki kikatumiwa kuwanufaisha Watanzania kwa ujenzi utakaofanywa na chombo chao, hivyo mzunguko utabaki nchini tofauati na tunapowapa wakandarasi toka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nategemea majibu toka kwa Serikali, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kumtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wanaomsaidia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa J. Z. Chiligati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawahi kuchangia Bajeti ya mwaka 2006, 2007 na leo mwaka 2008 nachangia tena. Ofisi ya Mheshimiwa Waziri ni sugu. Suala la *TIRDO* kumegwa ardhi yao na kuwapo *CCBRT*, *CCBRT* wana hati, *TIRDO* mpaka leo hakuna hati. Ni tatizo! Nimefuatilia sana hata kwa simu, lakini imeonekana hili suala lipo nje ya uwezo wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba: Je, huo sio ufisadi? Tatizo ni nini? Nimegundua hata michango ya humu ndani haisaidii. Naomba nijibiwe leo na kama haitawezekana, basi Mheshimiwa Waziri ataniwia radhi na nitaita kama hoja binafsi Bungeni au CCM.

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninawapongeza wote wanaohusika na Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi wanaishi vijijini, lakini pia wana maeneo yao makubwa kama mashamba, nyumba na maeneo makubwa ya ardhi. Kwa kuwa maeneo yao hayajapimwa kitaalam, naomba kujua Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha maeneo yao ili angalau nao waweze kupata dhamana ya kuchukua mkopo kwa kutumia nyumba zao na ardhi kubwa walionayo? Naishauri Wizara ijaribu kuliangalia kwa upya suala hili kwani ni muhimu sana kwa wananchi maeneo ya vijijini ambako maeneo yao hayajapimwa na hawana hata hati za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu wananchi ambao mradi wa ujenzi wa barabara zimepitia katika maeneo yao. Kwa kuwa kuna wananchi ambao nyumba zao maeneo mengi tu zimechorwa 'X' na ujenzi unaendelea na wananchi hao wakakubaliana kuhama maeneo hayo, naiomba Serikali ijitahidi kuwalipa hata wale wachache ambao hawajapata haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na maeneo ya vijijini ambayo hayajapimwa, bado kuna maeneo mengi Wilayani (mjini), hapajapimwa. Naiomba Wizara ya Ardhi ipime maeneo mengi ya mjini ili miji iweze kuonekana na majiji yaweze kuonekana vizuri zaidi na wananchi wengi wanaoshindwa kuendelea na ujenzi, kwa sababu viwanja havijapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niombe Serikali iweze kuipa kipaumbele Wizara hii, ni jinsi gani Wizara itaweza kufanikisha, kukamilisha utendaji wake, kwa sababu, pesa inayotengwa ni kidogo sana kiasi kwamba hata kama wangukuwa na juhudi kiasi gani, bila pesa ya kutosha, naomba kipindi kijacho Serikali iongeze fungu zaidi ili wizara ifanye vizuri kazi zake.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na mipango mizuri yenye lengo la kupunguza kero za Watanzania katika Wizara hii ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo michango michache kama ifuatavyo, kwanza ni kuhusu mikopo kwa ajili ya upimaji wa viwanja una umuhimu mkubwa kwa ajili ya kupunguza ujenzi holela. Naiomba ofisi ya Mheshimiwa Waziri itenge fedha zaidi katika mfuko huo pamoja na kulegeza masharti ili Halmashauri za Wilaya nyingi ziweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vingi hasa vya taasisi za Serikali vimeshindwa kupimwa kutokana na upungufu wa wapima na wathamini wa ardhi walioko katika halmashauri zetu. Hivyo napenda kufahamu mpango wa Waziri kupunguza tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Mara hususani Wilaya ya Tarime, kumekuwepo na ugomvi mkubwa wa ardhi wa muda mrefu na umesababisha watu wengi kupoteza maisha. Mkoa ulibaini kuwa tatizo kubwa ni ugomvi wa mipaka wa muda mrefu. Je, ni lini Serikali itatoa fedha zilizoombwa na mkoa za upimaji wa mipaka ili kuondoa kero hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, *open space* katika maeneo mbalimbali yamekuwa yakivamiwa kwa matumizi yasiyokusudiwa na vile vile kutokana na ujenzi holela katika maeneo mapya unasababisha *open space* kutopangwa. Napenda kujua mipango ya Wizara ya kuhakikisha hizo *open space* zinaendelea kuwepo. Ahsante naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa taarifa yake ambayo imelenga mikakati

ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005. Pia natoa pongezi hizo kwa Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa utendaji wao katika kutekeleza majukumu waliyopangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie maeneo machache tu ambayo yanaendelea kuleta kero kubwa kwa wananchi, mashirika mbalimbali ili Wizara kuweza kuyafanyia marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu baadhi ya nyumba za *NHC* ambazo wamepangishwa wananchi kwa muda mrefu bila kutoa malipo yoyote na bado hawajahamishwa. Nyumba hizo wanaendelea kuishi bila hata kuzifanyia matengenezo. Wanatumia kuni, vyoo vibovu, makaro mabovu. Je, Serikali au Wizara haioni kuwa sasa imefika wakati wa kuzipitia nyumba hizo na kuweka mikakati ya kuwahamisha watu hao au kuwalazimisha kuzifanyia matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wapo wananchi ambao wamekosa makazi na kwa kuwa zipo nyumba ambazo mpaka sasa hivi hazina watu ambao wanaishi humo, je, Wizara haioni kuwa wanapokwenda watu hao Shirika la Nyumba kutaka wapangishwe nyumba hizo vipingamizi ambavyo havina msingi ni kuwadhalilisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa Kiwanja kati ya Shirika la Tija la Taifa na Chuo cha *IMTU*. Kwa kuwa Wizara ya Ardhi iliwamilikisha Shirika la Tija la Taifa (*NIP*) kwa muda mrefu na wakaweza kujenga uzio uliogharimu shilingi milioni 46 na kwa kuwa fidia iliyotolewa na ile iliyobaki kamwe haifidii gharama walizotumia shirika hilo, na kwa kuwa Chuo cha *IMTU* hadi leo hii hawajakiendeleza kiwanja hicho ambapo inafikai miaka mitatu sasa, je, Serikali inatuambia nini kuhusu mgogoro huo? Je, Shirika la Tija la Taifa, Wizara imeona hivyo ni kuwatendea haki kwa kuwanyang'anya umilikishwaji huo? Je, kwa nini mgogoro huu umechukua muda mrefu bila Wizara kuupatia ufumbuzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo machache naomba kuwasilisha.

**MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na wenzangu wengi niwapongeze Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri na mipango mizuri. Naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu kutopima viwanja kwa haraka inasababisha ujenzi holela. Hiyo imesababisha *squatters* wengi wa kuharibu mipango mizuri ya Mipango Miji. Naomba tuimarisha Idara ya Upimaji wapewe nyenzo na siku nyingine misaada ili kazi hiyo iwe nyepesi, pili, wathamini wachache Wizara ya Ardhi. Hiyo inasababisha ucheleweshwaji wa uthamini wa nyumba zetu ili kupatiwa mikopo. Mikopo ikichelewa na mipango ya maendeleo huchelewa. Hivyo Wizara yote ina mipango gani ya kuongeza wathamini ili watu wapate mikopo yao mapema?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, vitengo vya ardhi katika halmashauri huchelewa au hugawa viwanja mara mbili mbili hivyo kusababisha kero na migogoro au kwenda

Mahakamani. Wizara ingetoa kompyuta na vitendea kazi muhimu ili kusiwe na marudio, na nne, mikopo ya nyumba ingetolewa hata kwa wafanyakazi wasio wa Serikali. Nyumba bora zinapunguza magonjwa ya milipuko badala ya familia nyingi kurundikana kwenye nyumba moja au chumba kimoja.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaali kuamka nikiwa mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa nitoe mchango wangu katika Wizara husika kwa kuzingatia umuhimu wa ardhi utapata mshangao ukitazama Bajeti ya Wizara mama ilivyo. Huwezi kusema wala kusengenya dhana ya kusema Serikali iko tayari ikazalisha kupitia ardhi. Kilimo kinahitaji ardhi, kilimo cha biashara katika nchi yetu hadi leo imeshindikana kupanda. Hii inatokana na vijana kuhama vijiji vyao na kwenda mijini. Kufanya hivi hupelekea miji yetu watu kusongamana. Miji inapojaa hupelekea ongezeko la watu omba omba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mipango miji, ukiangalia sasa mara nyingi watu wetu hufa kwa kuangukiwa na magorofa. Serikali sasa inapaswa itumie ardhi yetu kwa kujenga miji mipya itakayoweza kupunguza watu mijini, ardhi tunayo. Kwa kufanikisha ujenzi wa miji mipya kwa kujenga nyumba bora zenye bei nafuu kutaweza kuwaondolea matatizo watu wetu katika kuishi. Pia kufutilia Pato Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu waliomilikishwa ardhi. Kitendo hiki sio kibaya ila kinahitaji ukomo. Serikali ni vyema itakapowamilikisha watu ardhi wapewe kwa muda mahusisi. Ardhi ni lazima kwa Watanzania. Baada ya maelezo hayo kwa ufupi nasema ahsante.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kupongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Ningependa kumpongeza Mheshimiwa John Chiligati, Waziri wa Wizara hii, Katibu Mkuu, Kamishna, Wakurugenzi na wataalam mbalimbali kwa hotuba nzuri. Ninawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa hotuba hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitauielekeza katika mambo muhimu yafuatayo, kwanza ni kuhusu uhaba wa ardhi. Wilaya ya Korogwe kwa muda mrefu imekuwa na uhaba wa ardhi. Wananchi wengi wanashindwa kupata maeneo kwa sababu hawana ardhi ya kilimo na makazi. Zipo kampuni zilizouzwa mashamba ya kuzalisha katani lakini wameshindwa kabisa kuyaendeleza. Mashamba hayo ni Ngombezi, Tabora Mswaha, Magoma, Kurasi, Mangunga Chake Hale Mwelya na Hale Mwakinyumbi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi baada ya mashamba haya kufa, wamelazimika kuishi kando kando ya mashamba hayo na kuwa wakulima. La

kusikitisha sana hawana ardhi ya kulima. Matokeo yake wananchi hawa ni kwa kuishi maisha ya kimaskini sana. Toka nimekuwa Mbunge mwaka 1995 hadi leo mwaka 2008 sipati jibu la uhakika, kuhusiana na namna Serikali inavyotakiwa kuwasaidia wananchi hao kupata ardhi ya kulima.

Mheshimiwa Waziri mashamba haya ni mapori hayafanywi chochote *Katani Ltd.* wameshindwa kabisa kuyaendeleza wananchi wanaomba muda mrefu lakini hakuna jibu lolote. Suala hili sasa limekuwa la kisiasa na wapinzani wanachukulia suala hili kama Wizara yetu imeshindwa kutekeleza Ilani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni kuwa kwa kuwa Rais amekwishatangaza kuomba mashamba makubwa yalisiyoendelezwa wapewe wananchi, nasisitiza suala hili lipewe kipaumbele ili kuokoa hali mbaya ya Wilaya ya Korogwe. *Katani Ltd.* wameshawishi wananchi walime mkonge kwa njia ya *small holders*, lakini hali sio nzuri sana kama ilivyotarajiwa licha ya sisi viongozi wa kisiasa kuliamisha jambo hilo muhimu. Kama kuna kero sugu Korogwe ni hiyo ya mashamba. Naomba sana suala hili lipatiwe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kutuletea hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 inatoa maelekezo vizuri kabisa kwamba ardhi ya Tanzania ni mali ya wananchi na hakuna wageni kumilikishwa ardhi, wapeni wanaokodisha ardhi kwa muda fulani wa makubaliano. Ni kwa nini wawekezaji hapa nchini wamekuwa wanamilikishwa ardhi ya wananchi mfano mwekezaji wa *Gameti Game Reserve*?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tanzania wamekuwa wakichanganywa kwa fedha kidogo sana na hivyo kuuza ardhi yao bila kujua athari zake. Kwa kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu sheria za ardhi na kwa kuwa hali ya umaskini uliyokithiri ndiyo inayopelekea wananchi hao kuuza ardhi kinyume na taratibu. Serikali inachukua jukumu gani la kuelimisha jamii yote ya Watanzania kwa ngazi zote kuanzia kaya, vitongoji, vijiji na hata Taifa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kisheria wananchi wanapohamishwa kwenye eneo wanaloishi na kuliendeleza kwa sababu za kupisha mradi wa maendeleo wa jamii, ni kwa nini Serikali isingekuwa inafanya tathmini kwanza na kuwalipa ndipo iwaondoe badala ya kuvunja nyumba zao kwanza bila kuwalipa na kuwaacha wanateseka huku Wizara ikichukua muda mrefu kuwafidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwaeleze wananchi wa kata za Vumilia na Ushokola wilayani Urambo ni lini watalipwa fidia ya nyumba zao

zilizovunjwa tangu mwaka 2005 kwa sababu ya kupitisha nguzo za umeme hadi leo hajalipwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya makazi karibu mikoa yote inasitikisha sana. Hali hii inasababisha wananchi kujenga bila mpango na huduma muhimu kwenye makazi kukosekana. Inasikitisha zaidi hata miji midogo mipya inayoanzishwa bado imeanza kujengwa bila mipango miji. Ni lini Serikali itaanda mipango miji kwa mikoa yote na hasa maeneo ambayo bado hajaendelezwa ili tuweze kuwa na miji yenye viwango? Tutaendelea kujenga kiholela hadi lini? Ni lini Wizara itaandaa mpango mkakati wa kuhakikisha kuwa tunakuwa na programu endelevu ya kuboresha miji yetu ione kane kama miji ya wenzetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma ni Makao Makuu ya nchi na ndivyo ilivyo na Mkoa huu sasa unakuwa kwa haraka sana. Lakini sioni mpango maalum wa kupanua barabara zetu. Serikali imetulia, watu wananchi wanaendelea kujenga hadi njiani na barabarani wakati ni lazima baadaye zitahitaji kupanuliwa. Serikali inasubiri waje waanze kubomoa, ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ndiyo ilivyokuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam huko nyuma na sasa kuwekuwa ni tatizo kubwa sana. Foleni za barabarani zimekuwa ni kero hali inayoathiri hadi uzalishaji na uduni wa nchi, wafanyakazi hawafiki ofisini kwa muda unaotakiwa na hata wakifika wanaanza kuwaza jinsi ya kurudi nyumbani na wanafika usiku sana wamechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ndiyo tunayoitaka pia hapa Mkoa wa Dodoma ambapo kwa miaka mingi Wizara inajua umeandaliwa, ni mji mkuu wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ihakikishe imeweka mpango kabambe wa kuendeleza mji/mkoa huu bado mapema, tuisubiri kuja kuingiza gharama za kufidia kwa kuvunja nyumba za wananchi.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nimshukuru Mola kwa kunijalia siku ya leo kuamka hali nikiwa mzima niseme *Alhamdulillah*. Pia nimpongeze Waziri kwa hotuba yake iliyojaa imani, mwelekeo na nia njema kwa Watanzania. Baada ya maelezo yangu hayo sasa nianze kwa kutoa mchango wangu katika hotuba hii husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema, ardhi ni eneo pana la kuweza kutuletea maendeleo. Kuna utaratibu maalumu wa kumiliki ardhi hapa nchini. Kwa wale wa mirathi (ukoo) na wale wanaomilikishwa ardhi. Kwa upande wa watu waliopata ardhi kwa njia ya mirathi, mara nyingi haki yao huwapatia balaa na Serikali kwa sababu hati ya kumiliki kwa nini itokee hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wale wanaomilikishwa ardhi, kwa nini Serikali isitoe ardhi kwa muda maalum. Kutofanya hivyo ni kuwapa wageni ardhi yetu.



Ardhi ina maeneo makubwa ambayo ni matupu, kwa nini Serikali haijandaa utaratibu wa kuwapa watu maeneo hayo? Utaratibu huo utaweza kupunguza msongamano katika miji, Serikali iandae miji mipya kwa utaratibu maalum wenye umbile la miji ya kileo. Ramani za nyumba ziwe aina moja kutoka mji hadi mji. Hii itendeke pale mtu anapopewa kiwanja apewe na ramani ya ujenzi unaotakiwa. Serikali itakapofanya hivi miji itapunguza msongamano wa watu pia sura ya nchi yetu itang'aa. Kwa kuangalia hili mji uwekewe maeneo ya shule, hospitali, ofisi za Serikali na pia viwanja vya kuchezea mpira (viwanja vya michezo) na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu yale maeneo ya madini, mara nyingi Serikali imekuwa chachu kuwafitini wananchi wake. Hii inafanyika pale ardhi inapogundulika ina madini. Ubaya zaidi wachimbaji madini wadogo wadogo ndio wasiothaminiwa kabisa. Kwa nini Serikali isiwatengee maeneo watu wetu, jambo ambalo ni kuwapa ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo naitakia mema Wizara ili iweze kufanikisha azma yake.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Wizara, kwa maandalizi ya Bajeti nzuri na uwasilishaji mzuri. Nawapongeza kwa uendeshaji mzuri wa shughuli za Wizara. Matatizo mengi hasa ya ardhi yanaendelea kupungua.

Suala la wageni kupewa ardhi, pamoja na sheria kuzuia, lakini ziko njia ambazo wageni wameendelea kutumia ili kujipatia na kuendelea kutumia ardhi, kwa mfano, kuunda makampuni na hivyo kumilikishwa ardhi makampuni hayo na hivyo wageni kufaidika na ardhi kupitia makampuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupima viwanja, ni muhimu kupima miji mipya kabla wananchi hawajajenga sana, hii ni kuepuka na wananchi kulazimika kuvunjiwa nyumba ili kupima miji. Naunga mkono hoja.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri na wataalam wake wote kwa kuandaa hotuba hii nzuri iliyogusa sera ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina eneo kubwa kuwa la ardhi kiasi *square kilometer 930,000* na Watanzania wapato shilingi milioni 38; hivyo kulingana na eneo tulilionalo tunaweza kufikia haiwezi kuisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Watanzania waliomilikisha eneo kubwa sana kwa kilimo au mifugo lakini hawalimi wala hawafugi. Pamoja na kuwa watu hao wanalipa kodi lakini kitendo cha kuhodhi ardhi bila ya kuitumia ipasavyo ni kosa. Lakini baya zaidi ni kuwa baadhi ya maeneo hayo yamepakana na vijiji na wanavijiji wanakosa maeneo ya kulima na wanalazimika kuwapigia magoti wamiliki hao ili wapate angalu nusu ekari ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni udhalilishaji, Serikali inapaswa kuliangalia hili ili ardhi kama raslimali iwaneemeshe wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la uendelezaji wa maeneo mapya wananchi waliopo hapo kwa miaka mingi huonekana kama wavamizi hivyo busara haitumiki katika kuwaondoa. Mara nyingi nyumba zao huvunjwa chini ya usimamizi wa vyombo vya dola. Mtu anajiuliza ni kwa nini Serikali haijifunzi kwa hili, kwa kuongea na wahusika, kuwafidia au kuwatafutia maeneo mengine kabla ya zoezi la bomoa bomoa halijaanza. Mifano ya aina hii ni mingi na imeenea kila pembe ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linalosumbua Watanzania ni pale eneo linapogawiwa kwa wananchi mbalimbali yule mmiliki wa awali hapewi eneo la kutosha kwa ajili ya matumizi yake binafsi, mara nyingi anapewa kiwanja kimoja tu. Tunao mfano wa eneo la Kibada *block 23*, mmilikaji wa eneo lile amedhalilishwa sana kwa kupewa kiwanja kimoja tu wakati alikuwa anamiliki zaidi ya ekari mia moja. Je, huu si udhalilishaji au ukandamizaji Serikali lazima iwajali raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni nyumba za *National Housing* zinazokodishwa kwa wananchi mbalimbali. Nyumba hizi hasa zile za Kariakoo Dar es Salaam nyumba baada ya kukodishwa, wale waliokodi nao huzikodisha kwa bei kubwa sana, karibu hata mara kumi zaidi. Napongeza hatua ya sasa ya kuzipandisha bei nyumba hizo kwa asilimia 40. Ni hatua nzuri, lakini zoezi hili lirudiwe tena baada ya miaka miwili ili wajanja wasipate mianya ya kufanya biashara nyuma ya mgogo wa Shirika la Nyumba.

**MHE. MKIWA A. KIMWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo imejaa matumaini, lakini tunaomba matumaini hayo yasiishie kwenye makaratasi na iwe ni changamoto huko Wilayani, maafisa ardhi waache ukiritimba na waweze kuwapa watu ardhi kwa kanuni na taratibu zilizopo, pia kuzingatia sheria iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba upimaji wa mashamba na viwanja tunaomba uwe wazi na watu ambao wananyang'anywa mashamba yao na kuwa viwanja, tathmini iwe wazi. Wakati Halmashauri wanapeleka wathamini na wapimaji viwanja hivyo wawe wazi thamani ya wenye ardhi hiyo, kwani wameitunza kwa muda mrefu. Hivi sasa wapimaji wa viwanja katika jiji la Mwanza, wameleta malalamiko mengi kwani, wanapopima mashamba ya watu na kuwa viwanja, wananchi hawapewi thamani ya ardhi yao. Hujua tathmini hizo wakati wa malipo, na ndipo hujua kama wamelipwa malipo ya chini. Malalamiko haya yameonekana sana katika Jiji la Mwanza maeneo ya Kiseke, Senya, Busweru na na kadhalika kuwa zaidi, mpima viwanja hivi sasa ni Halmashauri ya Jiji, mgawa viwanja ni Halmashauri ya Jiji (muuzaji) mthamini viwanja ni Halmashauri ya jiji, hivi kweli kama mwananchi kaonewa katika uthamini wa ardhi yake amwone nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni mahakama, halmashauri ina mwanasheria? Huyu mwanakijiji atakuwa na uwezo wa mwanasheria kweli? Naiomba Wizara

iliangalie hili kwani ni kikwazo kwa wananchi. Pia naomba ufafanuzi kuhusu tathmini ya kuthamini na malipo kwani hapo Jijini Mwanza kunabibi mmoja ambaye eneo lake lilichukuliwa na Kanisa Katoliki na palikuwa na kibanda watu wakiwa wanaishi ndani. Thamani yake ilikuwa kama milioni moja na kidogo, lakini mpaka leo hajalipwa na sasa yapata kama miaka kumi. Tangu enzi za Mkuu wa Mkoa Bwana Mashishanga hadi hii leo. Watu wengine wamelipwa lakini bibi huyo bado hajalipwa na nyumba yake hivi sasa imezuliwa na baadhi ya kuta zimebomolewa. Bibi huyo hana uwezo wa kuwa anapanda mlima wa Kawekamo kila siku kumtafuta *Pastor*, na tangu uthamini ufanyike hadi leo bidhaa zimepanda bei na haziendani na thamani hiyo. Sijui ninyi kama wanamaendeleo na mna wanasheria, hivi bibi huyo afanyeje apate malipo ambayo yanaenda na wakati wa sasa? Tunawaomba msimamie haki na kuelimisha watu ambao uelewa wao ni mdogo sana. Wanapoteza haki zao kwa kutokuwa na uelewa wa kutosha. Ahsante.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri inayotia matumaini makubwa katika sekta hii muhimu kwa uhai na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wote wa Jimbo la Kwimba napenda kusema wazi kuwa naunga mkono hoja hii. Aidha, pamoja na pongezi hizi naomba leo maelezo dhahiri yatolewe na Waziri kuhusiana na mambo mawili ambayo ni kero sugu za sekta hii katika jimbo la Kwimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni mashamba yaliyomilikishwa katika Jimbo la Kwimba katika kata za Hungumalwa na Mwamala yamekuwa na migogoro kwa muda mrefu kutokana na wawekezaji hawajawahi kuyaendeleza kikamilifu tangu wawekezaji hao wamilikishwe ardhi. Mashamba haya yalimilikishwa kwa wawekezaji hao bila ushirikishi wa jamii iliyokuwa ikiishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo halmashauri ya wilaya ya Kwimba na Mkoa wa Mwanza wamejitahidi sana kuomba kufutwa kwa hatimiliki ya mashamba haya. Lakini kwa masikitiko makubwa Serikali imekuwa kimya kwa maombi hayo rasmi toka Mkoa wa Mwanza chini ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa Mashishanga na Halmashauri ya Wilaya chini ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya Kanali Mstaafu Peter Madaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Waziri ana hitimisha hotuba yake afanye mambo matatu, kwanza, atoe taarifa ya maendeleo ya ombi la Mkoa na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba la kufutwa hatimiliki ya mashamba yote hayo kama yalivyo. Pili, hatua nyingine yoyote ya kumilikisha mashamba hayo yote isifanyike bila kuwashirikisha wananchi wa vijiji vya Ilula, Shilembo na Shigangama katika kata za Hungumalwa na Mwamala na tatu, Mheshimiwa Waziri, mashamba yaliyokuwa yakijulikana kama *Adster farms* yalibadilishwa kuwa *Ilula corporation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo wananchi toka katika vijiji hivyo watakuwa kando ya redio zao kupata maelezo juu ya hatima ya mashamba hayo. Namwomba sana

Mheshimiwa Waziri asiache kutoa maelezo ya hatma ya mashamba hayo yaliyotwaliwa na wamiliki hao kwanza miaka ya 1980 hivi, hadi leo hayaendelezwa yamekuwa maeneo ya migogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja nikisuribi maelezo.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani kwa matayarisho mazuri sana ya hotuba ya Bajeti ambayo imesheheni mambo mengi muhimu na hatua mbalimbali zinazochukuwa kukabiliana na changamoto zinazoikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKURABITA, napongeza jitihada za Serikali katika utekelezaji wa sera hii. Lakini siridhishwi na kasi ya utekelezaji. Naishauri Wizara iongeze kasi ya utekelezaji ili wananchi wengi zaidi wafaidike na utaratibu huu mzuri.

Kuhusu Benki ya mikopo ya nyumba, nazipongeza juhudi za Serikali kuelekeza kutunga sheria itakayoanzisha mikopo ya umiliki wa sehemu ya jengo. Kama nilivyoeleza hapo juu, siridhishwi na kasi ya utekelezaji. Kwa nini uanzishwaji wa benki hiyo umechelewa sana? Kuna matatizo gani? Naishauri Serikali/Wizara iharakishe ukamilishaji wa sheria hii kwa ajili ya kuipa msukumo sekta ya ujenzi wa nyumba/makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara, sehemu kubwa ya shughuli za Wizara zinatekelezwa na Halmashauri za miji. Nina wasiwasi kama halmashauri za miji zina uwezo wa kutosha hususan, kiutaalam kuweza kutekeleza majukumu ya Wizara kikamilifu. Naishauri Wizara ihakikishe kwamba halmashauri zinawezeshwa katika nyanja zote ili utekelezaji wa majukumu ya Wizara yaweze kutekelezwa kwa mujibu wa mipango yake kama inayoainishwa katika hotuba hii ya Bajeti.

Kuhusu huduma za maji machafu (mifereji) barabara na kadhalika katika viwanja kabla ya ujenzi, sehemu nyingi mpya za ujenzi (*new plots*) hazina huduma muhimu kama vile vile barabara nzuri, mifereji ya maji na kadhalika. Aidha, Serikali inakusanya kodi za nyumba na viwanja bila kuboresha huduma muhimu katika makazi ya watu. Naishauri Serikali/Wizara ihakikishe upatikanaji wa huduma muhimu katika maeneo mbalimbali yanayotarajiwa kuanzisha makazi ya binadamu kabla ya kuruhusu ujenzi hususan katika maeneo mapya.

Kuhusu utaratibu wa kuzikopesha halmashauri ili ziweze kutekeleza wajibu wake wa kupima viwanja, napongeza utaratibu wa Serikali wa kuzikopesha halmashauri za miji ili kuzijengea uwezo wa kupima viwanja katika maeneo yao. Pamoja na utaratibu huu, inasikitisha kwamba halmashauri ya mji wa Tabora haijaweza kutekeleza wajibu wake wa kupima baadhi ya maeneo ya mji wa Tabora kama vile Kariakoo na Kidato kwa kisingizio cha ufinyu wa Bajeti! Inawezekana uongozi wa Manispaa ya Tabora haujui kama kuna fursa ya kukopa toka Wizarani kwa ajili hii. Napendekeza Wizara iitangaze fursa hii kwa manispaa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Ardhi – Tabora, hali ya majengo ya chuo hiki madarasa, ofisi za wakufunzi, mabweni na kadhalika hairidhishi. Naishauri Wizara itenge Bajeti maalum kwa ajili ya kuboresha majengo haya pamoja na mandhari ya chuo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Katibu Mkuu wa Wizara kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa na kuchanganuliwa maeneo yote muhimu ambayo yamepangwa kufanyiwa kazi mwaka 2007/2008 nawapongeza wafanyakazi wote kwa kazi nzuri ambazo wamekuwa wakifanya katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina machache ya kuyasema. Kuna maduhuli (mapato) yanayopaswa kukusanywa na Wizara hii kwa mfano, kodi ya viwanja, upimaji na viwanja na mengineyo. Naomba kujua Wizara imejipanga vipi au mkakati gani umewekwa ili kuhakikisha kuwa malimbikizo yote ya kodi ambayo hayajakusanywa hasa kwa upande wa viwanja ambavyo vilitolewa kwa wananchi lakini hawajawahi kulipia tangu wamepewa mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji na utoaji wa hatimiliki ya viwanja na mashamba umekuwa ukisuasua sana kwa muda mrefu, kwa uamuzi huu wa kuweka ofisi ya kanda ili kusogeza huduma ya utoaji wa hatimiliki kwa wananchi ni imani yangu tatizo hili litapungua lakini naomba kujua ni lini hatimiliki ambazo zimekuwa zikifuatiliwa na Shirika la Taifa la Nyumba na *SIDO* zitakamilishwa ili waweze kuendelea kukamilisha majukumu yao? Kuna viwanja vitatu vya *SIDO* vilivyoko Mkoa wa Singida vilivyokuwa vimemilikishwa kwa Shirika la *SIDO* na kupewa hatimiliki. Lakini viwanja hivi vimechukuliwa na kujengwa nyumba na Serikali na nyumba hizo kuuzwa kwa wafanyakazi. Je, ni utaratibu gani ulichukuliwa katika kuwanyang'anya *SIDO* viwanja hivyo bila kufuta hatimiliki hizo, na kuna utaratibu gani upo kuhakikisha kuna wanaopewa viwanja vingine kama fidia yao au kwa nini nyumba hizo zisichukuliwe na *SIDO* kwa vile viwanja hivyo wanavimiliki?

Je, Serikali au Wizara inalisaidiajie Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*) katika kutekeleza majukumu yake na katika kujiendelesha lenyewe? Kwa sababu limekuwa likionekana kama Shirika la kutoa huduma zaidi kuliko kujiendesha kibiashara, hasa pale watu waliouziwa nyumba au kupangishwa nyumba za *NHC* wanaposhindwa kulipa, wakishitakiwa au kutolewa ndani ya nyumba hizo Serikali au mahakama huingilia kati kitu ambacho kinakwamisha sana maendeleo ya shirika hili. Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kubadili au kurekebisha sheria iliyoanzisha *NHC* kama ndiyo kikwazo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilishiriki vipi katika kutathamini nyumba na mashamba ya wananchi wa Mbarali wa vijijij saba na vitongoji vinne walihamishwa ili kupisha upanuzi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Kwa kuwa kuna sheria mpya ya ardhi bila nyumba, mazao ina thamani, je, katika tathmini hii ilizingatiwa? Je, kwa sasa Wizara ina mkakati gani umewekwa ili kuhakikisha wananchi hawa wanapimiwa upya mashamba yao na viwanja vyao na kupata hatimiliki kusudi wasije wakasumbuliwa tena lakini vile vile kuwa na uhakika na mahali walipohamia ikiwa ni pamoja na upimaji na utoaji hatimiliki za vijiji vipya? Naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri Chiligati, Katibu Mkuu Salome Sijaona na watendaji wa Wizara hii kwa mabadiliko makubwa mazuri yanayoendelea kufanyika katika Wizara hii. Ninayo maoni machache juu ya Jimbo la Mbinga.

Katika hotuba hii iko mikoa, wilaya zimejitokeza katika miradi mbalimbali ya Waziri kama upimaji vijiji usajili wa hati, nyumba za kisasa lakini sioni Mkoa wa Ruvuma na hasa Mbinga. Kuhusu upimaji na ramani upo mgogoro kuhusu mpaka wa Ziwa Nyasa kama ilivyoenezwa katika hotuba. Mgogoro huu utaisha lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nyumba za makazi lini Mbinga itafikiriwa kuwa na mpango kabambe wa mji kama ilivyo kwa Chato? Na kuhusu suala la Teknologia, halmashauri ya Mbinga itapewa lini vitendea kazi hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango bora ya matumizi ya ardhi, naomba Mbinga pia iwekwe katika mpango huo kwa sababu ni wilaya ya mpakani, kuna hifadhi, misitu na kadhalika.

Kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 60 *NHC* imejenga nyumba za kupangisha katika miji midogo ya Chalinze (kata) na Ruaha (wilaya). Nilipochangia mwaka 2006 niliomba shirika hili lijenge nyumba katika wilaya na hasa zile zilizo pembezoni. Nilifuatilia *NHC* kwa kuwaandikia barua ambayo nilijibiwa kwamba *NHC* itafanya utafiti wa kujenga nyumba mikoani ili kujiridhisha. Bila shaka wamefanya na ndio maana *NHC* wamejenga Chalinze na Ruangwa. Ni jambo jema na naliunga mkono. Naomba sasa *NHC* kupitia Wizara hii ijenge jengo angalau *Block* moja ya gorofa tatu pale mji wa Mbinga.

Nikishirikiana na Halmashauri tutawapatia *NHC* viwanja na pia kuhakikisha wapangaji wanapatikana Mbinga kwa sasa imekabiliwa na tatizo la makazi kwa wafanyakazi. Hata kama ni kujenga na kuuza bado wateja watapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakubaliana nami kwamba Ruvuma haionekani sana katika mipango ya Wizara hii. Ujenzi wa nyumba na *NHC* Mbinga utasaidia sana kurudisha imani ya wananchi juu ya Serikali yao na shirika lao la *NHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii. Kwanza kwa niaba yangu na wananchi wa Jimbo langu la Mwanakwerekwe, naunga mkono hoja hii asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba hii kwa jinsi ilivyoweka mambo yake vizuri sana. Mimi naanza kuzungumzia kuhusu upimaji wa viwanja vya nyumba kwa wananchi. Mimi naomba wakati wa upimaji wa viwanja hivyo mambo muhimu lazima yapewe kipaumbele kama sehemu ya shule viwanja vya michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubomoaji nyumba kiholeala bila wananchi kupewa wakati wa kutosha wa kuhama mpango huu nao uondolewe kwa sababu wananchi huwa wanapata taabu sana. Kuhusu fidia kwa wananchi wanaobomolewa wapewe fidia haraka ili waweze kujikimu kujenga nyumba nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazidi kuunga mkono hoja hii.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuzungumzia suala ambalo Mheshimiwa Waziri amesema anatenga shilingi bilioni kumi kwa kulipia fidia ya watu Kurasini kwa madhumuni ya kupanua bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sasa ndipo tunapona kuwa sasa bandari ya Dar es Salaam imejaa na kuna haja ya kujenga bandari ya nchi kavu pale Ruvu. Nazungumzia haya kwa sababu tayari pana miundombinu ambayo inaweza kurahisisha usafiri, pale Ruvu ambapo barabara na Reli zinakutana ni tayari ni mahali bora. Nafasi ya kujenga bandari kavu ipo tele. Mahali pale pana nafasi ya kuweka sehemu za Bandari kavu kwa kila nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Ardhi isaidie Wilaya ya Morogoro Vijijini. Wilaya hii ni mpya. Hivi sasa wilaya ya Morogoro vijijini imeamua kuhama toka Morogoro mjini kwenda Kijiji cha Mvuha. Hapa ni katikati ya wilaya. Mheshimiwa Waziri tunaomba msaada wa kupimiwa viwanja vya nyumba na majengo ya wilaya. Tupo tayari hata kukopa ili halmashauri iweze kuhamia huko haraka tuwezavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyowasilisha kwa umakini. Nampongeza Katibu Mkuu na watendaji wote kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni kubwa, ina kazi nyingi na nyeti hivyo inastahili kuwa na Naibu Waziri. Hata hivyo nampongeza Mheshimiwa Kepteni John Chiligati kwa namna anavyomudu kuzifanya kazi zake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali haiongezeki lakini watumiaji wanaongezeka kwa hiyo, upo umuhimu wa kuwa na mipango madhubuti ya matumizi ya ardhi. Nchi yetu mpaka sasa ina ardhi kubwa lakini hali hiyo isiifanye Serikali kuiza kwa wageni. Pia iwepo sera nzuri na kwa kuzingatia thamani ya ardhi wananchi wanaohamishwa ili kupisha wawekezaji kama migodi kwamba wananchi hao wapewe hisa katika makampuni pamoja na fidia hiyo wanayolipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na usimamizi wa uthibiti mbovu wa Idara za Mipango Miji maeneo mengi yaliyopimwa wananchi wamejenga katika maeneo hayo. Matokeo yake maeneo hayo hayapitiki hasa katika mji wa Bukoba. Je, sasa kwa vile sasa hali ya kupitika hasa kwa magari inajitokeza ni hatua zipi zitakazochukuliwa? Upo umuhimu wa idara husika isimamie ujenzi ili kuhakikisha taratibu hazikiukiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa upangaji wa nyumba *NHC* haueleweki, yaelekea ulanguzi ndio unaoongoza ugawaji huo. Watu huuziana upangaji katika nyumba kana kwamba hazina mwenyewe. Vipi *NHC* nayo inabariki utaratibu huo au hayo inashiriki?

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na umuhimu wa thamani ya ardhi ni vyema ardhi yote na vijiji vyote vipimwe ili kuondoa utata unaojitokeza katika baadhi ya maeneo kuhusu nani mwenye ardhi.

Nakutakia kila la kheri Mheshimiwa Waziri Chiligati katika majukumu yako ndani ya Chama na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninampongeza Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri zinazoendelea na pia kwa hotuba nzuri sana iliyowasilishwa mbele yetu kujadili leo hii. Rasmi kabisa ninaunga hoja mkono asilimia mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba kuzungumzia kero za aina mbili tu, kwanza ni makazi mapya kwa watu kutoka mkoa ilibanana na nyumba za kuishi *NHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, makazi mapya kwa mikoa iliyobanana, Tanzania ni nchi kubwa yenye ardhi nzuri lakini msongamano wa watu uko kwenye baadhi ya mikoa tu ikiwemo Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Kagera na kwingineko. Mara kadhaa kauli za kisiasa zimekuwa zikitumika kuhamasisha wananchi kuhamia mikoa mingine bila mipango rasmi ikiwemo miundombinu ya barabara, maji, umeme, shule *dispensary* na kadhalika, azma hii haitekelezeki.

Swali ni lini sasa Wizara hii itaandaa sera mpya yenye mvuto wa kuchochea wananchi kuhama walikobanana na kuhamia kwenye maeneo yenye nafasi kubwa za kutosha na kuleta maendeleo kwa nchi yetu? Je, katika azma hiyo kuna uwezekano gani



wa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu wakaandaliwa maeneo yao rasmi baada ya kufikisha umri wa miaka 18 kwani hawana wazazi wa kuwarithisha masyhamba au eneo la kuishi? Je, ni lini Serikali itatatua tatizo la wanawake kupatiwa mashamba rasmi kwenye maeneo kama hayo? Naomba utakapohitimisha hoja nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumba za *National Housing*, huu ni utaratibu gani zinazochukiliwa kurekebisha hali iliyo jitokeza kwenye miji9 mingi kuwa nyumba za makazi za *NHC* kutumika kwa nyumba za biashara? Mfano wa Moshi Mjini unauweza kutumika hapa, kwani hii ni kero sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini tamko la Waziri la *Flats* kuuziwa wapangaji wake, wakiwemo wale wa Dodoma mfano *Mpwapwa flats* litatekelezwa. Jambo ili likiwekewa muda litakuwa jema kwa shirika na wakati wenyewe.

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu, kwa kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni leo. Nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Katibu Mkuu, Mama Sijaona, pamoja na Wataalamu wote kwa hotuba yao nzuri.

Nichukue tena nafasi hii, kuleta pongezi za dhati za Wananchi wa Mererani kwa serikali yetu kwa uamuzi wake mzuri wa kukubali Mererani kuwa Mji. Tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana serikali kwa kuendeleza mpango wa kujenga nyumba kwa ajili ya kupangisha na nyingine za kuuza. Naomba zoezi hilo lisiishie Dar es Salaam na Arusha tu, zoezi hili liende Manyara. Manyara ni Mkoa mpya viwanja tunavyo, tunaomba ufanye utaratibu wa kuuendeleza Mkoa wa Manyara sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu maeneo au mikoa ambayo zimekwishajengwa nyumba hizi. Kwa mfano, nyumba za biashara, kama maduka, wakati nyumba hizi zikishamalizika kujengwa, zinaingia mikononi mwa wenye uwezo wao ndio wanaopanga bei. Je nyumba hizi ni za wenye uwezo tu au ni za wananchi wote?

Ninasema hivyo kwa kuwa mtoto wangu mwenyewe, alikwenda *National Housing* kutaka fremu ya duka Arusha; alijibiwa kuwa hakuna walikwishapewa watu. Akaambiwa labda ukaonane nao, huenda kuna ambaye ameshindwa kufungua kwa ule muda uliopangwa basi atakupatia. Tulipofika kuulizia kuna mtu mmoja alikuwa na vyumba (fremu) nne na kila fremu alitaka tumpe kwanza Sh.10,000,000 milioni ndipo atuachie. Kwa hali hiyo, alikuwa akifanya biashara kwa vyote vinne ni sawa sawa na Sh.40,000,000. Kwa hiyo, kwa mtindo huu, utakuwa unazungukia matajiri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwepo na utaratibu mwingine mzuri ambao utamfaa mwananchi wa kawaida. Ukodishaji wa nyumba hizi usipitie kwa wale watumishi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa viwanja zaidi ya kimoja, serikali iangalie sana kwa kuwa tatizo hili linaongezeka siku hadi siku kutokana na watumishi wasio waaminifu. Wao ndio wanaosababisha; wana hati za bandia; kwa nini hati za bandi zitumike na Wizara ikae kimya? Hao watumishi wenu wanavyo vibali vya bandia; je, havijaonekana? Kwa nini wanaotoa hati hizi wasidhibitiwe?

Naomba Wizara hii isimamie utoaji wa vibanda vya biashara (fremu) na hati bandia zidhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa hotuba yenye kuonyesha dira ya maendeleo ya ardhi na makazi ya wananchi zikiwepo nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii, naomba nichangie machache:-

Kwa kuwa Mji wa Dodoma unakua na kuna ongezeko la haraka la watu na kwamba, wananchi wengi wanahitaji kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba na wana mahitaji makubwa ya viwanja, tunaomba Wizara itoe ushirikiano mkubwa kwa CDA ili viwanja vingi vipimwe. Vilevile tungependa kujua kama Wizara ina mpango wa kupima vijiji vilivyoye nje ya mipango ya CDA. Kama hakuna mpango huo, ningepomba vijiji hivyo viwekwe kwenye utaratibu kwani wananchi watajenga kiholela na matokeo yake, kukua kwa mji na kukutana na vijiji visivyopimwa na tutaharibu ukuaji mjini kwenye maeneo yasiyopimwa.

Naishauri serikali, maeneo yaliyopimwa ni vizuri yaweze kutolewa hati za kumiliki viwanja ili wananchi wazitumie kukopa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuweka azma yake ya kuanzisha benki ya mkopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hii itakuwa ni ukombozi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake na naunga mkono hoja.

Mchango wangu ni kuhusiana na viwanja vilivyoko kando kando ya ufukwe wa bahari. Sheria na Kanuni zinavunjwa, watu wanajenga bila ya kuzingatia kuacha mita 60 kutoka baharini na kati ya kiwanja na kiwanja. Nyumba zimeunganishwa bila ya kuacha nafasi ili wengine waweze kufika kwenye fukwe kwa ajili ya mapumziko. Naomba iweke mikakati ya makusudi kutatua tatizo hili.

Lingine, tuendeleo kupunguza urasimu wa watu kupima viwanja vyao mpaka kupata hati miliki, pamoja na kwamba hali hiyo ni nzuri, lakini bado baadhi ya ofisi zipo mikoani; urasimu upo. Wageni wana miliki ardhi bila ya kufuata sheria, inatakiwa kuongeza utaratibu wa udhibiti katika jambo hili na wasiwe na haki ya kumiliki zaidi ya ekari 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri na Timu yake kazi njema. Ahsante.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, huko vijijini wapo wananchi ambao wanazo rasilimali kama vile nyumba za kuishi, pamoja na nyumba za biashara, ikiwa ni pamoja na mashamba. Vyote hivyo hivi sasa havina hati miliki. Je, rasilimali hizo zinaweza hivi sasa kurasimishwa kwa lengo la kupata mikopo?

Je, Shirika la Nyumba la Taifa lina mpango wowote wa kujenga nyumba za makazi na za biashara kwenye miji midogo kama vile Miji ya Makongolosi (Lupa) na Mkwajuni (Songwe)?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri jinsi Wananchi wa Tanzania watakvayofaidika na ardhi ya nchi yao. Kwa kuwa mwananchi ana ardhi hasa inayogundulika ina mali mfano, madini, naomba yule mwenye eneo anayemiliki kienyeji anapofika mwekezaji yeye adhaminiwe kuwa ile ardhi iwe ndiyo mchango wake (*share*) yake katika biashara hiyo ya madini, shamba, hoteli na na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalochangia nina faida nalo. Mimi nimepewa kiwanja miaka ya themanini eneo la Tabata, wakati ninakiendeleza ikagunduliwa *double allocation*. Ikagundulika aliyekuwa Mkurugenzi wa Ardhi Wizarani, Ndugu Mtetewaunga ndiye mwenye eneo hilo. Ilipofuatiliwa iligundulika kuwa Ndugu Mtetewaunga alikuwa na maeneo mengi (viwanja vingi Dar es Salaam na Kibaha). Nilipofuatilia na kwa kuwa kwa wakati ule yeye aligundulika kuwa na viwanja vingi, akaniomba mimi na wenzangu katika eneo hilo lililo na viwanja vitano, tuzungumze ili yaishe lisije kumlipua magazetini. Alidiriki kusema ingekosa wandishi wa habari kulipua eneo hili, yeye hakuwa anakumbuka kwamba ana eneo hapo.

Wakati tunazungumza, wenzangu walikwisha jenga nyumba mimi nilikuwa na matofali elfu tatu na kibanda cha vyumba viwili. Mpaka sasa, hatujasuluhisha eneo hilo. Nimekuta matofali yangu na kibanda changu kimebomolewa na kuna mtu amejenga na matofali yangu na mashine ya matofali haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie suala hili. Ndugu Mtetewaunga kauza eneo hili kwa Ndugu Sanga, lakini wale wenzangu katika eneo wanaendelea kuishi. Naomba Tume ya Matumizi bora ya Ardhi iwe inasimamia jinsi Halmashauri inavyopanga miji/vijiji kiholela au kuanza kwa mfumo wa Shant Town. Je, inawezekana watu wa Tume kuja Mji wa Kibaha, kusaidiana na Halmashauri

kupanga Mji, baada ya tabia mbaya ya Maafisa Ardhi kugawa ardhi ovyo (kiholela) na kwa siri bila Halmashauri kujua?

Je, Tume pamoja na Kitengo cha CAG cha Kutathmini (*value for money audit*), wanaweza kuja kuona eneo la Kibaha Machinjioni jinsi mtu binafsi anavyogawa viwanja na Halmashauri imeshindwa kumchukulia hatua?

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wa Wizara kwa taarifa na mpango mzuri.

Ninaomba Wizara itatue mgogoro wa Hifadhi ya Mkungunero, iliyoanzishwa na Wilaya ya Kondoa na kupaswa kuishia mipaka ya Kondoa. Hivi karibuni, Hifadhi hiyo imeanza kutaka kutanuka na kuingilia Wilaya ya Simanjiro na Kiteto katika Wilaya ya Kiteto. Hifadhi ya Mkungunero inadai kuchukua jumla ya hekta 5,015 Wilayani Kiteto, Kijiji cha Orkiushi Oibour. Hatua hii inatishia kuhamisha vitongoji viwili vya Orkiushi Oibour kama vile Loombenek na Masaasi vyenye kaya 250, pia visima vya jadi 50 vitegemewavyo na vijiji vyote.

Naomba hii shida itatuliwe na mipaka ya Mkungunero iishie mipaka ya Wilaya ya Kondoa, kwani huu ulikuwa ni Mradi wa Wilaya ya Kondoa tu peke yake.

Naomba Wizara isaidiane na Halmashauri ya Kiteto na asasi za kiraia, kuandaa *Interim Land Use Plans* katika vijiji vilivyopata hati ya ardhi ya vijiji, ili wenyeji wauze kupata hati miliki za mila na kutumia hati hizo kwa kupata mikopo.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri. Nampongeza sana Katibu Mkuu, kwa kazi yake nzuri sana ndani ya Wizara hiyo. Nisiwasahau Watendaji wote wa Wizara.

Natanguliza kusema kuwa, naunga mkono hoja. Naishauri Wizara; kwa kuwa wananchi wanalalamika sana kwa kutotendewa haki ya malipo ya fidia wakati wanahamishwa maeneo yanayotakiwa kuendelezwa upya kama vile Kurasini; ni vyema serikali ambayo ni Wizara, ikawa inawajulisha kabisa kiasi cha fidia wanachopaswa kulipwa badala ya kungojea kuwapa cheki ambazo hazina maelezo ya kutosha. Nina maana, wahusika waambiwe kabla *value* ya mali zao ili kama kuna matatizo yarekebishwe kabla ya hundi kuandikwa. Pia naomba kila miji itenge *green area* kwa ajili ya kupanda miti, maua na bustani ndogo za vyakula.

La mwisho, naomba sana NHC wanapoingia ubia na waendelezaji wa viwanja vyao, hisa zao ziwe ni *value* ya soko ya kiwanja chenyewe na siyo vinginevyo. Mtindo wa sasa, hauna maelezo ya kisayansi na ya haki kwa pande zote mbili.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza timu nzima ya Wizara.

Ni mkakati gani wa kiutendaji wa kufikisha MKURABITA katika maeneo mengine ya nchi (Halmashauri ya Wilaya Songea); kama changamoto, Halmashauri za Wilaya zinazoweka mpango huo katika mipango yake; serikali inatoa msaada ukiachia bajeti finyu ya Halmashauri zetu?

Mpaka wa Tanzania na Msumbiji pale Muhukuru mahali tulipojenga daraja upande wa pili wa Msumbiji wenzetu wamepiga hatua kubwa upande wetu tuko nyuma. Halmashauri ya Wilaya inaomba sana tukasimiwe Sh. 60 milioni ili kuwezesha upimaji wa eneo hilo muhimu lililoko mpakani. Tunaomba Wizara itusaidie suala hilo. Kwa kuwa nia ya serikali ya kurasimisha ardhi ni kusaidia wananchi kutumia hati miliki za ardhi hata katika mikopo. Naomba elimu ya matumizi ya hati ianze kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Wasaidizi wake wote, kwa kushiriki ipasavyo katika kuandaa hotuba nzuri na fasaha aliyowasilisha Mheshimiwa Waziri mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kukiri katika ukurasa wa 38, ibara ya 47 kuwa, Wizara imeshiriki kutatua migogoro ya mipaka kati ya Vijiji na Hifadhi za Taifa, ikiwemo Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Waziri na Bunge lako Tukufu kwamba, suluhu baina ya baadhi Vijiji vya Kata ya Mikumi na Kata ya Ruhembe bado haijapatikana hadi sasa, kwa sababu wapimaji wa mipaka kutoka Wizara ya Ardhi hawakufuata kabisa maelekezo yaliyomo katika *G.N. No. 121* ya tarehe 13 Juni, 1975, ambayo ni *very clear and specific*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wapima kutozingatia maelekezo yaliyomo katika *G.N. No. 121*, mipaka imeingilia maeneo makubwa ya vijiji na mashamba ya wananchi katika vijiji na vitongoji vya Mikumi, Lumango, Kikwalaza, Gombati, Ruhembe, Kihelezo, Kitete, Mtambiko na Kidogobasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nilimwandikia barua mahususi Mheshimiwa Waziri, tarehe 01 Mei, 2008, kuhusu suala hili ambalo nililieleza kwa kina na kwa kirefu; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, kwa barua yake yenye Kumb. Na. EA 71/176/01 ya tarehe 21 Mei, 2008 alinjibu kuwa, niwe na subira kwa kuwa ameanza kulifanyia kazi tatizo hilo; sasa namwomba sana wakati akijumuisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, alijulishe Bunge lako Tukufu ni suluhu gani aliyofikia au bado analifanyia kazi suala hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni niliyoagizwa na Wananchi wa Kata, Vijiji na Vitongoji husika, wameniomba nimwombe Mheshimiwa Waziri akubali zoezi la kupima mipaka baina ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na vijiji/vitongoji husika lirudiwe, kwa kuzingatia kwa usahihi maelekezo yaliyomo katika *G.N. No. 121* ya tarehe 13 Juni,

1975 kama yalivyosainiwa hatimaye na aliyekuwa Mlezi wa Hifadhi zote za Taifa nchini. Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, kama nilivyomwandikia kwa hekima nyingi katika barua yangu kwake, napenda Mheshimiwa Waziri, pamoja na mimi na wananchi husika, tushirikiane kuutatua mgogoro huu uliodumu tangu mwaka 1999, *once and for all* na kuweka historia katika uhai wa Bunge la kwanza katika Awamu ya Nne ya Utawala wa Serikali yetu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasita kuunga mkono hoja hadi hapo Mheshimiwa Waziri atakapotoa ufafanuzi wenye nia ya dhati ya kuwatendea haki wananchi wa vijiji nilivyovitaja, kwa kupima upya na kwa uhakika, mipaka ya vijiji vyao na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ELIETTA N. SWITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ardhi ni nyeti. Kitendo cha serikali kuamua kumilikisha wananchi ardhi ili waweze kukopesheka ni cha busara sana. Hata hivyo, tunaiomba serikali itafute mbinu ya kuhakikisha zeozi hilo. Zoezi liende sambamba na kutoa elimu kwa wananchi wajue umuhimu wa kumiliki ardhi; ili wasimilikishe maeneo madogo ambayo hayawezi kuwaendeleza vilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ombi langu ni kwamba, Serikali sasa ione umuhimu wa uendelezaji wa maji na vijiji vya Mkoa wa Rukwa. Vijiji 21 vilivyokwishapimwa Wilayani Mpanda ni hatua nzuri na inaungwa mkono. Serikali inaombwa sasa iongeze kasi ya kupima na kumilikisha ardhi Mkoani Rukwa ili kuepusha migongano kati ya wafugaji na wakulima. Pia kukamilishwa kwa upimaji, kutawawezesha wafugaji kuwa na maeneo ya kutosha ya kuchungia mifugo yao hususan Bonde la Ziwa Rukwa ambalo limejaa wafugaji badala ya kuliacha litumike tu kwa kilimo, kwani eneo lina rutuba ya kutosha sana kwa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali haijawasaidia sana wananchi kuhusiana na wawekezaji wakubwa ambao hupewa ardhi katika maeneo ya vijiji na kuwafanya wanavijiji kubakiwa na maeneo madogo sana ya kulima. Hata kama ranchi ya serikali inaacha kutumika ni vizuri ardhi ile ikapewa wanavijiji waliopo maeneo yale badala ya kuwauzia wawekezaji. Jambo hili mara zote limeleta mtafaruku Rukwa. Rukwa ina mapori mengi, wawekezaji wazalendo waende kuwekeza kule. Kitendo cha kuweka wawekezaji katikati ya wanakijiji ni unyanyasaji mkubwa na kuwanyima haki wananchi na wala siyo utawala bora. Serikali inapaswa kujua kuwa wananchi wengi hawana uwezo wa kununua ardhi za ranchi zinazouzwa na serikali na tena wengi hawajapewa elimu ya MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, serikali inashauriwa kutenga maeneo ya wafugaji na kuwapa elimu ya kukuza nyasi kwa ajili ya mifugo yao katika maeneo waliyotengewa (zamu kwa zamu), wasilazimike kuhama hama.

Serikali iwapimie wakulima maeneo makubwa ya kutosha, yatakayowaletea maendeleo kwao na vizazi vyao vinavyoongezeka, bila kuwauzia wawekezaji ardhi ndani ya vijiji.

Vile vile Serikali iwape elimu ya kutosha wanavijiji kuhusu MKURABITA ili waweze kumiliki maeneo makubwa na kuyaendeleza. Pia elimu ya ujenzi wa nyumba bora na upandaji miti itolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. AISHA O. KIGODA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Kapteni John Z. Chiligati, kwa kuwasilisha hotuba yake. Nampongeza sana Mama Salome Sijaona, Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri yote, Waziri na Katibu Mkuu wanasaidie upatikanaji wa hati za nyumba; tatizo ni nini kuchukua muda mrefu? Mimi binafsi ni muathrika mkubwa. Kule Handeni tangu tumelipia ili tupatiwe hati ni kitendawili, tangu mwaka 2000 hadi leo. Dar es Salaam tangu nimepatiwa kiwanja kule Ndege Beach, nimelipia gharama zote, nimeletewa fomu kusaini na kupeleka kwa wanasheria. Tangu *stage* hii ifike na kuwasilisha, sasa ni takriban miezi miwili; kila siku tunafuatilia njoo kesho, njoo keshokutwa!

Katibu Mkuu, dada yangu, naamini suala langu utalimaliza. Tangu nilipowasiliana na wewe kuhusu viwanja vya Ndege Beach kama utakumbuka, bado watendaji wako hawajamaliza ile kazi. Hivyo, nakumbusha tena.

Wale walioko Wilaya ya Handeni; hati zao zinazotoka au zinapatikana wapi; mtaalam ukimuuliza anasema Dar es Salaam Makao Makuu, mara utaambiwa Moshi; sasa jibu sahihi ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri, nitamletea *Plot Numbers* ambazo nazifahamu zimelipia kila kitu lakini hati zimekwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawatakia Wizara kazi njema na kila la kheri.

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa dhati kwa kazi nzuri aliyoanza kuifanya katika Wizara hiyo. Nampongeza pia Katibu wake Mama Sijaona. Nawapa pole kwa mzigo mzito ambao siku za nyuma ulibebwa na Waziri na Naibu Waziri, lakini leo anaubeba Waziri peke yake wakati huo huo akiwa na majukumu mengi kichama. Hongera sana.

Naipongeza Wizara kwa Urasimishaji Ardhi mijini, kwa kutoa leseni za makazi kwenye maeneo yaliyojengwa holela na vijijini kutoa hati miliki za kimila. Utaratibu huu sasa unawawezesha wananchi wa maeneo hayo, kukopa kwa dhamana ya leseni na hati miliki hizo. Bado matatizo yapo kutokana na urasimu ndani ya mablenki yaliyomo kwenye mpango huo na uchache wa mablenki yaliyo tayari kutoa mikopo. Nashauri Wizara ikishirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Fedha, zianzishe programu ya kuzielimisha taasisi za fedha, kuwapa umuhimu wakopaji hawa wadogo sana na wafanyabiashara wakubwa. Pia serikali kupitia Benki Kuu iweze mkakati wa mablenki kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wakopaji wa aina hii.

Kama kuna kero kubwa kuliko zote kwa wananchi siku za nyuma, kero hiyo ilikuwa utoaji wa hati miliki. Naipongeza Wizara kwa kuanzisha utaratibu wa kanda na kuanza kutoa hati miliki na ushauri wa masuala ya ardhi kwenye ofisi za kanda, lakini kanda tano hazitoshi; nchi hii ni kubwa na malimbikizo ya hati miliki ni makubwa. Hivyo, nashauri Wizara ijitahidi kufungua kanda zaidi, ikiwezekana siku za baadaye kila mkoa uwe na ofisi yake ya kutoa hati miliki. Nafahamu yapo matatizo ya fedha na uchache wa maafisa ardhi, lakini fedha itatoka kwenye malipo ya hati zenyewe na kodi (ushuru) wa ardhi na majengo. Kuhusu wataalam, Wizara iongeze kasi ya kufundisha katika Chuo cha Ardhi na Mafunzo Kazini.

Naipongeza Wizara kwa jitihada ya kutatua migogoro ya ardhi, lakini kama inavyoonekana katika jedwali Na. 5, kati ya mashauri 15,422; mashauri yaliyotatuliwa ni chini ya nusu. Huko vijijini ipo migogoro zaidi ambayo mlalamikaji anatakiwa ajigharamie usafiri na usafiri wa anayemlalamikia. Wengi wanashindwa, kwa hiyo, nashauri serikali iongeze kasi ya utatuzi. Ikiwezekana mabaraza yawe yanakwenda kwenye maeneo ya migogoro ili kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri masafa marefu.

Migogoro ya mipaka baina ya wilaya na wilaya, vijiji na vijiji na kadhalika ni kweli ni mikubwa. Ingawa Mheshimiwa Waziri, unashauri Wakuu wa Wilaya waipatie ufumbuzi, suala hili ni gumu kwa sababu Wakuu wa Wilaya wenyewe ni wadau. Tatizo kubwa lipo kati ya mipaka baina ya Wilaya za Mijini na Vijijini. Kwa kuwa miji inakuwa haraka, viongozi wa mijini wanataka kutatua misongamano kwa kuingia vijijini. Tunalo tatizo hili Mkoa wa Pwani kati wilaya zinazopakana na Jiji la Dar es Salaam; kuna migogoro kati ya Temeke na Mkuranga, Ilala na Kisarawe, Kikondoni na Kisarawe/Kibaha, Kinondoni na Bagamoyo.

Nashauri jukumu la utatuzi liendeleo kuwa la Serikali Kuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi).

Mwisho, napenda kuipongeza Wizara kwa dhati, kwa jinsi inavyosimamia mpango wa matumizi bora ya ardhi kule vijijini. Katika wilaya yangu ya Kisarawe sasa tuna maeneo yaliyotengwa kwa kilimo, ufugaji, misitu na kadhalika. Mbali ya kupunguza migogoro baina ya (mfano wafugaji na wakulima) na makundi mbalimbali, sasa wananchi wanaanza kuelewa maana ya uzalishaji wa tija. Katika miji midogo kwa



mfano Kisarawe, Wizara imesaidia kutoa mkopo kwa Halmashauri ili kukamilisha upimaji wa viwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa John Zefania Chiligati, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa Wizara hii. Nampongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Bibi Salome Sijaona. Pia nachukue nafasi hii, kuwapongeza Wafanyakazi wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika rasilimali ya mtu maskini kwa nchi kama yetu Tanzania, ardhi ni rasilimali pekee inayoweza kumwondolea umaskini Mtanzania na ndio tegemeo kwa kila kitu. Tunapozungumzia maji, basi hifadhi yake lazima iwe ardhi, nishati, madini na kadhalika. Uhifadhi wake bado upo ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kutoa ushauri kuhusiana na suala zima linalohusu ardhi kwa ujumla.

Kwa kuwa rasilimali ardhi ndio pekee inayoweza kumwondolea umaskini mnyonge, basi ni muhimu sana elimu kama njia moja muhimu ya kuwaelimisha wananchi ili kufahamu umuhimu wa matumizi ya ardhi kama Sekta ya Ardhi kifungu cha 42(a), juu ya utekelezaji wa MKURABITA.

Kasi ya upimaji viwanja na mashamba kwa Halmashauri za Vijiji, Miji, Manispaa hata Majiji bado ni ndogo sana. Kwa kuwa wananchi wenyewe wapo tayari kuchangia gharama za upimaji, naomba Wizara kupitia Idara zake za Ardhi kwenye ngazi za Halmashauri, zipatiwe vifaa muhimu kwa shughuli ya upimaji ili urasimu usio na maana yoyote uondolewe. Aidha, watendaji wote wenye dalili za rushwa wadhibitiwe kwa kuwajibishwa.

Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (*CDA*) imulikwe, kwani watendaji wake hasa wa kugawa ardhi kwa matumizi ya ujenzi wa nyumba, Idara hii lazima itakuwa imejaa ufisadi, kwani ni dhahiri hata pale mahitaji ya kawaida ya maombi yaliyowasilishwa hakuna sababu ya msingi zinazosababisha waombaji kutopewa ardhi waliyoomba kwa ajili ya matumizi, jambo ambalo litafanya, Makao makuu ya nchi kukua kwa kwasi. Mfano mzuri, pale Waheshimiwa Wabunge walipowasilisha maombi ya kupatiwa ardhi hiyo mwaka 2006 hadi sasa hakuna aliyepatiwa mbali na kuona baadhi wakipatiwa viwanja kwa kutumia njia za panya. *CDA* lazima imulikwe!

Wilayani Iramba Idara ya Ardhi inahitaji vifaa na watumishi wenye taaluma katika kutekeleza majukumu yake kiufanisi. Wataalamu wanaohitajika ni Mpima Ardhi (*Land Surveyor*) na Mthamini (*Valuer*). Vifaa vifuatavyo vinahitajika: Gari, pikipiki, *GPS*, *Total Station* na *Steel Tape*. Vifaa hivyo ni muhimu kwa kutimiza kazi ya upimaji.

Baraza la Ardhi na Nyumba; Mwaka 2007 nilieleza tuu ya tatizo hili na Waziri wa kipindi hicho, Mheshimiwa John Mafuguli na Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, kwa pamoja walitoa ahadi kwamba, Wilaya ya Iramba itapewa Mwenyekiti wa kuendesha Baraza hili; hadi sasa shughuli hiyo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri, katika mipango yake ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natoa pongezi kwa hotuba nzuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2008/09.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji si baya, bali kile kinacholalamikiwa ni kumilikishwa ardhi mtu wa nje (sio raia) wa nchi (Tanzania). Atakayemilikishwa baadaye akimalizia muda huuza ardhi na kurudi kwao; hiyo si sawa hata kidogo. Wawekezaji wapewe ardhi kwa ridhaa ya wenye ardhi (wanakijiji), kwa kufuata sheria za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa maeneo mbalimbali ya muhimu ni maendeleo. Tatizo au matatizo ambayo hujitokeza ni kama ifuatavyo: Wananchi wanapohamishwa kwenye eneo, hutolewa bila kupatiwa hesabu sahihi ya mali walizonazo katika maeneo yao; matokeo yake hupunjwa malipo na huwa hawajui wafanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda wa kuhamisha wananchi si tatizo; tatizo ni uvunjaji wa sheria ya kuwahamisha wananchi hao. Sheria inasema ni miezi sita tu mwananchi anabanwa kutoendeleza kitu chochote na lengo hapo malipo yatolewe. Kinachofanyika ni kutolipwa kwa muda huo na yeye kutoendeleza chochote. Hivyo, serikali iwe inawajibishwa vikali katika uzembe huu.

MMheshimiwa Naibu Spika, ombi la ufafanuzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Ni lini gharama za fidia zitabadilishwa kutokana na mabadiliko ya kupanda gharama za uendeshaji?

(ii) Je, muda wa miezi sita wa kuwa ndani ya uthamini kwa mhusika kutokuendeleza kitu chochote uko pale pale?

(iii) Kwa nini kusitolewe adhabu kwa Halmashauri ambazo huchelewa kulipa fidia kwa wananchi walioandaliwa kuhama na baadaye wasilipwe kwa muda muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya na kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Pamoja na wananchi walio wengi hasa wanaoishi vijijini, maisha ya wananchi wengi yanategemea ardhi. Hivyo, naiomba serikali imilikishe ardhi kwa wananchi na kuwapatia hati miliki iliyokuwa na kikomo ili waweze kuitumia wao wenyewe, pamoja na familia zao na vizazi vyao vijavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali ya serikali, lakini kuna ambayo inamilikiwa na wananchi kwa kuwa na hati miliki ya maeneo hayo. Iwapo serikali inahitaji kuyatumia maeneo hayo kwa shughuli za maendeleo ni vyema ikafanywa tathmini na kuwalipa fidia inayolingana na thamani za maeneo hayo, badala ya kuwaacha wananchi hao wakihangaika bila mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni mali kwa hiyo elimu inapaswa kutolewa kwa wananchi kuhusu umuhimu na thamani ya ardhi ili iwasaidie kujikwamua katika umaskini na kuweza kuwa na maisha bora kwa kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni rasilimali muhimu na ya lazima kwa wakulima, wafugaji, pamoja na makazi ya wananchi. Ni vyema serikali ikapanga matumizi ya ardhi ili kubainisha maeneo ya wakulima, wafugaji na maeneo ya makazi pia na kuweka mabango kuanisha maeneo ambayo hayaruhusiwi kutumiwa na wananchi ili kuondoa usumbufu unaojitokeza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa lipatiwe mtaji ili liweze kujenga nyumba nyingi za kupanga na za kuuza ili wananchi waweze kupata makazi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali inapaswa kuwa makini katika uvunjaji wa majumba ya wananchi ili kuepukana na matatizo yaliyojitokeza katika maeneo mbalimbali ya wananchi kuvunjiwa kinyume cha utaratibu na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, serikali itenge maeneo ya viwanja vya michezo katika mashule yote ili wanafunzi waweze kushiriki michezo mbalimbali wanapokuwa shuleni.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri serikali katika yafutayo:-

- Iweke utaratibu endelevu wa kuelimisha viongozi wanaounda Mabaraza ya Ardhi na Kata, ambao kimsingi hawana ujuzi wa majukumu haya mazito ya kisheria wanayopewa.

- uwepo uratibu wa mikutano mikuu ya wananchi wote katika vijiji ili elimu ya ufahamu itolewe kwa wajumbe na viongozi wa ngazi husika na mtaalamu wa ardhi anayeweza kuheshimu madaraka yake kwa Afisa wa Tarafa au itakavyoonekana inafaa kuhusu sheria hii na taratibu zake.
- Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri washirikiane kwa karibu na vijiji kutatua kero ya ardhi.
- Hatua za kisheria zichukuliwe haraka pale zinapokiukwa na Wajumbe wa Kamati.
- Iwekwe wazi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji, Mjumbe mmoja wala serikali ya kijiji pekee, haiwezi kuwa na mamlaka ya pekee juu ya ardhi, pasipo wanakijiji wote.
- Kero/kesi za ardhi zipatiwe majibu mapema pasipo kuchelewa.
- Vijiji vielekezwe na visimamiwe kutenga maeneo ipasavyo, yaani maeneo ya kilimo, kuchunga, maziko, maendeleo na kadhalika.
- Ardhi ya kijiji isiuzwe, wala kubinafsishwa kwa mgeni (asiye raia), bila kuwa na ubia na raia (mwenyeji) ili kuondokana na matatizo ya matumizi ya ardhi, kinyume na matarajio.
- Atakayebadili matumizi ya ardhi pasipo kibali cha Serikali ya Kijiji, anyang'anywe.
- Wataalam walioajiriwa na serikali kisha wakatumba vibaya katika migao ya ardhi, washtakiwe sawa sawa na wahujumu wengine wowote wa uchumi.
- Serikali ianzishe vijiji na kata nyingine mpya ili kupanua maeneo ya kuishi.
- Kuhusu miji, serikali ianzishe miji mingine badala ya kubaki na miji ile ile. Aidha, huduma muhimu kama masoko, hospitali, vituo vya usalama vianzishwe katika miji hiyo mipya.
- Wawekezaji isipokuwa mashule, vituo vya huduma ya afya na huduma muhimu kama maduka, wasiachwe kuwekeza katika vijiji ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, nawasilisha.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi/Mashirika ya Umma na Watendaji wa Wizara, kwa kazi nzuri zinazofanyika mfano, upimaji wa viwanja umeshika kasi; utoaji wa hati miliki unaridhisha sana; Shirika la Nyumba la Taifa sasa linaendeshwa kwa ufanisi wa kutosha wa kibiashara; utatuzi wa

migogoro ya ardhi kwa kasi na mengineyo mengi. Hongereni sana na nawatakia mafanikio mazuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo:-

(a) Ili kuweka kumbukumbu vizuri za hati miliki ya ardhi nchi nzima na kuepuka udanganyifu na utoaji haki kwa zaidi ya mtu mmoja, nashauri itengenezwe Kanzi ya Data (*database*) ya hatimiliki zote zinazosimamiwa na Wizara (Msajili wa Ardhi).

(b) Wizara iweke Mpango Maalum wa kuhamasisha wananchi kuwa na hatimiliki ya ardhi wanayotumia, hususan ardhi ya makazi. Wananchi wengi vijijini wanaishi katika maeneo yaliyopimwa wakati wa kuanzisha vijiji vya maendeleo mwaka 1974, lakini hawana hatimiliki za viwanja vyao.

(c) Kwa kuwa miji yetu mikuu kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na kadhalika, ina sehemu kubwa ya makazi holela, nashauri serikali iweke mpango wa muda mrefu kubadili maeneo hayo ili kuondoa tatizo hilo. Utaratibu wa kurasimisha makazi holela tuone kama ni hatua ya muda tu. Suluhisho bora ni kubadili sura hiyo mbaya.

(d) Nakumbushia suala la mipaka ya ardhi kati ya Jeshi (JWTZ), Kambi ya 812 KJ na Vitongoji vya Nhelegani na Mwanshele/Lyandu Shinyanga Mjini. Utaratibu uliotumika kuweka mipaka ya Jeshi haukuwa shirikishi, hivyo kusababisha migogoro ambayo bado ipo.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri na yenye ufafanuzi wa kina kuhusu Wizara yake. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa vijiji vingi vimepimwa lakini hawajapata hati za kumiliki ardhi ikiwemo Wilaya ya Mpwaowa. Je, ni sababu gani za msingi zilizofanya hati za kumiliki ardhi zisitolewe? Je, katika Wilaya ya Mpwapwa ni vijiji vingapi vimepimwa na havikupata hati miliki?

Je, katika Mkoa wa Dodoma ni vijiji vingapi vimepimwa na kupata hati miliki? Je, serikali itakubaliana nami kwamba, iwapo vijiji vitapimwa na kupewa hati; hati hizo zitasaidia vijiji kupata mikopo kutoka vyombo vya fedha?

Kwa kuwa katika miji yetu mingi nyumba zinajengwa bila kufuata *master plan*; je, serikali ina mpango gani wa kurekebisha hali hiyo ili kupunguza migogoro inayojitokeza mara kwa mara ya kubomoa nyumba na kulipa fidia?

Kwa kuwa watumishi wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri za Wilaya wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kukosa vitendea kazi, usafiri (magari,

pikipiki na kadhalika) na vifaa vya kisasa vya kupimia ardhi; je, serikali ina mpango gani wa kuiboresha hali hiyo?

Je, serikali ina mpango gani wa kuwaendeleza Maafisa Ardhi kitaaluma ili kuboresha utendaji wao wa kazi?

Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Miradi ya MKURABITA inapelekwa Wilaya ya Mpwapwa na pia katika maeneo mengine ili wananchi waweze kunufaika na miradi hiyo ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Capt. John Zefania Chiligati, Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa hotuba nzuri yenye kutia matumaini.

Kwa kweli kwa upande wangu, nitaongelea juu ya ardhi. Rasilimali hii imekuwa ni chanzo cha migogoro, kuanzia ngazi ya familia hadi jamii kwa ujumla. Ikumbukwe kuwa, asilimia 80 ya Watanzania wanategemea ardhi. Wizara izingatie haki na sheria za ardhi ili kupunguza migogoro na migongano hiyo.

Wizara iwe na utaratibu wa kuwaelezea na kuwafafanulia wananchi sera na sheria zinazohusu utoaji na utumiaji wa ardhi ili waelewe haki zao; hii ina maana wananchi waelimishwe.

Naipongeze Wizara kwa kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005.

Namalizia kwa kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. MAULIDAH ANNA KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii na kuwaomba waelewe kwamba, ardhi ni kila kitu kwa binadamu na ingependeza wafanyakazi wote wa Wizara hii wawe waaminifu na wachapakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ndiyo inayotoa chakula, ardhi ikitunzwa vizuri bila kukata miti kiholela, hutoa maji safi ya kusaidia matumizi na pia hufanya mvua zinyeshe kwa wakati, ardhi wanadamu hujenga nyumba na kuishi, la mwisho binadamu anapokufa huzikwa ardhini.

Nchi yetu ni kubwa sana, kilomita za miraba 888,200; jinsi kitabu cha hotuba ya Waziri kinavyoeleza na katika kitabu cha hotuba akaeleza kwamba, mtu mwenye kumiliki ardhi, anamiliki mali ya mtaji muhimu unaomhakikishia maisha mazuri na akaendelea kusema hapo hapo, lakini hapa nchini wananchi walio wengi wana ardhi lakini bado ni maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ninalopenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni kuwa; kumbe serikali inaelewa kwamba hapa kwetu ardhi si utajiri; je, serikali itasaidiaje katika kumwezesha mwananchi aweze kupata utajiri kutoka kwenye ardhi anayomiliki?

Je, ni lini serikali itaishauri *NHC* kueneza au kujenga majengo mengi na kupangisha kwa kodi nafuu ili wananchi waishi kwenye nyumba nzuri, kuliko kuwaachia matajiri kufanya Mradi huo?

Je, ni lini serikali itawawezesha vijana wanaorandaranda bila kazi; wawapatie ardhi ya kilimo na kuwasimamia au kuwapatia mabwana shamba watakaowawezesha kulima kilimo cha mazao ya kuuza na kujikimu wenyewe?

Je, ni lini serikali itawasimamia wananchi wasijenge kiholela na baadaye kwenda kuwavunja nyumba zao na kuwaacha kwenye umaskini?

Je, Wizara ya Ardhi na Halmashauri wataacha lini kutoa maeneo yaliyowazi ambayo watoto hutumia kwa michezo na kuwapa watu kujenga?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yanaonyesha jinsi Wizara na Halmashauri wasivyo waaminifu kwenye kazi zao na pia baadhi yao kutokuwa na ubunifu wa kuweza kutoa haki kwa udhati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba tena Wafanyakazi wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wakae na kupanga jinsi ya kumsaidia mwananchi apate faida na ardhi yake na sio kumrudisha kwenye umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwakilisha.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Capt. Chiligati, kwa kazi nzuri anazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa Waziri wa sasa ni mgeni, lakini serikali ipo; natoa masikitiko makubwa kwa kuwa nina kero kubwa kwenye Wizara hii, kutoshughulikia malalamiko yangu tangu mwaka 2003 hadi leo sijapata jibu la maana. Kero yangu anajua Katibu Mkuu, Bibi Salome Sijaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nafuatilia hati ya Kiwanja Na. 594/B Sinza, ambapo hata ilifika *file* lake kupotea, lakini kwa kuhamia cheo nilichopewa na wanawake wa Mkoa wa Mwanza (Ubunge), nililazimisha hadi *file* likapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba sasa Waziri mwenyewe anisaidie nipate hati hii; ni muda mrefu nafuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naambatisha barua ambazo zinathibitisha kuwa ni uzembe unafanyika wa kutotoa hati miliki kwa mteja (Ndugu Alex Nyawazwa). Vithibitisho hivyo ni kithibitisho cha Mwenyekiti wa Mtaa na Afisa Mtendaji kinachoonyesha mmiliki ni nani; barua alizoandikiwa Ndugu Bohari mwaka 1987; na barua nyingine aliyoandikiwa Ndugu Bohari mwezi Juni, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri arekebishe utendaji wa Ofisi ya Ardhi Wilaya Kinondoni, wananchi wanazungushwa sana wakifuatilia matatizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kama nilivyoeleza hapa leo, Mheshimiwa Grace Kiwelu amefiwa na kaka yake na Wabunge wengine wamekwenda kumsindikiza Moshi. Halafu Mheshimiwa Masilingi, naye amefiwa na mke wa shemeji yake usiku wa kuamkia leo katika hospitali ya Hindu Mandal, kwa hiyo naye amekwenda Dar es Salaam kwenye shughuli hizo za mazishi.

Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.35 mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11. 00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilipositisha Shughuli za Bunge mchana wale niliotaka wazungumze wote waliweza kupata nafasi. Kwa hiyo, sasa nitamwita mtoa hoja, bahati mbaya mtoa hoja kwa sababu hana Naibu Waziri atakuwa na saa moja tu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mtoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi nihitamishe hoja ambayo niliwasilisha jana asubuhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii ama kwa maandishi ama kwa kuzungumza ndani ya Bunge



ama kwa mazungumzo tu nje ya Bunge, tumenufaika sana na maelezo yenu na ushauri wenu na tutaufanyia kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwa kusema humu Bungeni ni Waheshimiwa Wabunge 25 na waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wabunge 71 kwa hiyo, wanakaribia mia moja hivi. Kwa hiyo, kwa muda wa saa moja ni dhahiri kwamba siwezi kujibu yote na wenzangu walikuwa na siku mbili. Lakini wale Waheshimiwa Wabunge ambao sitawajibu wawe na hakika kabisa na waniamini kwamba yale waliyoyasema tumeyapokea na tutayajibu kwa maandishi na tutatekeleza yale ambayo yanatakiwa kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo kawaida nianze kuwatambua wale waliochangia, nadhani muda wangu huu hautahesabiwa kwa sababu majina ni mengi sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hautahesabiwa. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Meryce, Emmanuel, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Kepteni John Komba, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Dorah Mushi, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Mohamed Abdullah, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Elietta Switi, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Mwajuma Khamis, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Eustace

Katagira, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kusema humu Bungeni wa kwanza ni Msemaji wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa, msemaji wa pili alikuwa ni msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa John Cheyo na wingine waliofuata walikuwa ni Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Mwanawetu Zarafi, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Dr. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Peter Serukamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hoja nyingi sana kama nilivyosema sitazimaliza zote mnisamehe, lakini nitajitahidi kuzipitia zile ambazo nitaweza kuzipitia ila tu Waheshimiwa Wabunge muwe na hakika kwamba hoja zote zimepokelewa na zote zitafanyiwa kazi na zote tutazijibu kwa maandishi na mtazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja zilizotolewa na Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Hoja mojawapo ilikuwa kwamba Wizara kuendelea kuratibu shughuli zote za upimaji wa viwanja na ramani badala ya Halmashauri na Miji na Wilaya ambazo hazina wataalam wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu letu ni kwamba kimsingi kazi ya kupima viwanja ni kazi ya Halmashauri na labda nitumie nafasi hii kulifafanua hili kidogo. Watu wengi sana wanafikiri kazi ya kupima viwanja na kugawa viwanja ni kazi ya Wizara yangu, hapana. Kazi ya Wizara ni kutunga na kusimamia sera ya mambo ya Ardhi, Nyumba na Makazi, Sheria zinazohusiana na sekta hii na usimamizi wa jumla basi. Kazi sasa zenyewe za kuchora ramani huko, kupanga maeneo, kupima viwanja, kugawa viwanja, kulipa fidia ni kazi ambazo zinafanywa na Halmashauri za Wilaya, Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji zikisimamiwa na TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili jambo Waheshimiwa Wabunge wengi sana hawalijui, wanachojua ni kuwa Zahanati zipo kwenye TAMISEMI hilo wanalijua, barabara za vijiji zipo kwenye TAMISEMI hilo wanalijua, shule za msingi zipo kwenye Halmashauri. Lakini suala la Mipango Miji, kupima viwanja, kugawa viwanja hili nalo wajue kwamba na lenyewe lipo kwenye Halmashauri, mahali pa kuliulizia ni TAMISEMI. Sisi ni wadau kwa sababu ndiyo wasimamizi wakuu tunawapa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kimsingi naomba Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba mengi waliyokuwa wanazungumza jana na leo yale ya kiutendaji na kiutekelezaji kwa kweli ni kazi ya Halmashauri na chini ya TAMISEMI. Hata wale wataalam wanaofanya kazi hizo, wanaofanya *survey* kule, wanaopima viwanja, wanaochora ramani, wanaajiriwa na Halmashauri na Wizara yao ni TAMISEMI ndiyo inayowaajiri, ndiyo inayowahamisha, ndiyo inayowafukuza kazi wakifanya makosa hawapo katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana Waheshimiwa Wabunge wengine walikuwa wanazungumza kana kwamba hata wale wataalam wapo katika Wizara yetu walikuwa wanauliza kwa nini hatujawaajiri na kwa nini hatujawafukuza wanapofanya makosa hawapo katika Wizara hii, wapo TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nilitaka nilifafanue kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wanadhani kwamba shughuli zote za ardhi na wataalam na vitendea vipo chini ya Wizara yetu, sisi ni wasimamizi wa jumla tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya Kamati ilikuwa ni kwamba ardhi imekuwa ni kiini cha migogoro na migongano katika jamii ni vyema Mabaraza ya Ardhi na Nyumba yasimamie haki na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalo nataka nilifafanue vizuri kwa sababu Mabaraza haya yanayosikiliza migogoro ya ardhi yanaanzia katika ngazi ya kijiji halafu kuna Baraza la Kata, halafu kuna Baraza la Wilaya ni kama Mahakama ndogo za Ardhi. Sasa yale Mabaraza ya Vijiji na Mabaraza ya Kata hayapo katika Wizara yangu hayo yapo kwenye Serikali za Mitaa, yapo chini ya Wizara ya wenzangu TAMISEMI ndiyo wanayoyaunda kwa mujibu sheria na ndiyo wanaotakiwa kuyahudumia kama vile vikao kama ni karatasi, kama ni usafiri na kadhalika yapo chini ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu ni mdau, tunatengeneza sheria, maana yake sheria tunatengeneza sisi Wizara. Sasa kuisambaza Sheria ifike kule ni sisi na tumekwishatoa vitabu vingi sana nilijibu siku moja hapa swali karibu vitabu 20,000 tumekwisha kuvisambaza katika kila Kata na katika kila kijiji. Tunashirikiana na TAMISEMI kutoa elimu yale ni mambo ya usimamizi wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ambayo yapo moja kwa moja chini ya Wizara yangu ni Mabaraza ya Wilaya, haya yapo moja kwa moja chini yangu. Sasa kwa jumla haya Mabaraza yote kuanzia Baraza la Kijiji, la Kata mpaka Baraza la Wilaya haya yanafanya kazi chini ya sheria iliyounda Mabaraza haya ya mwaka 2002, wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria, ile haki kwa anayedai haki, inapatikana kupitia katika sheria ile. Tunajitahidi sana kusambaza zile sheria zifike kila mahali ili watu wajue sheria inasema nini ili kulinda haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya Tume yaani ile Tume ya Mipango ya Matumizi Bora ya

Ardhi, Kamati imesema wametengewa fedha kidogo hazilingani na majukumu na mimi nakubaliana nao kabisa kwamba hii Tume fedha ambazo imetengewa hazifanani na kazi zake. Lakini ndiyo uwezo wa Serikali, siyo Tume tu, hata Wizara nzima. Wangeniuliza mimi kama Waziri je, fedha nilizotengewa zinalingana kazi iliyopo mbele yangu? Ningesema vile vile hazilingani, lakini fedha tunagawana kulingana na uwezo wa Serikali. Sasa kama baba anakupa kile alichonacho, ukidai akupe zaidi ambacho hana unadai miujiza. Kwa hiyo, Bajeti ya hii Tume na Bajeti ya Wizara yangu kwa jumla tutaboresha mwaka hadi mwaka jinsi mapato ya Serikali yanavyoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la Kupanga Matumizi Bora ya Ardhi hii Tume ina wataalam inatakiwa itoke pale iende kwenye Halmashauri kule chini kwenye kijiji au kwenye Wilaya ndiko ikafanye ile kazi. Kama Halmashauri nazo zingekuwa zinatenga fedha kwa ajili hiyo, zingekachanganywa na hizo fedha za Tume wangepanya kazi kubwa zaidi. Lakini Halmashauri nyingi kabisa kama si zote hawana habari, hawetengi fedha hata kidogo kwa ajili ya Matumizi Bora ya Ardhi, lakini tunawasiliana na wenzangu wa TAMISEMI kwa sababu sasa tunataka tupime kijiji, tunataka tuweke masjala kule vijijini, tunataka tutoe hatimiliki kwa ardhi ya wanavijiji lazima sasa tushirikiane. Sisi Wizara tutaiongezea fedha hii Tume lakini TAMISEMI nao kupitia Halmashauri za Wilaya na wenyewe waweke fedha ili kazi hiyo tuifanye kwa haraka kwa sababu italeta ukombozi mkubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani naye alikuwa na hoja kadhaa. Moja ilikuwa ni kwamba Serikali kutotenga fedha za kutosha kwa ajili ya kupima maeneo ya viwanja na mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu letu ni kwamba ni kweli tungependa sisi kwa mfano vijiji tupime vyote hata kwa mwaka moja na uwezo upo. Mwaka juzi Tume walitengewa shilingi bilioni mbili na kwa mwaka mmoja walipima vijiji 3,000, theluthi moja ya vijiji walivipima kwa mwaka moja. Kwa hiyo, uwezo upo wa kupima, lakini sasa nyenzo ndilo tatizo. Lakini mazungumzo yaliyoendelea hapa Bungeni Serikali tumeyasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wametaka kazi ya kupima viwanja mijini ili miji yetu ipangwe vizuri, kazi ya kupima mipaka ya vijiji, kazi ya kugawa hatimiliki kwa wanavijiji zile hati za kimila wametaka Serikali iongeze nyenzo na uwezo ili Watanzania wapate hatimiliki na zile hatimiliki wazitumie kukopa mikopo kwa sababu ardhi ndiyo nyenzo peke yake waliyonayo ambayo inaweza ikawakomboza. Kwa hiyo, huo ujumbe Serikali tumesikia. Nafikiri Bajeti ya mwakani itakuja na sura tofauti ya kutekeleza haya ambayo mnataka yafanyike. Kwa hiyo, yaliyosemwa na Kambi ya Upinzani tunayakubali na ndiyo lengo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mabaraza ya ardhi na nyumba kwamba migogoro ya ardhi vijijini ni mingi na kesi nyingi zimefunguliwa katika mabaraza na kuna mrundikano wa kesi kama nilivyosema kwamba mabaraza ya vijiji na kata kama yangefanyakazi vizuri yangewezeshwa kesi kwenye mabaraza ya Wilaya zingepungua.

Lakini sasa utakuta hata kesi ambayo ingesikilizwa pale pale kijijini ama kwenye baraza la Kata nayo inapelekwa kwenye ngazi ya Wilaya.

Kwa hiyo, tunashauriana na wenzetu wa TAMISEMI ili wayawezeshe, wayasaidie mabaraza ya vijiji na mabaraza ya kata yafanye kazi vizuri ili matatizo yanayoweza kumalizwa pale pale kwenye vijiji au kwenye kata yaishie pale pale badala ya mashauri mengi sana kwenye Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa kuna hoja kwamba mabaraza ya ardhi ya nyumba yako katika mikoa michache na hivyo mashauri yanayosubiri yanakuwa mengi. Ni kweli kama tulivyosema katika hotuba yetu ya Bajeti, kwamba kimsingi tulitakiwa kila Wilaya tuunde Baraza la Ardhi la Wilaya. Hili Baraza ndiyo kama Mahakama ya Ardhi. Lakini tumeshindwa mpaka sasa kwa sababu ya uwezo wa kifedha. Unapounda Baraza katika Wilaya pale unaajiri hakimu wa kusikiliza, anaitwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli huyu ni hakimu. Ni lazima awe mwanasheria kuna mtu aliuliza hivi hawa wana vigezo gani hawa Wenyeviti wa Mabaraza kweli wana uwelewa wa sheria kuna vigezo gani? Nataka kukuhakikishia kwamba hawa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya ni wanasheria wa ngazi ya *degree* moja, *degree* mbili, ni wanasheria waliobobea na wengi walikuwa ni mahakama za Wilaya na Mahakama za Mikoa tulipotangaza nafasi hii kwa sababu ina malipo mazuri wengine waliacha kazi kule wakaja kuchukua. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni watu waliobebea, kwa hiyo, lazima tuwe na hela za kuwalipa hawa, lazima tuwe na hela za kuajiri wasaidizi wao, lazima tuwe na hela za kuwalipa wale wazee wa mabaraza. *Assessors* wale lazima tuwalipe posho, hawawezi kuwa wanakaa siku nzima pale halafu wanatoka mikono mitupu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uwezo wa fedha ndiyo tatizo ndio maana mpaka sasa tumefungua mabaraza 33 tu yaliyopo. Mwaka huu kwa mujibu wa Bajeti niliyosoma jana tunaongeza mabaraza katika Wilaya sita tu ndiyo uwezo wa kifedha tulionao. Kama nilivyosema katika Bajeti yangu jana tunaongeza katika Baraza katika Wilaya ya Geita, Wilaya ya Maswa, Wilaya ya Iramba, Wilaya ya Mkuranga, Wilaya ya Ukerewe na Korogwe. Kigezo kingine ni kwamba tunatazama kwanza yale maeneo ambayo yana kesi nyingi sana, maana tunatofautiana kati ya Wilaya na Wilaya, wingi wa kesi za ardhi.

Kwa hiyo, kigezo kimojawapo ni maeneo ambayo yana kesi nyingi. Kigezo kingine tunatazama umbali kutoka Baraza la hivi sasa lilipo katika Mkoa mmoja na eneo la pili ambalo lina kesi nyingi liko mbali kiasi gani. Lakini niseme tu kwamba tunao mpango wa kutafuta magari kwa hawa Wenyeviti wa Mabaraza haya ili waweze kwenda kwenye zile Wilaya ambazo hazina mabaraza waende wakasikilize kesi kule kule badala ya watu kufunga safari kutoka kwenye Wilaya aje Makao Makuu ya Mkoa kwenye Baraza. Tumeanza mazungumzo na wenzetu wa Benki ya Dunia na tunazungumzia habari za mkopo kimsingi wameshakubali, sasa ni taratibu/mchakato wa kutekeleza hilo. Tukiwapatia magari tutawasaidia sana wananchi badala ya wao kufuata Baraza liliko kwenye Wilaya fulani Baraza litawafuata huko huko waliko na kuwahudumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine katika Kambi ya Upinzani ilikuwa kwamba Serikali haijatengeneza mpango kapambe wa kupanua maeneo kwa matumizi endelevu. Hakuna ardhi iliyopimwa kwa matumizi ya kilimo, makazi mapya ya vijiji, mifugo na uwekezaji. Ni kwamba tume yetu ya matumizi bora ya ardhi sasa hivi imeshakamilisha mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi (*The national land use plan*) ambayo itaonyesha sasa katika kila Mkoa eneo gani la malisho, eneo gani la kilimo, eneo gani linafaa kwa kitu gani, kila Mkoa, kila Wilaya, kwa hiyo, hili litafanywa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutatafuta fedha ili tuje tufanye semina hapa ya Wabunge kuwaeleza suala zima la mpango wa Taifa wa mpango wa matumizi ya ardhi ili Wabunge vile vile waujue mpango huu na wasaidie kueleza katika majimbo yao. Kwa hiyo, huu mpango utaonyesha eneo hili ni kwa ajili ya kilimo gani, eneo hili ni kwa ajili ya makazi, eneo hili kwa ajili ya mifugo, uwekezaji hili la hifadhi, kila kitu kimepangwaje kwa nchi nzima kwa kila Mkoa, kwa kila Wilaya. (*Makofi*)

Vile vile kulikuwa na hoja kwamba ni wakati muafaka kwa Jiji la Dar es Salaam pamoja na miji mingine kupangwa upya yaani *replanning* ili ipendeze na iwe ya kisasa. Vile vile iwekewe mifumo ya maji safi na maji taka iboreshwe. Hili limezungumzwa na watu wengi pamoja na Kambi ya Upinzani lakini vile vile akina Mheshimiwa Peter Serukamba, wamesema haya na wakauliza hivi miji yetu inakwenda ovyo ovyo, hawa wako wapi hawa *town planners* wako wapi, Wizara ina mkakati gani tumehojiwa sana hapa. Sasa ni kweli kwamba miji yetu mingi inajengwa holela mbali na kwamba upimaji hauendi kasi, lakini vile vile yako matatizo ya msingi ambayo nimeeleza katika hotuba yangu na nataka vile vile Waheshimiwa Wabunge, nisisitize. Shughuli hii nimesema inafanywa na Halmashauri ndiyo jukumu lake kisheria Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna matatizo makubwa sana ya watalaam wa kufanya kazi hii kwenye Halmashauri. Nimeeleza katika hotuba yangu ya Bajeti kwamba kuna upungufu kwa mfano *surveyors* wapima karibu 70% wathamini kuna upungufu karibu 50%, mipango miji 74% upungufu. Sasa kazi kama imeshakosa watalaam kiasi hiki itafanyikaje? Lakini tunazungumza na wenzetu wa TAMISEMI kwa sababu wao ndiyo wanawaajiri watalaam hawa siyo Wizara yangu. Tunazungumza na wenzetu wa TAMISEMI ili watalaam hawa waajiriwe. Tutapangaje miji kama watalaam hawapo, nani atakupangia sasa kama watalaam wa kupanga hapo? Hawapo ndugu Waheshimiwa Wabunge. Hawapo kwa sababu kwenye Halmashauri na sisi Wabunge tunapiga kelele sana tunapokosa walimu, tunapiga kelele sana tunapokosa madaktari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sijasikia mtu anapiga kelele kwamba sisi Mji wetu hauna *town planners* au na mpango miji hakuna anayepiga kelele kwa hiyo, hata Halmashauri haziajiri. Tubadilike kama tunataka kweli miji ipangwe vizuri, vijiji vipimwe hawa wapima hao sasa na wako katika soko, lakini hatuajiri kwa sababu si kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu hii sekta ya ardhi na watalaam wa ardhi tuona sasa ni kipaumbele kama jinsi

ambavyo tunatoa kipaumbele katika madaktari, katika walimu, kabisa vinginevyo tutajitengenezea janga lingine mambo yanakwenda hayana mpangilio, hayajapangwa miji haijapangwa kwa hiyo siyo vizuri. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Peter Serukamba, ulisema mkakati uko wapi? Mkakati wa kwanza tuwapate watalaam wa kutosha wa kufanyakazi hii na wapo katika nchi hii. Pili, tuwape nyenzo za kufanyakazi hii. Halmashauri nyingi hazina vifaa hata vya kupimia tu. Wanaona siyo kipaumbele, tuwape vifaa. Halafu tatu zile sheria zetu tutaziimarisha za kuwasimamia wale sasa ambao ameshaajiriwa ameshapata vifaa, lakini anakiuka maadili ya kazi yake, viwanja anagawa mara mbili mbili nyumba hazina ubora yeye anakagua ovyo ovyo, sasa sheria zipo tumeshazitunga tutazitumia tuwadhibiti. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba je, mradi wa kuboresha makazi katika eneo Manzese umefikia hatua gani? Kuboresha yale maeneo ambayo yamejengwa holela holela yale ya *squatter* ni kweli tunao mpango wa kuboresha hizi *squatter* au *slum up grading* kule Dar es Salaam tunafanya Manzese, tunafanya Hananasif na tukipata fedha tutakwenda katika maeneo mbalimbali, kwa Manzese kwa sababu ndiyo hoja iliyoulizwa, uboreshaji wa miundombinu kwa kushirikishwa jamii umeendelea vizuri kwa fedha za mkopo wa benki ya dunia. Mpaka sasa eneo la Kata ya Manzese barabara mbili za lami zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lilikuwa limejengwa ovyo halijapangwa lakini ssa hivi limeshapangwa barabara zilikuwa hakuna sasa barabara mbili za lami tayari na kuna zingine sita ambazo zilikuwa hazipo zimetengenezwa. Alikuwa amejenga yaani hata kama mtu ana mgonjwa maana kupitisha gari hakuna barabara sita zimeshajengwa, mbili za lami, nne za changarawe na lazima sasa ubomoe wakubaliane wenyewe ubomoe baadhi ya nyumba ile barabara ipite na wanaobomoa walipwe fidia. Wameshalipwa fidia kwa hiyo, kazi imefanywa, mifereji ya kupitishia maji machafu tayari imeshawekwa katika hizo barabara, taa za barabarani zimeshawekwa, vituo vya kuchotea maji (*public water kiosk*) vimeshajengwa tayari, kwa sababu maeneo yale hata huduma ya maji ilikuwa hakuna na kazi inaendelea kwa sababu kwa kweli tungepata fedha tungefanya Manzese nyingi tu hapa nchini ambazo nazo tungeweza tukaziboresha lakini tatizo ni fedha lakini kazi imeanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine kuna tabia ya watendaji wa Serikali kuchukua ardhi ya wananchi bila makubaliano hususani eneo la Keko Matangini. Sheria yetu ya kutwaa maeneo kwa ajili ya huduma za umma sheria namba 47 ya mwaka 1967 inatamka kabisa kwamba Serikali ikichukua eneo kwa ajili ya huduma ya umma lazima mwenye eneo alipwe fidia na watu wa Kurasini mali zao zimeshathaminiwa na watalipwa fidia. Kusema kweli walishalipwa wakasema njooni mthamini tena hamkuthamini vizuri na Serikali ikawasikia, hii ni Serikali sikivu tukaenda tena tumethamini mara ya pili na sasa hivi wanaanza kulipwa fidia. Wakishalipwa fidia inabidi waondoke. Mzee Mapesa akasema waondoke waende wapi? Wametengewa viwanja kule Kibada tumepima maeneo katika watu ambao wanapata kipaumbele ya kupatiwa vile viwanja ni hawa wanaotoka Kurasini, tumepima viwanja tayari. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kilichobaki sasa ni kuchonga barabara tu katika lile eneo maana hapa mlikuwa mnasema mnapima viwanja hakuna barabara hata mahali pa kupitisha lori la mchanga lifike kwenye kiwanja changu sifiki, nataka kukuhakishia hivi viwanja vya sasa tunavyopima kule Dar es Salaam na kwingineko tunaweka na barabara. Kwa hiyo, watakwenda kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nisisitize suala la kupanua bandari ya Dar es Salaam ni suala lina maslahi makubwa sana ya uchumi wa nchi yetu. Ile bandari sasa hivi imekuwa ndogo, kuna msongamano mkubwa, lazima tuipanue. Bandari ile ndiyo inayohudumia mizigo ya Tanzania, Zambia, Congo, Rwanda na Burundi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, lazima Serikali huo mradi tuutekeleze, tupate bandari kubwa tuingize uchumi mkubwa ni chanzo kikubwa sana cha mapato katika ile bandari. Kwa hiyo, rafiki zangu wa Kurasini waende Kibada, kule bandari haiwezi kwenda Kibada kwa sababu hakuna bahari. Bandari lazima iwe pale Kurasini pana bahari wao waende kule viwanja vipo waishi kule huku tuweze kupanua bandari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine, nafikiri za Wapinzani niishie hapo, hoja nyinigi sana. Sasa hoja za Wabunge nianze na hoja ya dada yangu Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya* maana yeye peke yake tu ndiyo hakuunga mkono anasema mpaka kwanza apate maelezo, wote wameunga mkono, yeye akasema lazima apate maelezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, anasema kwa nini *TIRDO* hawajapewa hati ya kiwanja chao kule Dar es Salaam. Bahati mbaya hoja hii dada yangu Stella mimi nazungumza na wewe kila siku hili hujaniambia, angekuwa ameshaniambia mapema zamani sasa nina miezi mitano katika Wizara hii kwa kweli ningekuwa nimeshalimaliza, lakini bahati mbaya sijui ilikuwaje akaniviziavizia tu mpaka kwenye Bajeti. Lakini jibu ni kwamba *TIRDO* walikuwa na kiwanja chao lakini kile kiwanja kwa sababu walikiuka masharti ya kukiendeleza wakanyang'wanywa kwa utaratibu wa Serikali kutoa lile eneo kupitia kwa Rais aka-*revoke*. Baadaye *TIRDO* wakakata rufaa kwamba lakini katika *plot* hiyo kuna eneo fulani tumeshaanza kuliendeleza basi hilo ambalo tumeshaanza kuliendeleza tupeni, huko kwingine sawa wapeni *CCBRT*, lakini pale ambapo tumeshapaendeleza tupeni ulikuwa ndio ugomvi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Manyanya ugomvi huo umeshakwisha, Serikali imeshakubali hicho kiwanja ile sehemu ambayo wameiendeleza na sasa watapewa. Ila kinachogomba tu na wameshaelezwa kwamba lazima sasa walipie ada ya ile hati, hilo tu basi na hili si geni watu wote wanafanya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tusaidiane, mimi na wewe tuwaeleze walipe hiyo ada wakishalipa ada wakikaa siku mbili, tatu, hawajapata hati nipigie simu Mheshimiwa Manyanya na hili ungekuwa umeshaniambia mapema ningekuwa nimeshalimaliza, maana halina ugomvi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo sehemu nyingine katika kiwanja hicho hicho walichopewa *CCBRT* ipo sehemu ambapo *TIRDO* walikuwa wamejenga matenki haya ya maji machafu, wamejenga kwa gharama kubwa. Hilo eneo *TIRDO* wameshambiwa



mambo mawili, moja walipe fidia kwa hiyo gharama ya *TIRDO* waliojenga ile miundombinu pale au kama hawawezi kulipa fidia basi Serikali itakata lile eneo hili eneo lile lenye matenki ya *TIRDO* lirudi *TIRDO*. Kwa hiyo, hawa tumewapa hayo masharti wakubali ama wafidie gharama za *TIRDO* wabaki na hilo eneo kama hawawezi kufidia basi limegwe tuwape *TIRDO*. Mheshimiwa Manyanya, naomba tu uniunge mkono dada yangu kama unavyoniunga mkono siku zote ili kwa pamoja jambo hili tulimalize kwa manufaa ya *TIRDO*. *TIRDO* ni shirika letu sote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mbunge wa Mkinga yeye alisema kwamba Wilaya mpya ya Mkinga ina mahitaji makubwa ya kupimwa ardhi na kwamba MKURABITA waende haraka kukamilisha sehemu ya kupima mashamba. Sasa jibu ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ni kwamba kazi ya kupima ardhi, kupima vijiji, kupima Makao ya Mji wa Wilaya ni kazi ya TAMISEMI na Halmashauri yenu, sisi Wizara tuko tayari kushirikiana na ninyi katika kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko tayari kushirikiana na ninyi kama mtaandika andiko mkiomba mkopo katika ule Mfuko wa Kukopesha watu wanaopima viwanja na kwa sababu mfuko wenyewe si mkubwa sana mkichelewa mtakuta Halmashauri za wenzenu wameshakopa nyie mtabidi sasa mngoje mpaka mwakani. Kwa hiyo, tuko tayari kushirikiana na ninyi kimsingi ni kazi yenu Halmashauri ya Mkinga na TAMISEMI. Sisi ni wadau mkitaka ushauri wa kitaalamu tutatoa na vile vile katika kufanya mchakato wa kukopeshwa mpate fedha za kupima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, MKURABITA kuja kukamilisha kazi ya kupima vijiji kwanza niseme kwamba MKURABITA hiki ni chombo kiko chini ya Ofisi ya Rais hakipo katika Wizara yangu maana yake wengine hapa wanazungumza kwamba MKURABITA iko chini ya Rais ina Bodi inayojitegemea na Mwenyekiti wa Bodi tunaye hapa hapa Mheshimiwa Naibu Spika. Kwa hiyo, hii hoja nitaifikisha MKURABITA nitaibeba niifikishe kwa niaba yako Mheshimiwa, bahati nzuri Mwenyekiti naye anasikia yuko humu humu Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa mpaka kati ya majimbo ya uchaguzi Iramba Magharibi na Mashariki alizungumza Mheshimiwa Mgana Msindai. Mheshimiwa ndugu yangu hili nalo mwenye mamlaka ya kuweka mipaka ya majimbo ni Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Tume ya Uchaguzi, ndiyo sheria imewapa madaraka ya kuweza kurekebisha mipaka ya majimbo. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Msindai hili nalo nitalipeleka kunakohusika ili walifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Serikali imetoa shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya kuongeza eneo la ukanda wa uchumi baharini, kwa nini Serikali ya Tanzania imetenga shilingi bilioni moja tu badala ya shilingi bilioni mbili zinazotakiwa?

Mheshimiwa Mwambalaswa, ni kweli kwamba kama nilivyosema kwenye hotuba yangu wametupa msaada wa shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya lile eneo tunalotaka kuongeza la bahari. Sisi kwa mwaka huu tumetoa shilingi bilioni 1.29 karibu shilingi bilioni 1.3. Sasa tukichanganya na zile za Norway kazi itaanza, kwa sababu hii kazi haitakwisha mara moja. Kwa hiyo, mwaka ujao wa fedha tutakamilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili halina wasiwasi tumeshapeleka ombi Umoja wa Mataifa kutaka eneo hilo tuongezewe, ombi letu limeshafika pesa za kuanza kazi tunazo na kazi itanza. Kwa hiyo, ile *deadline* tarehe ya mwisho ya kupeleka ombi tarehe 13 Mei, 2009 sisi tumeshapeleka ombi kwa maandishi na maandalizi ya pesa yameshakamilika kwa hiyo hamna tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inashughulikiaje ugomvi wa mpaka kati ya Tanzania na Uganda eneo la Kakunyu na mpaka wa Tanzania na Malawi katika Mto Songwe, Mheshimiwa Paul Kimiti amezungumzia. Kimsingi hatuna mpaka wa Tanzania na Uganda na hatuna migogoro. Mwaka juzi tulishirikiana nao ule mpaka tukaweka *beacon* Tanzania na Uganda tukafyeka ule mpaka kwa hiyo, sasa hivi unaonekana vizuri sana na hatuna mgogoro na mpaka kiasi kwamba kama kuna mtu anavuka mpaka kwenda kufanya shughuli za uhalifu katika eneo la nchi nyingine sasa vyombo vya dola vina uhakika kabisa kwamba huyu amevuka mpaka, kwa sababu awali mpaka ulikuwa haueleweki eleweki kwa hiyo, tulikuwa tunavuka jinsi watu wanavyoona. Kwa hiyo, mpaka sasa uko wazi na kama kuna matatizo kule Kakunyu vyombo vya dola sasa vitashughulika bila mashaka yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Tanzania na Malawi kule Mto Songwe hatuna mgogoro kabisa kwamba yaani mgogoro kwa maana mtafaruku. Tatizo lililopo ni ule mpaka wetu ni Mto Songwe huwa unahamama mafuriko yakija unakuta yakihama na mpaka unahama. Tumeshakubaliana katika vikao vya pamoja kwamba tujenge mabwawa kila upande ili kudhibiti mafuriko ya mto na haya mabwawa hayo yatatumika kwa samaki, yatatumika kwa kilimo na kadhalika. Tukifanya hivyo yale mafuriko yatakuwa yamedhibitiwa, kinachogomba ni fedha tu za kuanza kutekeleza huo mradi. Tunazitafuta kwa pamoja tukishazipata tutajenga yale mabwawa ule Mto Songwe sasa utakuwa hauhamihami na tatizo la mpaka litakuwa limekwisha kati ya Malawi na sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo niunganishe na suala la Mheshimiwa Kapteni John Komba la mpaka wa Ziwa maana aliulizia. Mpaka wa Ziwa nao vile vile hakuna mtafaruku kwa sasa, lakini kila nchi ina tafsiri yake ndiyo tatizo lililopo. Malawi wanafikiri mpaka ni kwenye ufukwe upande wa Tanzania ndio mpaka. Sisi tafsiri yetu ni kwamba mpaka uko katikati ya Ziwa yaani wenyewe wana nusu na sisi tuna nusu. Sasa hivi kama nilivyosema kwenye kitabu changu cha hotuba kupitia Wizara ya Mambo ya Nje mazungumzo yanafanyika ili tupate muafaka tuwe na tafsiri moja ya mpaka. Sasa hivi uhusiano wetu na Malawi ni mzuri sana kwa hiyo, hakuna kelele. Lakini kuna siku watakuja Marais kwa sababu Marais wetu ni waungwana kuna siku atakuja Rais mwingine ataleta Majeshi mpaka kwenye ufukwe kwamba hapa ndio mpaka. Sasa kabla hatujafika huko nataka tukae tuzungumze, tuelewane tuwe na tafsiri moja ya mpaka. Hii ni kazi ya kidiplomasia na inaendelea kufanywa chini ya Wizara ya Mambo ya Nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kati ya Wilaya ya Chunya na Mbarali amezungumzia Mheshimiwa Victor Mwambalasa umekigawa kijiji cha Luhalanje. Hii mipaka kati ya Wilaya na Wilaya imo katika *Government Notice*. Hizi *GN*

tulishawasambazia Wakuu wa Wilaya wote na ziko ofisini kwa Wakuu wa Wilaya. Sasa ningependa kwanza kama huduma ya kwanza wazisome zile GN vizuri wawatumie wataalamu wa ardhi wachache waliopo huko huko kwenye Wilaya na Mikoa yao watafsiri hiyo GN mpaka unapita wapi ili kama GN ina matatizo basi watupe ushauri kwamba GN hapa ina matatizo haya na haya turekebishe hivi na hivi. Kama watalamu hawapo wa kutafsiri GN huko katika Mkoa wa Mbeya basi tutawasiliana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ili wataalamu kutoka Wilayani wa kutafsiri ile GN basi waje huko ili tumalize tatizo la Mheshimiwa Mwambalaswa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhaba wa vitendea kazi vya upimaji ardhi na wataalam katika Halmashauri nchini na pia bei ya kufanya survey ni ghali hili walizungumzia Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Mgana Msindai ndio walitoa hii hoja na nimeshaieleza kwamba ni kweli wataalamu ni wachache sana kwa sababu tulidhani hawa si muhimu hawana vipaumbele. Naomba Halmashauri na ninyi Waheshimiwa Wabunge wenzangu sisi wote ni Madiwani kweli kabisa jinsi tunavyochachamaa tunapeleka kuomba vibali vya kuajiri Madaktari, Walimu na kadhalika basi na hawa watu wa kupima ardhi na wenyewe tuombe tuwaajiri ili kazi hii ifanyike jamani, hawapo katika Halmashauri zetu nyingi. (Makofi)

Kuhusu bei za kufanya survey ni kubwa, ni kweli kwa sababu hata vifaa vyenyewe ni ghali vile vile tumeshaongea na TAMISEMI ili vinunuliwe na sisi kwa upande wa Wizara katika ile mikoa ambayo tunaona imeelemewa kabisa huwa tunapeleka walau hata seti moja au mbili zinakaa pale mkoani kama tulivyofanya karibuni kule Mwanza ziwe zinazungukazunguka katika zile Wilaya. Tunasaidia lakini wanaotakiwa kuzinunua ni wenzetu wa TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya upimaji na utoaji miliki iongezwe na upimaji ufanyike mapema ili kuzuia ukuaji holela wa miji. Sawa tunakubaliana ili kasi iongezwe tuweke moja kama nilivyosema wataalamu wawepo na pesa ziwepo kasi lazima itaongezeka. Kuna baadhi ya Halmashauri zinagawa viwanja bila ya ramani kupitishwa hali ambayo inasababishwa upungufu, usumbufu kwa wamilikishwaji wakati wa kuomba mikopo. Hili limezungumzwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Kama kuna baadhi ya Wilaya na Halmashauri zinagawa viwanja katika maeneo ambayo ramani hazijapitishwa hilo ni kosa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Richard Nyaulawa kama katika moja ya Halmashauri zako zinafanya hivyo kweli zinafanya makosa na sisi tutafuatilia kwa sababu kila ramani kwanza lazima ipitishwe rasmi ndipo viwanja viweze kupimwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mpango gani wa kuongeza kasi ya upimaji viwanja katika miji midogo hadi vijiji ili wananchi waweze kupata hatimiliki. Hili lilizungumzwa na Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Nadhani hili nimeshaleleza kwamba tatizo letu tuongeze wataalamu, tuongeze fedha na vifaa, tuongeze fedha za kulipa fidia kwa sababu unapopanua ule mji utakuta mashamba ya watu na mazao yao na kadhalika lazima unalipa fidia na lazima fidia tulipe. Hili jambo nasema ni suala la Halmashauri, TAMISEMI na sisi kama wadau wa Wizara yangu tutashirikiana kwa kutoa ushauri. Wizara ina mpango gani wa kuwezesha uundaji wa mpango wa miji ya Kasera, Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Mkinga. Nadhani hili

nimeshalisema kwamba ni kazi ya Halmashauri na TAMISEMI kwa kutaka ushauri Wizara yangu kama wadau na sisi tutawapa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la watu mijini ni tatizo kubwa likilinganishwa na jiografia ya nchi yetu hasa katika Jiji la Dar es Salaam, msongamano na kadhalika na kadhalika hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mbunge wa Chonga. Ni kweli ongezeko ni kubwa katika miji na bahati mbaya watu wanaingia mijini na upimaji wa viwanja mijini unakwenda taratibu kwa hiyo lazima wanajenga jinsi wanavyoona wenyewe. Ni tatizo kubwa kweli lakini nimesema kwamba tukiongezewa nyenzo tutaongeza kasi ya kupima viwanja ili tufukuzane kwa sababu hatutazuia watu wasije mjini kwa hiyo lazima sisi tufukuzane nao kwa kuwekea hiyo miundombinu na huduma ambayo inatakiwa. *(Makofi)*

Aidha, Serikali itafute maeneo yaliyopo wazi kama Kigamboni ili kupima viwanja na kupunguza msongamano huko, hili tualifanyia kazi. Katika mpango nilioueleza jana ule wa kuanzisha miji midogo midogo pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam. Jana nilisema katika hotuba yangu kwamba kwa kuanzia tumeweka maeneo matano, eneo la Luguruni na Bunju katika Manispaa ya Kinondoni, Pugu Kajiungeni Manispaa ya Ilala, Kimbiji, Kongowe, Mji Mwema Manispaa ya Temeke, haya maeneo tunataka yawe mji mdogo yenye huduma muhimu zote tena yamepangwa vizuri huduma za kisasa. Tukifika hatua hiyo kwanza mji wa Dar es Salaam utakuwa umezuia kwa sababu maeneo haya tusipowahi watu watajenga holela tu itakuwa tumezuia kwanza kupanuka holela lakini vile vile kutakuwa hakuna mtu kwenda mjini kwa sababu huduma za maduka makubwa zitakuwa kule, masoko yatakuwa kule, Mabenki yatakuwa kule, Posta iko kule, hospitali kila huduma zote zitakuwa kule na za kisasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo tumeanza na Luguruni pale tumeshapima lile eneo wananchi 259 mali zao tumeshazithamini sasa hivi tunawalipa fidia ili waweze wakapisha tupange vizuri pale na huduma zitakuwa pale. Mheshimiwa Charles Keenja anasema sawa mnalipa huduma baadae sasa waende wapi na aliulizia habari za kule Luguruni waende wapi. *(Makofi)*

Sasa pale kwanza niseme tunapolipa fidia mahali tunalipa ardhi yenyewe, sasa hivi ardhi ina thamani, zamani ardhi ilikuwa haina fidia. Lakini kwa sheria mpya iliyopitishwa na Bunge hili sasa ardhi hata kama tupu inafidia, mimea yake tunamlipa fidia, nyumba yake tunailipa fidia. Tunamlipa fidia vile vile kuhamisha mizigo yake huko anakokwenda, tunalipa ile gharama za usafiri iko ndani ya nini, tunalipa vile vile pango la miezi 36 huko anakokwenda kabla hajaanza kujenga nyumba yake mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hawa kwa kuanzia tumeshawalipa tayari fedha za miezi 36 ambazo atakuwa hana nyumba yake amepanga mahali. Tunawalipa hata kama alikuwa na biashara yake. Kwa hiyo, kwa kuhama ile biashara yake inatetereka nayo inapigwa mahesabu vile vile tunamlipa. Kwa sababu wakati mwingine tunasema Serikali inatuonea jamani hii sheria tuliyotunga hapa ni bora kweli, kwa sababu ina *package* ina vitu vingi ambavyo analipa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kuanzia watu hawa tumeshawalipa mahali pa kupanga kwa miezi 36. Lakini pale Luguruni jirani tuna mpango na tumeshaanza kupata viwanja 600. Hivi viwanja 600 wa kwanza kugawiwa watakuwa hawa kwanza tutakaowakuta pale hawatatoka. Halafu wa pili ni hawa watu 259 hawa nao vile vile watapata vipaumbele anayetaka katika viwanja pale atapata pale ili hizo huduma mpya za kisasa na wenyewe wawe karibu nazo na wenyewe wafaidi kwa sababu ni wadau katika kutengeneza hizo. Kwa hiyo, viwanja 600 ambavyo sasa hivi tumeshaanza kuvipima kando kando ya huo mji mpya wa Luguruni. *Plot* ya kwanza wanapata tunaowakuta pale, hawatavimaliza vitakavyobaki ya pili watakuwa hawa watu 250 hawatavimaliza, vitakavyobaki ndio watu wengine wataomba. (*Makofi*)

Katika jiji la Dar es Salaam watu wanajenga holela Mheshimiwa Lucy Owenya amezungumzia hivyo je lini *master plan* ya Dar es Salaam itarejewa, majengo yanaporomoka, hatua gani zitachukuliwa. Ni kweli *master plan* ya Dar es Salaam iliandaliwa mwaka 1979 na ikaanza kutumika mwaka 1985 lakini muda wake umekwisha mwaka 2005. Kwa hiyo, sasa hivi kama umesoma katika hotuba yangu ya mwaka huu wa fedha tunaanza kutekeleza *master plan* mpya ya jiji la Dar es Salaam, majengo yanayoporomoka.

Kwanza niseme kwamba Wizara yangu inasimamia upangaji kwamba hiki kiwe hapa kiwe hapa. Sasa tukishapanga lile eneo la makazi kusimamia wale wanaojenga ni Wizara nyingine, kusimamia na sheria wale wanaosanifu majengo, wale makandarasi, ametumia nondo sawa sawa au viwango vimekidhi au havijakidhi sasa hawa ni Wizara ya Miundombinu lakini Serikali ni moja tunashirikiana nao ili kuwabana hawa wanaojenga majengo ambayo hayakidhi viwango halafu baadaye yanaporomoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Ania Chaurembo, alikuwa na mambo mengi kweli sijui kama nitayamaliza yote. Kwanza lile la mabango kwamba lile eneo ambalo halifai kwa kujengwa kwa nini hamuweki mabango. Nasema ushauri ni sawa lakini anayeweka mabango katika miji mbalimbali sio Wizara yangu ni Halmashauri za Miji chini ya TAMISEMI. Nitafikisha salamu na bahati nzuri Mheshimiwa Ania Chaurembo ni Diwani katika Halmashauri kule Dar es Salaam na wewe tutasaidiana ili huu ushauri wako tuweze kuutekeleza ili asifikirie mara mbili kujenga pale kwa sababu atakuta kuna bango linalokatiza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mpango kabambe wa mji wa Dodoma haujatekelezwa kama ilivyopangwa. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally na baadaye Mheshimiwa Peter Serukamba waliuliza hayo. Swali hili limejibiwa mara nyingi kweli na Mheshimiwa Philip Marmo, Waziri mwenye dhamana ya mambo ya CDA. Ni kweli wenzetu Abuja wamejenga vizuri na mimi hivi karibuni nilipata nafasi kutembelea ule mji ni kweli wamejenga vizuri lakini pengine sisi tukitaka kujenga Dodoma kwa kutumia Bajeti ya Serikali, tulichojifunza itachukua muda mrefu kweli Dodoma haiwezi kujengwa na Serikali. Lazima sasa tutazame jinsi gani ya kushirikisha wadau mbalimbali na sekta binafsi na kadhalika. Abuja ndivyo alivyojenga na nadhani na sisi itabidi tutazame jinsi gani ya kushirikisha wadau mbalimbali kujenga Dodoma. Tunasema sisi Serikali Makao

Makuu ya Dodoma tutajenga Serikali peke yetu kwa Bajeti ya Serikali itakuwa ngumu kweli, lakini hii *message* imefika Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. (*Makofi*)

Kuhusu uvamizi wa maeneo mijini na kujenga holela na baadaye kuvunjwa wapewe *stop order* hili limezungumzwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Ndivyo inavyotakiwa na Halmashauri wale watu wa Mipango Miji wanatakiwa wafanye hivyo. Kwa nini mtu anaachiwa anajenga mpaka anamaliza ni suala ambalo niseme zamani Halmashauri nyingi zilikuwa zina watu, kazi yao ni kukagua tu maeneo tangu saa moja asubuhi mpaka saa kumi jioni kazi yao ilikuwa ni kupita kukagua maeneo ya mjini walikuwa wanaitwa *Land Angers*. Ukikuta tu mtu ameshaweka mchanga tu, au matofali katika eneo ambalo halistahili kesho yake asubuhi anakuta pale *stop* imeshawekwa baadaye nadhani Halmashauri zikaona kwamba watu hawa si muhimu wakawafuta. Sasa siku hizi mtu anavamia eneo anajenga anamaliza mpaka anahamia baadaye ndio tunakwenda kusema bomoa bomoa, tutazungumza na wenzetu waangalie utaratibu gani wa kufuatilia hivi viwanja kama zamani, utaratibu ulikuwa mzuri sana ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine miji midogo inaendelezwa kiholela kwa mfano Makambako, Chalinze, Tunduma, Ilula na kadhalika hayo yalizungumzwa na Mheshimiwa Richard Nyaulawa. Ni kweli lakini sasa hivi tunajitahidi kushauri kama washauri kwamba tuiwahi hiyo miji. Kwa mfano, mwaka huu tunashirikiana na Halmashauri zinazohusika tumeandaa mipango miji ya miji ya Makambako, Chalinze na Tunduma. Ni Wizara yangu tunashirikiana na Halmashauri zinazohusika ili tupange vizuri hiyo miji na mwakani uwezo ukipatikana wenzetu wa Halmashauri wakiweka pesa tutakwenda katika miji mingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *master plan* iandaliwe Loliondo, hayo yalisemwa na Mheshimiwa Michael Laizer na *National Housing* waje kule. Tumesikia Mheshimiwa, Halmashauri yako ijipange vizuri na sisi tuko tayari kushirikiana na ninyi katika kupanga vizuri mji wa Loliondo, *National Housing* kuja Mheshimiwa Michael Laizer nimeshakupeleka na kukukutanisha na Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing* mkazungumza nadhani mlielewana na mimi nitafuatilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naaibu Spika, miji midogo na mikubwa inajengwa kiholela hili nimeshalijibu. Maeneo yaliyoendelezwa Buguruni, Manzese na maeneo mengine yatafutwi mikopo ya kuyaboresha haya yalisemwa na Mheshimiwa Ania Chaurembo na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa. Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa akaendelea kusema hata baadhi ya maeneo yabomolewe halafu yajengwe ma-*flats* halafu wale waliobomolewa katika vijumba vidogo vidogo wapewe ma-*flats*, nadhani ni ushauri mzuri tu na wenzetu wengine wengi ndivyo wanavyofanya. Nafikiri tukishaanza ule utaratibu wa mikopo ya kujenga nyumba baadhi ya Mashirika ambayo yanabishana kujenga nyumba nafikiri utaratibu watautumia, ni utaratibu mzuri. Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa anasema vile vile katika baadhi ya nchi eneo fulani wanasema jengeni kwa ramani hii labda ramani mbili au tatu chagua hii ili majengo yawe ya namna moja kupendezesha mji. Vile vile ni ushauri mzuri miji mingine wanafanya nadhani na sisi tukafika hatua hivi tutafika tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunachofanya katika vile viwanja 20,000 vya Dar es Salaam tunachofanya wale wanaopata vile viwanja ziko ramani pale Manispaa za aina karibu sita. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Samahani kidogo. Ule muda wa kusoma majina hamja-include hapo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Zipo ramani kama za aina sita, mtu anapata kiwanja anaambiwa achague na kwa bei ya shilingi 50,000/= tu kwa sababu ukienda kuchoresha ramani yako watakupiga asilimia kumi ya bei ya jengo lako. Sasa nasikia baadhi ya Halmashauri zile ramani hawaziuzi eti wale wachoraji ramani wanasema wenyewe watakula wapi. Lakini nasema kwamba ule ni mchango wa Serikali ramani tumechora sisi Serikali ili kurahisisha watu wapate ramani kwa bei rahisi. Ntoa wito Manispaa za Dar es Salaam na Halmashauri nchi nzima wanaotaka zile ramani vile vile waje tuwape ili tuwarahisishie wananchi waweze wakapata zile ramani kwa bei nafuu kabisa na ni ramani nzuri kabisa. Kengele ya kwanza imelia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nitaongeza muda.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Nitashukuru sana maana hoja ni nyingi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko anasema Wizara yako ina mpango wa kukamilisha na kuandaa mipango ya muda mfupi miji ya Kibondo na Kasulu, je, mipango hiyo ya muda mfupi inahusika na mambo gani hasa? Jibu ni kwamba mipango ya muda mfupi ya matumizi ya ardhi yaani *Interim Land Use Plan* ni mipango ya kuongeza ukuaji na uendelezaji wa miji kwa kipindi kisichozidi miaka kumi ndiyo maana inaitwa *interim* yaani kipindi kifupi. Madhumuni ya mipango hii ni kuhakikisha kwamba matumizi mbalimbali ya ardhi yakiwemo ya makazi, biashara, viwanda, maeneo ya wazi, burudani na mengineo yanapangwa vizuri kwa ufasaha. Sasa baada ya miaka kumi kupita ndiyo utaandaliwa ule mpango mkubwa wa jumla wa muda mrefu unaitwa *master plan*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Lucy Owenya ameuliza jengo la jiko la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yaani Wizarani kwangu limejengwa chini ya waya ni hatari. Mimi nimeulizia lakini wamenihakikishia wataalamu kwamba pale mahali pamepimwa vizuri na wamenihakikishia hakuna hatari yoyote Mheshimiwa Lucy Owenya kwa hiyo mimi sina wasiwasi na wewe usiwe na wasiwasi. Serikali ihamasishe Mabenki pamoja na *NSSF* kujenga nyumba za *National Housing* ushauri wa Mheshimiwa Diana Chilolo. Nafikiri ni wazo zuri *NSSF* yaani ni Mashirika ya Umma, *National Housing* ni shirika la umma, mimi sioni sababu yoyote kwa nini wasishirikiane kujenga baadhi ya majengo, hili tutalifanyia kazi. Utaratibu wa kutoa kiwanja kwa kumpa masharti kwa muda wa miaka mitatu haufai hili lilisemwa na Mheshimiwa Laus Mhina, ni ushauri mzuri tutautazama hasa kipindi hiki ambacho hatuna mikopo ya nyumba. Tunaandaa mikopo ya nyumba kama nilivyosema jana sasa hivi bado haipo, kwa hiyo, mtu kumpa adhabu

miaka mitatu hujajenga tunakunyang'anya tunalitazama. Jukumu la kujenga nyumba liachiwe Halmashauri kama huko Ulaya. Vile vile ni ushauri tutautazama katika mazingira yetu tuone kama utatufaa, hatuna tatizo. Tatizo la Wizara imejiandaa vipi na ongezeko la watu katika miji ili kuweza kukabiliana nadhani nimeshalijibu hilo. Suala la *Tanganyika Packers* imekufa lakini wafanyakazi bado wapo katika nyumba hizo, kwanza nyumba hizo ni mali ya nani? Pili, kwa nini nyumba hizo zisiuzwe kwa wale ambao wako ndani ya nyumba hizo? Hii ni hoja ya Mheshimiwa Joyce Massunga, Mbunge wa Viti Maalum. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba eneo la *Tanganyika Packers* na nyumba ndani ya eneo hilo lilikuwa chini ya usimamizi wa Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma yaani *PSRC* na kisha kuuziwa kwa mwekezaji binafsi. Pili, *PSRC* mwenyewe hayupo, lakini yuko mrithi wake anaitwa *Corporation Holding Company (CHC)*, Wizara yangu itawasiliana na huyu *CHC* kujua hatma ya nyumba hizo na wananchi hao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Joyce Massunga tuachie Wizara yangu iwasiliane na *CHC* iliyerithi miradi ya *PSRC* tujue hatma ya zile nyumba na wale wananchi pale halafu baadaye tutakupa majibu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mortgage Finance* Wizara ianze na miji midogo na elimu itolewe Mheshimiwa Michael Laizer, ndivyo tutakavyofanya. Nimesema kwamba mpango wa kukopa watu wajenge nyumba au wanunue nyumba Muswada utakuja mwaka huu nadhani katika Bunge la mwezi Novemba, 2008 tutaleta Muswada huo na ukishapita Mheshimiwa Michael Laizer tutatoa elimu ya kutosha kabisa ili wananchi wafahamu na watu wa mabanki wafahamu ili na sisi tuweze kukopa tukajenga nyumba. (Makofi)

Mheshimiwa Emmanuel Luhahula aliuliza ni lini Wizara itasaidia kupanga matumizi ya ardhi ili maeneo ya wakulima na wafugaji yajulikane katika Wilaya ya Bukombe? Jibu ni kwamba mwaka huu wa fedha Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 100 katika Mikoa saba ukiwemo Mkoa wa Shinyanga na ikiwemo Wilaya ya Bukombe. Kwa nini Serikali haitoi elimu kwa wananchi kufanya maandalizi ya makazi hususan katika vijiji? Hili liliulizwa na Mheshimiwa Said Arfi. Suala la kutoa elimu kama nilivyosema tangu mwanzo ni jukumu la Wizara yangu, tukishirikiana na Halmashauri tutaendelea kuongeza kasi. Mheshimiwa Paul Kimiti aliuza kwa nini wadau wa makampuni binafsi wasitumie wanafunzi wa vyo vyetu ili wasambae nchi nzima na kuandaa hiyo mipango? Mheshimiwa Kimiti lipo tatizo tu la kisheria kwa sababu sheria imeelekeza tume ishirikiane na Halmashauri kufanya hiyo kazi na ishirikiane na wananchi wenyewe katika vile vijiji. Hizi ndio taasisi ambazo zimetajwa kisheria. Kwa hiyo, kusema wanafunzi wavamie nchi nzima pengine tutakuwa tunavunja sheria. Lakini hoja yako ni kwamba tutafute mbinu mbalimbali za kuharakisha kazi hii tumeipata na tutaifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa George Simbachawene anauliza MKURABITA utafika lini Kibakwe. Nimesema MKURABITA iko chini ya Ofisi ya Rais na nitafikisha ujumbe kwa sababu na mimi Wizara yangu ni mdau na tunafanya kazi kwa karibu na MKURABITA.



Mheshimiwa Kaika Telele ameulizia vijiji vyake vitapimwa lini na mpango wa matumizi ya ardhi kuondoa migogoro baina ya Batemi na Wamasai utanza lini? Jibu ni kwamba sasa hisi Mheshimiwa Telele tunayo mazungumzo na tulishafika hatua kubwa kabisa na Idara ya Wanyamapori ili kupima vijiji vyote vinavyozunguka *Lake Natron* na ambavyo vingi viko katika Wilaya yako. Kupima na kuviwekea matumizi bora ya ardhi, kwa hiyo, tunakuja na ujiandae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, anasema umilikiaji wa ardhi hapa nchini hauzingatii taswira ya uwezo wa ardhi kubeba watu na mifugo. Ni kweli lakini Mheshimiwa Mwalyosi baada ya kuwa na huu mpango wa Taifa wa matumizi bora ya ardhi ambao sasa watatupangia kwamba ardhi hii itumike vipi na nini, tatizo hili litakwisha na hii *master plan ya land use plan* ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la *double allocation* yaani kugawa viwanja mara mbili mbili, kiwanja kimoja kimepewa watu wawili lilikemewa kwa nguvu na wanaohusika vile vile wachukuliwe hatua. Hili liliulizwa na Mheshimiwa Paul Kimiti. Sasa hivi tumeshaanzisha mpango wa viwanja vyote kuwa katika kompyuta na tumeshaanza pale Makao Makuu tumeshamaliza na tumeanza kusaidia Halmashauri, mwaka jana tulifanya Halmashauri nane na mwaka huu nane ili mtu ukitaka sasa kuweka kiwanja kingine kompyuta itakugomea. Sasa huyo ambaye kompyuta imegoma yeye bado ana-*allocate* tu sasa huyo anafanya makusudi huyo sasa ni mharibifu tunamchukulia hatua. Maana hakufanya kwa bahati mbaya kafanya kwa maksudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Fuya Kimbita kaulizia kwamba ubia katika *National Housing* uzalendo uzingatiwe na wengi wamezungumzia jambo hili kuonyesha picha kana kwamba kule *National Housing* ubia kama unakwenda kwa Watanzania tu wa aina fulani na hauendi kwa Watanzania wote. Sasa mimi nimehoji hilo, wamenieleza kwamba ubia kwanza wanatangaza wazi, wanaomba. Kwa mfano sasa hivi miradi ya ubia iko 187, sasa Watanzania wazawa ni 70 kwa hiyo wale Watanzania wengine wale ambao aliwasema Mheshimiwa Fuya wako 117.

Kwa hiyo, kwa kweli sio picha nzuri kwamba huu ubia wanapata Watanzania wa rangi fulani, ndiyo wanapata hii miradi na Watanzania wa rangi fulani hawapati. Mimi ninachosema Watanzania wenzangu wazawa tunapopata miradi hii basi tufanye vizuri basi. Kwa sababu katika hawa 70 ambao wamepewa huo ubia ambao wamekamilisha ni wawili tu kati ya 70. Sasa hilo nalo tusilionee aibu, ukipata shughuli ifanye vizuri ili na sisi tujenge sifa nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mohammed Abdulaziz anasema Shirika la Nyumba la Taifa linahitaji kufanya vizuri shughuli zake lakini tatizo kubwa ni tatizo la Serikali ambazo hazilipi kodi. Kwa hili ni kweli na mimi Wizara yangu yenye dhamana ya *National Housing* tunawasaidia ili wote wanaotakiwa kulipa kodi walipe. Si Serikali tu hata watu binafsi kwa sababu tusipolipa kodi hili Shirika tutaliua na ni letu la umma. Kwa hiyo, hili tutalifuatilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Savelina Mwijage anauliza kwamba kwa nini Wizara isikarabati nyumba za *National Housing* ambazo zimechakaa sana na zinatia aibu na kwa nini Shirika haliuzi nyumba zilizopangwa kwa zaidi ya miaka 40? Tumeanza kuzikarabati nyumba nyingi za *National Housing* sasa hivi kila mwaka asilimia 25 ya mapato yote ya shirika yanayotokana na kodi ya nyumba yanakwenda kukarabati nyumba. Ndiyo maana ukipitapita kwenye miji yetu mingi kwa kweli hii kazi wameshaanza kuifanya na wanaifanya vizuri. Kuuza sasa hivi hawauzi lakini mbele ya safari hasa tutakapoanzisha ule utaratibu wa kuuza *flats* ambayo hiyo sheria hivi karibuni itakuja Shirika watafanya hesabu, hivi hizi *flats* tukipangisha kwa mwezi mmoja mmoja kwa miaka kadhaa tunapata shilingi ngapi na tukiziuza tukapata fedha tukajenga *flats* nyingine, watafanya hesabu na kama ikionekana kwamba kuziua inaleta faida zaidi basi watawauzia wale walioko katika zile *flats* kwa sababu sheria ya kuuza *flats* inakuja. Jengo lina *flat* ishirini kila mpangaji atanunua kale kasehemu kake na anapata hati ya sehemu yake katika hilo ghorofa. Lakini muda ukija sisemi tutaanza kuuza kesho lakini nasema muda ukifika. (Makofi)

Mheshimiwa Abbas Mtemvu, ameuliza vile vile kwamba maeneo makubwa kama yale ya kota za Magomeni, Tandika na *Chang'ombe flats* kwa nini yasiuzwe? Nimeshalijibu kwamba wakati haujafika lakini wakati ukifika hesabu zikifanywa zinaweza zikauzwa. Lakini kwa sasa hivi bado kidogo. Wizara ya Ardhi itenge fedha nyingi kwa ajili ya kupima viwanja ili wananchi waweze kugawiwa. Hili sawa nadhani baada ya hoja nyingi za Wabunge Serikali imesikia na nadhani mwakani Bajeti itaongezeka ili tuweze kufanya kazi kubwa zaidi. Pia Mheshimiwa Ania Chaurembo kule Bagamoyo, anasema walitoa shilingi 300,000/= lakini hamjapata. Lakini leo asubuhi hukuwepo lakini Mkuu wa Mkoa wa Pwani amethibitisha kwamba tulishawapa mkopo na wamepima viwanja 2,500 na sasa hivi wanavigawa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ania Chaurembo uende, ila kwa sababu wameshaweka na miundombinu ya barabara na mingine bei haitakuwa sasa shilingi 300,000/= lakini kikubwa ni kwamba mpate viwanja vyenu. (Makofi)

Mheshimiwa Lucy Mayenga alikuwa ana hoja nyingi kweli na jana alikuwa mkali kweli kweli. Niseme tu tumezipokea Mheshimiwa Lucy Mayenga na kuhusu *National Housing* kwamba utaratibu wa kupangisha nyumba kwa mtu kwenda kusema nyumba hii iko tupu, kesho yake ukienda wanasema mwenzako mwingine ameshakuwahi, hili tumelisikia na kama kweli mchezo huo upo tutazungumza nao, na mengine yote ambayo ulitukemea kweli kweli uwe na uhakika kabisa kwamba tumekusikia. (Makofi)

Hoja kwa kweli ni nyingi, nitazijibu kwa maandishi zote kabisa na naomba mnamini kwamba tutazifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hote haya naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa tunaingia hatua inayofuata. Katibu.

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

#### Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Kifungu 1001- *Administration and General*.....3,292,019,500/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Rished Abdallah, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Gaudance Kayombo, Mheshimiwa *Captain* John Komba, Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa George Simbachawene na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. (*Makofi*)

Tunaanza na Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba kuuliza swali dogo tu lakini linaweza kuwa kubwa kwa namna yake kwani namuulizia mtani wangu Mheshimiwa Kepteni John Komba. *Suppose* watu wa Malawi wakivamia mpaka *Mbambabay* Mbinga halafu Mheshimiwa John Magufuli akaenda akachoma yale makokoro yao je, tutawapiga au tutakaa chini tulie? Ahsante. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Kazi ipo, makokoro yamo kila kitu kimo. Mheshimiwa Waziri hebu jaribu kujibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu kwamba mpaka sasa kule kwenye mpaka wetu na Malawi, tunaheshimiana tu. Sisi Watanzania tunavua katika lile Ziwa, Wamalawi wanavua katika lile Ziwa. Mpaka sasa hatuna mtafaruku na hatuombi tupate mtafaruku. Ndiyo maana kwenye majibu yangu nikasema kipindi hiki pengine ndiyo kipindi kizuri sana cha kufanya mazungumzo ya kuafikiana kuhusu mpaka. Sasa hawa wanaovua lazima wafuate sheria kwa sababu ukivua Tanzania lazima uvue kwa kufuata sheria za Tanzania na ukivua Malawi lazima ufuata sheria za Malawi. Ukivunja sheria utakamatwa tu. Kwa hiyo, hata hao anaosema Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda wakivunja sheria, sheria itawabana tu. Lakini kikubwa nasema kwamba sasa hivi hatuna mtafaruku na ni wakati mzuri sana wa kufanya mazungumzo wakati wote tukiwa katika hali ya urafiki na utulivu.

**MWENYEKITI:** Napenda kusema kwamba ninaweza kuruhusu maswali ya nyongeza kama lazima. Sio kila mtu uulize swali la nyongeza kwa kulazimisha tu. Kama lazima mnaruhusiwa leo. Mheshimiwa Kepteni John Komba.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mpaka kati ya Malawi na Tanzania kupitia Ziwa Nyasa ni la muda mrefu, sasa linafikia miaka

44, hata Dr. Kamuzu Banda alituvamia bahati nzuri tukamzidi nguvu, tukamchapa, akarudi. Lakini hali ikabaki ile ile. Sasa hili jambo nikiuliza kila siku najibiwa tunashughulikia, tunalishughulikia. Hivi halina *time frame* ni lini hasa tufikie *deadline* kwamba mpaka wetu ni huu sasa? Maana inakuwa ni vurugu tu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Unajua nimekustahi tu kwa sababu mwenzako huyo alishauliza swali hilo. Kwa mujibu Kanuni ulipaswa usiulize. Lakini Mheshimiwa Waziri hebu mjibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishasema katika jibu langu la awali kwamba ni kweli pale kuna mgogoro ulijificha kwa sababu kila nchi inatafsiri tofauti. Sasa hivi kweli ni marafiki, tunaishi kwa amani lakini kuna kitu ndani ambacho kimejificha kwamba kuna siku hawa Marais wetu leo ni marafiki kwa hiyo, tunaishi kwa urafiki. Lakini anaweza akaja Rais mwingine mwenye tabia nyingine basi akaja akasema tu kwamba Tanzania hakuna kuvua ufukweni na akaanza kukamata Watanzania. Kwa hiyo, nikasema kwamba mgogoro huu dawa yake ni mazungumzo ya kidiplomasia. Sasa Mheshimiwa Kepteni mwenzangu ingekuwa ni vita au mpira tungekuwa tumeshamaliza. Lakini kwa sababu ni diplomasia inakwenda taratibu na ndiyo maana inaitwa diplomasia, kwa hiyo, mimi naamini diplomasia itafanya kazi tuwe na subira na mambo *Inshallah* yatakwenda vizuri. (*Makofi*)

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimekuwa nikichangia kuhusu Shirika la Nyumba la Taifa kufanya kazi zake katika sehemu za Wilaya kwa sababu kule Wilayani pia wapo Watanzania wanaoishi na hasa katika Mikoa ile ambayo hata Mheshimiwa Rais alitamka kwamba iko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipofuatilia kwa barua wakasema hawajaanza utaratibu wa kujenga Wilayani na watafanya utafiti na utafiti utakapokamilika wanaweza wakafikiri. Lakini niliposoma katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri inaonekana wamejenga Chato na Chalinze; ni kwa nini sasa Mbinga hawakujenga na maana yake utafiti umeshakamilika kama wameshaanza kazi. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba *National Housing* wameshaanza kujenga Ruangwa, Chato, Chalinze japo Mheshimiwa Peter Serukamba akasema sasa na Chalinze mnaanza kujenga maghorofa porini lakini ndiyo tumeshaanza kwamba hata huko porini Wilayani na wenyewe wanastahili vilevile kuwa na vitu vizuri tu. Sio vitu vizuri viwe mijini pake yake. Kwa hiyo, Mheshimiwa Gaudence Kayombo tumeanza, uwezo wa *National Housing* ni mdogo ndiyo maana hatujajipanua sana. Lakini tutakapoanza huu utaratibu wa kukopa ili kujenga na kununua nyumba *National Housing* nao watakapo vile vile. Watakopa wataongeza uwezo wao wa kujenga nyumba na *Inshallah* watafika katika maeneo mbalimbali na mimi sitasikitika kama na Manyoni wakifika si mbaya kwa sababu yote ni Tanzania. Lakini nataka kutoa ahadi kwamba sasa hivi *National Housing* wakipata uwezo kupitia utaratibu huu wa mikopo ya kujenga nyumba watafika mpaka Wilaya za vijijini na hawataishia mijini tu kama ilivyo sasa. (*Makofi*)

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu hapa Bungeni jana pamoja na mambo mengine niliongelea suala la baadhi ya Kanda hizi zilizopangiwa hati za kumilikishwa ardhi, kwamba zimepata bahati mbaya kwa sababu huduma hizo watapata mbali sana na nikatoa mfano wa Mikoa ya Kanda ya Kusini na Magharibi nikataja Mtwara na Kigoma. Nikasema sasa Wizara inge *revisit* uamuzi wake ili kuona zinawasaidia kwa sababu kwa muundo wa hizi Kanda maana yake zitapata huduma mbali sana jambo ambalo bado halisaidii kuondoa matatizo ya wananchi. Sasa sijamsikia Mheshimiwa Waziri aki-*comment* jambo lolote, je, anatuahidi nini watu wa Kusini na Magharibi kuturahisishia huduma hii haraka? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mchango wake wa jana alisema hili na kwa bahati mbaya muda wangu ulikuwa mdogo sikufika kutoa majibu yake lakini nashukuru amenikumbusha. Nia yetu ni kusogeza hii huduma ya kutoa hati karibu kabisa na wananchi na ndiyo maana tumepeleka kwenye Kanda. Kwa kweli kimsingi baadae tutafika kila Mkoa lakini kwa sasa hivi tumeamua twende hatua kwa hatua. Kwa sasa hivi tunaanza na Kanda tano lakini mwakani tunaongeza kanda mbili, tutaongeza Kanda ya Mtwara ambayo itahudumia Mtwara na Lindi halafu kutakuwa na Kanda ya Magharibu ambayo itakuwa Tabora, kwa kuhudumia Tabora na Kigoma. Kwa hiyo mwakani tutakuwa na Kanda saba ili kusogeza huduma. Kwa hiyo, Mheshimiwa Juma Njwayo tunakwenda tu kwa awamu, awamu inayokuja na Mtwara mpo. Lakini niseme tu kwamba sasa hivi Mtwara tuna ofisi ndogo ya Kamishna wa Ardhi, kwa sababu zamani tulimweka kabisa mtu pale lakini ikawa maombi ya hati yakawa machache sana. Anakaa mwaka mzima hati tatu. Kwa hiyo, ofisi hatukuifunga ipo pale, tuna karani zikishakuwa nyingi anatoa taarifa mtu kutoka Dar es Salaam anakwenda kuweka sahihi pale. Lakini mwakani tunaifungua rasmi kwa sababu tuna amini kabisa sasa watu watachangamka na ardhi na hati zitakuwa nyingi. Jiandaeni kupokea kituo mwakani. (*Makofi*)

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa kuongea nilizungumzia juu ya ramani ambayo ilichorwa na Wizara ya Ardhi ambayo ilileta upotoshaji wa mipaka kati ya JKT Chita na kijiji kilishasajiriwa na kupewa hati cha Ikule. Nilitaka kujua ni hatua gani za haraka zitachukuliwa kutatua mgogoro huu ambao umedumu miaka 13 na kuleta uhusiano mbaya kati ya Jeshi na wenyeji wao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Castor Ligallama katika mchango wake alitueleza hili tatizo la mgogoro wa mpaka kati ya JKT Chita na kijiji cha Ikule. Niseme tu kwamba tumepokea hoja yake na katika maelezo yake alisema kuna Tume zilishapelekwa pale na TAMISEMI vile vile Ofisi ya Rais ilishapeleka Tume. Kwa hiyo, mahali pa kuanzia tunapo tutaangalia hizi tume zilisemaje, *GN* zenye mipaka hiyo zinasemaje, ramani zimekaaje. Nadhani atuachie tulifanyie kazi kwa nia ya kulimaliza ili mwakani tukikutana hapa tuzungumze mengine, tusizungumze hili tena. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi. Katika Hotuba ya Waziri ukurasa wa 46 amezungumzia kuhusu mipango ya uendelezaji wa miji na vijiji. Lakini katika hotuba hii ametaja tu kwamba mpango ulipo katika mwaka 2008/2009 ni kuingiza kwenye mpango miji ya Kasuru, Kibondo, Maswa na Kyela na katika majibu yake kazungumzia pia kuongezea sehemu zingine za Chalinze na Makambako katika utaratibu huo. Lakini kwa kuwa kipengele kile kinazungumzia pia vijiji na mimi nikadhani kwamba mtu wa Kibakwe naweza nikapata fursa kwa sababu Kibakwe ni kijiji na hali ya Kibakwe inakuwa sana, uwekezaji ni mkubwa na nimeomba wawekezaji wajenge Benki lakini hatuna *master plan*. Kwa hiyo, mimi nikafikiri huu mpango wa utumiaji bora wa ardhi unaweza ukanisaidia. Je, Mheshimiwa Waziri unaweza ukanikubalia mdogo wako angalau na mimi ukaniingiza kwenye mpango huo kama kijiji, maana ulipotaja katika Mkoa saba na ukataja na Wilaya ya Bukombe nikategemea utataja na Kibakwe. Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tuliyojata kwenye hotuba ya Bajeti ndiyo uwezo wetu wa mwaka huu. Sasa nikiongeza na Kibakwe wakati uwezo wa kufika huko bado mwaka huu haupo, sasa ndugu yangu nitakuwa namdanganya na mimi nataka niwe mkweli. Lakini kama Halmashauri ya Mpwapwa itakuwa yenyewe iko tayari inazo fedha kwa ajili ya kupima kule Kibakwe na kupanga matumizi ya ardhi na akaomba Wizara yangu ishiriki kule kutoa utalamu hilo linawezekana. Lakini hata huko tunakokwenda tunatazamia Halmashauri nazo zishiriki yaani nguvu zao na nguvu zetu za Wizara zichanganywe zifanywe. Lakini kama Mpwapwa haina chochote kwa Kibakwe wategemea tu nguvu za Wizara peke yake na nguvu zetu kwa mwaka huu hazifiki Kibakwe! Sasa ndugu yangu Mheshimiwa George Simbachawene, napenda sana nifike Kibakwe nisaidie lakini nimefungwa mikono. Lakini natoa wito Halmashauri ya Mpwapwa kama ina fedha ya kupima Kibakwe sisi Wizara tupo tayari kushirikiana nao. (*Makofi*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya kutia matumaini niliyopewa na kaka yangu na Katibu wangu Mwenezi kuhusiana na suala la *TIRDO* naomba nipate ufafanuzi ufuatao.

Kwa kuwa katika kufuatilia kwangu nimegundua kwamba yawezekana Wizara yako inashindwa kushughulikia suala hili kwa kuwa linamuhusu kwa karibu sana Mheshimiwa ambaye ni Katibu wa CHADEMA Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa ambaye ana mahusiano ya karibu na *CCBRT*. Je, utanihakikishia kwamba wewe mwenyewe utachukua jukumu hili la kuhakikisha kwamba tatizo hilo linakwisha ikizingatiwa kwamba suala la kusema kwamba kiwanja kile kilikuwa hakijaendelezwa si kweli bali mimi naona ukweli ni kwamba wale wasaidiwe ardhi na kama walipima kimakosa basi ilikuwa ni muafaka kusahihisha kosa tatizo hilo kwa wakati?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie kwamba katika kushughulikia suala hili kwa sababu pale kuna kigogo anaitwa Dr. Wilbrod Slaa, Katibu Mkuu wa

CHADEMA ndiyo maana Wizara ikawa inapata kigugumizi kumaliza hapa, si kweli. Tena afadhali amekuwa CHADEMA angekuwa CCM mwenzangu ndiyo ingekuwa mbaya zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kawaida za kisheria zilitumika, kile kwanja kilitwaliwa kwa taratibu za kisheria kabisa; hakukuwa na njama wala kumkomoa mtu wakapewa CCBRT baadaye TIRDO wakasema kuna eneo walikuwa wameliendeleza warejeshewe. Serikali iliwarejeshea, ikawa hawapewi hati lile eneo walilorejeshewa na ndio hoja aliyoleta Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Mimi nakuhakikishia kwamba, sasa Serikali lile eneo ambalo TIRDO wameliomba inawapa. Walipe tu ile ada ya hati ili wapewe hati. Nami nasema mimi na wewe tushirikiane tulimalize, wao walipe ada na mimi nimwambie Kamishna pale naye atoe hati, basi tulimalize. Kwa hiyo, nataka kukuhakikishia kwamba, hili jambo litakwisha na kwamba... ile (b) yake sikuipata vizuri, naomba arudie (b).

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Nilikuwa nataka kufahamu kama wewe mwenyewe ndiye utakayehakikisha hivyo vikao vinafanyika, kwa sababu katika kufuatilia kwangu niliambiwa kwamba, Mheshimiwa Dr. Slaa hatoi ushirikiano.

**MWENYEKITI:** Jamani, Mheshimiwa Dr. Slaa naomba mumwondoe katika vitu hivi ni utaratibu wa sheria tu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli ni utaratibu wa sheria na nilishasema katika jibu langu la mwanzo kwamba, mimi mwenyewe nitasimamia kwa sababu jambo hili limechukua muda mrefu, hata bajeti iliyopita alilisema Mheshimiwa Eng. Manyanya na mwaka huu amelileta tena. Sitaki tena bajeti ijayo alilete tena, nataka tulimalize na mimi nakuhakikishia kwamba, nitasimamia ili liishe na wewe simamia walipe ada ile ya hati ndio kazi yako na wewe Mheshimiwa Mbunge mwenzangu nakutuma hiyo. Wakishalipa na mimi nitasimamia hati itoke. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Itabidi Eng. Manyanya *a-declare interest* yeye atakapokuwa anasimamia ni kama nani? (*Kicheko*)

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Nitasimamia kama Mjumbe wa Bodi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nahitaji ufafanuzi tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Nilipokuwa nikichangia asubuhi nilizungumzia kuhusiana na uvamizi wa shule Kawe ambapo viwanja viwili; Na. 665 na Na. 96 vya Kawe B na Mkwamani na vilevile nikampa vidhibiti. Sasa naona Mheshimiwa Waziri hajajibu kabisa. Kwa hiyo, sijui amedharau au ndio analifanyia kazi au ndio ile nguvu niliyokuwa nikiizungumzia inafanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusiana na lile suala zima la Keko Matangini; ni kweli kabisa nakubaliana naye kwamba, *compensation* inalipwa, lakini tatizo lililokuwepo kama nilivyoeleza awali ni kwamba, kuna usiri wa hali ya juu na kwamba, wananchi wanasainishwa tu makaratasi pasipokujua ni kiasi gani watapata *in return*.

Kwa hiyo, lengo la kuuliza lile swali ni kujua hiyo tathmini inafanyika kwa maridhiano pamoja na wale wananchi ama vinginevyo kwa sababu inasemekana kwamba, hadi hao wanatathmini pamoja na Mwenyekiti wa Kijiji wa eneo husika, anasema kwamba watakuja kuvamia usiku kuweka “X” kwa watu. Sasa nilikuwa nataka kujua hiyo tathmini inafanyika katika mazingira gani na kama kuna maridhiano ya kweli baina ya Serikali na wale wanakijiji katika thamani halisi ya ardhi ya lile eneo. Nashukuru.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Halima Mdee, alieleza katika mchango wake. Bahati mbaya tu, mambo yalikuwa mengi ile saa moja haikutosha. Si kwamba nilipuuza ila tu muda ndio haukutosha, lakini tumelichukua. Niseme tu kwanza, tumpongeze alikuwa muda mrefu yuko masomoni kwa mwaka mmoja, nasikia amefaulu. Tunakupongeza sana na vijana waige mfano wako ili msome mlichangamshe Bunge. Hongera sana kwa kufaulu masomo yako Afrika Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuhusu maeneo ya shule yaliyovamiwa, nataka kusema tu kwamba, nimelipokea, tutatazama kwa kushirikiana na Manispaa ya Kinondoni ilitokeaje eneo la huduma ya jamii; shule na kiwanja apewe mtu mwingine binafsi, yaani tu katika hali ya kawaida, tutajifunza nini kilichotokea. Kwa hiyo, naomba anivumilie tulichukue, wataalam wangu watashirikiana na wataalam wa Manispaa ya Kinondoni, tuone jambo hili ilikuwa kuwaje eneo la shule likachukuliwa na mtu binafsi, halafu tuone jinsi ya kuendelea nalo. Naomba tu anikubalie, sasa hivi sina majibu ya moja kwa moja, lakini uchunguzi utafanywa; Kinondoni tutawashirikisha, tuone tatizo ni nini na jinsi gani ya kulitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba hili zoezi lina usiri sana Keko Matangini. Si kweli kwamba, Watanzania wamezoea, yaani sijui tumejenga tabia gani tu ya kulalamika na malalamiko mengine ni nje ya utaratibu. Serikali inapokwenda katika eneo fulani kuchukua kwa madhumuni fulani; jambo la kwanza, wale wanaohusika katika eneo lile wanajulishwa kwamba, Serikali inataka eneo hili, kwa nini linatakiwa na lazima iwe ni kwa madhumuni ya umma, yaani Serikali inapokwenda kutwaa eneo fulani lazima iwe kwa madhumuni ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haiwezi kutwaa eneo, nikapewa mimi hayo siyo madhumuni ya umma. Wanaelimishwa eneo hili linatakiwa nini, wanaelimishwa vilevile utaratibu wa fidia utakuwaje na unafidiwa kitu gani. Elimu inatolewa kabisa wanapoanza kuthaminiwa mambo yao, haendi mthamini peke yake akakaa na mwenye mali pale, wanakuwepo pale Mwenyekiti wa Mtaa na Mjumbe wa Mtaa ule. Kwa hiyo, kunakuwa na timu ya watu kama watatu au wanne. Mali yake inathaminiwa, baadaye inahakikiwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tu watu hawataki kuhama pale, basi wanazua maneno mengi kweli. Kuna wengine wanakwenda mpaka mahakamani, kuchelewesha tu zoezi hili na kuchelewesha uchumi wa nchi. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mdee, kwa kweli hakuna usiri; zoezi tangu mwanzo elimu imetolewa kwa wale watu, wameelezwa madhumuni ya pale, wameelezwa uthamini utakwendaje, wameelezwa watakwenda wapi, wakihama pale waende wapi, yaani kila kitu wameelezwa kiko wazi kabisa. Naomba Mheshimiwa Mdee tusaidiane na wewe kuwaeleza wale watu kwa manufaa ya uchumi mpana wa nchi yetu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa staili yake ya kujibu ambayo ni *very convincing*, inakuita mpaka kwenye moyo ukubaliane naye tu. Kwa hili ambalo nitauliza, siyo kwamba lazima tukubaliane, ila tu naomba kama inawezekana tukajadiliana baadaye kama mchakato wa Taifa, nalo linahusu hati ya miaka 33 zaidi kule kijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anajua sisi sote tumerithi ardhi kutoka kwa wazazi wetu na sisi wengine tunategemea kurithisha watoto wetu kipande cha ardhi kilichopo na zaidi katika *areas* ambazo watu wamesongamana kama Kilimanjaro kule. Sasa ukianza kuwapa hati miaka 33 halafu baadaye tena waende kuita mkutano wa kijiji, unajua tena mahusiano ya kijiji, wengine wanasema wewe unalinga sana ondoka hapa na vitu kama hivyo. Mimi nasema utaratibu huo ni mwanzo wa migogoro katika vijiji vyetu zaidi kule tunakoenda. Kwa hiyo, najua hii imo ndani ya sheria, lakini sheria inaweza kuzungumzwa. Mimi nafikiri tungeongeza, badala ya kuwa tuna tabaka tatu za hati; 33, 99, zamani kulikuwa na 66 hapo kati kati, labda tungeongeza ya nne kwenye vijiji iwe *free hold*. Sijui anasemaje kwa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine dogo, mimi kama Mwenyekiti wa *Public Accounts Committee*, kila siku kuna *query* ya viwanja vya Serikali havina hati. Yeye kama Waziri mpya atahakikisha basi na kuna majengo mazuri sana yanajengwa siku hizi ya Serikali, kila kiwanja cha Serikali kina hati miliki ya Serikali.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi wa hoja za Mheshimiwa John Cheyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunazo hati za miaka 33 na miaka 99. Vilevile niseme kwamba, tunazo ardhi za kisheria za aina mbili au tatu, lakini kubwa mbili, hii ya tatu niache. Aina ya kwanza ya ardhi inayotambuliwa kisheria ni ardhi ya vijiji (*Village Land*), aina ya pili ya ardhi kisheria ni ile ardhi ya kawaida (*Public Land*), ambayo haimo katika eneo la kijiji. Sasa hizi hati za miaka 33 na miaka 99 zinatolewa kwenye *public land*, yale maaneo ambayo si ardhi ya kijiji, ndiyo yanayohusika na kupewa miaka 33 au miaka 99. Ardhi ya kijiji (*Village Land*) inapokuwa sasa mwanakijiji anamilikishwa, anapata hati inayoitwa hati ya kimila (*Customary Right of Occupancy*). Hii hati ya kimila haina ukomo ni ya milele, kwa sababu ni ardhi ambayo mnathiriana pale kijijini; anakufa babu, anakuja mjukuu. Kwa hiyo, nilitaka nitoe ufafanuzi huo kwamba, mawazo yake na

yangu na sheria inavyosema, ndivyo ilivyo kwamba, ardhi ya kijiji, hati ya kimila haina ukomo, mtarithiana ukoo wenu wote kabisa, labda baadaye mje muuze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma kidogo, viwanja vya Serikali vilikuwa havihitaji kuwa na hati kwa sababu ilikuwa ni kama Serikali unajipa hati yako mwenyewe kwa mali yako mwenyewe. Kwa hiyo, ilikuwa haina haja ya kupata hati, lakini mambo yanakwenda yanabadilika, sasa hivi tumeanza utaratibu vilevile kwamba hata sasa taasisi za Serikali wanaweza wakaomba hati na wao wakapata hati na tunawashauri wafanye hivyo kwa sababu sasa baadhi ya maeneo ya Serikali yanavamiwa. Sasa ukishavamiwa ukienda mahakamani huna hati, mahakama inasema wewe unasema ardhi hii ya kwako lete hati huna!

Kwa hiyo, ili tujiweke katika hali ya usalama, tuondoe ugomvi na wananchi wanaovamia vami maeneo ya Serikali, sasa hivi tunashauri kwamba, maeneo ya Serikali vilevile yapimwe na tuko tayari kuyapa hati.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka tu ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu yapo matatizo ambayo yanatusibu sisi ambao tupo katika fukwe za bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ya fukwe za bahari sasa hivi imekuwa ni mali kubwa sana na imefikia sasa kiwango cha kununua eneo au kipande cha ardhi katika fukwe ya bahari, gharama zake hazilingani na hali halisi ilivyo, lakini kila mmoja anaona kule ndio kwenye pesa nyingi na anaweza akafanya biashara kama hoteli za kitalii. Lipo tatizo, wakati wanamilikishwa maeneo yale, iwe katika Jiji la Dar es salaam au vijijini, bahari kule vijijini ndiko kunakojengwa hoteli za kitalii. Tunapowamilikisha na wanapoanza ujenzi na kwa vile katika maeneo ya vijiji tunaishi na wavuvi, sheria inasema tuache mita 60 kutoka kwenye bahari ndio ujenge pale inapoishia mita 60. Vile vile kati ya kiwanja na kiwanja, lazima kuwe na nafasi kwa wale wanakijiji waweze kufika katika ile *public land* ya mita 60.

Sasa wanapojenga wanaziba inakuwa ni kama uzio wa kilomita kwa kilomita kutokana na hoteli zilivyojengwa. Wavuvi wetu sasa wanakuwa hawana *access* ya kwenda kwenye ile *public land* na hatimaye wakafanya shughuli zao za uvuvi kutokana na hoteli za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini isitoshe hata Jiji la Dar es Salaam, maeneo ya makazi wanayoishi watu wanajenga zile nyumba zao na kuzungusha uzio wa ukuta. Wananchi wa Dar es Salaam wanashindwa kwenda kwenye *public land* ya *beach* angalau kupunga hewa. Hili limekuwa ni tatizo kubwa na imekuwa hatutoi nafasi au fursa kwa wananchi wengine kufika katika maeneo yale na kujipumzisha. Sasa Mheshimiwa Waziri, Halmashauri za Wilaya zimeorodhesha maeneo haya zimeleta Wizarani kwako, lakini tulikuwa tunahitaji msukumo wa ziada kutoka Wizarani. Sijui Mheshimiwa Waziri, hili utalitatu vipi ili tuondokane na haya matatizo na hatimaye kero hizi zinasababishwa na watu ambao hawataki kufuata sheria? Ahsante sana.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Mohamed R. Abdallah, Mbunge wa Pangani kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema Mheshimiwa Rished; ni kweli kwamba, kule kwenye fukwe tunatakiwa kuwe na nafasi ya raia na wao waende kupunga upepo kwa sababu ni eneo ambalo ni la wote, ile bahari ni ya wote. Sasa kama kuna watu kweli wanajenga wanaziba kila kitu mpaka wananchi hawawezi kupita na wao wakaenda kupunga upepo kule, ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo nilishalipata, nilishaletewa na Mbunge wa Kigamboni na nikamwambia kwamba, nitakwenda kuona hali ilivyo. Sasa hii ni mara ya pili, nasikia tena malalamiko hayo kutoka kwa Mbunge wa Pangani na amesema kwamba, Halmashauri imeshatuletea hili tatizo Wizarani. Wataalam wangu wote wa Wizara wapo ndani ya Bunge hili hivi sasa, kwa hiyo, wanasikia. Tukirudi tutatazama hilo tatizo la Pangani likoje ili tuweze kurudisha haki ya wananchi, wafike kupunga upepo kule baharini bila kuzuiwa na kuta au senyenge. (*Makofi*)

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa wananchi ambao wanakaa vijijini huwa wananyanyasika sana kuhusu ardhi zao, wakati mwingine shule zinajengwa au zahanati zinajengwa bila kushirikishwa, wanashitukia tu shule zimejengwa na kwenye ile sehemu unakuta kuna michikichi na mazao mbalimbali, lakini mwanakijiji yule anapokwenda kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji, wakati mwingine anaambiwa atoe posho kwanza ya Wajumbe wakati hiyo posho hana au wakati mwingine hiyo posho anaitoa, lakini pale maamuzi hayakamiliki anahamia kata. Kata inakuwa hivyo hivyo, anahamia Wilaya, mwisho anaenda mahakamani.

Anapokwenda mahakamani, unakuta anapewa hati ya kumiliki ile ardhi, lakini sasa unakuta ile *compensation* au fidia ya ile mimea haiapati, mwanakiji anasumbuka kuhusu ile fidia. Sasa Mheshimiwa Waziri, mimi nataka uwaambie wanakijiji wanaokaa vijijini hasa Kigoma Vijijini, wazee wengi sana wamekuwa wanasumbuka kuhusu mimea yao ambayo huwa inachukuliwa; je, wafanyeje?

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, hajasema anayewanyanyasa ni nani! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa suala la Mheshimiwa Sijapata Nkayamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya kutwaa ardhi kwa manufaa ya umma inasema kwamba, Serikali ikitaka eneo fulani kwa ajili ya shughuli ya umma, yule mwenye eneo anatakiwa afidiwe. Hii ndiyo sheria inavyosema kwa ujumla wake, lakini mazingira yanatofautiana; wakati mwingine kijiji kinakaa wanasema wanataka kujenga shule pale kijijini. Kijiji tu kimeamua kwamba tunataka kujenga shule, labda shule iliyopo

imeshajaa, wanataka kujenga shule ya pili ndani ya kijiji chao; haiwezekani watu wakashtukia kwamba shule tayari imeshajengwa, lazima wanashiriki katika kujenga hizi shule, yale madarasa lazima watakuwa wanashiriki kuyajenga. Katika mazingira hayo, Serikali ya Kijiji inachotakiwa sasa ikae na hao waliokuwa wanalima pale ielewane nao. Inawezekana kweli Serikali ya Kijiji haina fidia ya kuwalipa, lakini eneo lingine la huyu mtu aendelee kulima apate chakula na watoto wake, Serikali ya Kijiji inapaswa itoe. Kwamba, hili shamba lako tumejenga shule, wewe sasa ukalime eneo fulani. Vilevile nayo hiyo ni fidia maana fidia si lazima iwe pesa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Nkayamba, kujibu swali lako kama huo Mradi ni wa Serikali ya Kijiji; Serikali ya Kijiji inatakiwa ielewane na wale wenye shamba pale na fidia rahisi pale ni kumpa shamba lingine ili aendelee kulima apate chakula na watoto wake. Kama Mradi ni wa Serikali Kuu, imekuja pale ina Mradi na mmekubaliana nao, Serikali Kuu lazima itoe fidia, maana Serikali Kuu yenyewe pale haina ardhi, haiwezi ikatoa fidia ya ardhi, , kwa hiyo, lazima itoe fidia ya fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkayamba, unasema mtu amepata hati halafu ikaweje?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wazee hao wamekuwa wakisumbuka sana, unakuta wanatolewa kwenye sehemu waliyonayo, fidia hawalipwi na ardhi nyingine hawapewi, sasa wafanyeje?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nkayamba, si amesema hivyo. Kama ni ardhi ya kijiji, kijiji chenyewe kitawapa nyingine, kama ni ardhi ya Serikali Kuu, watawafidia. Sasa wewe hujasema ni ipi katika hayo?

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA:** Ya kijiji!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni ardhi ya kijiji, sasa kupitia Bunge hili na mimi ndiye Waziri wa Mambo ya Ardhi, nawaambia Halmashauri ya Kigoma, isimamie kijiji hicho kiwape eneo lingine hao walime, waendelee kupata chakula na watoto wao kwa sababu shamba lao la kwanza kijiji kimejenga shule. Nadhani wamenisikia na watakipa hicho kijiji ardhi nyingine waendelee kulima wale chakula na watoto wao. (*Makofi*)

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Mimi nimelazimishwa tu na Wizara kusimama, nadhani ndio mara yangu ya kwanza kusimama katika kipindi hiki. Katika Jimbo langu kuna mashamba tisa yenye ukubwa wa eneo la hekta 13,464.3, yalimilikishwa kuanzia mwaka 1986 mpaka leo hayajaendelezwa. Mimi nimechangia tangu mwaka 1996, nachangia kuulizia hatima ya mashamba hayo, sikupewa jibu. Mwaka 2001, Halmashauri ikaomba yafutiwe hati hizo, haikujibiwa. Mwaka 2002 wakaandika, hakuna jibu lililotolewa, mwaka jana nikachangia, hakuna jibu nililopewa. Sasa mimi nauliza; kuna matatizo gani katika mashamba hayo? Leo wakati nachangia kwa maandishi, nilimwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, wananchi wa maeneo hayo katika Kijiji cha Shigangama, Shilembu,

Ilula na Kibitilwa wapo kwenye redio hivi sasa wanasikiliza maelezo yake, kwa bahati mbaya hajajibu. Sasa watarudi nyumbani sijui wakaeleze nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba atoe maelezo; hatima ya mashamba hayo ni ipi? Niliomba kama hatua nyingine itaamuliwa kwa ajili ya mashamba haya, wananchi katika maeneo hayo washirikishwe kabla uamuzi haujafikiwa. Naomba maelezo.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda...

**MWENYEKITI:** Mwenyekiti!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Aha, Mwenyekiti! Samahani sana! Napenda kutoa ufafanuzi wa swali la ndugu yangu, Mheshimiwa Sakila, kama ifuatavyo:-

Katika hotuba yangu niliyoitoa jana, nilieleza kabisa kwamba, yale maeneo ambayo watu wamemilikishwa halafu miaka mingi imepita hawaendelezi na baadhi ya walimilikishwa wameshakwenda hata nje ya nchi kabisa hawaishi hapa, kwenye hotuba yangu hii nimesema kwamba, Halmashauri walete maeneo hayo, waombe miliki ile ifutwe ili yatumike kwa ukamilifu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kama Halmashauri yao walishaleta ombi hili miaka ya nyuma, pengine hata mafaili yameshafungwa kule Wizarani, hebu naomba wasumbuke tu walete tena kwa sababu mimi sasa nimetoa wito katika kitabu changu hiki. Walete ili kwa kweli tufute hizo miliki ili eneo hilo sasa wagawiwe watanzania wengine waliendeleze, tuinue uchumi wetu.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, niliulizia suala zima la *National Housing* wanarithisha madeni. Kwa mfano, unakuta kuna nyumba za *National Housing* zinadaiwa kodi nyingine shilingi milioni tatu, milioni sita mpaka milioni 13, lakini akija mteja mpya, wale wafanyakazi wa *National Housing* wanamwambia alipe lile deni ili aweze kupata hiyo nyumba. Sasa sijui wanatumia sheria ipi kumrithisha mtu ambaye siyo mwenye deni alipe deni lile na unakuta wale wanaodaiwa madeni yale bado wapo mjini?

Ningependa Mheshimiwa Waziri, anifafanulie ni sheria gani wanayoitumia kurithisha watu madeni na walikuwa wapi mpaka madeni yakafikia hapo yalipofikia?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja ya Mheshimiwa Lucy Owenya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo ndio leo nalisikia kwamba, mpangaji mpya anakwenda kuomba nyumba anaingia anaambiwa lakini aliyekuwa anakaa humu hakulipa deni, wewe sasa lipa. Sasa naomba unipe nafasi nikachunguze hili. Hata mimi sielewi sawa sawa, aliyesababisha deni mwingine na anayetakiwa alipe mwingine, yaani

ni sawa sawa mtu aliyekosa mwingine, anaadhibiwa mwingine. Naomba tu unipe muda nikalichunguze, nione ni nini hii ili kama kweli tatizo ni la dhati, tuweze kufanya marekebisho.

Ninachotaka kusema, natoa wito sasa hivi wapangaji wengi wa *National Housing* kwa kweli wanalipa vizuri sana. Kwa hiyo, wachache hao sugu waliobaki naomba na wao walipe, Shirika letu lipate afya, litufanyie kazi nzuri zaidi. Tatizo la kurithi madeni, naomba unipe muda nikachunguze ni nini hii ili kama lina ukweli tuweze kulitatua.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Kwa kumrahisishia Mheshimiwa Waziri, nitamletea *list* ya majina ya watu wote ambao wamerithishwa madeni. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Utakuwa umefanya kazi nzuri zaidi.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa MKURABITA na *TASAF* ni vyombo muhimu sana na vyombo hivi vyote vipo chini ya Ofisi ya Rais; na kwa kuwa Miradi ya *TASAF* imepelekwa Wilaya zote; Tanzania Bara na Visiwani na mwezi wa pili tulipata nafasi nzuri ya kutembelea Miradi ya MKURABITA Wilaya ya Handeni, pamoja na Bagamoyo. Sasa nini mikakati au mipango ya Serikali kuhakikisha kwamba, kwa bajeti zijazo Miradi hii inapelekwa Wilaya zote Tanzania Bara?

**MWENYEKITI:** Wewe umesema ipo Ofisi ya Rais, sasa unamwambia huyu ahakikishe; anahakikishaje jamani?

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu swali alisema kwamba, atamshauri Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo na mimi naomba amshauri Mheshimiwa Rais kwamba, miradi hii ya MKURABITA ipelekwe Wilaya zote.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Lubeleje ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ambayo inashughulikia masuala ya ofisi inayohusu MKURABITA na *TASAF* kama ifuatavyo: Utaratibu wa MKURABITA mpaka sasa ulikuwa katika *pilot stage* na sasa hivi utaratibu unafanywa katika bajeti hii ya mwaka 2008/2009 ili itekelezwe katika kila Wilaya; itahusu sekta karibu zote ambazo zitahusika na itahusu ubadilishaji wa sheria mbalimbali ili kurahisisha kurasimisha hizo mali ambazo zinakusudiwa.

**MWENYEKITI:** Nilitaka kusema MKURABITA siyo Mradi wala siyo Kitengo ni uratibu wa sheria tulizonazo ili ziweze kufuatana na mazingira. Kwa mfano, zoezi la kupima viwanja liende haraka zaidi lisichukue muda. Kwa hiyo, siyo kitengo, haya mambo sasa yameingia katika Wizara mbalimbali. Baada ya kutunga sheria zitakapoletwa na Wizara hizi, wao ndiyo watakuwa wanafanya kazi zile ambazo MKURABITA imejaribu kuangalia kwamba inachukua muda mrefu sana kutoa hati, hakuna njia iliyo rahisi zaidi, ndiyo ilikuwa madhumuni yake. Kwa hiyo, siyo mradi

peke yake, utaingia katika Wizara mbalimbali zitakazokuwa zinahusika. Huo ndiyo MKURABITA.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimemwomba Waziri anipe ufafanuzi kuhusu watu wanaoishi kwenye maeneo ambayo wamebanana sana, wakiwepo watu wa Mkoa wa Kilimanjaro. Niliuliza kwamba, hivi Serikali ina mpango gani kutoa maelekezo rasmi kwamba wale ambao wapo tayari sasa kuhamia kwenye eneo lingine katika nchi yetu wawe wamepangiwa, lakini pia nikawa nimeulizia uwezekano wa maeneo hayo ambayo watahamishiwa endapo watakuwa wamewekewa miundombinu ya barabara, umeme, mashule na vitu kama hivyo ili iwe kama motisha kuliko watu wanakaa eneo moja tu na kubanana pale wakiwepo wa Mkoa wa Kilimanjaro na mikoa mingine kama Dar es Salaam ambako wamebanana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nikawa nimeuliza kwamba, wapo vijana wetu wanaoishi kwenye mazingira magumu; katika hali ya utoto unakuta kwamba kuna watu wengi wanawasaidia wengi wao pia ni yatima, wanapofikia umri wa miaka 21 wanakuwa watu wazima hata ile kuwasaidia tena inakuwa imekwisha. Kwa sasa wamekuwa wengi lakini hawajui watapata wapi maeneo yao wenyewe waweze kumiliki nyumbani kwao. Nikauliza je, Serikali inalijua hilo na imejiandaa vipi kwa vijana hao au hapo baadaye tunatarajia vijana hawa sasa wawe majambazi au wasiwe na nyumba; wawe na shida toka utotoni mpaka katika uzee wao? Huo ndiyo ufafanuzi niliokuwa nimemwomba Waziri wa Ardhi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ufafanuzi kwa hoja za Mheshimiwa Shally Raymond kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu watu ambao wapo katika maeneo ambayo wamebanana sana, ardhi imekwisha na bado wanaongezeka Serikali inafanyaje; kwenye maelezo yangu ya awali nilisema kwamba, kuna Tume ya Mpango ya Ardhi na nimesema kwamba, Tume ile imeshamaliza Mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi. Wameitazama Tanzania nzima Mkoa kwa Mkoa; maeneo gani yanafaa kwa kitu gani, yapi ambayo sasa hivi bado yako tupu watu wanaweza kwenda kukaa kule. Kupitia Mpango huu na nimesema kwamba, tunajiandaa kuja kutoa semina kuhusu jambo hili katika Bunge; ni jambo kubwa na jipya, hatujawahi kuwa na Mpango wa namna hii tangu Uhuru.

Kwa hiyo, Mpango huu utatupa picha ya maeneo ambayo sasa hivi yameshajaa na maeneo ambayo sasa hivi bado yapo tupu na tufanyeje ili waende kule. Kwa hiyo, Mpango huu utajibu hili swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapowapeleka watu mahali fulani ambako sasa wamebanana, huwezi kuwatupa tu porini ni lazima ufanye huduma za mwanzo ili mahali pale watu waweze kukaa. Kwa hiyo, jambo hili litakuwemo katika Mpango wa Taifa wa matumizi ya ardhi. S wali lake la pili, Mheshimiwa Shally Raymond hili kwa kweli si

swali la Waziri wa Ardhi ni Wizara nyingine tu, lakini nasema; hao vijana kama ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Vijana na Kazi ama *NGOs* imekuza vijana sasa wanataka wafanye shughuli labda ya kilimo na kitu kingine, kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa sababu Wizara ya Ardhi yenyewe haina ardhi lakini kwa kushirikiana na wenye ardhi ambao ni Serikali za Mitaa, hatutashindwa. Vijana kama wameshakuwa *organized* wanataka kulima, hatuwezi kushindwa kuwapa ardhi ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, kama kuna vijana walio kwenye mazingira magumu wa miaka 21 wamejikusanya katika vikundi wanataka wapangiwe mahali wafanye shughuli za kulima; Tanzania ni kubwa sana na ardhi ni kubwa sana, tunawakaribisha watapata ardhi.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri atumie huruma zake kwa kiwanja *Plot 1273 Masaki*, ambacho nilipewa tarehe 12 Februari, 1990; kwa bahati mbaya sijapata hati ingawa ninayo malipo niliyolipia mpaka mwaka jana. Naomba anifafanulie au anaweza akaniambia tuonane naye baadaye?

**MWENYEKITI:** Profesa, unajua kuna kanuni kabisa inasema mtu anapozungumza suala fulani kama ana *personal interest* itabidi aseme na thamani yake na nini. Mimi nadhani hilo wewe ungelichukua ukaongea na Waziri kuliko kuiambia dunia nzima. Mheshimiwa Waziri, kama unataka kujibu lakini nilifikiri haipendezi!

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba tu kaka yangu Mheshimiwa Profesa Mtulia, aje na hizo nyaraka zake na tutasaidiana tu wala asiwe na wasiwasi. Aje tutamsaidia kama tunavyowasaidia wengine wengi tu na wewe una haki ya kusaidiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*..... Sh. 4,247,309,630  
 Kif. 1003 - *Policy and Planning*... .. Sh. 789,488,040  
 Kif. 1004 - *Management Information System*... .. Sh. 286,144,840  
 Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*... .. Sh. 169,139,520  
 Kif. 1006 - *Procurement Management Unit*... .. Sh. 232,964,840

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Land Development*... .. Sh. 1,260,698,099  
 Kif. 2002 - *Survey and Mapping*... .. Sh. 1603,384860  
 Kif. 2003 - *Registrar of Titles*... .. Sh. 398,734,360  
 Kif. 2004 - *Valuation Unit*... .. Sh. 251,569,000



Kif. 3001 - *Physical Planning Division*..... Sh. 245344318  
Kif. 3002 - *Housing Division*... .. Sh. 1,484,314,720  
Kif. 3003 - *Disrict Land and Housing Tribunal*... .. Sh. 1,836810,273

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

### **Fungu 48 - Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 - *Adminstration and General*... .. Sh. 134,847,000  
Kif. 1002 - *Finance and Account*..... Sh. 482,500,000  
Kif. 1003 - *Policy and Planning*... .. Sh. 575,000,000  
Kif. 2001 - *Land Development*... .. Sh. 364,690,000  
Kif. 2002 - *Survey and Mapping* ..... Sh.7,831,831,000  
Kif. 3001 - *Physical Planning Division*... .. Sh. 9,388,668,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya  
Matumizi bila mabadiliko yoyote)  
(Bunge lilirudia)*

## **T A A R I F A**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa  
mwaka 2008/2009  
yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu Wizara ameichukua juzi tu. Amejibu kwa

ukamilifu sana na umeturidhisha sisi sote na tunakutakia kheri wewe na Wizara yako ili muweze kufanya kazi nzuri zaidi mwaka ujao. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha matangazo kwamba, Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake; wiki ijayo watafanya maonyesho kwenye Viwanja vyetu vya Maonyesho katika Jengo la Utawala kuhusu dhana mbalimbali zilizopo katika Wizara hiyo. Kwa hiyo, Wabunge mnakaribishwa pale kwa sababu mtakapojifunza mambo kama ya *RITA*, yatawasaidia kwenye Majimbo yenu kuweza kuwaelimisha wananchi faida ya *RITA* na mambo mengine yanayofanana na hayo. Tunayo semina ya kutathmini mambo ya *African Peer Review Mechanism*; kutathmini nchi inaendeshaje utawala bora. Semina hiyo ipo tarehe 9 Agosti, 2008, saa tatu asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Kesho tarehe 8 Agosti, 2008 timu yetu ya *Netball* na timu yetu ya *Football* watakuwa na mashindano ya mpira saa kumi katika Kiwanja cha Jamhuri, watahindana na Timu za *PPF*. Pia tarehe 9 Agosti, 2008 timu zetu hizo pia zitashindana na Timu ya *NMB*, wataanza mchezo saa tisa na siku ya tarehe 8 Agosti, 2008 wataanza saa kumi katika Uwanja huo wa Jamhuri.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tarehe 8 Agosti, 2008 pia kutakuwa na chakula cha jioni na dansi katika Ukumbi wetu wa *Basement* saa moja na nusu. Tarehe 9 Agosti, 2008 pia kutakuwa na dansi na bendi zitakazotumbuiza mojawapo itakuwa ni *TOT Respect*; nadhani mnaifahamu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 9 Agosti, 2008 tutakuwa pia na semina mchana saa saba, kwa sababu asubuhi kuna semina ya *APRM* halafu saa saba ndiyo itakuwa semina nyingine ambayo itaendelea na Siku ya Jumapili. Semina hii imeandaliwa na *TGNP*, watakaohusika ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati ya Huduma za Jamii na Wabunge Wanawake wote.

Waheshimiwa Wabunge, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Estherina Kilasi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, Jumamosi tarehe 9 Agosti, 2008, kuanzia saa tano na nusu asubuhi katika Ukumbi Na. 227, wanatakiwa kuhudhuria Kikao Maalum cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati yao. Ofisi inatangaza kwamba, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mheshimiwa William Lukuvi, anawatangazia Wabunge wote kwamba, kesho tarehe 8 Agosti, 2008 kutakuwa na Sherehe ya Ufungaji wa Maonyesho ya Wakulima Nanenane. Sherehe hizo zitaanza saa tisa mchana kwenye Viwanja vya Nzuguni; Wabunge wote mnakaribishwa. Kwa wale watakaotaka kwenda, usafiri utakuwepo hapa ofisini.

Tumekuwa na wiki fupi kwa sababu kesho ni sikukuu hatutakuwa na Bunge. Kwa hiyo, nawatakieni shughuli njema ya Nanenane na *weekend* njema kwa semina na mikutano inayohusika na burudani zilizoandaliwa, mnakaribishwa wote. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu, katika wiki hii tumefanya kazi vizuri; niwatakie mapumziko mema jioni hii.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka Siku ya Jumatatu tarehe kumi na moja saa tatu asubuhi. Tutaanza na Wizara ya Viwanda na Biashara.

*(Saa 01.17 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 11 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*